

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 3 Julai, 2008**

*(Mkutano Ulianaza Saa Tatuhu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo ni Alhamisi nusu saa ya kwanza tutatumia kwa kumwuliza Maswali ya Papo kwa Papo Mheshimiwa Waziri Mkuu. Leo kwa bahati nzuri namwona Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kumwuliza Waziri Mkuu kila siku ataanza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani halafu tunaendelea na wengine.

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je, ni nini msimamo wa Serikali juu ya uhalali au kutokuwa halali Rais Mugabe wa Zimbabwe?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed swali lake zuri na muhimu sana kama ifuatavyo:-

Nadhani na yeye atakuwa ameshuhudia kwamba katika kikao kilichokuwa kinaendelea Sharm – El Sheikh mtazamo wa viongozi wote wa nchi huru za Afrika ilikuwa ni kumsaidia Rais Mugabe aweze kukaa chini na kuzungumza na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Kwa hiyo, mimi tafsiri yangu ni kwamba wanaunga mkono juhudini za kujaribu kutatua mgogoro ule kwa njia ya majadiliano. Sidhani kama Tanzania itakuwa na msimamo tofauti zaidi ya ule ambaa nimeuona kwenye Kikao. (*Makofit*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Kwa kuwa *AU* imeshauri kwamba iundwe Serikali ya pamoja na kwa kuwa utaratibu wa *winners takes all* ndiyo utaratibu unaotumika katika nchi zetu hizi za Kiafrika hasa zile ambazo zimetawaliwa na Waingereza. Kwa hapa kwetu utaratibu huo umetakiwa ufanywe kwa kura ya maoni ni kwa nini Rais Kikwete ambaye ni Mwenyekiti wa *AU* na vile vile ndiye aliyesikilia msimamo wa kuwa na kura ya maoni. Kwa nini asingewashauri wa Zimbabwe nao

wakaitisha kura ya maoni ili wafanye Serikali ya pamoja kama walivyofanya kwa Tanzania? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu rafiki yangu Hamad Rashid Mohamed swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kura za maoni kwa upande wa Zimbabwe ni maamuzi ya Serikali yenyewe ya Zimbabwe na hatuna sababu hasa ya kujaribu kuliuliza sana hilo. Mambo haya yanaamuliwa kulingana na mazingira halisi yanayo- *prevail* wakati huo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** *Microphone* yako hatukusikii jaribu tena. Tumia nyingine.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naam nakushukuru. Siku ya Ijumaa tarehe 27 Juni, 2008 katika ofisi yako ilitamka kwamba Zanzibar si nchi.

**NAIBU SPIKA:** Ofisi ya Waziri?

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo, ilisema kwamba Zanzibar si nchi na bila Zanzibar hata Tanzania hakuna na Zanzibar ina mamlaka yote, ina Rais wake, ina mihimili yote, ina wimbo wake na hali kadhalika bendera yake. Je, utawaelezaje wananchi wa Zanzibar kuhusu suala hili kwamba kweli si nchi kutokana na ilivyo kama nchi nyingine?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kidogo nimeshtuka sana. Swali hili linanikanganya kidogo kwa sababu Katiba iko wazi kabisa kwamba hii ni nchi moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni nchi moja lakini yenyе Serikali mbili. Hivyo ndivyo tulivyokubaliana.

Kwa hiyo, suala la Zanzibar kuwa nchi halipo mpaka hapo pengine Katiba itakapokuwa imerekebishwa kulingana na mazingira halisi yatakayojitokeza. Lakini kwa sasa ni nchi moja isipokuwa ina Serikali mbili na kuna maamuzi yanafanywa ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar lakini mengine ni ya Muungano ndiyo inabidi tushirikishe pande zote mbili. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na sera pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, rasilimali za nchi hii ni muhimu katika kuwakomboa wananchi wetu kwa ustawi wa jamii nzima. Moja ya rasilimali hizo ni gesi ambayo tumeigundua hapa Tanzania kwa wingi. Pamoja na mikakati ya Serikali ni hatua gani ambazo tayari zimekwishachukuliwa ili kuiokoa hii nchi na tatizo la upandaji wa bei ya mafuta katika dunia?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah najua ni mmoja kati ya Wabunge ambaye anafuatilia sana sana uendelezaji wa suala hili la gesi. Ninachowea kukuambia gesi Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah *of course* Waziri wa Nishati na Madini atajaribu naye kulieleza wakati anawasilisha Bajeti yake. Lakini nilitaka nikuhakikishie tu kwamba hatua ambazo zimeanza kuchukuliwa ni nzuri sana. Kwa maana kwamba kwa mfano gesi ile ya Mtwara licha ya kwamba itatusaidia kupata umeme kidogo pale na pengine uzalishaji wa saruji lakini ni azma ya Serikali vile vile kuchimba visima zaidi *STET* kwa ajili ya kupata uwezo mkubwa zaidi wa ile gesi.

Kwa hiyo, tunaamini tutakwenda vizuri na huo utaratibu. Lakini hata hii ya Songosongo na yenyewe tayari ya Serikali imejipanga kupanua ule mfereji wake wa kupitisha *gas* ili tuweze kuwa na gesi nyingi zaidi iweze kutumika majumbani lakini vile kwa matumizi mengine kwa ajili ya kituo chetu cha Ubungo. Kwa hiyo, naamini jitihada zinazoendelea kwa maana ya mpango ni kujaribu kwa kadri itakavyowezekana kupata *private sector* iwe *involved* katika uchimbaji wa gesi kwa kadri itakavyowezekana. (*Makofî*)

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yake mazuri na fasaha.

Pamoja na ulivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu utakubaliana na mimi sasa kwamba zinahitajika juhudzi za makusudi kwa viongozi wetu wa juu kama wewe na Mheshimiwa Makamu wa Rais na Rais mwenyewe kutoa kipaumbele kwa maana ya kuwa na *eyes on, hands on* kwa Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha kwamba azma inatekelezwa haraka kabisa kwa sababu ya *crises* tunazoziona mbele ya safari? (*Makofî*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Rished kwamba kwa kweli msimamo ndiyo huo. Tunalikazania hili kwa sababu tunataka tuondokane kabisa na tatizo hili la umeme hasa huu wa kukodishe mitambo mbalimbali. Gesi ni umeme wa uhakika, lakini gesi vile vile ni *foreign exchange*, lakini gesi vile kwa matumizi ya nyumbani ni jambo la msingi sana. Kwa hiyo, tumebahatika kwa hiyo lazima kwa kweli na sisi tutumie kila *energy* kuhakikisha rasilimali hii inatumika inavyotakiwa. Hilo naweza nikuhakikisha kabisa. (*Makofî*)

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali mara kwa mara imekuwa ikisikika ikisema bila kuwashirikisha wananchi na vyombo vyao vyaa uwakilishi huduma zitolewazo zitaathirika. Sambamba na hilo Serikali imekuwa ikipeleka fedha nyingi sana kupitia mfumo wake wa *D by D* katika Halmashauri zetu kwa lengo la kuinua ufanisi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali lakini na kuinua kiwango cha uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma.

Lakini Vikao vya Baraza la Madiwani vimekuwa vikipewa siku moja tu. Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati sasa wa kuongeza siku za Vikao vya Baraza la Madiwani vya kujadili na kupidisha Bajeti vya kufuatilia matumizi ya fedha za umma na miradi mbalimbali ili kutoa fursa zaidi kwa Halmashauri hizi kusimamia miradi na matumizi mbalimbali katika Halmashauri? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu rafiki yangu Mpina kama ifuatavyo:-

Analolisema ni kweli. Rasilimali kubwa sana sasa inakwenda kwenye Halmashauri zetu. Lengo la Serikali ni katika kuimarisha mfumo mzima wa madaraka kwa wananchi. Sasa kwa upande mmoja anazungumza namna tunavyochakata Bajeti kwenye Halmashauri zetu kwamba inachukua siku moja.

Lakini hii ilifanyika hivyo kwa sababu tunaamini kabisa kwamba kabla ya siku ile ya Bajeti huwa kuna Kamati ya Fedha ambayo huwa inapata vile vile muda wa kupitia vizuri sana matayarisho ya Bajeti. Lakini kwa kuwa jambo hili si mara ya kwanza kulisikia, nadhani iko haja pengine tukalitazama angalau tukaweka siku mbili kwa maana ya mjadala wenyewe wa Bajeti kwenye Halmashauri ili wasiburuzwe tu Madiwani hata kwa mambo ambayo wangeweza pengine wakapata muda wa kuyatafakari. Kwa hiyo, nadhani tutali-*take up seriously* tuone kama itawezekana kuanzia *financial year* inayokuja.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyojibu kwa ufasaha maswali yetu. Swali langu la leo ni swali ushauri. Katika nchi yetu upanuzi wa miji huambatana na kitendo cha kuwahamisha wakulima wadogo wadogo wa mihogo, mchicha kwenda nje ya mji na kuwafanya maskini zaidi kwa sababu kule hukosa ardhi na huduma zile ambazo wakati mwingine huzipata katika miji.

Mwelekeo huu ukiachwa uendelee utawafukuza watu maskini na kufanya nchi nzima ya Tanzania ijae majengo. Je, nini mtazamo wako Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni kwamba wakati umefika wa kuelekeza wale viongozi wa Miji kujenga nyumba za maghorofa badala ya kujenga *bungalows* ambazo husababisha maeneo kutumia makubwa zaidi katika upanuzi wa Miji?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mzee wangu Mheshimiwa Makwetta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo matatu pale ambayo mimi haraka haraka nayaona kwamba ni muhimu wa wananchi wenyewe hasa wale wanaoishi mijini kuzingatia sheria za Mipango Miji. Maana kikwazo kimojawapo ni kwa sababu usipoheshimu suala la Mipango Miji ndipo unakabiliana na matatizo ya hama nenda kulia, nenda kushoto. Kwa hiyo, jambo la kwanza ni sheria; tukizifuata zinaweza zikapunguza ile dharuba ya kuhamishwa kila wakati.

Lakini jambo la pili ni kweli kwamba ni vizuri na kwa kweli tulishalisema hili na katika baadhi ya miji kama Mwanza tumeshauri sana hawana maeneo ya kutosha na kwa hiyo, tulipokuwa kwenye *program* ya kujenga shule za sekondari tukashauri wajaribu kujenga maghorofa ili kuweza ku-*accommodate* watoto wengi zaidi.

Hilo ni jambo linalowezekana hata kwa maeneo mengine. Tahadhari ambayo mimi naitoa katika suala hili ni kwamba kwa sasa ninavyoona bado tuna tatizo la uwezo wa wasimamizi wa majengo ya maghorofa. Kwa hiyo, wakati nalikubali lakini lazima vile vile tuwe *conscious* kuhakikisha kwamba tukiazimia hilo basi kila Halmashauri ihakikishe inao wahandisi wa kweli na wenye uwezo wa kufuatilia ujenzi huo hatua kwa hatua. Vinginevyo tutaleta matatizo kama yaliyotokea juzi au kesi hasa ile ya China watu wameacha kutazama lile lililofanyika wanazungumza uwezo wa mkandarasi aliyejenga jengo la ghorofa. Nalikubali lakini itabidi lifanyiwe kazi ya ziada. (*Makofi*)

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi asubuhi hii ili niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hapa kwetu Tanzania sasa kumeshamiri kuwepo kwa mauaji ya makundi mbalimbali kama vile wakongwe na maalbino; na kwa kuwa, kwa hivi sasa Jimboni kwangu Tandahimba kumejitokeza mauaji ya wanawake kwa kuwakata koromeo, hivi leo ninavyoongea jumla wanawake sita wamekatwa koromeo akiwemo mwanafunzi wa darasa la sita katika Kijiji cha Milindu.

Jambo hili ni kinyume cha Katiba kwa maana ya haki ya kuishi; na kwa kuwa mwanzo wa ngoma ni lele na kwa tabia ya watu sisi wa Kusini ambao ni wapole, mambo hayo ni mapya; na kwa kuwa hali hiyo inawafanya wananchi wa kule wasiende mashambani kwa hofu; na kwa kuwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Mkoa imechukua hatua lakini imeshindwa, maana hadi sasa hakuna ye yeyote aliyekamatwa wala kukisiwa. Je, Serikali inaa hidi nini kudhibiti hali hiyo kwa wananchi wa kule? Ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpe pole sana Mheshimiwa Mbunge wa Tandahimba kwa tatizo hilo kubwa lililoibuka hivi karibuni. Sina hakika huko kisingizio ni nini! Maana katika maeneo mengine tunaelewa. Kuna wachimbaji wa madini wanatafuta hili na wanatafuta lile, sehemu nyingine ni fikra za kichawi tu na ushirikina. Kwa Tandahimba Mtwara naona jambo limeibuka ambalo si la kawaida na ni jipya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge na kwa kweli kuwaahidi wananchi wote wa Mtwara nitalichukulia jambo hili kwa uzito unaostahili kujaribu kuhakikisha kwamba *IGP* na timu yake wanasimamia vizuri uchunguzi wa haraka kuona hasa ni kwa nini na akina nani ili tuweze kwa pamoja kukabiliana na hilo tatizo ambalo si zuri sana. (*Makofi*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kumekuwa na juhudhi za mara kwa mara za kusaidia kuondoa tatizo sugu la maji hapa nchini. Serikali imejitahidi kuweka programu na miradi mbalimbali ya maji, lakini kuna hii ambayo ipo sasa hivi ya Benki ya Dunia ambako kuna mradi wa *RWSSP*. Mwaka

chini 2003/2004 kuna Wilaya za mwanzo zilianza kuingia kwenye programu hiyo lakini bado zina matatizo. Mwaka 2004/2005 kuna Wilaya 50 ikiwemo na Wilaya ya Nzega nazo zimeingia kwenye *Project* hiyo, lakini bado mradi huo una matatizo. Je, hivi kiini cha matatizo hayo ni nini? Ni Halmashauri zetu, ni Mikoa au ni Benki ya Dunia wenyewe na Serikali inasemaje hapo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika kwanza Waziri wa Kisekta anayehusika na Maji itakapofika wakati wake atalieleza zaidi jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninataka nimwambie tu Mheshimiwa Lucas Selelii kwamba Mpango huo wa Maji kupitia Benki ya Dunia si yeye tu karibu nchi nzima kuna malalamiko makubwa sana, na ndiyo maana atakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi alipowasilisha Bajeti ya Serikali lilijitokeza hili kwa nguvu. Serikali ikasema itakaa chini kujaribu kutafakari namna bora zaidi ya kutekeleza mpango huo.

Sasa tatizo hapo ni kwa sababu tunategemea msaada kutoka nje. Sasa na misaada hiyo inakuwa na masharti mengi, na mchakato wenyewe mpaka kufikia kumpata mzabuni ni mrefu kweli kweli.

Kwa hiyo, nadhani dawa ni sisi wenyewe kwanza ndani ya Serikali kukaa tena upya na kuona nini tufanye ili kwa kweli tatizo hili au kero hii ya maji iweze kupata suluhu mapema inavyowezekana. (*Makofi*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumzia suala la ardhi. Ardhi toka nchi yetu ipate uhuru kumekuwepo na Sheria, Maazimio na Miongozo na Sera mbalimbali. Wakati wa Azimio la Arusha *Nyarubanja* ilipigwa marufuku. Nilikuwa nataka kujua Serikali yake sasa hivi inasema nini kuhusu suala la *Nyarubanja* kabla sijauliza swali langu. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali lako lote huwezi kutega watu.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kama suala la kuhodhi ardhi halikubaliki katika Sheria na Sera za nchi, inakuwaje watu wanahodhi ardhi na tatizo hili liko kule Mpanda na hususan wapiga kura wa Jimbo la Mpanda Kati ambao hawana maeneo ya kulima wanalahizimika kwenda katika maeneo ambayo yamekamatwa na watu hasa kule Kakese kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu analifahamu tatizo hilo, na wanapewa vipande vya ardhi kulima na kisha walipe mazao, eka moja ya mpunga atoe gunia sita kwa mwenye ardhi. Je, suala hili Serikali inasemaje?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Said Arfi, kwa kuuliza swali hili. Lakini angeeleza kidogo *background* yake ingeweza kuwa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wa kabilia la Wasukuma wamehamia kwa wingi sana katika Wilaya ya Mpanda na Rukwa kwa ujumla. Kilichotokea wamekuta maeneo kule yako wazi hayalimwi na wenyeji na mengi yalikuwa ni mabonde mazuri sana.

Kwa hiyo, walikaa kwenye maeneo hayo kwa sababu yalikuwa *empty* sehemu kubwa na sehemu zingine zilikuwa zikitumika kwa uvuvi tu na kuwinda wanyama wa porini. Imetuchukua karibu miaka 20 hivi kutambua kwamba ardhi ile kumbe ina thamani kubwa sana. Walichokuwa wamefanya hao jamaa baada ya kuona ardhi ni nzuri wakahodhi maeneo makubwa tu kwa sababu hayakuwa na mtu yejote.

Sasa wamekuja wametambua na wao wanasema karibuni hili ni eneo langu ukitaka eka moja lete gunia tano. Ndiyo hasa msingi ulipoanzia. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hakuna *Nyarubanja* kwa maana ya mfumo ambao unakubalika hapa nchini. Lakini jambo hili ni changamoto kwa Mkoa wa Rukwa hasa kwamba ni vizuri tukakaa, tukazungumza na wafugaji hao wajaribu kukubaliana utaratibu mzuri wa namna ya kumiliki ardhi iliyopo hivi sasa, na wale wenye maeneo makubwa kupita kiasi. Maana wengine wanachukua ekari 300, wengine wanachukua ekari 1,000, lakini wanalima kidogo sana. Sasa hii inataka tu maamuzi ya Kimko na wakikubaliana inawezekana hii kabisa likapungua kwa kiasi kikubwa sana. (*Makofi*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo hili linafahamika kama alivyokuwa ameleezea Mheshimiwa Waziri Mkuu; katika kijiji cha Kakese kulikuwa na shamba ambalo linafahamika kama shamba la Benki.

Mheshimiowa Spika, eneo hili limeleta matatizo makubwa sana na hatimaye Serikali ya Kijiji cha Kakese ikaamua kuiomba Serikali iweze kufuta Hatimiliki ya eneo hilo ili wananchi hao waweze kugawana eneo hilo na kulima. Kwa sababu mwenye Hati ya kumiliki eneo hilo ameshindwa kuliendeleza. Je, Serikali sasa inaweza kufikiria kumwomba Mheshimiwa Rais kufuta hati hiyo kama ilivyopendekeza Serikali ya Kijiji?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, utatuwia radhi naona maswali yote ni ya Mpanda, lakini acha nijaribu kulijibu. Mimi ninachowea kumwahidi tu Mheshimiwa Said Arfi, ni kwamba *okay* tukae pamoja tulione hili jambo.

Mimi sidhani kama lina mgogoro mkubwa. Tunaweza kabisa tukapata hiyo Hati ikafutwa ili mradi kweli, lile eneo haliendelezwi. Kwa hiyo, nadhani ni letu tu, tukizungumza nadhani tunaweza tukalimaliza vizuri. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana. Kwa wale waliopata nafasi ya kuuliza maswali wameuliza wote, na ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ukae maana maswali yamekwisha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, masomo tuliyoyapata leo wale wengine wote waliouliza maswali wameuliza vizuri sana kwa sababu ni maswali ya kisera ya kitaifa, hata Mheshimiwa Waziri Mkuu ameweza kuyajibu.

Kama Mheshimiwa Waziri Mkuu asingekuwa anatoka Mpanda suala la ardhi lingekuwa tatizo na lingefutwa. Lakini kwa sababu nilijua na ye ye anatoka huko huko labda anaelewa elewa. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, cha kujifunza ni kwamba tunapomwuliza Waziri Mkuu Maswali ni lazima yawe maswali ya kitaifa na ya kisera kwa sababu atajibu kama Waziri Mkuu. Lakini ukimwuliza kuhusu kijiji fulani mpaka kule nyumbani kwako hawezo na siyo shughuli yake. Kwa hiyo, mmeefanya vizuri na waliouliza maswali wameuliza kwa kifupi.

Kwa hiyo, wiki ijayo nadhani tutaongeza orodha ya Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu inaelekea mkiuliza kwa kifupi na Waziri Mkuu akajibu tunaweza kupata nafasi watu wengi zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naendelea na *Order Paper* ya kawaida, Katibu endelea na *Order Paper*.

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 152

### **Miji Kujengwa bila Mipango Miji Mizuri**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (K.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa ubora wa Miji ni kuwa na Mipango Miji mizuri:-

Je, ni kwa nini Miji yetu na Miji midogo inaendelea kujengwa bila kuwa na mipango Miji inayosaidia Miji na Miji midogo kujengwa kisasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba ili Miji yetu iwe na Maendeleo endelevu inategemea kuwepo kwa Mipango Miji mizuri.

Mipango Miji mizuri ni ile inayoandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mipango na kusimamiwa vizuri katika hatua mbalimbali za utekelezaji na kufanyiwa mapitio (*Review*) kila haja ya kufanya hivyo inapojitokeza hasa kutokana na ongezeko la idadi ya watu, mabadiliko ya kiuchumi, sera na sheria.

Baadhi ya Miji na Miji Midogo katika nchi yetu imekuwa ikiendelea kujengwa bila kuzingatia Mipango Miji inayosaidia Miji na Miji midogo kujengwa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato mzima wa Maendeleo ya Miji, sheria zilizokuwa zikitumika ikiwa ni pamoja na Sheria ya Mipango Miji na vijiji (Sura 378 ya mwaka 1956) haikuwa shirikishi kwa kuwa utekelezaji wake ulikuwa hauzingatii baadhi ya vipengele ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadau muhimu katika kupanga, kutekeleza na kusimamia shughuli mbalimbali za uendelezaji Miji. Sheria hiyo ilirekebishwa na kuitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulipa msukumo suala la Maendeleo ya Miji hapa nchini Serikali kuitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeandaa mipango ya aina mbili ya kuongoza uendelezaji wa Miji.

Mipango hiyo ni ya muda mrefu ambayo utekelezaji wake huchukua miaka ishirini (*Master Plans*) na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya muda mfupi ambayo huchukua miaka mitano hadi kumi (*interim land use Plans*).

Halmashauri ambazo tayari zimekamilisha mipango ya matumizi ya ardhi ya muda mfupi ni Tandahimba, Tunduru, Namtumbo, Masasi, Babati, Simanjiro kwa eneo la (Mererani), Bukombe katika la eneo la (Ushirombo) na Misungwi. Halmashauri zinazokamilisha miji hiyo ya muda mfupi kwa sasa ni Mvomero, Kongwa katika maeneo ya (Kibaigwa), Bunda, Chato, Kasulu, Kibondo, Maswa na Kyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mipango ya muda mrefu (*Master Plans*), maandalizi yamekwisha kufanyika katika Jiji la Mwanza, Dar es Salaam, Manispaa ya Mtwara/Mikindani na Kigoma. Napenda kuhimiza Halmashauri ambazo zina mipango ya muda mrefu au mfupi kuandaa mipango ya kina (*detailed lay outs*) ili kuweza kupata viwanja vyta kupimwa na kuendeleza.

Aidha, ili kuhakikisha kwamba mji midogo inapoanzishwa inalo eneo la kutosha, Mamlaka ya miji mdogo pamoja na vigezo vingine, inapaswa kuwa na shughuli za kimji na kuwa na eneo lisilopungua kilometra za mraba 580 kwa ajili ya kuendeleza.

Katika hatua nyingine, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri husika imekuwa inaandaa mipango ya kuendeleza upya maeneo ya kati ya miji (*Redevelopment schemes*). Mipango hii inaandaliwa ili kuwezesha uwekezaji mpya na kufanya m aeneo hayo yawe yenye thamani kubwa ya ardhi hatimaye yaweze kuchangia ipasavyo katika uchumi wa miji hiyo na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto tunayopata kuhusu mipango miji ni kukua kwa kasi kwa miji hapa nchini ni pamoja na idadi ya watu katika miji yetu imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 4.5 kwa mwaka. Inakadiriwa kwamba ifikapo mwaka 2025, nusu ya Watanzania watakuwa wanaishi mijini. Kutokana na ongezeko kubwa la watu mijini, mahitaji ya makazi yaliyopangwa yataongezeka.

Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuliona suala hili kwa mtazamo chanya na kuchukua hatua za makusudi za kuhakikisha kwamba miji inapimwa na kupangwa ili kuzuia upanukaji wa maeneo yasiyopangwa mijini. Pia nawaasa wananchi kuacha tabia ya kujenga katika maeneo yasiyopimwa na badala yake waombe viwanja vilivyopimwa kutoka katika Halmashauri zao. Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itahakikisha kwamba Halmashauri zinaandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto hiyo.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Sheria zipo na Serikali ndiyo inayofahamu hata harakati za kiuchumi za watu wa nchi hii. Lakini sasa utakuta kwamba mara nyingi hizi bomoa bomoa zinazotokea zinawachukiza wananchi, wanaichukia Serikali yenyewe bila sababu za msingi. Je, Serikali pamoja na mipango yote iliyosema imejiandaa vipi katika kuzipa Halmashauri hizi uwezo wa fedha lakini pia na watumishi kwa ajili ya kufanya hii miradi ya mipango miji katika kipindi cha miaka ya hivi tuzungumzie hasa kwa Bajeti ya mwaka 2008/2009? Suala la kwanza. (*Makofi*)

Lakini swali la pili Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali wakati mwingine itambue tu kwamba tunavyo vyuo vikuu, tunao wataalam wa kutosha, tunaweza tukafanya miradi midogo midogo na tukapunguza kero hii. Hata siku moja hujasikia wananchi kikiitwa kupewa viwanja vilivyopimwa. Lakini umakuta vinatolewa kimya kimya. Je, Serikali haioni jambo hili ndiyo linalosababisha watu kujenga kiholela katika miji yetu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru sana kwamba leo asubuhi hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia suala la kujenga miji yetu kwa kufuata sheria wakati alipokuwa anajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Makwetta. Ninachoweza kusema hapa cha kwanza anazungumzia suala kujenga uwezo kwamba je, Serikali inafanya nini ili kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu zinakuwa na uwezo ili ziweze kukabiliana na hali hii ya mipango miji. Utaratibu tunaokwenda nao sasa hivi ni huu wa *D by D Decentralization by Develution* kwa maana ya kupeleka madaraka zaidi kwa wananchi na kwa maana ya kupeleka *resources* zaidi kwa wananchi ili kuzipa Halmashauri zetu uwezo wa kuweza kukabiliana na mambo mbali mbali na changamoto hizi ambazo nimezizungumza hapa. Hivi juzi tu utakumbuka kwamba tulii-commission *TRA* kwa kupitia Sheria isaidie kuokota kodi za nyumba katika miji ili

waweze kuwa na uwezo mkubwa wa kutunisha mifuko yao kwa ajili ya kazi kama hizi ninazozungumzia hapa.

La pili ambalo anazungumzia kwamba tunavyo vyuo vikuu vingi katika nchi yetu hapa, sikuipata vizuri sana mantiki yake pale. Lakini anasema kwamba inaonekana kwamba viwanja vinatolewa tu kienyeji enyeji. Mimi nataka nikiri kwamba kumekuwako na matatizo makubwa katika ugawaji wa viwanja. Ni kweli anavyosema Mheshimiwa Simbachawene.

Lakini utaratibu wa nchi unamtaka mtu yoyote ambaye anataka kumiliki eneo apate kibali kutoka kwenye Halmashauri inayohusika, akienda tu akajenga kienyeji hivi, baada ya pale ataambiwa hapa inapita barabara, utasikia greda limeingia pale na matokeo yake wananchi watakuwa wanalamika. Rai ya Serikali na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba tufuate taratibu zilizowekwa katika Halmashauri. Kwa sababu utaratibu mzima wa ku-*plan* uko katika Halmashauri yenyewe inayohusika. (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba niongezee moja tu kuhusu uwezo wa Halmashauri kwamba tumejiandaa vipi. Sasa hivi kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wanatukopesha fedha katika Halmashauri mbalimbali ili tuweze kupima viwanja. Kwa hiyo, nitoe wito tu kwa Halmashauri mbalimbali kwenda kwa wenzetu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuomba mikopo ili waweze kupima viwanja mbalimbali.

Kuhusu suala la kutoa viwanja kinyemela. Kwa sasa hivi suala hili limepungua. Mifano tunayo, kwamba viwanja vikishapimwa, vinatangazwa, vikitangazwa ndipo wananchi wanaenda kuomba kwamba nataka kiwanja sehemu fulani. Kwa hiyo suala hili kwa sasa angalau limepungua. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ilikuwa kwamba useme hivyo hivyo. Naona tumetumia muda mwangi hapa na Wizara yenyewe ya Ardhi bado. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Shoka Khamisi Juma.

Na. 153

### **Mapambano dhidi ya ufisadi nchini**

**MHE. SHOKA KHAMISI JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 imeelezwa kuwa chama kikipata ushindi, basi Serikali itapambana na ufisadi kwa kuwachukulia hatua za

kisheria, kiutawala na za kinidhamu wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya ujisadi, na kwa kuwa Chama cha Mapinduzi kilipata ushindi na kuunda Serikali:-

Je, sasa Serikali inawachukulia hatua gani za kisheria, kiutawala na kinidhamu wale wote waliohusika na ujisadi wa kuchukua mabilioni ya fedha kwenye akaunti ya madeni ya nje *EPA*?

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamisi Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kuna mabilioni ya fedha yalichotwa kwenye akaunti ya madeni ya nje (*EPA*) kwenye Benki Kuu ya Tanzania kinyume na utaratibu. Suala hili ni mionganini mwa masuala yanayomkera sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wananchi wote kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala lililoulizwa bado liko kwenye uchunguzi ambao unakaribia kumalizika, nashauri Mheshimiwa Mbunge awe na subira kwa sasa, majibu kamili ya hoja yake yatapatikana baada ya ripoti ya uchunguzi kukamiliika.

**MHE. SHOKA KHAMISI JUMA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, na mie nitavuta subra mpaka hilo suala likamiliike. Lakini pamoja na hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza. Kwa kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi aliliambia Bunge hili kupitia Kauli za Mawaziri kuwa fedha hizi si za wananchi yaani si fedha za Serikali na wenyewe ni wafanya biashara na wengine hata hapa duniani hawapo tena wameshafariki. Sasa je, ikiwa fedha hizi si za Serikali yaani si za wananchi, kwa nini waliozichukua wakaambiwa wazirejeshe benki wamrejeshee nani fedha hizi wakati si za wananchi, wanamrejeshea nani? Swali la kwanza. Swali la pili.

Je, kwa nini Serikali iliwaamuru hawa watu waliochota fedha kuwa wazirejeshe benki kabla hawajapelekwa Mahakamani na tunasema nchi hii inafuata Utawala Bora. Kwa nini kwanza wasingepelekwa Mahakamani na Mahakama ndiyo ikaamua kwa watu hawa warejeshe fedha hizi au ikiwa kuna hukumu nyingine yoyote itakuwepo itoe Mahakama, lakini siyo itoe Serikali wakati nchi hii inafuata Utawala Bora? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kwani nikiunda Tume sio Utawala Bora. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba masuala hayo bado yanashughulikiwa na hiyo Kamati. Kwa mimi hapa kujibu itakuwa ni kuingilia kazi za ile Kamati. Sote tunatakiwa tusubiri yote hayo yatajibika wakati taarifa ya Kamati itakapotolewa. (*Makofi*)

**Kuviwezesha vituo vya Wale mavu vya Kasulu**

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya awamu ya nne inapongezwa na wananchi wa Wilaya ya Kasulu kwa kuanzisha vituo zaidi ya kumi na mbili (12) vya wale mavu:-

- (a) Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuvipatia vituo hivi ruzuku ya chakula?
- (b) Je, ni lini Mratibu wa Elimu Maalum atawezeshwa kupata usafiri ili atembelee vituo vyote mara kwa mara kuona Maendeleo na Matatizo yaliyopo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Muhamma Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, kama ifuatavyo:-

Awali, Serikali inapokea pongezi za wananchi wa Kasulu kwa uanzishwaji wa vitengo zaidi ya 12 vya wanafunzi wenye ulemavu. Aidha, wananchi hao kupitia kwa Mbunge wao ndiyo wanaostahili kupongezwa kwa juhudzi za kuanzisha na kusimamia vitengo hivyo ambavyo ni muhimu kwa kuwaelimisha vijana wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Muhamma Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Halmashauri za Miji, Wilaya, Manispaa au Jiji huzipatia fedha vitengo vya wenye ulemavu fedha za ruzuku kwa ajili ya chakula cha wanafunzi na mahitaji mengine ya kielimu. Fedha hizo hutengwa na Halmashauri husika kwa kuzingatia mahitaji ya shule kupitia katika Bajeti yake ya elimu ya kila mwaka. Nashauri Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kutenga fedha katika Bajeti yake kwa ajili ya kuendesha vitengo hivyo 12 vya wenye ulemavu vilivyoanzishwa.
- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafahamu uzito wa majukumu waliyo nayo Waratibu wa Elimu Maalum wa Wilaya katika uboreshaji na utoaji wa Elimu hapa nchini. Kwa sababu hiyo, Serikali kupitia Halmashauri za Miji, Wilaya, Manispaa au Jiji inaona umuhimnu wa kuwapatia usafiri watalaam hao kadri ya fedha itakavyoruhusu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lenyewe hapa linazungumzia jinsi ambavyo vituo hivi *under funded*. Kwa kuwa kuna shughuli nyingi ambazo zinatakiwa kufanyika katika vituo hivi. Je, .....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kimaro, naomba urudi ulikokaa. Mheshimiwa Mporeogomyi endelea. (*Kicheko*)

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Kwa kuwa vituo hivi *under funded* na kwa kuwa vina mahitaji mengi ili viweze kufanya kazi nzuri zaidi kuliko vinavyofanya hivi sasa. Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuambatana nami ili aende kuvitembelea vituo hivi ajiridhishe juu ya matatizo walinyo hivi sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mtera naona ungekuwa umerudi ulipokaa. Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba vitengo hivi vinapatiwa ruzuku na Serikali za Mitaa pamoja na Serikali Kuu kwa maana ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu.

Sote kwa pamoja tunashirikiana. Wenzetu wa TAMISEMI huzigharamia kwa matumizi ya kila siku na Wizara ya Elimu hutoa ruzuku yake kwa ajili ya vifaa vyta kufundishia na mambo mengine ya kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili. Namwahidi nitafanya ziara Mkoa wa Kigoma na nitapata fursa nzuri ya kuvitembelea vitengo hivyo. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna vituo vyta Taasisi za watu binafsi na vile vyta mashirika ya dini ambavyo navyo pia huwa vina vituo vyta kulelea hao watoto. Lakini ruzuku wanayopewa ni ndogo sana na maeneo mengine wanakuwa hawapewi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba vituo vyote kwanza vinapewa ruzuku. Lakini pili vinahakikisha kwamba wanavipatia ruzuku ambayo inatosheleza. Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kufanya hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba Serikali inatambua vituo vyta kulelea watoto au wanafunzi wenyewe mahitaji maalum kwa maana ya asasi za kiraia na kwamba baadhi ya asasi hizi huwa zinapata wafadhili wake. Kama nilivyema katika jibu la msingi asasi hizi za kiraia zinapokuwa na mipango yake inapaswa kuleta taarifa zake kwa Wizara zinazohusika ili tuweze kuona kama kuna uwezo wa kuzisaidia.

Swali lake la pili Mheshimiwa Naibu Spika, naomnba niseme tu kwamba tutalifanya kazi baada ya kupata takwimu sahihi za vitengo hivi ili tuweze kutambua aina mbalimbali za uhitaji wake. (*Makofi*)

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Swali la msingi linalezea kwamba Wilaya ya Kasulu ina zaidi ya vituo 12 vyenye walemaru. Tena hawa ni watoto wadogo. Naomba kuuliza.

Je, Wizara ya Afya imajaribu kwenda Kasulu na kujiuliza kama kule watoto wamepata nini ama chanjo za akina mama ama watoto hawakupata chanjo za polio mapema kwa sababu kwa vyovoyote vile lazima kuna tatizo. Napenda kuiuliza Wizara ya Afya imewahi kufanya lolote kuhusu hili?

**NAIBU SPIKA:** Tunasema tutibu ugonjwa na siyo *symthoms*. Waziri wa Afya au? Wizara ya Elimu *okay!* Wizara ya Afya ooh. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida panapotokea hali kama hiyo utafiti hufanywa. Mwaka jana tulibaini kuwepo kwa idadi kubwa sana ya wanafunzi katika mkoa fulani. Mara moja tulipeleka timu ya wataalam na tulibaini baadhi ya mambo.

Moja, ulemavu mbalimbali husababishwa na mambo mengine ya kitaalam ambayo pengine itabidi tupate nafasi kubwa zaidi ya kuelezea. Lakini madawa ya kulevyta, uvutaji wa sigara, bangi na madawa makali wakati wa ujauzito huweza kusababisha, pamoja na vipigo wakati wa ujauzito. (*Makofii*)

Na. 155

### **Vijana wa Kike wanaojiunga na VETA**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa vijana na kike wanaojiunga na mafunzo ya ufundi stadi (*VETA*) ni wachache ikilinganishwa na idadi ya vijana wa kiume na kwa kuwa, mwanamke mmoja akielimishwa ni sawa na kuelimisha jamii:-

Je, Serikali, ina mikakati gani ya kuhamasisha vijana wa kike na wanawake kujiunga zaidi na vyuo hivyo ili kuboresha maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Wizara inaendelea kuhamasisha wasichana kijiungu na elimu ya ufundi stadi kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- (a) Kutoa nafasi sawa za mabweni kati ya wavulana na wasichana katika vyuo vinavyojengwa na vinavyokarabatiwa.
- (b) Kuongeza na kuimarishe fani za mafunzo zinazowalenga zaidi vijana wa kike; kama vile fani za Uhazili, Mapambo na Urembo, Ushonaji wa nguo, Huduma za Hoteli, kuweka umeme nyumbani, Uongozaji wa Watalii na Upakaji rangi.
- (c) Kuweka msukumo katika kuajiri walimu wa kike wa ufundi stadi ili wawe mfano wa kuigwa (*role models*).

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi hizi za Wizara zimezaa matunda, katika mwaka 1996 idadi ya vijana wa kike waliojiunga na mafunzo ya ufundi stadi katika vyuo vya *VETA* na vyuo vya asasi zisizo za Serikali ilikuwa 4,700 au asilimia 12 ya wanafunzi wote. Katika mwaka 2007 idadi ya vijana wa kike katika vyuo vya *VETA* na vya asasi zisizo za Kiserikali imefikia 53,413 au asilimia 44 ya wanafunzi wote. Haya ni mafanikio makubwa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kumwuliza, kwa kuwa wanafunzi wanaohitimu mafunzo ya ufundi stadi *VETA* wengi wao wanakosa ajira, sambamba na kukosa vifaa vya kuendeleza vipaji vyao na kujipatia ajira wao wenyewe.

Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kuwapatia mikopo ya vifaa na fedha wanafunzi hao wanapomaliza vyuo vya *VETA* ili kuweza kujiajiri wenyewe na kujikwamua kiuchumi? Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza naomba niseme katika mafunzo yanayotolewa katika vyuo vyetu kuna somo la ujasiriamali. Hivyo pamoja na stadi zingine ambazo mwanafunzi atakuwa anapata atakapokuwa amehitimu atakuwa amewezeshwa kupatiwa maarifa yatayomwezesha kujipatia mtaji. Aidha upo mpango wa kuona kwamba wale watakaokuwa wanahitimu sasa waweze kupatiwa vifaa vitakavyowawezesha kujiajiri moja kwa moja na baadaye kuweza kuvilipia pole pole. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa nchi yetu imejikita zaidi katika utafutaji wa mafuta na gesi na *uranium* hususan katika mikoa ya Kusini, Mtwara, Lindi na Ruvuma na mafanikio makubwa yamepatikana. Lakini wachimbaji hao kutoka

nchi za nje huajiri vijana au mafundi *welders* na mafundi kama vile mafundi mchundo kutoka nchi za nje. Je, Wizara itakubaliana na mimi kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha kitengo maalum cha kufundisha vijana wetu ili kazi hizo zifanywe na sisi wenye? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba katika vyuo vinavyotoa mafunzo stadi, moja ya Kanuni zake ni kuangalia mahitaji ya mahala chuo kilipo. Kwa hiyo, kama mahala chuo kilipo ni masuala ya madini, stadi hizo zitakuwepo. Kama ni masuala ya uchimbaji wa mafuta stadi hizo zitakuwepo. Vivyo hivyo kama ni wafugaji au ni masuala ya uvuvi. Kwa hiyo, naomba niseme ushauri wako tunaupokea. Tutaufanyia kazi. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mashirika ya Dini katika nchi yetu ya Tanzania yamekuwa yakifanya kazi nzuri sana ya kuendesha vyuo vya ufundi kama kile kilichopo katika Jimbo la Peramiho kinachoendeshwa na Shirika la Dini la wa-Benedictine na wanafunzi wale wamekuwa wakipatiwa vifaa na kila kitu wanapomaliza mafunzo yao.

Je, Serikali haioni kwamba sasa hivi kuwekwe utaratibu angalau wa kuwatambua vijana wale na kuwaunganisha katika vikundi vya kazi za ujenzi katika maeneo ya vijijini ili waweze kuwa wanapata ajira ya moja kwa moja wanapomaliza mafunzo yao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba Serikali inavitambua vituo vyote au vyuo vyote vya binafsi vikiwemo vya mashirika ya dini na mfano huo wa kuwapatia vifaa ndiyo ambao na Serikali tunaufanyia kazi ili tuweze kuwawezesha.

Swali la pili la kutaka wapate kazi katika maeneo mbalimbali naomba niseme tu niwaombe wananchi kwa ujumla watambue stadi walizo nazo vijana hao na kwamba wawapatie ajira au kazi zitakazokuwa zinatolewa katika maeneo husika pale ambapo wataalam hawa watakuwepo.

Na. 156

### **Upungufu wa Wahadhiri Nchini**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA (K.n.y. MHE. DR. CHARLES M. MLINGWA) aliuliza:-**

Kwa kuwa, kuna tatizo la upungufu wa walimu/wahadhiri katika Taasisi za Serikali za Elimu ya Juu, hususan vyuo vikuu:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kurekebisha sheria na taratibu za vyuo vya umma ili kuruhusu ushiriki wa wataalam wengine wenye sifa walio nje ya vyuo washirikishwe katika ufundishaji?

(b) Je, kwanini Serikali isiige wenzetu katika suala hili muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) atajibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kuna upungufu wa wahadhiri katika Vyuo Vikuu vingi vya Umma hapa nchini. Upungufu huo unatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na Serikali kusitisha ajira katika miaka ya tisini wakiwemo wataalam hao na ongezeko la wanafunzi linalotokana na upanuzi mkubwa wa vyuo vikuu nchini.

Hakuna sheria au utaratibu wowote unaozuwia wataalamu wengine walio nje ya vyuo kushiriki katika suala la ufundishaji katika vyuo vya umma. Vyuo vimekuwa vikajiri wataalamu Watanzania ambao wako nje ya vyuo kufanya kazi kama wahadhiri wa muda, *part-time lecturers*, kwa kuzingatia sifa zao kila uhitaji unapojitokeza.

Hata hivyo Serikali kwa kushirikiana na vyuo husika inao mkakati wa kuongeza wahadhiri kwa kudhamini kuwasomesha wakufunzi wasaidizi 80 kila mwaka kuanzia mwaka 2005/2006. Aidha, kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Serikali ina mpango wa kuwakopesha wahadhiri wa vyuo vikuu vya umma wanaosomea shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kushirikisha wataalamu wengine wenye sifa walio nje ya vyuo katika ufundishaji hutumika katika nchi nyingi duniani. Utaratibu huu husaidia katika katika kubadilishana uzoefu na watu wanaofanya kazi nje ya vyuo. Kwa hiyo, tutaendelea kuufanya kazi ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, kama hatua mojawapo ya kukabiliana na tatizo la upungufu wa wahadhiri katika vyuo vikuu nchini.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri. Nina maswali mawili. Swala kwanza, kwa kuwa watafiti wengi wanasayansi wanaofanya shughuli za utafiti mara nyingi wanakuwa ni mabingwa hasa katika masomo ya sayansi. Ndiyo katika jibu lake alivyosema na nchi zingine za jirani na zilizoendelea zinatumia sana wataalam hawa. Je, Serikali inaweza ikatamka na kuanza kuwatumia watafiti hawa, wakafundisha katika vyuo vikuu vyetu kwa wakati wao?

Pili, kwa kuwa katika jimbo la Shinyanga Mjini kipo chuo cha Kizumbi ambacho ni tawi la Chuo Kikuu cha Moshi, na Chuo hiki kina eneo kubwa sana na *infrastructure* zake zipo nyingi. Je, Serikali inaweza ikasema ni lini sasa itapeleka pale wataalam wahadhiri wa kuanza kufundisha kwa sababu tunategemea muda si mrefu stashahada na vyeti vitaanza kutolewa pale?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Baada ya kusema hivyo ningependa nijibu swali la Mheshimiwa Immanuel Luhahula kama ifuatavyo:-

Kwanza vyuo vikuu vyetu vinawatumia sana watafiti na wataalam wa sayansi ambao wako katika taasisi zetu nje ya vyuo vikuu. Wanawatumia katika kufundisha katika fani maalum na pia katika kusaidia kama wataalam wa kuhakiki mitihani na kuangalia *standards* katika mitihani ya vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili Serikali inasomesha wahadhiri wa vyuo vikuu na vyuo vishiriki mbalimbali hapa nchini ikiwa ni pamoja na chuo kishiriki cha Kizumbi kilichoko kule Shinyanga na Serikali itaendelea kuwasomesha na kupeleka wataalam kulingana na jinsi ambavyo programu za chuo kile zilivyo.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa niulize swali la nyongeza. Kwa vile suala hili la msingi kwa kweli linagusa suala zima la muda wa kustaafu wahadhiri wa Vyuo Vikuu na tatizo hili limetokea sana hapa nchini baada ya sheria ile ya kuwataka hata walimu wa vyuo vikuu wastaa fu miaka 55 katika kipindi kilichopita na tukajikuta walimu wote ambao ni mabingwa wako nje ya vyuo na tukaanza sasa kuwarudisha kwa mkataba.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kurekebisha sheria pengine kukawa na utaratibu maalum pengine kwa walimu wa vyuo vikuu ili hawa hata akiwa mzee, aweze kuendelea kutoa huduma kwasababu *brains* zao mara nyingi zinakuwa bado zinafanya kazi kuliko kuwastaafisha wakati bado wana uwezo wa kufanya kazi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba huko nyuma hili tatizo lilijitokeza kwamba maprofesa na wataalamu wa vyuo vikuu wanafika miaka 55 na wanahitajiwa kustaafu. Baadaye umri wa kustaafu katika vyuo vikuu uliongezwa mpaka miaka 60, lakini hata hivyo bado wataalamu wengi wale wanaweza kufanya kazi na akili zao zinachaji na ni vizuri kuwatumia kwasababu hakuna wengine tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuwatumia wataalamu hawa kwa muda kwa maana ya kuwapa mikataba lakini vyuo vikuu vitaangalia kwa undani zaidi tatizo hili na kuona kama inawezekana kuwapa nafasi maalum ili waendelee kufundisha kama ambavyo wanafanya huko kwenye nchi za Scandinavia.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba suala hili tutaliangalia na tutalitekeleza kama ambavyo tunaona itakuwa ni manufaa kwa vyuo vikuu vyenyewe. (*Makofi*).

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha. Mwongozo wa Spika.

**MHE. EMMANUEL J. LUAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68, inaruhusu Mbunge, yejote kusimama na kuomba muongozo wa Spika, lakini niko kwenye Kanuni ya 38(3) na (6). Inasema cha tatu, “*Kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu, kitakuwa kila siku ya Alhamisi na hakitazidi dakika 30.*” Kipengele cha (6), “*Maswali kwa Waziri Mkuu, yatafuatiwa na Maswali mengine kwa Mawaziri, kwa dakika 60 kama yatakavyokuwa yamepangwa.*” Lakini kifungu cha 43 kinaema, “*Muda wa maswali Bungeni, utakuwa dakika 90, isipokuwa katika Mkutano wa Bunge la Bajeti, ambapo muda utakuwa dakika 60.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako kwasababu tumeuliza maswali kwa Waziri Mkuu, dakika 30 na baadaye tena tumeuliza dakika 30 maswali kwa Mawaziri badala ya 60 kama Kanuni inavyosema. Naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nadhani umesema sahihi. Maswali katika kipindi cha Bunge la kawaida ni saa moja nanusu, wakati wa kipindi cha Bajeti ni saa moja, siku ya Alhamisi ni saa moja tunagawana Waziri Mkuu, nusu saa na Wabunge, nusu saa siku ya Alhamisi tu. Kwa hiyo hiyo Kanuni isipokuwa siku ya Alhamisi. Tunaendelea, Katibu.

Kuna matangazo ya wageni. Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wa Mheshimiwa Ramadhani Maneno na Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu. Hawa ni wenyeviti wa *CCM* wa Kata 16 na Makatibu wa *CCM* wa Kata hizo 16 wakiongozwa na Mwenyekiti wa *CCM* wa Wilaya ya Bagamoyo, Mheshimiwa Omar Kabanga. Naomba asimame Mheshimiwa Omar Kabanga.

Halafu yupo na Katibu wa Mbunge, Jimbo la Chalinze, Ndugu Kaisi Chambo, yuko wapi huyo? Halafu na Katibu wa Mbunge, Jimbo la Bagamoyo, Ndugu Magreth Masenga, asimame. Na wale Wenyeviti wetu wote wasimame na Makatibu wao. Hapo

maana yake Bagamoyo yote imeshafika, karibuni sana tunategemea mutajifunza machache kutokana na Wabunge wenu. (*Makofi*).

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, huyu ni Mheshimiwa Charles John Luyenze, Diwani wa Kata ya Mwanyili Wilaya ya Magu. Yuko wapi Mheshimiwa Diwani? Ahsante. Tuna wageni wa Mheshimiwa Paul Kimiti, ni mdogo wake, Kanali Mstaafu Boniphace Kimiti, akiwa pamoja na wajukuu zake Mheshimiwa Kimiti, naomba wote wasimame walipo, ahsante. (*Makofi*).

Tuna wageni wa Mheshimiwa Damas Nakei. Hawa ni viongozi wa viongozi, wataalamu na wakulima wa pareto, wako 12 kutoka Babati Vijijini. Wametoka Mbeya na Iringa kwa ajili ya kujifunza. Wageni hao naomba wasimame walipo, asanteni sana, nadhani mmejifunza mambo ya pareto. Sasa tuna wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, hawa ni wanafunzi 56 kutoka shule ya Msingi Kikombo, Mpwapwa. Naomba wasimame walipo nadhani na walimu wao wapo, wasimame wote walipo. Ahsante sana, walimu tunashukuru na watoto tunashukuru mumekuja. Kwa hiyo ni hao hao, ambao ni walimu 7 ambao wameambatana na Mkuu wa Msafara, Mwalimu Renatus Simbachawene, ambaye ni dada yake na Mheshimiwa, Mwalimu Renatus, tunaomba tumwone. Kwa hiyo, ni dada yake na Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*).

Tuna wageni wa Mheshimiwa Joyce Masunga, hawa ni mama Jimmy na Mama Anna Sele, wote wanatoka Shinyanga. Mama Jimmy na Mama Anna Sele, wako wapi? Ahsanteni sana. Tuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, hawa ni Ndugu Saleh Ameshimbagi, Katibu Kata wadi ya Mungoni, Zanzibar, yuko wapi huyu? Halafu tuna Ndugu Ali Miraji Hassan, Katibu Mwenezi Kata au wadi kikadi, hii ni Zanzibar. Halafu tuna Ndugu Miraji Abdallah Abdallah, Katibu wa tawi la CCM Paje, halafu tuna ndugu Awesu Shaban Ramadhan, Katibu wa tawi la CCM Kitongani. Ahsanteni sana kwa kuja. (*Makofi*).

Halafu tuna wanafunzi 31 kutoka *CBE* ambao wanaendelea na mafunzo kuhusu Bunge, ambao leo wameandaliwa chakula cha mchana na Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge. Wanafunzi wetu wale wasimame. Ahsanteni sana na tunakushukuru Mheshimiwa Idd kwa kuwakaribisha wageni wetu kwa namna ya pekee. (*Makofi*).

Sasa tuna matangazo ya kazi, kwnza kabisa Mheshimiwa Sweet, Katibu wa Chama cha Wanawake wa Bunge, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya maandalizi ya *Motherhood Day*, kuwa leo tarehe 3 Julai, 2008 kutakuwa na kikao cha Kamati, saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge.

Nadhani mnafahamu mnapokutana kila wakati. Amesema kikao hiki kitafanya katika ukumbi wa mapumziko hapa Bungeni. Nadhani ni katika vyumba vyahapahapa. Naomba wajumbe msikose kwa sababu muda unakwisha. Halafu Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na utawala kuwa, kutakuwa na kikao cha dharura katika ukumbi Namba 231, saa 5.00 asubuhi Saa 5.00 hii asubuhi kuna kikao cha dharura.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yamekwisha. Katibu endele na *Order Paper*.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2008/2009 – Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu

(*Majadiliano yanaendelea*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Najua orodha ni kubwa sana, wengi hawatapata nafasi kwa sababu kwa utaratibu wetu hapa tunaweza kuwapata wajumbe 11 tu asubuhi hii na hawa ndio wafuatao kwanza. Atakuwa Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga. Tuanzie na hao kwanza. Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Nakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza asubuhi hii ya leo katika hotuba ya Waziri wa Miundombinu. Lakini kabla sijaanza kuchangia ninaomba nitoe pongezi kwa Waziri wetu Mkuu, Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa niaba ya wananchi wa Dodoma, nimwambie tu kwamba sisi tutampa ushirikiano wa karibu sana katika kutekeleza kazi zake za ujenzi wa Taifa. (*Makofit*).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nimpongeze Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, pamoja na Naibu wake, Kaka yangu Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu pamoja na watendaji wote wa ofisi hiyo kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuandaa Bajeti hii na kuonesha jinsi wanavyotekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kwa dhati kabisa. (*Makofit*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa juhudni kubwa ambayo inaionesha katika kuendeleza Mji wa Dodoma na hasa katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Naipongeza sana Serikali yetu na nina amini kwamba spidi hiyo ikiendelea muda sio mrefu ndani ya miaka 5 au 10 mji wa Dodoma unawenza ukawa zaidi ya Jiji la Dar-es-Salaam. (*Makofit*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia katika kuangalia katika kitabu hiki cha hotuba ya Waziri wa Miundombinu, ukurasa wa 78. Kuna maelezo yaliyotolewa pale kuhusu usajili wa Makandarasi nchini na wameonesha idadi ya Makandarasi ambao wamesajiliwa katika nchi yetu na nina amini kabisa kwamba Makandarasi hao waliosajiliwa ndio wanaopewa kazi za kujenga barabara, majengo makubwa katika nchi yetu. Naipongeza Serikali kwa hatua hiyo nzuri ya kuwasajili Makandarasi wengi, lakini ninachopenda kujua ni kwamba je, kuna sheria yoyote inayomlazimisha au inayomwongoza Mkandarasi wa Kigeni anapojisajili nchini kwetu awe na *joint venture* na mzalendo. Kwa sababu sasa hivi ndani ya nchi yetu kuna

Wakandarasi wengi sana wa kigeni, wanafanya kazi kubwa, wanapewa *contract* kubwa za kujenga barabara za nchi yetu, wanajenga majengo makubwa ya Serikali, lakini je, wazalendo wanawatumiaje hawa Makandarasi wa kigeni?

Mimi ninaamini kabisa kwamba Makandarasi, hawa wa kigeni tukiwatumia vizuri na hasa katika *joint venture* na Watanzania watakapoondoka ujuzi waliokuja nao watauacha kwa wazalendo. Lakini je, kuna sheria yoyote ambayo inamlazimisha huyu Mkandarasi wa kigeni, hasa wale wa daraja la kwanza la I, II, III, IV na hata daraja la V, kwamba anapojisajili nchini awe na ubia na Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii pia itatusaidia katika kujenga uwezo kwa makandarasi wetu. Lakini pia tukumbuke kwamba nchi yetu ni tegemezi na pesa tunazopata kutoka kwa wafadhaili kujenga nchi yetu, zingine zinatumika katika ujenzi wa barabara. Sasa kama Makandarasi wazalendo hawanufaiki na pesa zinazotoka nje, pesa zinatumiwa na Makandarasi wa nje bila kuwa na ubia na Watanzania. Ina maana hizi pesa tutakuwa tunazipata na zinarudi kwa wenyewe wahisani waliotupa, kwasababu Makandarasi wenyewe ni watu wa kutoka nje. Naomba Waziri, atakapokuwa anamalizia anisaidie kujua hili kwamba watanzania wanaingia ubia na Makandarasi wageni ili kuwajengea uwezo na uzoefu na ujuzi. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kujua kwamba hawa Wakandarasi wana *limitation* ya kuajiri wageni, kwasababu inawezekana *Top Management* katika Makandarasi hawa wa kigeni ni wageni watupu na inawezekana kabisa kwamba hata wanaoendesha toroli hizi za kubeba matofali na simenti na nini, ni wageni.

Sasa naomba kujua kwamba je, hawa watu Makandarasi wanaoingia wakigeni wanapewa idadi ya wataalamu wanaotakiwa kuajiriwa katika kazi hizo? Isije ikawa kwamba hata kazi ndogo ambazo wangeweza kufanya watanzania wanafanya wageni. Najua kabisa kwamba katika ofisi zetu wanatakiwa wageni watano tu, lakini je, katika kazi hizo za kutengeneza barabara, kujenga majengo makubwa, na hasa majengo haya ya Serikali, wanaruhusiwa wangapi kufanya kazi kwenye miradi? Na wale ambao wanakiuka sheria hiyo, wamewahi kupewa adhabu? Au wamewahi kufungiwa kazi? Au sheria imewahi kuchukua mkondo wake kwa hao wanaokiuka taratibu za nchi? (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma katika kitabu hiki cha hotuba ya Waziri wa Miundombinu, ukurasa wa 66. Nimeona maeneo ambayo serikali inafanya juhudhi katika kutafuta pesa za kuwalipa wale ambao wanahusika na kulipwa fidia maeneo ambayo uwanja wa ndege unapanukliwa. Lakini katika Mkoa wa Dodoma, uwanja wa ndege utakuja kujengwa katika eneo la Msalato.

Sasa ukurasa wa 66 naomba kunukuu Serikali inasema hivii, “*Aidha Serikali itaendelea na taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa viwanja vya Pugu, Majohi, Buyuni, kwa ajili ya makazi ya wananchi wa Kigilagila na Kipunguni. Wananchi wa Kigilagila na Kipunguni wanahamishwa ili kupisha upanuzi wa kiwanja cha ndege*

*cha kimataifa cha Julius Nyerere,”* mwisho wa kunukuu. Sasa nimeona maeneo yaliyotajwa lakini eneo la Msalato, wananchi wa Msalato, sikuona wametajwa eneo gani?

Kuna shilingi 1,000,600,000/= zimetengwa na serikali kwa ajili ya upanuzi wa uwanja wa msalato, sasa sielewi kwamba hizi bilioni 1.6 ni kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi hawa au ni kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege. Wananchi wa Msalato hawafanyi maendeleo yoyote tangu walipoambiwa kwamba eneo lao linajengwa uwanja wa ndege.

Hakuna Maendeleo yoyote wanayofanya, hawajengi nyumba, hawalimi mashamba, hawajengi shule, hawajengi zahanati, kwasababu wanasubiri Serikali, kuwalipa fidia. Lakini mpaka sasa hivi hivi ninavyoongea wananchi wale hawajalipwa fidia. Ninaomba kujua kwamba hawa watu hizi shilingi 1,000,600,000/= ndio zilizotengwa kwaajili ya kulipa fidia au hizi pesa zimetengwa kwa ajili ya kazi gani? Na ninaiomba Serikali kwamba ingefanya haraka kuwalipa fidia hawa wananchi ili wafanye shughuli zingine za maendeleo kuliko kukaa kila siku wanasubiri Serikali kuwalipa fidia. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichangie kuhusu ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati. Tangu nilipoingia katika Bunge, hili mwaka 2005, kila tunaposimama Wabunge wa Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Manyara na hata Mkoa wa Iringa, tunaulizia suala hili la ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati. Kuna kiasi cha pesa kimetengwa, lakini pesa hizi serikali haijazungumza kwamba ni kwa ajili ya ujenzi au usanifu wa kina unaendelea au upembuzi yakinifu unaendelea, wananchi wanaomba kujua kwamba barabara hii itajengwa lini? Barabara hii ni muhimu sana kwa Maendeleo ya wananchi wa Manyara, wananchi wa Dodoma na wananchi wa Iringa. Iringa wanalima sana mazao ya aina mbali mbali, Dodoma sasahivi tunalima sana alizeti, ulezi, na mtama na Manyara ni wakulima wazuri sana vile vile. (*Makofi*)

Kwa hiyo barabara hii ikifunguliwa itatusaidia sana wananchi wa mikoa hiyo mitatu. Naomba Serikali ione umuhimu wa kuanza ujenzi wa barabara hiyo. Na kama itaanza basi tunaomba kwasababu sisi katika Mkoa wa Dodoma, Wilaya ya Kondoa pale daraja la Kolwa halipo. Tunaomba ujenzi uanze katika Mkoa wa Dodoma ili daraja lile lijengwe. Maana daraja lile wakati wa mvua wananchi wanasubiria hata kama una mgonjwa, mwananchi anasubiria mpaka maji yapungue. Hivi Taifa hili lililohuru wananchi wake wakae kusubiria maji yapungue ndio wapitie wakati Serikali yetu ina pesa na ina uwezo kabisa wa kujenga barabara hiyo na hata hilo daraja. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichangie kuhusu barabara hiyo hiyo eneo la Iringa – Dodoma, kwamba limetengewa shilingi 574,000,000/=. Je, hizi pesa zilizotengwa bado ni upembuzi yakinifu tu? jamani hao wapembuzi yakinifu, wanafanya kazi miaka mingapi kukamilisha kazi zao? Wananchi wanateseka na wajue kwamba, wananchi wanateseka wanapofanyakazi taratibu.

Tuliambiwa kwamba serikali inatafuta pesa kwa ajili ya kujenga barabara hii na mimi naamini kwamba Serikali yetu ni sikivu na inaendelea kufanya juhudhi kwamba wananchi waweze kupata barabara hii ya Dodoma – Iringa. Tunaomba kabla ya 2010, basi barabara hizi mbili ziwe zimekamilika kwasababu ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM). (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangazwa pia na barabara inayotoka Dodoma kwenda Morogoro. Barabara ambayo ilijengwa tu mwaka jana, lakini eneo la Kongwa, barabara hii imeanza kuwa na mashimo. Sasa sijui yule *consultant* anayesimamia kuangalia kuwa barabara imejengwa vizuri amefanya kazi gani? Ninaomba Wizara hii, ikakague tena hiyo barabara na Waheshimiwa Wabunge, nyie ni mashahidi mnapopita kutoka Dar-es-Salaam. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongelee Wilaya ya Chamwino na Wilaya ya Bahi, ambazo ni Wilaya mpya. Mimi kwa mtazamo wangu nilidhani Serikali, itatilia mkazo sana uendelezaji wa barabara katika Wilaya hizi mbili, Chamwino na Wilaya ya Bahi, lakini hakuna pesa zilizotengwa kwa ajili ya kuendeleza hizi barabara mbili. Katika Mkoa wa Dodoma Wilaya ambayo ni kongwe kabisa ni Wilaya ya Mpwapwa lakini unapoenda Mpwapwa kipindi cha mvua, ujiandae kwamba ukifika kule lazima umeze *panadol*. Kwa sababu njia nzima mtakuwa mnagongana vichwa, njia nzima ni mashimo. Kwa hiyo naomba Serikali iwafikirie hawa watu wa Mpwapwa.

Lakini hata watu wa Wilaya ya Chamwino inayoungana na Wilaya ya Kondoa, lakini ukipita barabara ya Dabalo – Itiso, Jimbo la Mheshimiwa Chibulunje, hakuna barabara. Mimi naiomba Serikali, iwahurumie hawa wananchi wa Wilaya ya Chamwino, Wilaya ya Bahi, Wilaya ya Mpwapwa kwasababu ni Wilaya ya muda mrefu, basi wapate angalao barabara ya kupita wananchi. Wilaya ya Chamwino kuna mazao mengi mno, Kata ya Dabalo, Kata ya Itiso, kuna mazao mengi mno na hata baadhi ya Wabunge, wanalima maeneo hayo, lakini shida wanayopata kipindi cha mavuno ni shida ambayo tunashindwa kuelezea. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tuliomba pesa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka *Shabbiby* na kuingia *Chako-ni-chako* ili kupunguza msongamano wa magari ndani ya mji. Kama tunavyo jua mji wa Dodoma unakuwa kila siku na sasa hivi kuna ujenzi wa vyuo vikuu kama 4 hivi. Kwa hiyo msongamano wa magari unaweza kuwa zaidi ya Dar-es-Salaam kwa miaka 5 ijayo.

Lakini pamoja na kuomba pesa kwa ajili ya kujenga barabara kilometra 2 tu, mwaka jana hatukupata hizo pesa ingawa tuliongelea kwenye *Road Board* na tukaleta maombi katika Wizara ya Miundominu, lakini mpaka leo hizo pesa hazijaja. Tunaomba tupate pesa kwa ajili ya kujenga kuanzia kwa *Shabbiby* pale mpaka *Chako-ni-chako* kupunguza mrundikano wa magari mengi mjini. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*).

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa na mimi nafasi kuichangia hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote napenda kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene, kumpongeza Waziri Mkuu, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza baada ya yeye kuwa Waziri Mkuu. Nampongeza saana mtoto wa mkulima kuwa Waziri Mkuu. Nampongeza vilevile mtani wangu, mwanangu Shukuru, kwa hotuba nzuri pamoja na babu yangu Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia katika hotuba yenyewe. Nitaanza na kuzungumzia matatizo ya watu walionileta, sauti ya Bukene. Halafu nitakuja matatizo ya Nzega, kama Wilaya yangu, nitaingia taratibu Mkoani, halafu Taifa. Maana yake nitaanza na tofali kuweka msingi, halafu nyumba, boma, halafu paa ndio unapata nyumba kamili ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kuzungumzia ahadi alizotoa Rais, wakati anazunguka kuomba kura mwaka 2005 na wala sitaki niulizwe nitoe ushahidi. Ushahidi ni mimi mwenyewe mmoja wa wale amba tulikuwa tunazunguka akininadi pamoja na madiwani katika Kata zote alizungumza hiyo, kwamba atatengeneza barabara ya kutoka Mambali kuja Itobo, kwa kiwango cha changarawe. Na atatengeneza barabara ya kutoka Nzega – Itobo – Igusulwe kwenda Kahama, barabara inayokwenda Burundi, Rwanda, kwa kiwango cha changarawe vilevile.

Lakini nimesoma makabrasha yote sijaona utengenezaji wa barabara hizo na sasa hivi tuko nusu ya safari ya ahadi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichoona ni kwamba kuna pesa zilizopangwa kwa ajili ya kutengeneza sehemu korofii na sehemu korofii siyo barabara yote, kwa misingi hiyo basi, naomba kukumbusha ahadi ya Mheshimiwa Rais na si vizuri kuangusha ahadi ya mtu mkubwa, mzito, mtu wa kilo kama yeye, akitoa ahadi yake halafu haitekelezwi. Kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, Waziri pamoja na Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu ahadi hizi, zitekelezwe, ni kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kiwango cha changarawe kinachozungumzwa na Mheshimiwa Rais siyo kiwango cha changarawe cha wasiwasi, kiwango cha changarawe hiki lazima kiwe bora yaani *quality* ya kiwango cha changarawe iwe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mfano hai, ukitoka Tabora ukiwa unakuja Bukene kabla hujafika Mambali, kuna Mkandarasi mmoja anaitwa Porion, huyu Mkandarasi anatengeneza barabara kwa uhakika, anatengeneza barabara makini, barabara ya changarawe ukiiona utafikiri lami. Ndiyo tunawataka Ma-contractor wa namna hii. Kwa hiyo, naamini kauli ya Rais itakuwa ya kiwango cha ubora yaani *quality* kama ya

huyu bwana Porion na ningeomba apewe mkataba huo yeye ili atutengenezee barabara hizi alizotuhidi Mheshimiwa Rais.

**MBUNGE FULANI:** Unampigia debe!

**MHE. TEDDY LOUISE KASSELLA – BANTU:** Ndiyo nampigia debe! Nataka ubora wa barabara siyo bora barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija harakaharaka katika ahadi ya Mheshimiwa Rais, ile barabara inayotoka Nzega - Itobo – Igusule, alisema kwamba anaomba itengenezwe kwa kiwango cha changarawe. Lakini ukiingalia kwenye vitabu na ukifika pale Nzega, ile barabara ni *T3* maana yake ni *Track Road* inayotoka Dar es Salaam kupita Dodoma, kwenda Mwanza au kwenda Kahama Mpaka Burundi na Rwanda. ‘Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni’. Hii barabara inatakiwa itengenezwe kwa lami ni *T3*. Kwa hiyo, ukiondoka hapa, unapofika Nzega, inapotea ile *T3*, inakuwa vumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi inasema *T3*, ni barabara ya lami sasa ukifika Nzega watu wana *diverge* wanakwenda kwenye barabara inayokwenda Mwanza ambayo ni *T8*, wanaacha *T3*, kile kipande hakiendi. Kwa kweli kinatakiwa kitengenezwe kwa lami na ni haki yetu kupata lami na *T3* ipo pale na kwenye vitabu ipo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba haki yetu tupewe hatudai zaidi ila tunataka haki yetu, tunataka haki yetu sasa kwa sababu sasa tumejua wakati ule hatukuwa tumejua, tulisogezwa upande, tukapigwa buti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba barabara hiyo iwekwe maanani, inayotoka Nzega ambayo Rais aliahidi lakini iko kwenye kiwango cha lami, ni *T3*, itoke Nzega iende Itobo ipitie Mwamala iende Ibusule itoke katika Jimbo langu inaingia Msalala Kikabongwa na kuendelea Kahama, Burundi, Rwanda, Uganda na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemaliza mambo ya barabara ya kwenye Jimbo langu, naomba niende harakaharaka barabara ya Tabora - Nzega. Barabara ya Tabora - Nzega na yenewe ni ya lami lakini haitengenezwi na unajua barabara ya lami inapotengenezwa, mambo mengi yanaseoga, miji inajitengeneza yenewe, biashara zinasogea katikati pale, vijana wanapata ajira, tunapunguza majambazi yasiyo na pesa kwa sababu kila mtu anaweza kujifikiria kufanya kazi. Hata ukimuuliza kijana unataka kufanya kazi, anasema nahitaji kuwezeshwa. Akiwa pale, anaweza kuuza vitunguu pale Busondo, akalima vitunguu na mwingine akaiza vitunguu na mwingine akaiza mahindi na mwingine akaiza Kuku na mwingine akaiza mayai na kadhalika. Lakini kama hakuna kazi, watakuwa *jobless*, hakuna kinachomvutia, atangojea kuchomochomoa wanaopita kwenye mabasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba barabara hii na yenewe iwekwe katika nafasi ya kutengenezwa ili tuunge ule mtiririko wa kutoka Tabora kuingia Mkoa wa Shinyanga na Mwanza na watu wawze kufanya biashara zao hapo kutoka Tabora kwa biashara za kuleta Shinyanga kupeleka Mwanza, Musoma, Kenya au kupeleka Uganda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende harakaharaka, *Airport* ya Tabora. *Airport* ya Tabora, tunaisahau lakini kimsingi Tabora ni Makao Makuu ya *Brigade* ya Magharibi, kiulinzi na usalama tunahitaji *Airport* hiyo lakini unakuta haishughulikiwi. Inatufaa hasa kama kwa mfano wakati wa Idd Amin, ilitufaa sana na hatujui leo na kesho itakuwaje. Kwa hiyo, tunahitaji kufufua *Airport* ya Tabora kwa misingi ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wawekezaji wanahitaji kwenda harakaharaka Tabora kuangalia hali halisi ya historia ya Livingstone, Tembe na mambo mengine waweze kufanya vitu vyao na kurudi haraka na kufanya kazi nyingine. Kwa hiyo, naomba *Airport* Tabora, ifanyiwe matengenezo haraka, pesa zipatikane na ifufuliwe upesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nyingine tumepewa kama ile ya kwenda Ipole - Itigi – Tabora, nawashukuru kwa kuzipata, lakini tunachoomba tupate pesa haraka kwa sababu zikichelewa pesa hizi zikaja wakati wa mvua hazina maana. Unatengeneza barabara mwezi Novemba na mvua zinaanza mwezi Novemba kwa hiyo unakuwa hujafanya kitu chochote, unakuwa unatupa pesa bure. Kwa hiyo, busara zitumike, ikiwezekana, pesa hizi zitolewe mapema mwezi wa nane zianze kufanya kazi yake vizuri ili mwezi wa kumi na mbili kuwe na barabara za kutosha na kuhakikisha tunaunga na Mpanda ili mazao ya kutoka Mpanda yawewe kufika Tabora na kuendelea kama sehemu nilizosema nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu reli. Reli inapita Bukene lakini kwa bahati mbaya au nzuri ni katikati kwa hiyo sisi watu wa Bukene tunapata mateso kabisa kuliko hawa wanaozungumza wa Kigoma na Tabora, wenyewe wana mabehewa. Sisi ni treni inatoka Mwanza ikifika Bukene imeshajaa na milango imefungwa. Kwa hiyo, anayeweza kuingia ndani ya treni ni yule Mwanamke aliyeava suruali na yule ngangari kwelikweli maana anapita katikati ya mabehewa, pale kwenye nafasi. Mabehewa ya zamani yaliyoharibika pale katikati kuna nafasi ndiyo anaweza kuchoma akaingia na akaendelea lakini mwengine hawezi. Kwa hiyo, wazee hawawezi kusafiri, ambao wanaona aibu, ile aibu ya kawaida ya Mwanamke, hawawezi kusafiri, wafanyabiashara hawawezi kusafiri, kwa hiyo ni hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kutoa ushauri. Kwa kuwa, reli imekuwa na *share* ya Serikali, kwa nini wasitupe hisa na sisi watuwezeshe sisi Watanzania hasa tunaotoka katika reli, *central line*, tununue hisa hizo, tusimamie sisi wenyewe kwa sababu ‘uchungu wa mwana anaujua mwenyewe Mama’, kuliko kuwaachia hawa ndugu zetu waliokuja kununua na wenyewe wanategemea mkopo hawana chochote kama tulivyo sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tufauti yake ni nini? Tuhamasishwe kama tunavyohamasishwa sasa hivi kujitayarisha kununua *NMB*, kwa nini Serikali isituhamasishe sasa kujitayarisha kununua hisa, tununue mabehewa mapya, tuongeze *trips*. Zamani treni ilikuwa inapita kila siku baadaye ikawa siku nne, baadaye siku mbili na baadaye itakuwa hakuna kabisa maana tunakokwenda kama pale Bukene hakuna treni kwa lugha nyingine, huwezi kupata kwa namna hiyo. Kwa hiyo, tuhamasishwe ili tuweze kununua na kutengeneza treni au reli nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upanuzi wa reli kuna ...

(*Hapa kengele ya Ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. TEDDY LOUISE KASSELLA – BANTU:** Ni ya pili hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo!

**MHE. TEDDY LOUISE KASSELLA – BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Anayefuata ni Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, ajiandae na Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, ajiandae.

**MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa.

Ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake hii nzuri na pia nampongeza Naibu wake kwa ushirikiano anaoutoa hadi hotuba hii ikakamilika pamoja na wataalamu husika na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa wadhifa alioupata kuwa Waziri Mkuu. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa chimbuko la Mawaziri Wakuu wa Tanzania, ni Liwale na Mawaziri Wakuu wote waliokuja baada yake yeye walifanya ziara Liwale, nakuomba kwa heshima na taadhima uje kufanya ziara Liwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli, naiomba pia Serikali kwa makusudi kabisa ipige marufuku biashara ya chuma chakavu. Nasema hivyo kwa sababu miundombinu mingi kama reli, madaraja na kadhalika, huharibiwa na biashara hii, hujuma nyingi inatokana na biashara hii ya chuma chakavu. Kwa hiyo, naomba Serikali izingatie hayo vinginevyo itafute utaratibu uliokuwa bora ili madaraja na reli zetu zibakie salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kukamilisha barabara ya kutoka Nangurukuru – Mingoyo. Eneo hilo sasa hivi pamoja na marekebisho ya mara kwa mara, inapitika kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutoka Lindi au kutoka Mtwara sehemu ambayo ilikuwa imebakia ya adhabu kubwa sana, ni kutoka Somanga - Ndundu. Ninaishukuru sana Serikali na kuipongeza kwa kumteua Mkandarasi Karafi, kufanya kazi katika eneo hilo. Naiomba Serikali ifuatilie kwa karibu ili kazi hiyo iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande hicho cha kilimita 60, kusema kweli, kimekuwa kero kubwa sana kwa abiria watokao Kusini Lindi na Mtwara kuja Dar es Salaam na *vice versa*. Nadhani kwa kumpata Mkandarasi huyu na kama Serikali itazingatia kumlipa vizuri na kufuatilia kwa karibu, matatizo hayo hatutayapata tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa hapo, ingekuwa ni vema pia hata Vyama vya Upinzani, vitoe hongera kwa Serikali yetu, kwa kuwa mimi nakumbuka kabisa wakati wa uchaguzi mdogo wa Tunduru hata Vyama vya Upinzani, vilishughulikiwa pale na majambazi. Kwa hiyo, kukamilika kwa eneo lile, utakuwa ni usalama mkubwa kwa abiria na mali zao. Kwa hiyo, nahimiza Serikali kazi hiyo ifanyike mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, narejea kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais. Naishukuru Serikali kwa kufuatilia kwa karibu mno ahadi za Rais katika Wilaya ya Liwale. Nianze na daraja la mto Ruhuu. Leo hii napenda kuliarifu Taifa kwamba daraja la Mto Ruhuu katika Kijiji cha Lilombe ambalo lilikuwa ni kero na Mheshimiwa Rais akatusaidia kutoa ahadi, limekamilika mwaka jana na lilifunguliwa na Mheshimiwa Rais. Mwaka huu, Mwenge umekimbizwa kupitia kijiji cha Lilombe kwa kutumia daraja hilo na kuendelea hadi Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja hilo, ni kiungo kikubwa kwa Wilaya ya jirani Nachingwe, Masasi hata kuelekea Tunduru. Naishukuru sana Serikali na Mheshimiwa Rais kwa juhudhi zilizofanywa kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa pamoja na uongozi wa Wilaya, DC wangu kwa kufanikisha ahadi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande kilichobaki ambacho tunakihitaji sana kikamilike, ni kutoka Nangurukulu kwenda Liwale. Ukitoka Dar es Salaam kwa kupitia barabara ya kutoka Nangurukulu hadi Liwale, inawarahisishia sana wananchi wa Liwale na wafanyabiashara kusafirisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia barabara hiyo. Hata mabasi kwa kipindi kile ambacho hakuna mvua wakati wa kiangazi hadi hivi sasa ninavyozungumza, mabasi kutoka Dar es Salaam yanayotoka asubuhi saa moja au saa kumi na mbili, yanafika Liwale saa tisa, hayo ni maendeleo. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati wa masika, barabara hii hujifunga. Kwa hiyo, adha ya wananchi wa Liwale ni kwamba wanazunguka mpaka Lindi na ukitoka Lindi ndiyo unafika Liwale kilomita kama 300 zimeongezeka kwa vyovyote vile kwa hesabu za kawaida inaonyesha kwamba maisha ya wana Liwale ni magumu endapo barabara ya Nangurukuru kwenda Liwale moja kwa moja haitatengemaa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuwa Rais alitoa ahadi na mwaka jana jitihada zimeshajionyesha ila tu kutokana na wingi wa mvua barabara hii haikupitika wakati wa masika ilijifunga na uongozi wa Mkoa kwa kushirikiana na *TANROAD*, Lindi walitoa makadiro ya zaidi ya kama bilioni 1.4 kwa ajili ya kukarabati barabara hiyo kiwango cha changarawe ili iweze kupitika kipindi chote cha mwaka, naomba Serikali iangalie suala hilo. Nimeambiwa kuna milioni 600 lakini sina uhakika kama milioni 600 ndiyo zitadhibiti sehemu korofi za barabara ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale hasa ukitalia maanani kwamba hata bei ya mafuta sasa hivi imepanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za *TANROAD*, Lindi lakini naomba Serikali iwe macho, itusaidie sisi wana Liwale ili kile tunachozungumza kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania basi iwe maisha bora kwa kila mwana Liwale kwa kutumia barabara hiyo ya kufika Liwale! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda sehemu ya reli. Kusema kweli mimi nimesoma St. Michael na St. George, miaka ya 1965 hivi na nilikuwa natoka Iringa kwa basi la *Railway, Second Class* mpaka Dodoma na unaingia hapa Dodoma unapanda treni mpaka Dar es Salaam na ilikuwa wakati huo kusafiri kwa treni ni *luxury*, unajiona kwamba wewe unasafiri lakini leo ninavyoambiwa na Wabunge wenzangu wa kutoka maeneo hayo, aha, ni kero! Naomba suala hili litazamwe kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata jiografia ya zamani sasa hivi inabadilika, nilikuwa najua Kaliua, Mpanda kwa kuwa treni zilikiwa zinakwenda maeneo hayo lakini nasikia sasa hivi njia hizo zimekatizwa hata ile ya kwenda Moshi ina matatizo, hata ya kwenda Tanga pia nasikia pia kuna migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huwa nashangaa badala ya jiografia kuongezeka maana kulikuwa na kitabu kilichokuwa kikiitwa *Dadly Stamp*, kilizungumzia kwamba patakuwa na reli mpaka Songea kwa miaka ijayo. Kilichojojiteza ni kwamba hata ile ya kutoka Nachingwea kwenda Mtwara iling'olewa na palikuwepo ya kutoka Masasi ambayo inakutana Nanganga kuja mpaka Mtwara lakini sasa hamna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, usafiri wa reli ni muhimu, naomba kabisakabisa wakati tunaendelea kuboresha, tunapigia kelele usafari wa reli, ninaomba pia itafutwe mbinu kuweza kufufua reli ya kutoka Nachingwea kwenda Mtwara na pia ile ya kutoka Masasi kuja kijiunga Nanganga. Tuta bado lipo, sehemu korofii zitakuwa chache kwa kuwa lile tuta bado lipo tunaweza kabisa tukapanga mipango yetu kuelekea huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu yote ikiwa na mawasiliano ya barabara, kusema kweli, bidhaa mbalimbali kutoka sehemu moja kwenda nyingine, itakuwa ni rahisi mno kuliko sasa hivi tunalia matatizo ya njaa wakati tunaelewa kabisa kwamba mahindi yapo Rukwa na maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda sasa kwenye bandari, naomba sana bandari ya Mtwara, Lindi, Kilwa na ile ambayo sasa hivi inafikiriwa ya Bagamoyo kujengwa na ile ya Dar es Salaam pamoja na Tanga ziboreshwe ili ziweze kuvumilia au kuhimili ushindani wa kibiashara. Tuna eneo kubwa sana la Pwani na bandari pia tunazo nyingi lakini tunashindwa kuzitumia bandari zetu kwa manufaa ya maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tuna *strip* hiyo kutoka Mtwara mpaka kufika Tanga na Wabunge wa maeneo hayo wapo, kilichojojiteza katika ufuutiliaji wa karibu, nimekuta hakuna hata mjumbe wa Bodi wa Bandari aliyetoka katika maeneo hayo. Sisemi hivyo kwa kuwa nahitaji kazi hiyo ila mimi kusema kweli huwa sipendi ghasiaghasia lakini ingekuwa vizuri sana Mbunge mmojawapo aidha wa Mtwara, Dar es Salaa, Tanga, Kilwa na Lindi apatikane ili aweze kushiriki katika Bodi ya

Wakurugenzi wa Mamlaka hiyo vinginevyo hizo bandari zinaonekana kama ni *dry ports* ambapo sivyo. Naomba Serikali iliangalie suala hilo kwa makini na ione ni utaratibu gani utatumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Liwale kwenda Nachingwea, naishukuru sana Serikali kwa juhudhi iliyofanya lakini bado zina kasoro. Ile barabara ukiiangalia inakuja vizuri mpaka Mbwenkuru lakini kutoka Mbwenkuru kuja Nachingwea kuna maeneo bado yanahitaji matengenezo na ninadhani *TANROAD* hawana pesa za kutosha kufanya kazi hiyo. Naomba wapewe fedha za kutosha waweze kufanya kazi hiyo ili barabara ile iweze kukamilika na iweze kupitika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi, tunapata dhiki na wakati mwingine namuonea huruma Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba ambaye ndiye Jimbo lake la Nachingwea kwa kuwa yeye hawezi kupiga kelele basi mimi naendelea kupiga kelele ili barabara hiyo ifike Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana barabara hiyo ishughulikiwe vinginevyo hawa wa Vyama vya Upinzani, wanapenyapenya kwenye maeneo yetu halafu wanazungumza vitu vya ajabu sana. Sasa kama Serikali haiwi macho kwa hilo, mnatuweka katika hali ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo yote, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ila isipokuwa ile ya mwisho uliyosema Vyama vya Upinzani vinajipenyeza, ndiyo nchi yao! (*Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Joyce Martin Masunga na Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, ajiandae, natumaini na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu naye atafikiwa.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini nichukue nafasi hii vilevile kumshukuru Rais kwa kumteua Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, kuwa Waziri wetu wa Miundombinu na mimi nikiwa kama Mjumbe wa Kamati hiyo, najua kazi ataiweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja katika barabara yetu ya Dar es Salaam – Mwanza. Kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa pamoja na matusi yote anayotukanwa, namuomba avumilie lakini wananchi tunaelewa kazi aliyoifanya na hasa wananchi wa Shinyanga tunamshukuru sana maana sasa barabara ile ni nzuri na inapitika, ni safi na sasa hivi viuno vyetu vinakwenda murua kabisa bila matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie barabara ndogo kutoka Manyoni. Kuna barabara moja ya vumbi ambayo Wakandarasi wanakwenda taratibu sana. Juji tulikuwa na Waziri wa TAMISEMI, tumepita kwenye barabara hiyo, tukitoka Shinyanga

na hatukupanda ndege, ile barabara hakuna cha kwenda VETA, wala cha kwenda Chuo cha Usafirishaji, pale kuna *Masunga Style*, maana barabara ile ukitaka kusema uende kama kawaida, haiwezekani, ulishaona mtu aka- *overtake* kushoto? Ile barabara mtu ana-*overtake* kushoto, unaweza uka-*overtake* kulia na unaweza ukaenda katikati na hii yote itasababisha ajali nyingi. Nakuomba Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, upite kwenye barabara ile, ujionee mwenyewe kwa macho yako na uwaambie wale Wakandarasi wafanye kazi kwa haraka kama Spika anavyosema kwa *Standard and Speed.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Shinyanga kuna barabara ambayo ilishatengenezwa awali, hii ni kutoka Shinyanga kwenda Mwanza. Hii barabara watu wanachukua hela tu yaani kwa ulaini, ni bandika bandua, nayo ni barabara ya Ilula – Misungwi. Ni bandika bandua kila wakati hela zetu zinakwenda hapo. Naomba hiyo barabara kama ni kutengenezwa, itengewe fedha basi itengenezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie barabara za Tabora, hawa ni jirani zetu. Hivi unaposema ‘mzigo mzito mpe Mnyamwezi’ ndiyo mzigo wenyewe huu? Juji hapa Mheshimiwa Lucas Selelii, anafurahi kupewa bilioni kumi, Mheshimiwa Lucas Selelii, bilioni kumi si pesa, haitoshi kwa barabara zetu za Unyamwezini. Naomba Wanyamwezi waangaliwe, ni kweli mzigo mzito mpe Mnyamwezi lakini sasa hivi wapunguziwe mzigo wapewe watu wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niende kwenye barabara zetu za Shinyanga, naomba tufungue ukurasa wa 174, daraja la Sibiti. Daraja hilo, safari hii tumetengewa pesa pale mwenyewe unaziona, hivi hili daraja mnalijua au mnalisikia redioni? Hili daraja watu wa Mara wanapita pale, watu wa Mwanza wanapita, Shinyanga tunapita, Kagera wanapita, Watu wa Burundi na Rwanda wanapita, naomba hilo daraja litengenezwe. Hayo mambo ya kutuambia kwamba upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, umetuchosha Wasukuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika ukurasa wa 175, kuna barabara ya kutoka Mwigumbi, Maswa, Bariadi na Lamadi. Mwaka jana mmetupa milioni 400, leo hii mnatupa milioni 80 zifanye nini? Hazitoshi na wala hauwezi ukaanza ujenzi. Lakini ukienda pale chini, kuna barabara kutoka Kolandoto, Lalago, Mwahunzi, Lalago tena kwenda Maswa, mwaka jana mlitutengea milioni 200 sasa hivi mmetuwekea 00, hivi Wasukuma mnataka tufanyaje? Tuishie mjini tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mjini kwenyewe hapa mnakotaka tuishie vumbi tele, Waziri wa TAMISEMI ameona mimi mwenyewe hapa nakoho kwa sababu ya vumbi, hakuna barabara wala nini mjini kote pale ni vumbi tele pamoja na kwamba tumejitahidi kuweka taa, taa na vumbi ni sawasawa na kuvaan suti halafu umetia ndala unatembea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie habari ya reli. Watanzania wote tulijua kwamba ingalau sasa reli inachukuliwa na hao wenzetu na Serikali tuna 49%, mambo yatakuwa poa, sasa mambo ni mabaya kuliko pale zamani. Hivi hii reli inakuwaje? Si afadhali basi muwafukuze, tuendelee sisi wenyewe tu kama kawaida?

Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, alisema jana pale kwa huzuni sana, ndivyo tunavyoishi Wasukuma na Wanyamwezi. Sasa hivi ndugu zetu hawaji Dar es Salaam kututembelea, watapanda nini? Tumezoea kupanda treni, treni bei nafuu hata na matobolwa siku hizi hatuletewi Dar es Salaam hivyo wanakula wenyewe, tunaomba mtusikilize.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niruke hapo niende moja kwa moja kwenye hali ya hewa. Hali ya hewa kila siku tunasikia kwenye redio, ohoo, mvua itanyesha, manyunu hapa na pale, hii yote ni kwa sababu hawana vitendea kazi vyatosh. Tunaomba Mamlaka ya Hali ya Hewa, wapewe fungu kubwa, wanunue rada za kutosha, tunahitaji rada saba, sasa hivi tuna rada moja nayo haijaingia bado, rada moja ni Sh. 2bn/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujua hali ya hewa, itatusaidia Watanzania wote kwa ujumla. Mtu atajua kesho kuna mvua asitoke, walemaru watajua kesho kuna mvua wakae nyumbani kwa sababu wenzetu hawawezi kutembea vizuri watalowana. Wakulima kwetu sisi Wasukuma, wanawake tunatengeneza matobolwa, tutajua leo tuyaanike matobolwa au tusianike. Sasa msipowapa hii taarifa ya hali ya hewa, itakuwa tabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshajionea, kuna mambo yanaweza kujitokeza sehemu fulani labda kuna hatari inataka kutokea, watu wa hali ya hewa hawawezi kuona, wapeni vitendea kazi, wapeni fedha za kutosha zitasaidia Watanzania wote kwa ujumla. Naomba hilo Mheshimiwa Waziri, alielewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuzungumzia kuhusu majengo. Majengo ninayotaka kuzungumzia ni majengo ambayo sasa yanajengwa kwa maana ya Wizara yetu ya Miundombinu. Naomba wawape watu maelekezo, majengo ya Serikali, majengo ya watu binafsi, wakumbuke kwamba na walemaru wapo katika jamii hiyo ambapo ni asilimia kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimejionea mwenyewe, kuna huyo mlemavu, ananisikia hapo juu, amepita anatembea hapa kwenye hizi ngazi kidogo aanguke. Nimeshindwa kuingia Bungeni humu, nikaanza kuuliza, hivi kweli hakuna kitu cha kuwaingiza humu ndani hawa walemaru? Bahati nzuri akaja mama mmoja akasema vipo vifaa vyatosh kuhusu kufikirishwa, nafikiri huyu mlemavu hakujua kama kuna kitu tunachowapandisha kuwaingiza mpaka hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchukua nafasi hii, nipongeze sana Bunge letu, mmetengeneza barabara zote kwa sisi wenyewe miguu mizuri na wale walemaru. Kila siku namwangalia Mheshimiwa Mkanga anavyopita na leo nimeona kumbe hata walemaru wanapokuja hapa Bungeni, naomba watoe ripoti mapema wapewe kile kitu cha kuwapandisha wafike hapa juu vizuri bila matatizo yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yangu ya kusema haya ni kwamba, hawa walemaru tumewasahau. Sisi wenyewe tumeshindwa kujijua kwamba ni walemaru watarajiwu, kama si leo kesho. Naomba tuwasaidie sehemu popote watakapokuwepo ili

waweze kupita vizuri na kukaa kwa utaratibu mzuri kwa sababu na wao ni binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nirudi nyumbani. Mwaka jana nilisimama hapa, nikaomba mtusaidie barabara ya Shinyanga - Old Shinyanga. Naomba niseme maneno yafuatayo, naishukuru sana Serikali, barabara hiyo imekwishaanza kujengwa na Wanajeshi sasa hivi wananiwikiliza wanafurahi sana ila wanasema angalau wapewe fedha za kutosha ili barabara ile iweze kutengemaa kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naomba usiniambie nikae kwa sababu sikupata nafasi, ni vizuri nizungumze, Waziri yejote atajibu. Kuna madaraja nchi nzima unawenza kusema kwamba Halmashauri ijenge lile daraja, yale madaraja huwa, ni makubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba tunapowaambia Waheshimiwa Mawaziri, watuelewe maana kama hilo daraja utasema ulijenge, huwezi kulijenga ukalimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Shinyanga Mjini, tuna madaraja mawili ambayo ni ya hatari, daraja la Mshikamano na la Ndala. Tunamwomba Waziri anayehusika na madaraja haya aje ayatazame, atajua haya ninayosema ni kweli na nimetumwa na wananchi wa Shinyanga. Atakayekuja kama anataka nifuatane naye mimi niko radhi na kwa sababu ni mwanamke mwenzangu, nitafurahi maana ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Waziri akiziona barabara hizi atawaambia watu wa *TANROADS*, watusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana mwenyewe ungekuwepo pale ungeshangaa, ni vumbi linatimka. Kama Waziri wa TAMISEMI leo angekuwa anajibu maswali pale ungemsikia sauti iko kama yangu, ni vumbi hakuna mfano. Sasa tunaomba tusaidiwe, hivi hawa watu wa Singida, Nzega, pale Mjini barabara lami tupu, hivi wamekwenda kwa Mganga gani mniambie nami ili niende nipate hiyo lami! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, kwa haya niliyoeleza, Serikali iweze kutusaidia. Pia nichukue nafasi hii kwanza kumwomba Mheshimiwa Dr. Kawambwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Mheshimiwa Dr. Kawambwa, kaanza vizuri na sisi ndiyo wajumbe wake, tunapomwelekeza anakubali. Naomba tuikubali bajeti hii ili kwa kweli tuendelee kufanya naye kazi, yeye ni msikivu na ninyi wenyewe mmemwona. Kwa maana hiyo, nasema naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote, nawatakia kila la kheri, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge na wananchi, hiki alichosema Mheshimiwa Masunga, kwa wageni wa nje, kama tuna walemavu, kwenye ngazi hapa unapopanda, ipo mashine kabisa, inakuwa *operated automatic*, anakaa mlemavu pale, anapandishwa, kama ana kitichake, anakaa, anapandishwa mpaka *level* ya pale *public gallery* halafu anaendeshwa huku. Kwa hiyo, ipo mashine ya namna hiyo.

Kwa sababu inatakiwa iwe *operated* na mtu, jana nilikuwa na wageni, tumeijaribu kwa sababu muda mrefu haifanyiwi kazi, ikaleta kidogo mushkeli lakini ipo na inafaa.

Kwa Wabunge wanaoingia hapa, zipo *avenues* za kupita tu, wao wenyewe wanafahamu hakuna tatizo.

Kwa hiyo, kwa wageni, kama kuna mlemavu hasa wa viungo, kuna utaratibu wa mashine inam-*lift* juu halafu inamweka kwenye *level* hiyo. Tunaendelea na Mheshimiwa Dorah Mushi na Mheshimiwa Zaynab Vulu ajiandae.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu.

Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima nikaweza kuwepo katika Bunge lako Tukufu.

Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu pamoja na Naibu wake na wataalam wote kwa kuileta hotuba hii nzuri mbele ya Bunge lako Tukufu. Bila kuisahau Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa sera zake nzuri ambazo zimewezesha kujibu kero nyingi za Watanzania zilizomo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la barabara ya *KIA* – Mererani. Barabara hii ni mbovu sana tena inachafua mazingira ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro.

Pili, barabara hii ni ya aibu kwetu sisi wananchi wa Manyara.

Tatu, barabara hii inachangia vifo vingi vya akinamama na watoto kutohana na ubovu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia vifo vya akinamama, ni kwamba wanapopatwa na dharura kwa mfano wakati wa kujifungua, tukitaka kuwapeleka Hospitali ya Rufaa kama vile *KCMC* au *Mount Meru*, inakuwa vigumu sana, hata ungempa Dereva Sh.300,000/= au Sh.400,000/= ukamwambia mpeleke mgonjwa wangu *Mount Meru*, hawesi kukubali kwa sababu barabara ile ni mbovu sana, haipitiki. Barabara ile ina urefu wa kilometra kumi na tano wala hazifiki kilometra ishirini na wakati wa masika inageuka kuwa mto, haifai kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikwambie, unapoanza safari asubuhi unawenza ukalala njiani siku mbili ndipo unafika Arusha. Barabara hii inatudhalilisha watu wa Manyara kwa sababu gani? Mungu ametupa madini ya thamani kubwa lakini tunapokuja kuangalia barabara wanayopita wale wawekezaji, hakika ni mbaya mno, ni aibu kwetu wananchi wa Manyara. Tunaacha mali zetu zinachukuliwa na wageni kwenda kutengeneza barabara nchini mwao na sisi tunabaki na vilio vya akinamama? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia hilo kwa sababu mimi ni mmojawapo wa waathirika ambapo nilifiwa na mtoto wa ndugu yangu, wakati alipokuwa akajifungua. Alijifungua mapacha akawa ameishiwa damu, wakati huo ulikuwa ni wa mvua barabara

hazipitiiki kabisa. Nilitafuta kila namna ya kuweza kuokoa maisha ya mtoto yule na mapacha wake lakini haikuwezekana, alipoteza maisha pamoja na watoto wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati mwingine unaweza kusema nipae, unajariibu kuulizia wale watu wanaoruka kwa ungo wako wapi wanisaidie? Wakati huo hawaonekani kwa sababu hawajui biashara ya kubebe abiria, wao wanabebe kimazingara. Hao watu wanaoruka kwa ungo wangejua Mererani wakati wa mvua kuna biashara, nafikiri wangejaa kule na wangepata fedha nyingi sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu, pia kuna jirani yangu alifariki kwa kupoteza damu nyingi wakati anapelekwa hospitali ya *KCMC*, akafariki njiani na vifo vingi vya watoto vinatokea na huu ni mwaka wa tatu nasimama katika Bunge hili Tukufu nikizungumzia suala la barabara ya Mererani, kulikoni? Kuna nini barabara hii haitengenezwi? Ni fedha hakuna au ni nini? *Tanzanite* jiwe moja tu lina uwezo kujenga barabara ile. Kwa nini Serikali haitoi majibu, haisemi barabara ile itengenezwe na wawekezaji au wapo pale kwa kuchukua madini yetu na kuondoka kwenda kujenga nchi nyingine na sisi tunaachwa na mashimo huku akinamama na watoto wachanga wakifariki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu, pia imeathiri akinamama wajasiriamali. Kwanza kabisa, kuna *group* la akinamama walichukua mikopo, sasa kwa sababu biashara zao ni za nyanya sokoni na za samaki, waliondoka na ule mkopo kwenda kuchukua bidhaa zao, wanaporudi hakuna pa kupita, gari limekwama, kubebe mizigo yao kwa kichwa hawawezi, imebidi samaki waoze, ilibidi wengine wahame Mererani, wamekimbia, watalipa na nini mikopo ile? Hii inachangia kurudisha hata uchumi wetu nyuma na inatisha kabisa. Kwa nini watu wa Mererani tunaachwa vile, kwa nini tumesahaulika, kwa nini Serikali yetu haitaki kuikumbuka barabara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu wa Awamu ya Tatu na ya Nne walikwishatoa ahadi hizo na kusema kwamba barabara ile itajengwa tena kwa kiwango cha lami. Kauli ya Rais ni kauli nzito, hapa duniani ya Mungu ni ya kwanza na ya pili ni ya Rais, kwa nini haitekelezwi, kuna nini? Kwa nini kauli za Marais wetu wawili hazitekelezwi, barabara hii ina kilomita ishirini tu, kulikoni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba barabara hii itengenezwe haraka kwa kiwango cha lami, la sivyo kwa kweli ndugu yangu Mheshimiwa Kawambwa, nitaondoa shilingi leo kutokana na barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi, ni miaka mitatu toka nimepata kura za Ubunge, nimechaguliwa na kuambiwa nenda katutetee kwa ajili ya barabara ile. Nimeongea mwaka wa kwanza sijasikika, mwaka wa pili sijasikika, huu ni mwaka wa tatu, wa nne na wa tano tunamaliza kipindi, hivi nitarudi tena Manyara kwenda kusema jamani nipeni kura? Inarudi pale pale watu wanaposema Wabunge wa Viti Maalum siyo Wabunge, hivi sisi sio Wabunge halali? Kwa nini hatusikilizwi? Kwa nini hatupati majibu mema, sisi tutakwenda kuwaambia nini wananchi wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru pia Kampuni ya *Tanzania One*, wakati mwingine wanasaidia kidogo, wamejaribu kukarabati barabara hii lakini ukarabati wao si mzuri kwa sababu wanabeba ule udongo wanaotoa migodini wanamwaga barabarani. Mvua inaponyesha, udongo wote unakuwa tope, unazolewa na maji na tatizo linabaki palepale. Huku nao wanasema kwamba tunakarabati barabara ya Mererani – *KIA* kwa Sh. 500m/=, hivi kweli inawezekana? Sh. 500m/= kwa mwaka ni nyingi sana lakini ukiangalia ile kazi iliyofanyika pale haifanani na Sh. 500m/=. Naona ufuatiliaji ndiyo tatizo kwa sababu wanapodai kwamba wanatengeneza barabara ile kwa Sh. 500m/= ni wazi kwamba watapunguziwa kodi lakini je, ni kweli kwamba wanatengeneza barabara ile kwa Sh. 500m/=? Ingekuwa basi barabara hiyo wanatengeneza kwa kokoto hiyo ni nafuu lakini kutoa udongo wa mgodini ambao hauna gharama yoyote na kumwaga barabarani, kusema Sh.500m/= zimetumika kujenga barabara, hilo siliamini kabisa. Naomba kauli za Marais wetu, zitekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni barabara ya Orkesment kwenda Babati. Lah!! Tunashindwa la kusema, watu wa Simanjiro tumeachwa, tumesahaulika. Kutoka Orkesment kwenda Babati, ni mwendo wa siku nne kwenda na kurudi tena hiyo umeharakisha sana, unakwenda kulala Arusha, siku nyingine ndiyo unakwenda Babati, Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ilikuwa hajajiandaa na hiyo barabara au kama Serikali ilikuwa hajajiandaa kuunganisha huu Mkoa, kwa nini basi tunatesa wananchi wetu? Wananchi wetu wanapata tabu, vitendo vingi vya ubakaji viko Mkoa wa Manyara, kwa nini? Hata ukimkamata mtu amefanya tendo lile ukamshtaki, yule mama ambaye mtoto wake amefanyiwa hana uwezo wa kwenda Babati, kwanza gharama kubwa, barabara ni mbovu, kwa hiyo mtu anabaki na maumivu yake. Naomba suala hili la barabara ya kutoka Orkesment kwenda Babati, liangaliwe sana, ni mbovu sana, naomba lifikiriwe ili hii barabara iweze kutengenezwa na kupitika huku Serikali ikijiandaa kwa ajili ya kuweka lami. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi Dar es Salaam kwenye foleni za magari. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa kwa Jiji la Dar es Salaam hasa ukiangalia wafanyakazi na wafanyabiashara, hili ni tatizo kubwa. Utakuta mfanyakazi ametoka nyumbani kwake asubuhi anakwenda kazini, kutokana na ile foleni, mpaka afike kazini ni saa tatu, saa nne, utakuta yule mfanyakazi analipwa kwa mwezi kama kwamba alifanya kazi kwa masaa yote, hii inakuwa hasara sana kwa vyombo husika hasa tunapozungumzia utandawazi. Ni tatizo kumlipa mtu ambaye hajafanya kazi kwa yale masaa ambayo umempangia. Hili ni tatizo kubwa, kwa hiyo, naomba Wizara ya Miundombinu, iangalie uwezekano wa kutafuta wataalam ambao wanaweza kuona jinsi gani ya kuunganisha barabara hata angalau hizi foleni zipungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara inayokwenda *Airport*, barabara ile ni tatizo. Siku moja nilichelewa ndege. Kama utakuwa na haraka au kuna kitu cha lazima, inakuwa ni tatizo kubwa. Niliondoka mjini, pale *city centre*, nikijua kwamba nitatumia muda wa saa moja, ndege yangu ilikuwa inaondoka saa tisa kamili, nikatoka kwenye saa

saba na nusu. Siku hiyo mvua ilinyesha, nimefika Airport saa moja usiku, ndege ilishaondoka saa nyingi, nilibaki kushangaa nifanye nini, wala sikuwa na namba zao za simu, nipige simu hata ni-*cancel* safari, basi nikabaki nimechanganyikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali iangalie, foleni zinaleta hasara kubwa kwa Taifa letu sababu magari yanapotembea kwa mwendo mdogo yanakula mafuta mengi na hivyo inabidi Serikali iagize mafuta kwa wingi na lazima itumie fedha nyingi za kigeni kwa kuagiza mafuta nje na hapo utakuta fedha yetu inashuka thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofii*)

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia yale ambayo naona muhimu kuingia katika kumbukumbu za bajeti hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia kusimama mbele ya Bunge hili nikichangia kwa mara ya tatu toka niwe Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, napenda nichukue nafasi hii, kwa kuwa ndiyo mara yangu ya kwanza toka Mheshimiwa Waziri Mkuu alipoteuliwa, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza kwa nafasi aliopewa na Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Vilevile nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa kwa kushika Wizara nzito lakini *Inshallah*, Mwenyezi Mungu atamjaalia yeeye na Naibu wake Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu na watendaji wao wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niwapongeze pamoja na kwamba pongezi zenyeWE kidogo zitakuwa na masuala ya kutaka ufanuzi lakini ni wajibu kuwapongeza kwa bajeti nzuri waliyoiwakilisha na nawatakia kila la kheri, lakini naiomba Serikali iangalie Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni nyeti sana, hii ndiyo Wizara ambayo imeshika mgongo wa Taifa hili kwa maana kwamba ukizungumzia suala la miundombinu unazungumzia suala la uchumi wa Taifa hili la Tanzania. Kwa hiyo, ni vema ikaangaliwa kwa sababu malalamiko yote haya tunayoyazungumza hapa, ni kutokana na ufinyu wa bajeti. Ninaposema ufinyu, maana yangu ni kwamba ni fedha ambazo zimegawiwa kwenye Mikoa na Idara mbalimbali kwamba hazitoshelezi. Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali kuiangalia kwa makini na kuipa kipaumbele zaidi Wizara hii ili iweze kufanikiwa katika malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena kwa mara ya tatu kuitaka Serikali iuangalie sana Mkoa wa Pwani. Mkoa wa Pwani, Mwenyezi Mungu ametujalia. Mkoa

wa Pwani, ni kiungo cha Mikoa mingine yote hapa nchini Tanzania, huwezi kwenda kokote kama hujapita Mkao wa Pwani iwe umetumia barabara, maji au anga, lazima kwa vyovyyote vile ukitoka kona moja kwenda kona nyininge upite Mkao wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali, jamani ninyi mnapiga kelele lakini nataka niwaambie kitu kimoja kwamba, Mkao wa Pwani lami tunayojua ni inayotoka Dar es Salaam, Morogoro *Road* lazima ipite Kibaha, Chalinze na kuendelea au uende Tanga, huku ukienda Mikoa ya Kusini tunashukuru sana Serikali barabara iliyoanzia pale Kongowe, Kibiti, imefika sasa inaingia Rufiji nayo pia tunaishukuru lakini maeneo mengine ambayo yanapaswa yatengenezwe kwa lami kwenye barabara ambazo ndio ziko kwenye Mkao na fedha zake zinatoka Serikali Kuu kwa kweli ukisema kitu lami, watu wanafikiri labda unazungumzia sukariguru inayokwenda kumwagwa barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunazungumzia miundombinu na tunataka kupunguza adha ya matatizo ya foleni. Nashukuru Serikali imeliona, imetenga feda kwa ajili ya barabara inayotoka Ikwiriri kwenda Mkongo mpaka Mloka. Ikitoka Mloka itaingia Vikumburu halafu baadaye inatoka Kisarawe, Kisarawe unaweza kutokea Kibaha – Bagamoyo ukaelekeea kama unakwenda zako Arusha au Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali, barabara hii ifikiriwe kuwekwa lami kwa sababu ikiwa barabara ya vumbi bado tatizo liko pale pale. Tunaposema barabara ya lami tunamaanisha itasadia sana. Kwanza hawa watu wa Ikwiriri, Mkongo, Mloka, Vikumburu, Kisarawe watanufaika, hata wawekezaji watakwenda, hivi hamwonei huruma Mkao wa Pwani? Viwanda unavita futa, matunda yote yale Mwenyezi Mungu aliyo tujalia yanafia shambani, watoto wanafanya kuchazea mpira wakati wa msimu, kwa sababu magari yanashindwa kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani nawaomba sana sana hizi barabara zitengenezwe na ziwe katika kiwango cha lami. Unatengeneza barabara kilometra moja, kilometra moja inasaidia nini? Yaani kama vile unanawa uso unaishia kwenye pua, huku kwenye mdomo hufiki. Hakuna faida, kwa kweli kilometra moja haisaidii. Unatoka kwenye vumbi na makorongo unaingia kwenye lami kilometra moja umemaliza shughuli, tatizo liko pale pale, hakuna mwekezaji ye yeyote atakayeweza kwenda, hakuna mtu mwingine ye yeyote atakayeweza kusema aende kujenga viwanda kule. Ukiangalia akinamama na akinababa wanavyopata tabu kwa ajili ya barabara zile hasa nyakati za mvua, utawahurumia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri tunaoujua kule nyakati za mvua ni malori, malori hayo hayo tunasaidiana na magunia ya mkaa, mbao na kadhalika. Sasa ufike wakati barabara hizi za Mkao wa Pwani zijengwe kwa lami. Tunapotengeneza barabara za ndani ya Mkao wa Pwani tunaokoa janga la foleni kwa mkoa wa Dar es Salaam. Huna sababu utoke Rufiji unataka kwenda Bagamoyo upite Dar es Salaam. Hana sababu Mheshimiwa Kawambwa anatoka Bagamoyo anakwenda kumsalimia mwenzake Kibiti au Utete apite Dar es Salaam, atatoka Bagamoyo, ataingia Kibaha, ataingia Kisarawe, atakwenda zake Rufiji bila matatizo. Naomba suala hili liangaliwe kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ahadi nyingi za Rais, mojawapo ikiwa ya Kivuko cha Utete, nimeona kwenye hotuba ya bajeti lakini isiishie kwenye maandishi, ahadi hii ilitolewa mwaka 2005 leo tupo mwaka 2008, naomba sana kivuko cha Utete kifikiriwe. Kwanza kitasaidia msongamano, barabara hii ya kutoka Kibiti kwenda Lindi, Mtwara itakapokamilika, hakutakuwa na bughudha wengine wataamua wapite Utete au wapite kwenye daraja la Mheshimiwa Mkapa. Hivi ni vitu ambavyo vinapaswa viangaliwe kwa makini na kuweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba, kuna barabara inayotoka Bagamoyo lakini kwenye ujenzi inaanzia Mlandizi – Makofia – Mzenga hadi Kisarawe. Barabara hii nayo ni kiungo, inaweza kuwasaidia wananchi wasisumbuke tena kwenda Dar es Salaam. Ninachoomba suala la barabara hii ya Mlandizi – Makofia - Mzenga – Manerumango liangaliwe kwa makini. Kwa sababu gani? Kwa sababu barabara hii ilikuwa inafadhiliwa na Ubalozi wa Denmark, Ubalozi umesitisha ufadhili wake. Je, ina maana wananchi wanakosa haki yao kwa sababu mfadhili ameshindwa kuiendeleza na tunawatakia maendeleo na kama Serikali iko tayari kuiendeleza hiyo barabara je, itaiendeleza kwa kiwango cha lami kwa sababu tumechoka barabara za vumbi kwa Mkoa wetu wa Pwani. Tunahitaji na sisi tupate lami kama Mikoa mingine kwa sababu na sisi pia tuna haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana tunapoambiwa ati Mkoa wa Pwani tuko pembezoni. Hii siielewi kabisa, Mkoa wa Pwani ni kitovu cha Mikoa mingine yote, leo iweje sisi tuwekwe pembezoni? Kwa kweli nafikiri hapa kuna haja ya kuliangalia suala hili kwa makini sana na nitaomba nipatiwe majibu ya uendelezaji wa barabara hiyo ya Mlandizi – Makofia – Mzenga hadi Manerumango.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, ninaishukuru Serikali kwa kuweza kutupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Mafia. Kweli hili limekuwa ni mkombozi mkubwa sana na tunahitaji ujenzi huo na ushirikiano ambao tayari wananchi wanauonyesha basi uende haraka. Wananchi walikuwa wanapata tabu sana hasa akinamama. Jamani ilikuwa ni aibu, huwezi ukapanda meli au boti au mashua na mume, watoto na wakwe zako, ni aibu unapofika mahali inapotia nanga. Lakini sasa gati hiyo itakapojengwa itakuwa ni mkombozi kwetu sisi watu wa Pwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama vile haitoshi, wanaopanda meli hizo au jahazi hizo kwenda Mafia ni lazima wakapandia kwenye gati ambalo limejengwa Nyamisati. Tunaishukuru Serikali kwa kutupatia hilo gati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barabara ya kutoka Bungu, Ruwaruke mpaka Nyamisati ni tatizo kubwa sana na bandari ile ya Mafia itakapokuwa imejengwa maana itakuwa imepanuliwa, imekuwa kubwa basi magari makubwa yatahitaji kupita katika barabara ya kutoka Bungu, Ruwaruke hadi Nyamisati, tunaomba na yenewe ifikiriwe kuongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia huku kwenye kitabu cha hotuba ukurasa wa 123 kwenye jedwali inaonyesha kilomita moja, haitoshi, tunazungumzia utandawazi, tunazungumzia maendeleo ya nchi hali kadhalika na Mikoa, haitoshi kilomita moja. Barabara ile naomba nipatiwe jibu ni lini itaweza kupanuliwa zaidi, kwa sababu sasa hivi inapitika, lakini mvua zikinyesha ni tatizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia barabara ya kutoka Mkuranga mpaka Kisinju iangaliwe kwa jicho la huruma na yenyewe iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwa Mkao jirani, Kivuko cha Kigamboni. Tumechoka, tunajua pantoni inatengenezwa, lakini *speed* iongezwe. Sijasikia pantoni imepakia watu, watu wale wako pale wanatafuta jinsi ya kuzishika roho zao, inavutwa na pantoni nyingine mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana katika bajeti niliuliza, je, Serikali inajua watu wangapi wanaingia kwenye pantoni ile wanapovuka kutoka ng'ambo moja kwenye ng'ambo nyingine? Sikupatiwa jibu, lakini nafikiri nitapatiwa jibu katika bajeti hii. Je, kiwango cha fedha kinachotozwa kwa ajili ya nauli ya abiria wale wanaotoka upande mmoja kwenda upande mwingine, zinatumikaje fedha zile? Kila siku pantoni ni mbovu na kama pantoni inazalisha kwa nini basi Serikali kama haina uwezo, fedha zile zisitumike katika kutengenezea pantone?

Mheshimiwa Naibu Spika, pantoni nyingine inatengenezwe yenyewe uwezo wa kuchukua watu 2,000 na magari 50, sijui kule katika barabara hayo magari 50 yatapita viyi, kumetengenezwa? Njia ya kuweza kusafirisha msongamano wa watu 2,000 kwa pamoja au tunategemea miundombinu ile ile iliyokuwa imetengenezwa pale mwanzoni? Hayo, ninapenda nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bandari ya Bagamoyo, barabara hizi zikitengenezwa hakutokuwa tena na tatizo la watu la kuhangai ka kupita mpaka waende Dar es Salaam. Mizigo itakayotoka Bagamoyo inayokwenda Arusha, inayokwenda Moshi hata watu wa Mombasa wanaweza wakaja wakachukulia mizigo yao pale Bagamoyo. Kwa hiyo, ni muhimu hivi vitu vikaangaliwa kwa sababu tunapotengeneza bandari na tutakapotengeneza barabara na asa kheri Mwenyezi Mungu anaweza akatujali jamani Mkao wa Pwani wawekezaji wakaja, wakajenga viwanda, tukapata ajira, zile ajira tulizoahidi zitatoka humo humo katika hayo tutakayokuwa tumeyafanya.

Vilevile tuna mbuga ya *Selou*, tukiwa na barabara nzuri, watalii na sisi tutawapata. Hivi kila siku, watalii watoke huko wanakotoka waende Mikoa ya Kaskazini kwa nini wasije na Mkao wa Pwani? Mimi ninaiomba sana Serikali iangalie sana Mkao wa Pwani, ituwezesha, tunashukuru hizo barabara, lakini itafikia wakati na sisi tutasema tunafunga barabara zetu katika maeneo yale ambako watu wanapita na sisi mpaka tutakapoongezewa fedha za kupatiwa barabara za lami katika Mkao wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru, lakini nitaomba nipatiwe majibu kwa yale ambayo nimeyaomba. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, Mheshimiwa Anastazia Wambura, ajiandae, Mheshimiwa Mariam Mfaki ajiandae na pia Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda naye ajiandae.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nizungumze machache kuhusu Wizara ya Miundombinu. Kwanza kabisa, naomba niunge mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza toka baadhi ya Mawaziri walipoteuliwa na hasa Mheshimiwa Waziri Mkuu alipoteuliwa na Mawaziri wengine, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda kwa muda wote ambao nimemfahamu toka huko nyuma ni kwamba ni mtu makini na toka achaguliwe kuwa Waziri Mkuu, ameonyesha uwezo mkubwa sana katika kuyajua masuala muhimu na makubwa ya Taifa hili na ya Kimataifa. Anafahamu kwa usahihi masuala mbalimbali *no matter controversial they are.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, yanayotolewa na Serikali hivi sasa, ni majibu makini na kwa msingi huo, Serikali yake ni makini zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Katika Ulimwengu wa kiutandawazi kama tulionao hivi sasa, ili Serikali iweze kuheshimika zaidi inabidi kuwa na majibu sahihi na ya wazi na yasiyo funika funika mambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa kwetu sisi na viongozi wengine wote katika nchi nzima hii ni kumpa msaada unaostahili ili nchi yetu iende mbele. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakupongeza sana. (*Makofi*)

Mwisho, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kumteua Waziri Mkuu huyu, pongezi sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninaomba pengine niongee hivi. Sifa ninazozitaja hapa juu zinakisafisha sana Chama chetu cha Mapinduzi. Maana ninaamini tunakokwenda, tunakwenda vizuri kwa maana ya kuvunja mitandao ya ufisadi ili kukisafisha Chama cha Mapinduzi. Ni lazima sisi viongozi tuelewe ya kwamba uhusiano wa wanamtandao wa ufisadi, haukujengwa juu ya imani wala haukujengwa juu ya uelewa fulani fulani au dhamira fulani fulani iliyo sahihi au maelewano ya dhati kati ya mafisadi hao bali katika maslahi yapitayo, yaozayo na yanayosahaulika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mafisadi tuwashughulikie ili Chama cha Mapinduzi kiwe safi, maana Chama cha Mapinduzi ni safi hakina ubaya ila wapo watu wachache ndani ya Chama cha Mapinduzi wanaokichafua Chama hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa akili ya mafisadi, wao wanafikiri kutawala ni kuamini nguvu ya fedha lakini nguvu ya hoja, ndiyo muhimu sana kuliko ile nguvu ya fedha ambayo ni ya muda mfupi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Dr. Shukuru Kawambwa. Nilikuwa naye Chuo Kikuu, ninamfahamu, kama *Engineer* mzuri ambaye amepelekwa mahali pake panapostahili, pongezi sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Ninampongeza sana Naibu Waziri wake naye ni mtu makini, mtu sahihi na mtu safi. Nampongeza pia Katibu Mkuu na Wakurugenzi wengine wote ndani ya Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye hoja. Ninaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu mkubwa wa kuanza kushughulikia ujenzi wa barabara za Mkoa wa Kigoma. Mimi baadhi ya viongozi tulikuwa hatuelewani kwa sababu ya barabara ya Mwandiga –Manyovu. Barabara hiyo, ni kiungo muhimu sana na nchi jirani ya Burundi. Wao wamejenga barabara yao mpaka kwenye mdomo wetu, ni safi, ukiingia pale saa moja unakwenda zaidi ya kilomita 100, kwetu kilomita 60 unakwenda kwa masaa matatu au manne, ni aibu. Lakini nashukuru Serikali imeliona hilo na kwamba sasa watakwenda haraka kuijenga hiyo barabara ya Mwandiga-Manyovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kidahwe-Nyakanazi, nayo ni muhimu pamoja na ile ya Kigoma-Tabora, Kanyani-Mpanda. Hzi barabara zote ni viungo muhimu na Mikoa ya jirani ili kupeleka mazao kwenye masoko yanayotoka katika Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni wakulima wazuri, watu wa Kigoma ni wakulima wazuri sana, wana nguvu na ni wachapakazi sana watu wa Kigoma. Tutengenezeeni barabara, tutafanya kazi kubwa ya kulisha nchi hii. Maana uwezo tunao, ardhi tunayo, ardhi ambayo ni safi haijachoka kama ardhi nyingine zilizokwishachoka kwa sababu ya *intensive use of ammonia*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ahadi za Serikali kwa ajili ya *potential zilizopo* katika Mkoa wa Kigoma, sasa wapo wafadhili ambao wapo tayari kuwekeza katika Mkoa wa Kigoma. Kwa mfano, Wachina wapo tayari kuwekeza kwenye usafiri wa majini, (*water transport*). Watu wa Dubai kupitia Mfuko wa ABU DHABI, wako tayari kuwekeza katika *Special Economic Zone* ya Mkoa wa Kigoma. Baada ya ahadi za Serikali za umeme kutekelezwa na huduma zingine, wapo tayari kuja. Tuupe kipaumbele Mkoa wa Kigoma, nchi yetu itaona matokeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya pembezoni kwa maana ya kutumia uchumi wa kijiografia, ina maana kubwa sana kwa maendeleo ya Taifa hili. Ujenzi wa Daraja la

Mto wa Malangarasi, unafungua Magharibi yote na ipo biashara kubwa sana tutafanya sasa na Mikoa ya pembezoni kwa maana ya kwenda Kongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Kigoma, ni muhimu sana na nimepata habari kwamba kiko kwenye *detailed design*. Kiwanja hiki, ni muhimu sana kwa kuifanya Kigoma kuwa Kituo Kikuu cha Kibiashara katika nchi za Maziwa Makuu na Benki ya Dunia, inalitambua hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Kigoma umechaguliwa na Benki ya Dunia kama *one of the strategic border cities* ambayo itaongeza utalii katika Mkaoa huu kwa kiwango kikubwa katika upande ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kisiri-Buhigwe, ninaishukuru Serikali imetenga fedha karibu shilingi milioni 600 kwa ajili ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye barabara hii, ninaomba daraja nililokwisha kulizungumzia miaka kadhaa iliyopita ambako kuna mto mkubwa ambaa unahatarisha maisha ya watoto wanaokwenda shule katika Wilaya ya jirani, Wilaya ya Kigoma Vijijini. Wajengewe daraja ninalotoka Kinazi kwenda kijiji cha Nyamihanga. Daraja hili, ni muhimu sana kwa sababu pengine katika viongozi wakubwa wa nchi hii waliokwishakufika katika kijiji kile, ni mimi ndiyo nimefika pale, lakini nafika kule kwa kuvua suruali, navaa kaptula ili niweze kuvuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana mto wenye ni mkubwa. Mto Mutungurusi, ni mkubwa sana unaopita pale na hakuna mtu mwengine ambaye amewahi kufika kule. Kule tulitakiwa kujenga shule tumefanikiwa lakini hospitali hatujajenga. Kwa hiyo, lazima watu wa kule waende hospitali ya Kigoma Vijijini nayo ni matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya ninayazungumza kwa kweli kwa uchungu mkubwa. Kwa sababu kijiji kile ni kijiji ambacho kinazalisha chakula sana na watu wa kule ni wakulima sana na watu wengine wamekuwa wakihamia kule, lakini daraja hakuna, barabara hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuuliza swali hapa Bungeni, nikaambiwa kwamba Serikali itatenga fedha kupitia Mfuko wa Halmashauri. Nikaenda kwenye Halmashauri, Halmashauri wakanambia hakuna fedha za kujenga hiyo barababara zilizotengwa. Sasa sijui nimkimbilie nani? Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, alizungumzia barabara za mipakani ambazo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Mkaoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara inayotoka Kibande kwenda Nyamgali kwenda Munyama kwenda Kilelema na upande wa pili inakwenda Mugera na ile barabara inaweza kutoka pale ikaenda mpaka Makele sehemu ya pili. Mimi naomba barabara hizo zijengwe lakini zifanyiwe kazi ambayo ni nzuri na kisha tuweze

kuishukuru Serikali yetu, maana Serikali yetu sasa ni makini na sasa ni Serikali sikivu na Serikali inayoelewa mambo yanavyokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumze neno moja linalohusu Wahandisi wetu wa Barabara, *TANROADS*. Mwenzangu jana alizungumza habari ya *TANROADS*, akaonyesha wasiwasi namna gani Mkurugenzi Mkuu wa *TANROADS* alivyaoajiriwa. Hayupo katika orodha ya watu waliochaguliwa kushika nafasi ile, lakini alivyochukuliwa haifahamiki lakini akachukuliwa na wale watu watatu wakawekwa pembeni. Akaambiwa awape kazi, akaona hao asiwaweke kwake, akawarudisha Wizarani. Alipowarudisha Wizarani, Wizara ikasema hapana, hao ni wa kwake awatafutie Mikoa, akakuta nafasi za Mikoani amekwishazijaza, akaona ahaa, hao wasubiri tu tutawatafutia nafasi. Toka mwaka jana mwezi Agosti, mpaka leo wanalipwa zaidi ya milioni mbili hawafanyi kazi, ma-*Engineer* watatu. Yupo Nyiti, Chacha na mwingine anaitwa Ndyamukama, wote hao ni ma-*Engineer* wazuri tu katika Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkurugenzi huyu alipoajiriwa yeye kwenye *CV* yake imeonyesha kwamba yeye ni *Purchasing Consultant*, hana *Degree* ya *Engineering*, amesoma *Purchasing* na amesoma *Construction Economics* na alipoingia pale kupewa hii kazi, haijulikani alivyopewa hii kazi ni usanii ulifanyika akapewa kazi hii. Mshahara wake ni *dollar* 8,500 takriban milioni kumi na zaidi. Analipwa *pension allowance monthly* ya *dollar* 850 ambazo ni zaidi ya shilingi milioni moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, anapoingia kazini anapewa *Commencement Allowance* ya *dollar* kama 10,000 hivi. Analipwa *dollar* 400 (*cost of medical expenses monthly*), analipwa *Housing Allowance* ya *dollar* 2,200 na marupurupu mengine anapewa. Mwisho wa mwaka analipwa *dollar* 102,000 inayoitwa *Annual Performance Bonus*, huyo ni mtanzania ameajiriwa kama *expatriate*, misingi iko wapi, siyo *Engineer* anawa-frustrate wengine ndani ya *TANROADS*, walichunguze hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni la kuangalia vizuri sana na sasa anaanzisha utaratibu wa kuweka mikataba kwamba wafanyakazi wa *TANROADS*, wawekwe kwenye mikataba. Lakini kiini kikubwa ni kwamba anataka wale asiowataka kila baada ya mwaka awafukuze kazi. Maana watapewa mwaka mmoja, sasa wao wanasema hawataki hilo.

Mheshimiwa Waziri, ninataka majibu juu ya suala hilo. Aliajiriwaje huyo bwana aliyewadhalilisha Watanzania wenzake, wenye uwezo, wenye nguvu na waliosomea hizo kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha ajabu zaidi anawaonea wafanyakazi wenzake. Yupo mfanyakazi mmoja alikuwa anafanya kazi pale Kibaha alikamata malori, yale malori yakalipishwa shilingi 18 milioni lakini yote yalikuwa yamebeba zaidi ya tani 70 na nyaraka zipo. Kesho yake aliandikiwa barua haraka haraka baada ya kuona siku inapita yule bwana hajatoka akapiga simu kwa *Manager* wa yule jamaa, mbona hajaondoka, nataka aondoke, kwa kuipatia Serikali mapato?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja, na ninaomba maswali yote niliyouliza yajibiwe na Mheshimiwa Waziri na maelezo sahihi yaletwe hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Mariam Mfaki ajiande na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda ajiandae na nafikiri Mheshimiwa Athuman Janguo pia ajiandae na Mheshimiwa Godfrey Zambi ajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.

Awali ya yote, napenda kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, kwa maandalizi mazuri sana ya hotuba yao ya bajeti ambayo yameweza kuonyesha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, inayoonyesha waziwazi sera za Chama zinavyosema, utekelezaji wake na vile vile tunakwenda wapi, tukiwa na maana kwamba tunataka kufanya nini katika kipindi hiki cha mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda pia niipongeze Serikali kwa kusaini ule mkataba wa matengenezo ya kipande cha barabara kilomita 60 kuanzia Ndunu hadi Somanga na vile vile imeweza kutenga shilingi bilioni 12.5 kwa ajili ya matengenezo ya kipande hiki cha barabara, hongera sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hii barabara ilikuwa ni kero kubwa sana kwa wakazi wa Kusini na ilikuwa ni chanzo kikubwa sana cha kurudisha nyuma uchumi wa maeneo hayo na hata uchumi wa Taifa kwa ujumla. Ni mategemeo yangu kwamba kwa kweli pamoja na kwamba Serikali imeshatenga fedha na imesaini mkataba sasa itazingatia kwamba matengenezo ya barabara hii yaanze mapema iwezekanavyo ili kuepuka ile adha ambayo wananchi wamekuwa wakiipata ya kulala kwenye lile pori nene kabisa la Mhoro. Nadhani Serikali italicizingatia hili na kulifanya kazi mapema iwezekanavyo kwa sababu hakuna kisingizio.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa nianze kutoa mchango wangu kwa usemi mmoja unaosema kwamba ‘la mgambo likilia kuna jambo’, nadhani sote tunaufahamu. Kutokana na usemi huu, nataka niwaombe watendaji wote wa Serikali wajue kwamba Wabunge tunapouliza maswali hapa Bungeni si kwamba tunajifurahisha, tunauliza maswali haya tukitaka masuala yote ya msingi yatafutiwe ufumbuzi na hivyo naomba hii iwe ni fursa kwao kutafuta maeneo yote yenye udhaifu yanayohusiana na lile swalii na wayatafutie ufumbuzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie sasa kuhusiana na suala moja ambalo amelizungumzia pia Mheshimiwa Mporegomyi linalohusiana na tozo ya barabara katika vituo vya mizani. Kwa kweli kumekuwepo na malalamiko mengi siku nyingi na malalamiko haya ndiyo ambayo yalinipelekea mimi kuuliza swali linalohusiana na eneo ya tozo ya barabara katika vituo vya mizani mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili swali mimi nilitaka kujua ni *percent* gani ya magari makubwa ambayo yanalipia hii tozo ya barabara kama faini na pia nilitaka kujua kwamba wale ambao wanakwepa hii tozo, wakati mwingine kama abiria wanapoteremshwa ili wavuke kwa mguu kila kituo je, Serikali ina msimamo gani kuhusiana na hili? Kwa kweli, sikuweza kupata majibu yanayoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado mpaka sasa malalamiko yamekuwa ni mengi, ni mengi na hili suala bado halijatafutiwa ufumbuzi, sijui kama kweli kuna lolote ambalo limeshafanyika tangu nimeuliza hili swali mwaka 2006, nadhani Serikali itanipatia majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko makubwa kwamba abiria wa mabasi wanapokaribia vile vituo vya mizani vya kupimia, hata kama basi halijajaza, abiria wamekaa kwenye siti zao, hakuna aliyesimama, lakini baadhi huteremshwa na kuvushwa wanaambiwa watangulie mbele ili kusudi gari liweze kupita pale, wakati mwingine wanapandishwa kwenye daladala zinawavusha. Wakati mwingine wanadhalilishwa kwa kuambiwa watoke siti za nyuma ili waweze kukaa kwenye ngazi za mlango wa gari. Kwa kweli huu ni unyanyasaji na udhalilishaji. Abiria wale ambao wanakuwa wakibaki ndani ya gari, huwa wanashuhudia vitendo ambavyo vinaashiria rushwa kwa sababu huwa wanaona wakati mwingine kuna malipo ambayo yanatolewa kwenye hivi vituo vya mizani bila kufuata utaratibu kitu ambacho ni kiashiria kikubwa cha rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko pia kwamba abiria huwa wanatozwa kiasi kikubwa sana kwa vile vifurushi ambavyo wanakuwa wamebeba. Kibegi kidogo tu labda cha nguo, kinatozwa gharama kubwa na hawa makondakta wanadai kwamba kuna gharama nyingi sana ambazo huwa wanazilipa pale kwenye kituo cha mizani. Kwa kweli, naomba sana Serikali iendelee kulifuatilia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala pia ya malori. Malori pia hata yawe yamezidisha uzito au hayakuzidisha uzito lazima waache kitu kidogo kwenye vituo hivi vya mizani. Misingi yenye we ya kulipia pasipokuwa na utaratibu, ni kwamba wanapofika tu pale wanaanza kutishiwa. Gari linapogusa tu mzani wanaambiwa umezidisha kilo 2000 labda kilo 900 wakati dereva mwenyewe anajua kwamba kiasi alichobeba ni kile anachotakiwa kubeba na risiti za mzigo anakuwa nazo. Kwa hiyo, pale anatajiwa gharama ambazo ni kubwa na hawezu kuzilipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika ule ubishi ubishi, anaambiwa labda alipie nusu pengine ameambiwa laki mbili baadaye, anaambiwa sasa ili tukusaidie lipia laki moja au lipia shilingi elfu sitini ili uweze kupita. Akiendelea ubishi anaambiwa ashushe mzigo ili aupange upya. Sasa mtu ana tani labda 40 pengine magunia 400 ya nafaka, ni

ye ye na kondakta wake wayashushe wayapakie upya. Kweli ni udhalilishaji na hili wakati mwingine huwa linapelekea kulala kwenye vituo vya mizani pasipokuwa na sababu lakini ukija kufuatilia zaidi, kile kiasi ambacho wanaambiwa kwamba wamezidisha, si kweli. Ukifuatilia zaidi unakuta kwamba hakuna chochote kile kilichozidi. Atalipia ile fedha lakini kwa kweli si halali. Wakati mwingine wapo pia ambao wamejaribu kuomba wapewe risiti kwa kile ambacho wamekilipia na ile risiti ya kompyuta inaonyesha kwamba uzito ule ni pungufu ya kile kiasi ambacho kinahitajika/kinaruhusiwa. Kutokana na hayo, kuna dalili kubwa kwamba magari yote ambayo yanapita pale na yanapimwa huwa yanalipia visivyokuwa halali, ni machache sana ambayo yanalipia ilivyo halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa ambayo ameisoma Mheshimiwa Waziri kwamba Serikali imejitahidi kupunguza idadi ya magari ambayo yamekuwa yakizidisha uzito, kwa kweli mimi sikubaliani na hiyo taarifa labda angetuambia imepunguza idadi ya magari ambayo yanalipia faini kihalali, hapo ningekubali. Au angesema kuna ongezeko kubwa la idadi ya magari ambayo yanazidisha uzito na kulipa faini pasipokufuata utaratibu. Kwa kweli kutokana na manyanyaso ambayo wanayapata abiria na wanayoyapata wale ambao ni wahudumu wa magari makubwa, naomba baadhi ya wale wanaofanyakazi kwenye vile vituo vya mizani, kwa kweli wajisikie vibaya kwa kukiuka maadili ya kazi zao. Hawa ni watu ambao wameaminiwa, wamepewa dhamana na ninaomba wasijifanye kuwa vi-Mungu mtu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijaribu kuomba takwimu kutoka Wizarani kufuatia lile swalı langu la mwaka jana na bahati nzuri nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu alinipa ushirikiano mzuri sana. Takwimu nilizopipata ni kwamba magari 1,732,363 yamepimwa uzito kwa kipindi cha Julai 2007 hadi Mei 2008. Yaliyozidisha uzito na kulipa faini, ni magari 28,637 ambayo ni asilimia 1.65 tu. Kiasi cha fedha ambacho kimekusanya ni shilingi bilioni 2.2, huo ni wastani, haiingii akilini. Napenda nitoe mapendekezo kwa sababu mimi naona huu utaratibu unaotumika hapa ni sawa na kumuua nzi kwa kutumia risasi, hatuwezi tukawapata ni kazi ngumu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kama kweli Serikali itachunguza na kuona kwamba asilimia kubwa ya magari yanayopita yamezidisha uzito na kulipa kiasi cha fedha ambacho ni kinyume cha taratibu, ni vizuri ikaweka utaratibu ule wa kulipa *flat rate* kwa mfano magari yote makubwa yanayopita pale, yakilipa shilingi 20,000, Serikali inaweza ikakusanya shilingi bilioni 34.6 kwa kipindi hicho ambacho kimetajwa. Potelea mbali kwamba labda nusu yake tuseme mengine hayabebi mizigo yanakuwa labda ni matupu pengine yameenda bidhaa, labda nusu yake yakilipa tu hizo shilingi 20,000 Serikali inaweza ikapata shilingi bilioni 17.3. Nadhani kuna dalili kubwa kwamba Serikali inapoteza fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza pia pengine ni vizuri Serikali ikakaa na wadau hawa ili iweze kuona wafanye nini. Iangalie matatizo haya kwa undani zaidi na ipange kama ni kuamua kulipa hiyo *flat rate*, nadhani wanaweza wakaamua kulipa kiasi

kikubwa hata zaidi ya shilingi 20,000 kutokana na adha ambayo wananchi wengi wanaipata pasipo kuwa hata na msingi wa matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda unaniacha, ninaomba wakati wa kuhitimisha hoja, Mheshimiwa Waziri anipatie majibu kwa maswali yafuatayo:-

Kwamba barabara zetu zimetengenezwa kubeba uzito kiasi gani na kama pengine labda tani 20 au 30, ni vipi kwa yale magari ambayo unakuta yana tani 50 na hili gari limekuwa limepita kwenye *weigh bridge* na kuonekana kwamba halikuzidisha uzito wowote?

Swali lingine, ni kwa nini hizi *rates* za faini haziwekwi pale wazi kwenye vituo hivi vya *weigh bridge*.

Swali lingine ni kwamba hawa wafanyakazi wanaokuwepo pale kwenye hivi vituo, wanajua misingi hasa ya kutoza hizi faini, wanaelewa?

La mwisho, ninapenda kujua kama Serikali inaona kweli kuna tija kwa huu utaratibu ambao imeuweka. Kwa sababu nadhani hivi vituo vya mizani vimejengwa kwa gharama kubwa sana. Jana nimesikia kwamba ni vituo 29 katika Tanzania na vyote vimetumia gharama kubwa sana na wafanyakazi wale wanalipwa. Je, kuna tija yoyote kwa kukusanya shilingi bilioni 2.2 kwa mwaka na wanatarajia hizi pesa ambazo zinatumika kwa *ku-maintain* hivi vituo zinarudishwa vipi, kitu gani ambacho kitarudisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama muda bado unaniruhusu, naomba nizungumzie tu kidogo hizi bandari ambazo tumezisema kwamba zinafanyiwa ukarabati kwa madhumuni ya kukuza uchumi wa nchi yetu basi hii kazi ifanyike haraka na hasa ukizingatia ile bandari ya Mtwara ambayo inaweza ikasaidia kuwa kama ndiyo *supplement* ya Dar es Salaam kwa sababu inaweza ikawa ni chanzo kikubwa sana cha kukua kwa uchumi wa maeneo ya Kusini pamoja na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani niishie hapo na baada ya kusema hayo, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa mawazo yangu kuhusiana na Wizara hii ya Miundombinu.

Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima kwa siku ya leo mpaka tunaweza hata kuchangia hoja hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kijana wangu, Mheshimiwa Dr. Shukuru, Naibu Waziri, ndugu yangu, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje na watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa hii hotuba ambayo kwa kweli

imeonyesha kwa makini ni jinsi gani Wizara hii inavyotekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Naamini hata walioisikiliza, wameshaona kumbe suala la utekelezaji wa Serikali unaanzia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine niseme tu kwamba wenzetu, watani zetu Wapinzani, Waswahili wanasema, ‘usione vinaelea vimeundwa’. Kwa hiyo, hivi vyote vinavyoendelea kuonekana, vimeundwa na vimeundwa na Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndugu yetu Mheshimiwa Pinda, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na jinsi anavyoendesha nchi hii na Serikali yake na kwa kweli ameonyesha umahiri, uaminifu na uwezo wa hali ya juu sana. Mimi nimtakie kila la kheri na wala asije akarudi nyuma, aendelee na uzi huo huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuchangia hoja na nianze na ujenzi wa nyumba. Nimesoma hiki kitabu cha Miundombinu, katika ukurasa wa 70 na 71, wameweka utaratibu wa kujenga nyumba za watumishi wa Serikali pamoja na ofisi. Naomba tu labda niseme moja ambalo kwa kweli pengine halipo hapa kwenye hotuba hii lakini lilikuwepo kwenye hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu ujenzi na naamini Wizara hii ndiyo inayoshughulikia ujenzi kwa ujumla kama ilivyoelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Ofisi ya Waziri Mkuu Dar es Salaam, mimi nashindwa kuelewa, Ofisi ya Dodoma ya Waziri Mkuu bado sio nzuri na kwa kweli inahitaji mabadiliko, inahitaji kujengwa upya, kwa nini ikajengwe Ofisi ya Dar es Salaam ambayo ni nzuri badala ya kujenga ya Dodoma? Mimi niiombe tu Wizara na niiombe Serikali kwa ujumla kwamba kwanza wakaingalile ile Ofisi ya Dodoma ya Waziri Mkuu, waikague vizuri na waone ni wapi panastahili kujengwa sasa Ofisi ya Waziri Mkuu. Mimi naomba tu kwa kweli niseme kwamba badala ya kujenga Dar es Salaam naomba ijengwe Dodoma. Naomba nipate maelezo kwa nini wameamua kujenga Dar es Salaam wakati sasa hivi tuko kwenye mchakato wa kuifanya Makao Makuu ya Serikali kuendelea kuwepo Dodoma, hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, nimeona katika kitabu hiki cha hotuba kwamba wametenga viwanja vya kujenga nyumba za watumishi. Sasa naomba pengine niikumbushe Serikali pamoja na kwamba wametutengea maeneo fulani ya kujenga nyumba za watumishi lakini mimi niiombe Serikali kwamba ianze kufikiri kwamba Dodoma panahitajika nyumba ziongezeke. Kabla sijaihimiza Serikali, niwaombe tu wananchi wa Dodoma wajue kwamba utaratibu wa kujenga nyumba kwa ajili ya wageni na watu wengine wanaokuja Dodoma ni wajibu wao, wale wenye uwezo wajenge. Lakini niiombe Serikali vile vile badala ya kuendelea kujenga Dar es Salaam majengo mengi hebu wabadili mawazo sasa majengo haya yaje yajengwe Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu, naamini kwamba Waheshimiwa Wabunge mlioko humu na mnaoishi Dodoma kwa muda mrefu kidogo baadhi ya wengine hawana nyumba mnabaki mnahangaika. Sasa ni kwa nini Serikali ijenge nyumba nyingi za watumishi Dar es Salaam badala ya Dodoma na wala hapatakuwa na utata katika kubadili huo utaratibu wa kujenga nyumba za watumishi Dar es Salaam kujenga Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana mkafanye mabadiliko katika Ofisi yenu, katika nyumba nimehesabu kama viwanja vitano vinajengwa Dar es Salaam basi viwili mje muombe mjenge Dodoma ili watumishi na wananchi na watu wengine wanaohitaji nyumba Dodoma waweze kuishi humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la nyumba Dodoma, ni kubwa sana. Kwa hiyo, ndugu zangu watendaji wa Serikali, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, naamini hayo mabadiliko mtakwenda kuyafanya badala ya kujenga hizo nyumba zote tano Dar es Salaam basi mjenge mbili Dodoma, tatu Dar es Salaam. Niombe sana Serikali na kama hamtafanya hivyo basi mniambie kwa nini hamtaki kubadilisha huo utaratibu. Kuna sababu gani za msingi za kuweza kuendelea kujenga majengo mengi Dar es Salaam? Hilo nimeishia hapo, naomba niendelee na lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Dodoma- Iringa – Dodoma - Babati. Hii barabara sina uhakika ni nani ambaye hajui, ni nani ambaye hakuisoma kwenye historia, ni nani ambaye hana habari zake? Jambo la kushangaza barabara hii pamoja na kwamba ipo kwenye historia lakini bado inakuwa nyuma nyuma. Lakini hata hivyo, bado niishukuru Serikali kwamba imetenga kiasi cha fedha cha shilingi bilioni 12, sijui ni kuanza au kuendeleza upembuzi yakinifu. Mimi niombe sana Serikali, maadam imeshanza na madam imetenga fedha basi isije ikafika mahali tena barabara hii ikaachwa, mkaendelea na barabara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu kwamba itakapofikia sasa mnaanza kujenga, hebu mje muanzie hapa hapa kati ya mji kwa umuhimu wa mji huu. Mkandarasi mwingine aanzie Dodoma kwenda Iringa ambapo tayari imeshapata fedha, hii ya Dodoma/Iringa, basi waje waanze Dodoma kwenda Iringa na Mkandarasi mwingine akija kupatikana aanzie Dodoma kwenda Babati, maana siku za nyuma ilisemekana kwamba barabara hii ilishapata wafadhili, ilishapata fedha miaka ya nyuma huko, ikaanzia Arusha ikaishia Minjingu matokeo yake Dodoma huku haikujengwa, naiomba Wizara ifanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Serikali kutoa fedha za ujenzi wa barabara wakati mvua zinanyesha. Ni jambo la kusikitisha na kwa kweli ni

kama vile hujuma. Mvua zikinyesha fedha zinatumwa na Wakandarasi wanatafutwa wanaanza kujenga barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja katika kikao cha *RCC*, niliuliza hivi inakuwakuwaje kwamba sasa hivi mvua zinaendelea kunyesha, barabara zinatengenezwa, maana yake ni kwamba mvua zikiisha na barabara zimeisha. Kwa hiyo, niombe Serikali iweke utaratibu na iangalie majira ya Mkoa hadi Mkoa, ili iweze kupeleka fedha hizo za kutengeneza barabara kwa utaratibu mzuri na ili zitumike vizuri. Labda inadhaniwa kwamba kwa kuwa ni fedha za Serikali basi hata zikichukuliwa na mvua hakuna ambaye atahoji. Sasa naomba nihoji hilo, ni kwa nini Serikali inatoa fedha wakati mvua zinaendelea kunyesha na kutengeneza barabara ambazo zinachukuliwa na mvua?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na sehemu ya barabara hiyo hiyo kuhusiana na suala la barabara za Mikoa. Barabara za Mikoa kwa fedha zinazotolewa, hazitoshii kabisa. Utakuta kwa kweli Waheshimiwa Wabunge, wanalamika kwa sababu hazitoshii matokeo yake ni kwamba wanatengeneza sehemu korofi mwaka hadi mwaka, wakija kupata vihela kidogo wanaburuza tu huku pembedi matokeo yake sasa barabara zimekuwa finyu hata kama ni kupishana inakuwa taabu. Naomba sana suala hili la barabara liangaliwe vizuri na Serikali iongeze bajeti katika fedha za kutengeneza barabara za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie madaraja hasa kwenye barabara za Mikoa. Nina mfano mzuri tu wa daraja la kutoka barabara hii ya Kondoa kuitia Mondo, Busi kwenda mpaka Kolo na kuzunguka mpaka Kondoa. Kuna daraja la Pahi, Mkandarasi amepewa daraja lile kujenga, anajenga daraja kwa kutumia nondo hizi sijui milimita 12, ndio ndogo zaidi na daraja lenyewe lina urefu labda wa mita 150, 200, hivi kweli ukitengeneza hivyo maana yake ni nini? Ndiyo mapatano kweli na Serikali kutumia milimita 12 kutengeneza daraja, hii ni hujuma. Kwa hiyo mimi naomba sana Wahandisi wa Mikoa, naamini wako juu hapo wanatusikiliza na hasa wa Dodoma, aone kwamba hilo suala sio jema na Mheshimiwa Waziri hilo suala uliangalie na kwa kweli kuna haja ya kufuatalia kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ninachotaka kusema hapa, ni suala la uaminifu. Mimi naamini Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, hawa ni vijana wa wakulima na naamini ni waaminifu na bahati mbaya upimaji wa hizi fedha zinapokwenda kufanya kazi huwezi kuzipima, ni ngumu sana. Magreda yale mimi nikiyaona yakismama barabarani, yakianza kulima barabara, naona yanatumia fedha nyingi sana. Lakini niombe sana basi angalizo hilo kwamba kuwe na uaminifu, mimi sijapata kusikia hata siku moja fedha zimebaki katika kutengeneza barabara, hata siku moja haitawenza kutokea. Lakini basi angalau zikiisha barabara iwe imeshalimwa vizuri na hata wananchi wanaopita pale wajue huyu Mkandarasi aliyepewa hii barabara

amefanya kazi nzuri. Si kana kwamba wananchi hawaoni, wanaona na ndiyo wanaotufikishia sisi wawakilishi wao malalamiko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la fedha zilizotolewa kuhusu ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Msalato. Naomba kama ni kwa ajili ya kuwalipa kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Bura, mmeandika kwamba ni za kuwalipa wananchi ambao watakuwa wameathirika na ujenzi huo. Naomba kabisa zoezi hili lifanyike kwa uangalifu na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika hotuba ya Wizara ya Miundombinu.

Kwanza kabisa, nianze kwa kumpungeza sana Waziri, Mheshimiwa Dr. Kawambwa, Naibu wake, Mheshimiwa Chibulunje, Katibu Mkuu wake, Ndugu Chambo, Naibu Katibu Mkuu, Mama Mapunjo na wataalamu wote. Nianze haraka kusema kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri wa Miundombinu, ni nzuri sana. Ni hotuba ambayo imegusia maeneo hata yale ya pembezoni. Hatuwezi kumaliza maeneo yote lakini inafurahisha kwamba maeneo yale ya pembezoni kama Lindi, Mtwara, Mbambabay, Kigoma, Sumbawanga yamegusiwa katika hotuba hii.

Sasa nadhani changamoto kubwa sasa ni utekelezaji, hotuba nzuri, changamoto ni utekelezaji. Lakini katika utekelezaji huo lazima iandamane na kujali muda, ucharaka wa maamuzi pamoja na tathmini ya matokeo kutokana na fedha zitakazotumika maana ni *value for money*. Hili ni muhimu kwa sababu rasilimali, ni chache na miradi ya barabara mara nyingi ina gharama kubwa sana. Sasa hili ni la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba katika hotuba hii, barabara ya Tanga – Horohoro, imepewa umuhimu. Lakini nilitaka kusisitiza kwamba Mheshimiwa Waziri wakati wa utekelezaji wa barabara ya Tanga – Horohoro, lazima uende sambamba na uboreshaji wa bandari ya Tanga. Hili ni angalizo muhimu sana kwa sababu kila kitu kina pande mbili. Tutakapotengeneza barabara ya Tanga – Horohoro, kwa kiwango kizuri, tukasahau bandari ya Tanga, inawezekana kabisa ile ikawa ni *outlet* ya mizigo kutoka Tanga na sehemu zingine za Tanzania kwenda bandari ya Mombasa. Kwa hiyo, tutakuwa tunatengenezea mapato wenzetu badala ya kujitengenezea sisi wenywewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Bagamoyo – Saadani – Tanga, inabidi ipewe umuhimu wake.

Tumefurahi sasa kivuko cha Pangani kimetengewa programu maalum lakini vile vile hotuba imeonyesha umuhimu wa kufufua reli ya Tanga hadi Moshi na vile vile bandari yenyewe ya Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), una vipengele vitatu. Kwanza, ni kukuza uchumi, pili kuendeleza huduma za jamii na tatu ni suala zima la utawala bora. Sasa napenda kusema hapa kwamba kwa sisi watu wa Jimbo la Handeni, mchangano mkubwa katika kutuwezesha kuendelea na mikakati hiyo kwa nguvu zaidi, ni kufungua barabara zetu. Kwa hiyo, naomba sana programu zilizoanza katika kipindi cha mwaka wa jana kuhusu barabara ya Mkata - Handeni, barabara ya Korogwe - Handeni kuelekea Dumila, programu zile ziwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile nashukuru sana Wizara kwamba imeona umuhimu wa kuendelea na mradi ule wa *PMMR*. Sasa nina hakika kwamba kitu kitakachoangaliwa hapa ni utangazaji mzuri wa zabuni, lakini vile vile la msingi litakuwa ni uchaguzi mzuri wa Mkandarasi ili kazi itakayofanyika pale iwe na tija kwa Jimbo letu la Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tunapozungumzia barabara za kufunguliwa, tunasahau sana kipande hiki cha katikati kuanzia Korogwe hadi Morogoro, Korogwe hadi Kilosa lakini vile kuanzia Korogwe hadi Kiteto na hatimaye Dodoma. Nina hakika kabisa mipango kama itawekwa sawa sawa ya kuendeleza ujenzi wa barabara ya Korogwe - Handeni – Mziha –Mikumi –Kilosa, itafungua eneo ambalo lina uwezo mkubwa sana wa kuongezea mapato nchi yetu. Haya ni maeneo ya kilimo. Lakini hata eneo la Handeni – Kibirashi - Songea na Chakwale, ni eneo sasa hivi ambalo lina *potential* kubwa sana kwa upande wa madini, mazao ya mbao na vile vile mazao ya chakula. Sasa haya ni maeneo ambayo nadhani katika mipango yetu tuiangalie kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barabara hii ambayo tayari iko katika utaratibu wa kufanyiwa upembuzi yakinifu na imeelezwa vizuri katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lazima ichukuliwe kwamba ni barabara *strategic* kwa maana ya kuunganisha Ukanda wa Kati (*Central Corridor*) na ukanda wa Tanga kama ilivyoelezwa kwenye hotuba yake. Hii itapunguza sana gharama zinazopatikana kati ya mawasiliano ya maeneo ya Mikoa ya Kaskazini, Mashariki pamoja na Mikoa ya Kati na ile ya Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema ni kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri ilikuwa ni nzuri, tunaomba miradi ambayo imegusiwa katika Wilaya ya Handeni iwe ni endelevu, itekelezwe lakini la msingi Wizara ijali muda, iangalie *value for money* na vile vile ijifunze kutohana na makosa ambayo yamejitokeza hapo nyuma ya kuchagua

Mkandarasi halafu baada ya muda Mkandarasi yule hamalizi ile kazi, anatafutwa Mkandarasi mwingine, hiyo itakuwa ni gharama kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mawazo ya Waheshimiwa Wabunge wengine waliosema kwa barabara hizi ndefu si vibaya kuangalia utaratibu wa kuweka Mkandarasi zaidi ya mmoja ili kuweza kumaliza ujenzi wa barabara hizi kwa wakati na hapo hapo kupunguza gharama za Taifa katika sekta hii ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzoni, naunga mkono hoja hii. Namwombea Waziri, tija nzuri ya kuhakikisha kwamba hotuba yake hii nzuri ambayo kwa sasa tunasema ni nadharia, kiutendaji iwe *reflective* hivyo hivyo. Naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi ili na mimi nichangie katika hoja hii ya Miundombinu.

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi na uwezo wa kuja kusimama hapa ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na kumpongeza sana ndugu yangu, Mheshimiwa Dr. Kawambwa, Naibu wake, Mheshimiwa Chibulunje, Katibu Mkuu na watendaji wao wote kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa hotuba hii ambayo kwa kweli inarutubisha Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Imechambua utekelezaji hatua kwa hatua na kuonyesha malengo tunakwenda wapi, nasema hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utalenga katika maeneo matatu. Kwanza mgao wa Mfuko wa Barabara na hasa barabara za Vijijini. Pili, hali ya barabara za Wilaya ya Kisarawe na mwisho nkipata nafasi nitazungumzia umuhimu wa kuboresha usafirishaji kwenda nchi za jirani kwa maana ya bandari zetu kubwa. Tatu, barabara na reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na Mfuko wa Barabara, kwa mujibu wa Sheria iliyounda Mfuko huu ya mwaka 1985 na marekebisho yake ya 1998 na 2006, Mfuko huu umepangwa ugawiwe asilimia 70 kwa barabara kuu na asilimia 30 barabara za vijijini. Nasema kwa wakati ule hii ilikuwa sahihi, lakini sasa nadhani kuna haja ya kufanya mabadiliko ili kupeleka uzito vile vile katika barabara za vijijini, angalau zifikie asilimia 40 ya mapato yanayopatikana katika mfuko huu. Nina sababu zifuatazo:-

Moja, ni kwamba kama nilivyosema, miaka ile ya nyuma hali ya barabara zetu kuu ilikuwa mbaya sana lakini tunaipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya, imeziboresha sasa hivi tunataja tu maeneo fulani fulayo bado hajafikiwa.

Pili, barabara kuu zina nafasi za kuwavutia wawekezaji hata binafsi na wawekezaji kutoka nje, taasisi za kimataifa na wahisani wa nchi mbalimbali.

Tatu, barabara hizo zinaweza kuvutia wawekezaji kwa maana ya (BOT) Jenga, Tekeleza na Jilipe.

Nne, barabara za vijijini ni nyingi kwa hiyo kiwango ambacho sasa hivi tunachopewa kimekuwa kama tone katika bahari.

Tano, Halmashauri ambazo ndizo zenyenye jukumu la kujenga barabara hizi za vijijini uwezo wao kifedha ni mdogo mno.

Mwisho, kama ilivyoonyeshwa katika Ibara ya 99 kwamba mfuko huu unakua haraka sana. Kwa hiyo basi jinsi unavyokua vile vile na mgao wa kupeleka kwenye barabara za vijijini, ungeonyesha kwamba unakua ili tuweze kumudu matatizo ya barabara hizi ambazo ndizo zinazokusanya na kuweza ku-feed barabara hizi kuu tunazozungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya barabara za Wilaya ya Kisarawe ni mbaya sana. Nimezipigia kelele mara nyingi, lakini inaonekana kana kwamba tunapozungumza maeneo ya pembezoni, hapa ningependa kutofautiana kidogo na ndugu yangu Mheshimiwa Zainab Vulu, anayeshangaa kwamba inakuwaje Mkoo wa Pwani unaitwa wa pembezoni. Unaitwa wa pembezoni kiuchumi, sio kijiografia. Uko karibu na Dar es Salaam, lakini kiuchumi uko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kisarawe nadhani katika Wilaya saba za Mkoo wa Pwani pengine inaweza ikawa inashika mkia katika suala hili. Kwa hiyo basi, kuna haja ya kuhakikisha kwamba barabara hizi tunaziboresha. Barabara za vijijini tunazo nyingi na kama mfuko huu tutakuwa tumeuungeza na Kisarawe ikapatiwa sehemu yake, barabara za maeneo mbalimbali kama vile kutoka Kisarawe yenyewe kwenda Mzenga, kutoka Mzenga kwenda Mafizi kuititia Gwata, mpaka Dororo ambako hakupitiki kabisa, zinaweza kupata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambayo ameshaitaja hapa Mheshimiwa Vulu, nadhani nikusemee Mheshimiwa Waziri kwa sababu huwezi kujisemea mwenyewe,

ambayo inatoka Bagamoyo kupitia Makofia/Mlandizi/Mzenga hadi Maneromango, ilipata msaada wa *Danish Aid*, lakini baada ya Mfuko ule kwisha, barabara hii, hasa sehemu ya kutoka Mzenga kwenda Maneromango, ni mbaya wakati wa mvua inapitika kwa shida.

Barabara ya kutoka Vikumburu kujiunganisha na kule Rufiji kwa ndugu yangu Profesa Mtulia tunaipigia kelele kila wakati kwa kweli, sio barabara! Haipitiki! Kwa bahati nzuri, Mheshimiwa Waziri ulikuwa katika msafara wa Mheshimiwa Rais mwaka jana alipotembelea Wilaya ya Kisarawe na umepata ushahidi kwamba wananchi wa Kisarawe mambo mawili waliyopigia kilele, moja ilikuwa sekta yako ya zamani ya maji na ya pili barabara. Ahadi zimetolewa na mimi naamini wewe kutoka kwenye sekta ya maji kuingia kwenye barabara umefika mahali ambapo sasa zile ahadi unawenza ukazitekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara za Mkoa kuu mbili; ya Kisarawe - Pugu mpaka Vikumbulu. Naona hapa katika ibara ya nane kumetajwa barabara ambazo Serikali imezikamilisha kwa lami kilomita sita! Nafikiri Mheshimiwa Waziri ameshauriwa vibaya. Ingekuwa ni mimi nisingeingiza mle. Wakati kuna barabara ambazo zimetengenezwa za kilomita 200 halafu unatia na barabara ya kilomita sita tena baada ya mimi kuipigia kelele tangu mwaka 1996 mpaka mwaka 2001, ndiyo barabara inaanza kujengwa, hizo kilomita sita kwenye barabara yenyе urefu wa kilomita 105 sio kitu.

Mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri itabidi sana alifikirie hili na barabara hii kwa bahati hii ulifika wakati ijengwe kwa mpango wa *ORET* ambao ni ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Uholanzi. Kwa bahati mbaya haikujengwa kwa sababu Tanzania ilishindwa kutoa mchango wake wakati Waholanzu walikuwa tayari kutoa mchango wao na pili mkandarasi vilevile ambaye alikuwa ameandalowiwa kwa barabara hii alionekana kwamba ni feki.

Namwomba Mheshimiwa Waziri arudi nyuma, aangalie namna gani barabara ya Pugu kwenda Vikumburu inaweza kuendelezwa kwa lami badala ya kila wakati tunasifia kilomita sita kwa muda wa miaka karibu mitano sasa tunasifia barabara hiyo hiyo. Kilomita sita mimi kwa kweli nadhani sio lolote wala sio chochote. Barabara ya Mzenga kwenda Maneromango nimeitaja na kwa kuwa ni ya Mkoa na ambayo inaunganisha Wilaya karibu nne, Bagamoyo, Kibaha, Kisarawe unakwenda hadi Rufiji kweli ni barabara muhimu ambayo inaunganisha maeneo mengi, kwa kweli ingepewa umuhimu unaostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda unayoyoma na napenda sasa nizungumzie suala la usafirishaji kwenda nchi za jirani. Kama walivyosema wazungumzaji wenzangu na mara nyingi tumezungumza, ni kwamba nchi hii inaweza ikapata mapato makubwa sana na kuongeza uchumi kwa kupata fedha za kigeni kwa kusafirisha mizigo inayopitia Bandari za Dar es Salaam, Tanga na ingawa Mtwara haiendi sasa hivi, lakini tukiziboresha tunaweza tukapata fedha nyingi sana.

Wakati mmoja nilipokuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bandari, Marehemu Mwalimu Nyerere alituita mimi na aliyejewa Waziri wa Mawasiliano, akasema nchi hii kuna maeneo mawili tu ambayo yanaweza yakatuvusha sana. Nayo ni utalii na matumizi ya Bandari zetu kwa sababu tuna nchi sita ambazo zinategemea sana Bandari ya Dar es Salaam. Lakini kwa bahati mbaya kuna matatizo ya msongamano ambao unatokana na sababu mbalimbali. Moja uwezo wa usafirishaji wa nchi kavu kwa maana ya barabara na reli ni mbovu na hautoshi. Pili, ni urasimu ambao upo katika taasisi zetu wenyewe. Mfano ule ambao umeelezwa sana na wenzetu wa Kusini.

*TRA* wanaona taabu kupeleka maofisa kule Mtwara ili kusudi Bandari ya Mtwara iweze kutumika. Huo ni urasimu. Wasafirishaji ambao wanatumia *Clearing and Forwarding Agencies* vilevile wamekuwa wengi hawajafanya kazi kwa kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya ushuru wa forodha kuwaweka *ma-agent* ambao ndio watakaofanya kazi ya kusimamia hili badala ya forodha yenyewe, mimi nadhani tumeweka urasimu usiokuwa na msingi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia kwamba Bandari ya Dar es Salaam iweze kuongezewa uwezo kwa maana ya kuhakikisha kwamba tuna watendaji wazuri. Hapa lazima niseme kwamba ule mkataba wa *TICS* uangaliwe upya, hasa ile sehemu ya nyongeza ikiwezekana ifutwe na zitangazwe *tender* ili wapatikane wengine watakaoweza kufanya pamoja na hawa *TICS* ili walete ushindani.

Nikizungumzia Bandari ya Tanga, matatizo yake kwa kweli makubwa ni matatu. Moja, ni kwa sababu ya kina kifupi. Kwa hiyo, meli hizifikasi pale kwenye gati; mbili, ni kwa sababu hakuna shehena ya kutosha na tatu ni usafiri mbovu wa reli ambao wakati mwingine inakuwa imefungwa kabisa. Kwa haraka haraka niseme tu kwamba Bandari ya Tanga inaweza ikawa na nafasi kubwa sana, kwa sababu suala la shehena ndogo ukiweza kujenga Bandari ukaiimarisha na hasa kwa kuihamisha kutoka pale ilipo ukaipeleka katika *site* ya mwambani ambako kuna kina kirefu, Bandari ile inaweza ikafanya kazi vizuri sana. Tukijenga reli kutoka pale Mwambani, ukaiunganisha na ya sasa na ukaiimarisha hadi Arusha halifu ukajenga mpaka Ziwa Victoria, utakuwa umeshatatua tatizo la mizigo kutoka Uganda, Burundi, Rwanda na Congo, itakuwa inaweza kupitia kule. Kwa hiyo, yakifanyika haya ninaamini kabisa Bandari ile itakuwa inafanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Mtwara ndiyo yenyе kina kirefu kuliko nyingine zote tatu lakini kwa bahati mbaya ni kwamba hakuna usafiri wa kuaminika wa nchi kavu, kuunganisha bandari ile na sehemu iliyobaki ya Tanzania Kusini na nchi za jirani kama vile Malawi.

Lakini pia kuna tatizo la tuta lile. Lile tuta ni jambo, dogo sana unaleta *dragging equipment una-drag* lile tuta meli zinaingia mpaka pale. Lakini pana haja vilevile ya kuongeza ukubwa wa ile bandari kwa maana ya kuweka magati zaidi ili meli zaidi ya mbili au tatu ziweze kufunga gatini kwa wakati mmoja. Kwa maana hiyo, tukiweza kuyafanya hayo, ninaamini kabisa bandari zetu zitawenza zikazalisha vizuri sana na

zikatuletea tija kubwa sana kwa mapato ya fedha za kigeni na kuondoa tatizo la msongamano na kuhakikisha uchumi unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, staki kengele nyingine inigongee, ninaamini kabisa kwamba Serikali imesikia na watayaangalia haya masuala kama nilivoyapanga, Mfuko wa Barabara, barabara mbaya za Wilaya ya Kisarawe na bandari zetu pomoja na kuimarishe reli na kuongeza barabara. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi bila shaka niwe msemaji wa mwisho kwa mchana wa leo. Lakini kabla sijaendelea, naomba niseme tu kwamba mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Bunge inayosimamia Sekta ya Miundombinu na kwa maana hiyo, maoni ambayo yalisomwa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Mohamed Missanga na mimi nakubaliana nayo kabisa. Hata hivyo, nina maeneo machache ambayo nafikiri ninaweza nikatoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, tuna kazi kubwa sana ya kufanya hususan kwenye sekta ya miundombinu. Kwa sababu sekta ya miundombinu ndiyo inayobeba uchumi wa nchi, kama hatuwezi kuwa na miundombinu mizuri, kwa vyovoyote vile, shughuli zetu za kiuchumi zitakuwa haziwezi kwenda vizuri hata kidogo. Ndiyo sababu tunakuja hapa tunazungumza habari za ujisadi na mimi naomba niwaombe wenzangu wote bila kujali itikadi ya vyama kwamba tupige vita ujisadi na hii iwe ajenda ya kudumu kwetu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa zinazopotea kwa njia za ujisadi ni mabilioni ya hela. Wote ni mashahidi humu ndani, *billions of money* zinapotea kwa njia za ujisadi. Sasa Watanzania watatuelewaje Wabunge tusipozungumza masuala ya ujisadi na Wabunge wenye we tukajichanganya tukasema tusizungumze habari za ujisadi wakati hela zinapotea nyingi kwenye maeneo ambayo hayawaleti wananchi wote maendeleo. Lakini sisi wa CCM Ilani imeandika kabisa kwamba lazima tupige vita rushwa na kwa maana hiyo na vitendo vyote vinavyofanana na rushwa. Sasa mimi nitashangaa sana kama tunasema kwanini tunaleta ajenda ya ujisadi ndani ya Bunge? Ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimewasikiliza wapinzani, sio Wabunge wapinzani humu ndani, lakini hata huko nje. Kuna Mwenyekiti mmoja wa Chama cha CUF kule Mbeya nimemsikia akizungumza kwenye Mikutano ya hadhara anasema lazima tutumie matatizo yaliyo ndani ya Serikali, sasa, ndani ya Chama cha Mapinduzi wanavyogongana kuzungumzia habari za ujisadi ili mwaka 2010 tuwachafue zaidi kwa wananchi. Ndiyo ajenda yao. Kwa hiyo, mimi nataka kusema kwamba sisi tuongoze mapambano haya ya Ujisadi bila kuogopa hata kidogo. Kwa maana hiyo, wote wanaotuhumiwa na ujisadi mimi nadhani Sheria zipo na Sheria hizo zichukue mkondo wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Mheshimiwa Rais amewahi kuzungumza na ni kibwagizo sasa kwenye moja ya matangazo kwenye Televisheni na Redio. Anasema wananchi hawakatai watu kuwa matajiri, lakini wananchi wanachoshangaa ni mtu anapoingia madarakani leo hana na kitu, lakini kesho amekuwa tajiri. Mheshimiwa Rais, anasema haya ndiyo wanayohoji wananchi. Sasa kama Mkuu wetu wa nchi anazungumza haya, kwanini sisi Wabunge tusimuunge mkono Rais wetu? Lazima tumuunge mkono! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya *preamble*, naomba nizungumze matatizo ya barabara kule Jimboni kwangu. Kuna barabara ya Mlowo - Kamsamba ipo kwenye kitabu ambacho Mheshimiwa Waziri amesoma kwenye hotuba yake ukurasa 128. Barabara hii imetengewa hela tangu mwaka wa fedha ulioisha, lakini kazi zilizoendelea bado haziridhishi. Barabara hiyo imegawanywa kwenye vipande vitano. Bado vipande viwili havijapata wakandarasi. Vipande hivyo ni Mlowo – Halungu takribani urefu wa kilomita 30, lakini pia kutoka sehemu ya Itumbula mpaka Kamsamba kwa sababu ni barabara moja yenye urefu wa kilomita karibu 130.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vipande viwili hivyo bado havijapata wakandarasi na hata vipande ambavyo vimepata wakandarasi bado *speed* ya ujenzi hairidhishi. Sasa mimi naogopa kwa sababu pesa zilizotengwa zilikuwa takribani shilingi bilioni 1.8 na vitu vinapanda bei, *variations* zitakuwa kubwa na baadaye tutasema kwamba barabara imeshindikana kwa sababu ya vitu kupanda bei.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri alisimamie hilo na ahakikishe kwamba barabara hiyo inajengwa vizuri. Lakini pia tuzingatie ubora. Barabara hiyo katika Wilaya ya Mbozi ndiyo msingi mkubwa sana kiuchumi ukiondoa barabara ya Iyai- Tunduma kwa maana ya kutoka Dar es Salaam - Tunduma kwa sababu barabara hii pia inakata pia Wilaya ya Mbozi. Lakini kwa barabara za Wilaya ya Mbozi, barabara ya Mlowo – Kamsamba ni ya muhimu sana kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ubora wake inapojengwa, naomba sana uzingatiwe kwa sababu sehemu zilizolimwa bado wanaweka matope, wanaweka kifusi ambacho mvua zikija bado barabara hii haitakuwa na ubora wa kuhimili mvua zinazonyesha na kwa maana hiyo, tutakuwa tumepoteza pesa nyingi sana. Barabara hii inapanuliwa vizuri, lakini ubora wake bado unaweza kuendelea kuwa ni tatizo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake wa *TANROAD* wafuatilie suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna barabara sehemu nyingine barabara hii iko pia kwenye kitabu hiki ambacho Mheshimiwa Waziri amekisoma ukurasa wa 128, kuna barabara ya Zelezeta –Magamba – Itaka. Barabara hiyo haijakamilika. Meneja wa *TANROAD* wa Mkoa wa Mbeya anajua nadhani bila shaka hata uongozi wa *TANROAD* Makao Makao wanajua kwamba kuna kipande ambacho hakijakamilika kuanzia sehemu inayoitwa Magamba mpaka Iporoto takribani kilomita kumi. Kipande hicho hakijalimwa kabisa lakini.

Sasa naomba hili Mheshimiwa Waziri anihakikishie pamoja na kipande kingine kiko eneo hilo hilo nililotaja kwenye kitabu. Barabara ya Msangano - Utambalila au Utambalila - Msangano, hakuna barabara. Hilo suala tumeshawahi kulizungumza, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari amewahi kulijibu suala hilo akasema tulipeleke kwenye *TANROAD* kule Mkoani, kwenye *Road Board* tumeshalizungumza, lakini sasa tunataka Wizara ichukue jukumu kuhakikisha kwamba maeneo haya ambayo yanaonekana yapo kwenye barabara zilizokamilika na hayajakamilika sasa yakamiliishwe.

Mimi nisingependa kwa kweli nije nisimame kwenye vifungu na ukizingatia kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati na Waziri tuna uhusiano naye vizuri, hakuna matatizo. Kwa hiyo, naomba tu atakapokuwa ana-*wind-up* anijulishe ni lini maeneo hayo ambayo hayajakamiliishwa yatatengewa fedha ili barabara ziweze kukamiliika kama yanavyoonekana kwenye vitabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie kwa ufupi sana eneo la barabara kuu ya Iyai -Tunduma. Eneo la Songwe barabara hii inajengwa kila mwaka na tangu imejengwa imekamiliika haijapita miaka miwili, mitatu, lakini barabara sehemu hiyo imebomoka yote. Ukienda tena kwenye vitabu ukurasa wa 138, barabara hii imetengewa shilingi milioni 960 kwa kukarabati kilometra 1.8 na barabara hii imetoka kukamiliika sio muda mrefu na imetumia *billions of money*, leo inatengewaa shilingi milioni 960 ili iweze kukarabatiwa jambo ambalo ni zuri, lakini wajenzi wake wanakuwa wabovu. Hivi *liability period* inasema nini? Mimi ninahisi *liability period* hata inakuwa haijaisha barabara imeshaharibika na bado tunatenga hela nyingi sana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wale wanaojenga tuhakikishe kwamba hizi kazi tunasimamia kwa ubora zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri na wataalam wake kwenye Wizara kwa kututengea shilingi bilioni 13 katika Uwanja wa Ndege Songwe. Tuna imani sasa uwanja huu utakamiliika kama ilivyopangwa na zile hadithi sasa za kusema: Ooh, tumeahirisha! Hatutazisikia tena. Tunaulizwa maswali mengi na Watanzania kwamba kulikoni uwanja wa ndege wa Songwe, hebu tuondoe ile minong'ono ambayo ili kuwa inasema kwamba nadhani kulikuwa na mpango wa kuhamisha kile kiwanja kupeleka maeneo mengine.

Lakini Serikali imeonyesha dhamira ya kwamba kiwanja kile kikamile, lakini wakati tunakamilisha kiwanja hicho tuangalie pia hata maeneo ya kiuchumi, kwa sababu tukikijenga kiwanja bila kupanua maeneo ya shughuli za kiuchumi kule maana yake ule uwanja utabaki hauna kazi yoyote. Aliyekuwa Waziri wa Mipango - Mheshimiwa Ngasongwa kwenye bajeti ya mwaka jana, alitueleza eneo lile ni moja ya maeneo yaliyowekwa kwa ajili ya kiuchumi (*Special Economic Zones*).

Kwa hiyo, naomba basi ile mipango iliyowekwa iweze kufanya kazi vizuri ili uwanja unapokamiliika na maeneo mbalimbali ya kiuchumi ambayo watu wengi watapenda kwenda huko, basi yawe tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TAZARA*. Kwenye Kitabu cha Bajeti Mheshimiwa Waziri anasema *TAZARA* wanapewa shilingi milioni 100. Shilingi milioni 100 inasikitisha, zinafanya kazi gani hizi hela? Mimi naomba Mheshimiwa Waziri atueleze sawa sawa. *TAZARA* na *TRL* nadhani wanatozwa *fuel levy*. Ni hela nyingi sana na *fuel levy* ninavyojuza zinakwenda kwenye ujenzi wa barabara, kule kwenye reli hakuna ujenzi huo wa barabara zaidi ya *ku-maintain* reli yenewe.

Sasa mnapowapa shilingi milioni 100 mnataka zifanye kazi gani na kwa nini basi muwatoze *fuel levy*? Muwape nafuu basi, wasitozwe *fuel levy*. Hili naomba Waziri atufafanulie. Lakini malipo kwa wastaafu wa *TAZARA* ni jambo lingine ambalo Mheshimiwa Waziri alisemee, suala la karakana ya *TAZARA* Dar es Salaam ipo *under utilized*, inasemekana ni *second largest workshop in Africa*, lakini matumizi yake is almost 25%. Naomba Mheshimiwa Waziri pia alitolee maelezo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Taasisi ya Hali ya Hewa. Tulizungumza kwenye Bajeti ya mwaka jana na juzi kwamba tunataka tununue rada kwa ajili ya *ku-monitor* hali ya hewa na kwa maana hiyo, kutoa tahadhari kwa wananchi wa nchi hii. Lakini mpaka leo na hili pia na lenyewe linasuasua. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atueleze, lakini kununua rada moja tu kwa nchi kubwa hivi sidhani kama inasaidia. Ninaomba Mheshimiwa Waziri kwenye Bajeti ya mwakani aje na mpango utakaoonyesha kwamba tumedhamiria kununua rada nyingi zaidi pamoja na vifaa vingi zaidi vya kupimia hali ya hewa ili tuweze kutoa tahadhari kwa wananchi wetu na kwa maana hiyo, waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumza kwa ufupi niwapongeze tu hawa wakala wa ujenzi *TBA*, wanafanya kazi nzuri sana. Wanajenga nyumba kwa ajili ya watumishi wa Serikali. Naomba waungwe mkono na naomba Serikali iwape nguvu zaidi ili waweze kuendelea kujenga nyumba kwa kuwasaidia wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Taasisi za Serikali kupanga Ofisi. Taasisi nyingi za Serikali zinapanga ofisi kwenye majengo ya watu binafsi na tunalipa pesa nyingi sana. Nitoe tu mfano, mimi nilifanya kazi kwenye Mamlaka ya Hali ya Hewa, naomba ni-*declare* hivyo; inapanga ofisi pale Ubungo plaza, inalipa zaidi ya milioni 400 kama kodi kila mwaka. Hivi tungetenga hela hiyo kwa miaka miwili au mitatu tukawapa bilioni tatu au nne si tutakuwa tumeokoa hizi fedha ambazo tutaendelea kulipa!

Lakini pia kuna taasisi nyingi za Serikali na najua *TRA* wanapanga kwenye majengo ya watu. Kwa nini tusiokoe fedha za Serikali? Hebu naomba tuwe na mpango endelevu ambao unaweza ukahakikisha kwamba tunaondoka kwenye kupanga kwenye ofisi za watu binafsi na nina hakika inawezakana na sitashangaa hata ofisi za Serikali kama Wizara na zenyewe nazo zikawa zina-*operate* kutoka kwenye majengo ya watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ambalo napenda nilizungumzie ni hili suala la *development corridors*. Mimi nitazungumzia sana *central corridor*. Mwaka huu kwenye Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja tulipitisha hapa *protocol* ambayo inazungumzia namna ambavyo tutaweza kuendesha hizi *corridors*. Naomba niseme kwamba kama hatuwezi kuhakikisha kwamba tunaimarisha Bandari ya Dar es Salaam, hii *central corridor* tunayoizungumza haitafanikiwa hata siku moja. Mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri, ameelingiza kwenye kitabu, lakini lazima tuwe na mipango madhubuti kuhakikisha kwamba Bandari ya Dar es Salaam inafanya kazi sawa sawa, tunaondoa msongamo wa makontena pale, tunaondoa urasimu Bandari ya Dar es Salaam, ndipo tunaweza kwenda mbele. Vinginevyo, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kengele inigongee, ninaomba niseme tu kwamba naunga mkono hoja hii nikitumaini kwamba Mheshimiwa Waziri atafafanua baadhi ya hoja ambazo nimeshazisema. Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hautoshi kwa msemaj i mwingine kuweza kuchangia. Sasa utaratibu wa jioni tukirudi, tutakuwa na wasemaji wawili. Nao ni Mheshimiwa John Momose Cheyo na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. Kwa hiyo, watatosha, tutampatia dakika 30 na Waziri mtoa hoja atatumia dakika 45 halafu tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi.

Asubuhi Mheshimiwa Luhahula aliuliza kuhusu utaratibu na kifungu alichokuwa anaki-refer kilikuwa ni kifungu cha 38(6). Kifungu chenyewe cha 38 ni kuhusu maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa kifungu kidogo cha sita kinasema: “*Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yatafuatiwa na maswali mengine kwa Mawaziri kwa dakika 60 kama yatakavyokuwa yamepangwa kwenye orodha ya shughuli ya siku hiyo.*”

Napenda kusema kwamba kifungu hiki kina kasoro. Kina kasoro kwa sababu siku kinaangalia ukichukua nusu saa ya Waziri Mkuu na nusu saa ya maswali kwa Mawaziri ni saa moja. Kwa hiyo, nakwenda kwenye Kanuni inayosema wakati wa Mikutano ya Bajeti kipindi cha maswali ni saa moja. Sasa hakijachukulia hatua kwamba wakati wa Bunge la kawaida basi saa za maswali ni saa moja na nusu. Kwa hiyo, itachukua nusu saa na itabakia dakika sitini. Kwa hiyo, kifungu hiki kina matatizo na itabidi kifanyiwe utaratibu unaopaswa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka jioni saa kumi na moja.

(*Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni*)  
(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge mchana, nilikuwa nimesema tutakuwa na wasemaji wawili, halafu tutamwita Naibu Waziri, halafu mtoa hoja, tuingie kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, msemaj i wetu wa kwanza alikuwa Mheshimiwa John Momose Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nataka kushukuru sana kwa kunipa hizi saa za mwisho mwisho ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu juu ya hoja ambayo iko mbele yetu.

Kwanza kabisa, nataka kutambua mjadala huu wa Miundombinu umekuwa mjadala ambao kusema kweli kama Serikali inasikia, imesikia vilio vyta Wabunge wote na wa Kambi zote. Wote wametueleza kinachohitajika na nataka kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa *contribution* zao ambazo wamefanya.

Lakini, zaidi nataka kumpongeza Ndugu yangu Mheshimiwa Zitto kwa kuweka angalau mapendekezo mbalimbali ambayo Serikali inaweza ikayafikiria na ndio kazi yetu upande huu. Hapo nataka kuwaasa tu ndugu zangu kwa moyo kabisa; tuko hapa kujadili fedha za Serikali. Kwa hiyo, siyo mambo kwamba ni ya chama au nini, ni fedha za Serikali. Kwa hiyo, ni vizuri tukashirkiana wote ili tujadili ni jinsi gani tunaweza tukapata ufanisi katika fedha za Serikali na kwa sasa hivi tunazungumzia juu ya fedha za miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika hoja ambayo nataka kuleta, kwanza, nataka kuzungumzia zaidi kwamba fedha ambazo Mheshimiwa anapewa hazitumiki vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua bajeti ni ndogo na umeona wewe mwenyewe, kila anayesimama, “nipe barabara”, nipe daraja”. Nami hapa nina barabara 25 ambazo ningesema nipe. Sasa, tunatoa wapi hizi barabara? Kwa hiyo, nimeona hebu niangalie kwa nini hatujengi barabara za kutosha? Katika kujaribu kuendeleza hoja yangu hii, naweza tu nikatoa mfano wa kwanza; ukurasa wa tisa, Mheshimiwa Waziri ametuambia kwa mfano; sentensi ya mwisho: “Barabara zilizokamilisha upembusi yakinifu ni mbili ambazo ni Maganzo – Maswa – Bariadi – Mkula – Ramadi kilomita 171 na Bagamoyo – Sadani – Tanga, kilomita 150.” Ile ya Sadani naona inapitia kwake kule. Lakini, kama tayari upembusi umekamilika, ukiangalia katika vitabu hivi, hakuna hela. Sasa tumetumia karibu bilioni moja kwa barabara zote mbili kufanya upembusi yakinifu kwa sababu gani kama hatuna fedha? Ukiacha hili bila kujenga sasa hivi, ndio kusema ule upembusi yakinifu uliofanywa ni sawa sawa na bure kwa sababu utakapoanza tena kuangalia, itabidi u-*apply figures* nyingine tofauti ili mradi uweze kukaa sawa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kinachonisikitisha ni kwamba, hivi Serikali kwa nini haioni hii kujenga miundombinu kama vile sawa sawa na miradi ya watu binafsi? Mtu akianza kutengeneza, kwa mfano, anataka kujenga kiwanda, cha kwanza, anafanya *feasibility study*, kama huu upembusi yakinifu tuliofanya. Akimaliza hapo, anafanya *funding* yote kabisa inakamilika na ikiishakamilika sasa anakwenda anatengeneza kiwanda mpaka mwisho, kwa sababu anajua anasipofanya hivyo, akisimama katikati, bei ya mambo mbalimbali yatakuwa yamegeuka. Lakini, Serikali hatujifunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote ya Serikali ambayo ni sehemu nyingine, kwa nini hatujengi? Miradi yote ya Serikali haimaliziki kufuatana na bajeti na ninaweza kutoa mifano mingi na mingine ya kusikitisha. Kwa mfano, barabara ya Kusini kule, naweza nikatoa mfano barabara ya Mbwemkuru – Lindi – Mingoyo, wameanza mkataba, ni shilingi bilioni 51.4.

Leo mradi huu mpaka zilizolipwa ni shilingi bilioni 93, karibu mara mbili. Sasa tunasema tunajenga kilomita 95 za hiyo barabara na wakati ambapo tunafanya upembuzi yakinifu tunasema gharama yake itakuwa shilingi bilioni 51. Mwishoni ni sawa sawa na barabara mbili ambazo ni 95 mara 95. Sasa kama unatumia 95 mara mbili, utajengaje barabara ya kutoka Mwigumbi kwenda Lamadi? Hauna hela kwa sababu menejimenti ya miradi hii siyo sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hiyo tu, leo hii tuko katika barabara ya katikati, kuna kilomita 120 ukishatoka Bahi pale, unakwenda Manyoni kufika karibu na Singida, haipitiki! Sasa, huku lami, mbele lami, katikati hapa homa tupu. Mimi sifikiri kwamba hiyo barabara itamalizika katika muda wa chini ya miaka miwili! Lakini, barabara imeanza zamani na ngojea itakavyopata gharama sasa. Mojawapo ya sababu itakuwa kwamba wewe unaambiwa tarehe fulani unilipe, hulipi mpaka yule mkandarasi anaamua kuchukua vyombo vyake. Ni matumizi mabaya ya fedha. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, hata ukiangalia barabara ya Nangurukuru – Mbwemkuru na yenyewe kilomita 95. Huyu alianza kwanza hata wale waliokuwa wanaangalia hii *contract* wangeshangaa. Shilingi bilioni 39, sasa hivi karibu iko shilingi bilioni 70. Namna hii hatuwezi kujenga barabara. Kwa hiyo, mimi ninachosema, labda Waziri lazima arudi kwenye ofisi yake akaangalie ni jinsi gani watajipanga ili kuhakikisha kwamba *contract* ya shilingi bilioni 50 inakuwa ni *contract* ya shilingi bilioni 50 tangu mwanzo mpaka mwisho. Hii ina maana kwamba labda basi tuangalie anaajiri watu wa namna gani *TANROADS* kwa mfano. Je, anaajiri watu amba wanakidhi mahitaji ya kuwa *Chief Executive* au kuwa *Engineer* au vipi! Lazima tuangalie yote hayo. Na sisi, mimi nikiwa Mwenyekiti wa *PAC* tutategemea *CAG* aangalie hii sekta ya barabara, aifanyie kweli *value for money examination*. Hivi pesa tunazoweka mle, tunapata fedha au vipi? (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujengi barabara kwa sababu hatuwezi ku-*manage contracts* zetu. Hii ndiyo *massage* kubwa ambayo nataka kuipelekea Wizara hii na nitapenda kuelewa kwamba Waziri anaweka mikakati gani kuhakikisha tunaondokana na janga hili? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, jambo la pili; Wafadhili wengi walikuwa wameacha kwamba hawatutengenezei barabara, hawataki kujiingiza katika barabara na hivi karibuni kidogo, wengine wameanza kurudi kidogo kidogo. Lakini, zaidi kwa sababu walikuwa wanasema tunatengeneza barabara, hakuna matengenezo (*no maintenance*) na ndio maana Bunge likaona ni vizuri tutengeneze Mfuko wa Barabara. Lakini, Mfuko huu, hivi tunapata fedha zote zile ambazo tunapaswa kupata? Mbona hata kwenye Wilaya kwa mfano, kama Wilaya yangu ya Bariadi, Wilaya ya Bariadi tuliahidiwa mwaka jana

kwamba tungepewa milioni, tena vimilioni vidogo vidogo, tungepewa milioni 384. Mpaka tarehe 15 Mei, tumepewa shilingi milioni 185. Tutajengaje barabara na sisi tuna barabara mbovu na tunataka kuhakikisha kwamba wananchi wetu ni wakulima wa pamba safi kabisa, wanaweza kupeleka mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tumeponga tutengeneze barabara ya Inalo – Mahembe. Kama tunapewa nusu ya hela ambazo tumepewa, tutapeleka wapi? Tulikuwa tumeponga Sawida – Mbita – Mwanzoya – Ngulyati – Gambosi, Ngulyati – Mwamulapa – Bagangabili – Gambasingu – Mwamapalala – Nkoma, bado ziko nyingi; Budalagujega – Gambasingu, Byuna – Nkwitwabie – Nkololo – Mwasinasa, tutajenga vipi? Hizi barabara, mimi sizungumzii Jimbo langu tu, utasema barabara inayotoka kwenye Jimbo langu iende wapi, ni lazima iende Bariadi nzima. Kwa hiyo, tunasema labda kuna haja sasa ya kuangalia upya huo Mfuko, tunapata fedha zote na kwa wakati na ni bure. Sisi tunangojea, mwezi kama wa Desemba unatupelekea fedha, tufanye nazo nini wakati huo ndio wakati kuna mvua nyingi? Tutafika wapi? Kwa hiyo, ningeshauri kwamba, nimeona hapa Mheshimiwa Waziri amesema kuwa anataka kuangalia upya sheria ya Mfuko huu, lakini hiyo ni pamoja na menejimenti ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, naungana mkono kabisa na wale wote waliozungumia mambo ya Reli. Hili ni jambo la kufa na kupona na Serikali yetu isijiumeume. Najua hapa tumepewa sababu nyingi, sijui nini! Sijui hakuna mtu aliweka sahihi! Sijui hakuna *due diligence!* Mambo yote yale hayatusaidii. Tunachotaka, reli ya kati ifanye kazi Dar es salaam mpaka Kigoma, Dar es salaam – Tabora – Mwanza, watu wetu watembee kwa raha.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 45 ya uhuru watu wanakanyagana kifuani, halafu mtu aje asimame hapa, “mimi chama”, siyo mambo ya chama! *We are saying*, tumia fedha vizuri, fanya *contract* nzuri ambazo kweli zitawezza kutusaidia. Kwa sasa hivi, naona bado, pamoja na kwamba imepata Mwekezaji, lakini Serikali isiiupe hii reli ya kati. Ukiangalia, mimi nina hakika baadae tutakuja kuangalia katika mikataba ile, utaona ile mikataba haitusaidii. Serikali msijivue kwa jambo la miundombinu. Kama ninyi hamna fedha, naungana na watu wote kabisa, kwamba sasa nchi yetu tunaweza kukopesheka. Kuna *sovereign bonds* ulimwenguni kote, kopeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata upande wa Hazina, tuangalie, huwezi ukaendesha kila kitu kwa *cash*, kwa *cash*, ni sawa sawa na mtu unajenga nyumba kwa *cash* ndivyo Watanzania tunavyofanya. Lakini, Serikali kwa nini tuisiangalie utaratibu wa *cash* kwamba labda sasa hivi umepitwa na wakati na zaidi katika miradi mikubwa kama ya barabara. *Why not Accrue Accounting?* Kwa nini kila siku tunatumia kile tulichonacho? Lakini ukiangalia tena huku unatumia kile ulichonacho, huku bado tunapata matatizo. Mimi naona utaratibu wa jinsi ambavyo tunawekeza fedha na zaidi kwa fedha za miundombinu, hatujapata bajeti itakayoweza kukidhi mahitaji ya Wizara hii ya Miundombinu na Wizara hii ni ya maana sana.

Mtu akipata barabara, hata MKURABITA inaingia, kila kitu, unakuwa umeishamkomboa. Atawenza kujitafutia fedha, atawenza kufanya biashara, atawenza kufika

anakotaka, utapeleka huduma mbalimbali kwa urahisi zaidi, ataweza kujisaidia yeye mwenyewe. Lakini, bado hatujaipatia namna ya kuipa fedha hii Wizara. Mimi nashauri Serikali iangalie upya, tusikae *cash cash cash* na *cash* yenyewe ndiyo tunaitumia vibaya hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukufahamisha kwamba *front bench* haina mtu na nilikuwa naomba mwongozo wako kuhusiana na taratibu za tamaduni za Mabunge ya Jumuiya ya Madola.

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu tunaendelea na *debate*, siyo kwamba tumefikia maamuzi, hili halina tatizo, wanaohusika wapo!

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwa sababu naamini watu waliokuomba ni wengi, kwa hiyo, najihesabu kwamba ni mionganoni mwa wale waliohatika kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kwanza niishukuru Serikali kwa jitihada zake kubwa inazozifanya katika kujenga barabara nchi nzima na hasa barabara yetu ya Kusini. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaarifu ndugu zangu wa Kusini kwamba kipande ambacho tumekuwa tukikilalamikia kwa muda mrefu cha Ndundu – Somanga, sasa hivi kimepata mwelekeo mpya wa kutengenezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara ya Miundombinu, nikianzia na Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Dr. Kawambwa, Katibu Mkuu wa Wizara -Ndugu yangu Chambo, vile vile Meneja wetu wa *TANROADS* - Ndugu Mrema na vile vile Mkurugenzi wa Mfuko wa Barabara, Mtani wangu - Bwana Haule. Nawapongezeni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pondezi hizi kwa kuelewa kwamba Wizara hii ni ngumu. Karibu miaka yote Wizara hii ni Wizara ambayo inapata misukosuko sana kwa sababu macho ya wananchi wote wa Tanzania, macho ya Wabunge wote huwa wanaelekeza katika Wizara hii. Kikubwa ambacho naweza kukifanya ni kuwaombea dua wapate nguvu, afya na ujasiri wa kuweza kutekeleza yale yote ambayo wanalazimika na wanawajibika kuyatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea kwenye barabara ya kutoka Masasi – Tunduru – Songea, tuna furaha kwamba barabara kutoka Masasi – Mangaka, sasa hivi imeishaanza kujengwa na matarajio yetu ujenzi ule ni kwa kiwango cha lami.

Tunashukuru sana. Namtumbo – Songea, *MCC* wameishaweka hela zao pale, hivi karibuni nayo itaanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tunduru baada ya kusikia hotuba ya Waziri Mkuu ambayo ilionyesha kwamba kipande hiki cha Mangaka – Tunduru – Namtumbo mwaka huu hakipo katika mpango, kwa kweli kulizua mijadala minge sana. Baada ya hotuba ile wananchi wa Tunduru waligawanyika vikundi kwa vikundi wakiwa wanajadili hotuba ile hasa kwa kuzingatia kutoonekana barabara hiyo ya kutoka Mangaka – Tunduru – Namtumbo.

Ninachopenda kuwaeleza wananchi wa Tunduru ni kwamba, tuendelee kuvuta subira. Tuvute subira kwa sababu naamini kabisa azma ya Serikali iko pale pale, ahadi iliyotolewa na Rais wetu iko pale pale na ahadi hii ni ya miaka mitano na leo tuko nusu safari, takriban sasa hivi ni miaka miwili na nusu. Bado tuna bajeti mbili mbele yetu. Kwa hiyo, muda wa kuihukumu Serikali haujafika. Hiyo ndiyo rai yangu kwa wananchi wa Tunduru na mimi kwa nafasi yangu kama Mbunge wa Jimbo lile, bado nina jukumu la kuikumbusha Serikali kwamba mliahidi hilo kule Tunduru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba aliyoitoa Mgombea wa Urais kuitia tiketi yetu ya CCM, alianza kwa kuwaomba radhi wananchi wa Tunduru kwamba: “mniwie radhi nimechelewa, muda ambao nilitakiwa kufika hapa, umenikuta njiani sababu kubwa ni ubovu wa barabara. Lakini, ninaamini kama chama changu kitanisimamisha mwaka 2010 (ambapo nina hakika chama chetu kitamsimamisha) sitachelewa tena kwa sababu barabara hii itakuwa imewekwa lami.” Hiyo ni kauli sisi tunaichukulia kwamba ni kauli mutribu ambayo Serikali inaazimia itaitekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, sio hilo tu, kipindi cha uchaguzi mdogo, Tunduru ilibahati kufikiwa na viongozi wengi wa ngazi za juu wa chama chetu na moja ya ajenda katika mikutano mbalimbali ili kuwa: “Tupeni Mtutura ili aongeze nguvu ya kujenga barabara hii.” Wananchi wa Tunduru hawakuweka ajizi, wakasema Mtutura hiyo, tunawapeni! Kwa hiyo, naamini Serikali haina sababu yoyote hasa ukizingatia kwamba Mtutura mwenyewe bado anaikumbusha Serikali katika ujenzi wa barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nilikuwa nasafiri kwenye basi, tulipofika Ndandumu, kipindi hicho lazima Ndandumu usimame pale, uvuke kwenye Pantoni. Nililazimika kutelemka na abiria wenzangu, tukaenda kwenye mgahawa mmoja hivi. Miiongoni mwa abiria tuliokuwa katika gari ile, aliquwepo mama mmoja wa Kindengereko akiwa ameongozana na mtoto wake.

Tulipofika kwenye mgahawa, yule mama akaagiza chai pamoja na mkate. Mimi nilikuwa jirani yao kidogo. Yule mtoto aksauliza swali moja: “Mama, nianze sai, nianze nkate?” Sasa, mama akamwambia: “anza sai.” Mimi nikamwuliza kwa nini unamwambia aanze chai? Aanze “sai” hiyo, kwa nini unamwambia aanze “sai”? (kwa sababu ni watani zetu wale) yule mama akasema “endapo ataanza sai na mkate ukiwa mkononi mwake, gari likisema twendeni, ule mkate ataubeba ataingia nao kwenye gari.” Kwa kweli siku

ile nikaanza kuwaheshimu kidogo hawa ndugu zetu Wandengereko, nikaona kwamba na wao kidogo wanafanana fanana na Wamakonde na Wayao kwa akili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nimesema hivyo? Dhamira ya ujenzi wa barabara hii kutoka Mtwara hadi *Mbambabay* ni kuitumia Bandari ya Mtwara, ndiyo dhamira yake na kuchochea maendeleo ya Mikoa ya Kusini. Hii ni pamoja na Mbeya pamoja na Rukwa. Sasa, cha kushangaza, ujenzi wa barabara hii inakuwa umeanza Mtwara ukaishia Masasi. Tunasema kwamba lile lilikuwa lengo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masasi, Mangaka, hatuna tatizo na hilo. Sasa imekuja kurukwa Tunduru, inaanza kujengwa Namtumbo – Songea – *Mbambabay*. Hapa kwa kweli tunaona badala ya kuanza “sai”, hawa wenzetu wameanza mkate. Kwa sababu uchumi wa Tunduru, hii siyo siri, ni korosho na soko la korosho kwa kweli linaelekezwa katika Bandari ya Mtwara. Hivi sasa kama uwezo wa Serikali tunasema kwamba (Mwenyezi Mungu apishilie mbali) unakwisha: Je, ukombozi kwa wananchi wa Tunduru utapatikana vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, kwa kipande hiki kilichobaki, kati ya Masasi – Mangaka – Tunduru – Namtumbo, kama kuna uwezekano mdogo wa pesa unapatikana, basi tunaiomba sana Serikali ianze ujenzi kipande hiki cha kutoka Mangaka – Tunduru ili tuweze kusafirisha korosho zetu, tuweze kusafirisha mpunga wetu na uchumi wa Tunduru uweze kuimarika. Hilo ndio ombi la wananchi wa Tunduru katika *plan* ya ujenzi wa barabara hii. Zikipatikana pesa nyingine, basi, tuelekeze nguvu zetu kutoka Tunduru kuunganisha na Namtumbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunasubiri hiyo lami, niliomba hapa wakati nachangia bajeti ya Wizara ya Fedha kwamba watu wa Tunduru tunaamini *Subira min Allah* (Kila mwenye kusubiri yuko na Mwenyezi Mungu). Tutaendelea kusubiri.

Ndugu yangu hapa ananiambia *Inallah Maswabirina*, ni kweli kila mwenye kusubiri yuko na Mwenyezi Mungu. Tutaendelea kusubiri tukiwa tunaamini kwamba ahadi ya Serikali ni miaka mitano. Mwaka 2010 siyo mbali na siyo karibu, Serikali itaweza kuvuta kasi yake na kuweza kutengeneza barabara hii.

Lakini, wakati tunasubiri, basi, barabara yetu ipitike mwaka mzima. Zile sehemu ambazo ni korofi, basi ziangaliwe. Naamini kabisa Serikali italiangalia hili kwa mapana sana kwa kuzingatia kwamba mchango wa wananchi wa Tunduru ni mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba vilevile Serikali hasa kupitia mfuko huu wa barabara, tunayo matatizo makubwa sana ambayo Halmashauri yetu haiwezi kumudu kulinganisha na kiasi cha pesa ambacho tunapata. Tunalo daraja la Mto Muhesi ambalo linaelekea Kijiji cha Kalulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja lile makisio ya awali yalikuwa shilingi milioni mia moja, katika shilingi milioni mia tano na kitu ambazo zinapelekwa Tunduru, ukitoa

shilingi milioni mia moja na kitu kwa ajili ya kutengeneza daraja lile, Tunduru itaishiwa pesa kiasi kwamba barabara nyingine zitasahaulika kabisa.

Tunaomba kupitia Bunge letu Tukufu ndugu yetu na kipenzi chetu, swahiba wetu, Haule atuangalie kwa jicho la huruma ili atuongezee pesa katika Halmashauri yetu tuweze kujenga daraja lile ili ndugu zetu wa Kalulu nao wajisikie kwamba wako katika nchi yetu, hawajatengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni daraja ambalo linakwenda katika mbuga ya *Selous* na daraja ambalo linapitisha wawindaji wa kimataifa, kwa hiyo, ni daraja muhimu sana kwa mapato ya fedha za kigeni kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna barabara ya kwenda Ngapa, nayo inahitaji pesa nyingi ambazo Halmashauri yetu haiwezi kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sijui kengele ya pili italia saa ngapi, nasema kabisa naunga mkono hoja hii wakati naendelea kuzungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, narejea kwenye Bandari ya Mtwara. Bandari ya Mtwara imekuwa kilio cha muda mrefu na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote wa Bunge hili Tukufu kwa sababu wamekuwa wakizungumzia bandari hii bila kujali kwamba wao wanatoka eneo gani. Hii ni kudhihirisha kwamba bandari hii ina umuhimu wa Kitaifa.

Naiomba Wizara iangalie suala hili kwa umakini sana umuhimu wa kutumia bandari hii. Tulikuwa na mzozo kidogo na wenzetu wa *TRA*, naomba mzozo huu uishe ili bandari hii iweze kutumika hata kwa mizigo ya sasa hivi iliyopo Dar es Salaam, ili ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam uongezeke kwa kuendelea kutumia Bandari ya Mtwara na Bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ukimaliza, yale uliyokusudia kuongea ni bora kukaa chini ili kupisha shughuli nyingine zenye manufaa kwa Taifa letu ziendele. Nakushukuru sana.

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ni muhimu sana katika kuchochea urchumi wa nchi. Naomba ushauri huu uzingatiwe hasa ikizingatiwa kuwa, mwaka huu wa fedha inaonekana hakuna miradi mipya itakayoanzishwa mbali na kuendeleza ile inayoendelea. Si vizuri tuwe na tabia ya kuendelea kuzikarabati barabara zetu mfano:-

Barabara ya Mwanza – Shinyanga Boarder ambayo 2006/07 ilipangwa Sh. 1.6, 2007/08 ilipangwa Sh. 200,000,000 na 2008/09 imepangiwa Sh. 900,000,000, kiasi hicho kilichopangwa ni kidogo sana kwa barabara hiyo.

Barabara ya Mwanza - Nyamenge - Mwanza mwaka huu wa fedha 2008/09, hakuna fedha iliyotengewa hata kidogo kwa ajili ya *rehabilitation*. Je, ikiharibika itatumia pesa gani?

Ujenzi wa Mwanza Airport haujulikani umetengewa kiasi gain, kwani kiasi kilichotengwa cha Sh. 1,000,000,000 kimejumuisha ujenzi wa Airport ya Kigoma na Mwanza. Je, kiasi gani kimetengwa kwa Mwanza Airport? Tusinghau Mwanza Airport ndiyo *hub* ya Kanda ya Ziwa, tunaomba katika bajeti ijayo pesa zitengwe za kutosha kwa ujenzi wa Airport hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze kwa dhati Meneja na Mhandisi wa *TANROAD* (Mkoa wa Mwanza), Ndugu Kadashi, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kusimamia vizuri fedha zinazotumwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara zetu mkoani Mwanza. *Value for money* inaonekana tofauti na zamani. Naomba asirudi nyuma, asimamie vizuri zaidi na kuwabaini Makandarasi wababaishaji.

Kutokana na hiyo, naomba ujenzi wa Daraja la Mto Simiyu upande wa Mangisu uanze, kwani hii ilikuwa ahadi ya bajeti 2007/08, ambapo *CEO* wa *TANROAD* aliahidi kuwa, mwaka 2007/08 angetenga Sh. 50m kwa ajili ya usanifu lakini haikuwa hivyo, mwaka huu wa fedha nasikia zimetengwa Sh. 150m. Kama ni kweli nashukuru na kama sivyo basi naomba majibu ya kina na lini daraja hilo litaanza kujengwa na siyo usanifu.

Kama Mbunge, si vizuri tuwe tunabishana na Serikali; ahadi zinazotolewa ni vizuri zikatekelezwa, si tabia nzuri suala hilo hilo likawa linaulizwa kila kipindi cha bajeti, kwa kufanya hivyo ni kupunguza heshima ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yake. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa mawasiliano ya barabara ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu; na kwa kuwa barabara zinasaidia sana huduma ya usafiri wa abiria/wananchi na kusafirisha mazao ya chakula na biashara; na kwa kuwa barabara nyingi zimeharibika hapa nchini na hasa za vijijini zikiwemo barabara za Wilaya za Mpwapwa na Chamwino kama vile barabara ya kutoka Mbande - Kongwa - Mpwapwa - Mlali - Pandambili; barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo/uchumi wa Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa; na kwa kuwa fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya *Periodic Maintenance, Routine Maintenance* na *Spot Improvement* ni kidogo sana na matengenezo yanayofanyika ni kidogo tu (*Light Grading*) na sio *heavy grading*: Je,

Serikali itatenga fedha za kutosha lini ili barabaa hiyo ifanyiwe matengenezo makubwa ikiwa ni pamoja na kuweka lami barabara ya kutoka Mbande - Kongwa Mjini - Mpwapwa: Je, Serikali itatenga lini fedha za kutosha ili barabara kutoka Chenene - Itiso - Izava – Dosidosi na barabara ya kutoka Manyhali - Chalinze - Kiegea - Kazania - Chimaligo hadi Nghambi zifanyiwe matengenezo makubwa kuliko hali ilivyo sasa fedha ni kidogo sana?

Kwa kuwa barabar ya kutoka Mbori (Matomondo) - Inzomvu - Godegode (*Railway Station*), ilikuwa chini ya Mkoa; je, ni sababu zipi zilizofanya barabara hiyo iondolewe kwenye orodha ya barabara za mkoa na lini barabara hiyo itatengenezwa na mkoa matengenezo makubwa?

Kwa kuwa mwaka jana Septemba, 2007 Mheshimiwa Rais alipofanya ziara Wilaya ya Mpwapwa na kutembelea Bonde la Umwagiliaji la Lumuma – Wilaya ya Mpwapwa alipita barabara ya kutoka Mpwapwa – Vinghawe – Kimagai – Godegode hadi Lumuma, aliona barabara hiyo ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa Wilaya ya Mpwapwa na kuagiza barabara hiyo ifanyiwe matengenezo makubwa; na kwa kuwa barabara hiyo ipo chini ya Halmashauri ya Mpwapwa na kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa hawana fedha za kutengeneza barabara hiyo: Je, Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na TAMISEMI watatenga fedha za kutosha ili barabara hiyo ifanyiwe matengenezo makubwa na kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOEL NKAYA BENDERA:** Kwanza, ninapongeza Hotuba nzuri sana ya Waziri. Naipongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mchango wangu nitauelekeza katika mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Mji wa Korogwe umepata hadhi ya kuwa mji. Mji huu kwa kupata hadhi hiyo, unahitaji kuwa na miundombinu inayofanana na hadhi ya mji, hasa barabara. Katika Bajeti ya mwaka 2007/08, niliahidiwa kuwekewa lami barabara za kilomita saba. Nafurahi kusema kazi hiyo itaanza kwa kuwekewa lami kilomita mbili kwa barabara ya *Cultex* hadi Miami kuititia msikitini hadi kwa Seif. Barabara hiyo hivi sasa imekamilika. Jambo la kusikitisha ni kutoanza kwa barabara inayofuata ya kutoka Mwembeni au *Transit Hotel* hadi TTC Korogwe kilomita moja. barabara hii ni muhimu kwa sababu ndio inayotumiwa na wananchi wengi toka Kata ya Mtonga, Msambazi, Ngombezi, Msisala, Kwengoma na Mzeri kukimbiza haraka wagonjwa kwenda hospitali ya Wilaya ya Magunga.

Barabara nyingine niliyoahidiwa ni ya kutoka Majengo Hospoitali - Mountain View - Kanisa la Roman Katoliki hadi kwa Shekh Ramia km 2. Barabara hii ni muhimu sana kwa sababu ndio inapita katikati ya Mji wa Korogwe na ndiyo inayotumiwa na wananchi wengi.

Barabara ya mwisho niliyoahidiwa ni kutoka kwa Mkuu wa Wilaya, kupitia Usalama wa Taifa hadi Kijiji cha Kwamkole km 2. Barabara hii inaelekea kwenye ofisi nyeti na ndilo eneo ambalo Viongozi wetu Wakuu wa Wilaya wanakoishi. Barabara zote hizi zina jumla ya km 5 na hii ni Ahadi ya Serikali. Nikiwa mwakilishi wa wananchi, nilikwishawaeleza wananchi juu ya utekelezaji wa barabara hizi kwa awamu. Sasa zoezi linaposhishwa linaniweka katika hali mbaya kisiasa. Ninaomba sana nifikiriwe barabara hizi kuendelea kutengenezwa hata kwa awamu ili wananchi waone kwamba sikuadanganya.

(b) Daraja la Kwasigi katika Kijiji cha Msambiazi, Korogwe linaunganisha Kata ya Msambiazi na Kata ya Ngombezi kupita Mto Luvu au Mto Pangani. Daraja hilo huu ni mwaka wa tano sasa halijakamilika. Lipo tatizo la wananchi kushimdwa kwenda shamba kwa sababu ya ukosefu wa daraja hili, wanalahazimika kuzunguka masafa mrefu na kutumia saa tatu kwenda shamba tu. Ninaomba Wizara iangalie ufumbuzi wa suala hili nyeti. Daraja hili haliishi kulikoni?

(c) Ipo ahadi ya muda mrefu ya Barabara ya Korogwe hadi Handeni kuwekwa lami lakini suala hili limekuwa likisuasua. Je, ni lini sasa barabara hii itawekwa lami?

(d) Samani za Nyumba za Mawaziri hazifai ziondolewe; ni jambo la aibu na kusikitisha kwa samani zilizo kwenye nyumba za Mawaziri - Victoria Mwananyamala. Samani hizo zilinunuliwa feki zote zimebomoka. Makabati, vitanda, meza, viti vyote vimebomoka. Vifaa hivi viliagizwa toka nje ya nchi, lakini sio imara. Ninaomba Wizara ihakikishe vifaa vilivyopo vinaondolewa mara moja na kuwekwa vinya.

Je, Wizara haioni busara kununua au kutengeneza samani imara toka JKT na Magereza amba wao wanatengeneza vifaa imara vyta mba halisi za hapa nchini? Suala hili ni nyeti, lipewe uzito na utekelezaji wa haraka.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja. Nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kwa hotuba yake. Nampongeza pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Ezekiel Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa na Ndugu Chambo Omar, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote wa Wizara, kwa kazi nzuri.

Pamoja na pongezi, nachangia kama ifuatavyo: Barabara za Korogwe – Handeni, Handeni – Mkata ni muhimu sana kwa maendeleo ya Wilaya ya Handeni na Kilindi. Ubovu wa barabara hii kiungo cha Wilaya ya Kilindi hadi Mkoa wa Arusha na Dodoma, kero yake imedumu miaka mingi hasa wakati wa mvua. Pamoja na *TANROADS* kutengeneza maeneo korofi, bado tatizo ni kubwa. Nashauri sehemu zile korofi sana kama maeneo ya Sindeni – Misima (Kwedikuyu), ingefaa daraja lijengwe na fedha zinazotumika kila siku bila mafanikio au patengenezwe kwa kiwango cha juu. Tatizo la *TANROADS* kutengeneza barabara bila kuchimba mifereji ya kutolea maji barabarani, badala yake barabara wanaifanya tuta, inasumbua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Handeni tunahitaji nyumba ya Serikali ya Mganga Mkuu (DMO). Tunaomba mtujengee katika Wilaya ya Handeni, kwani daktari inamuwia vigumu sana hasa wakati wa usiku anapohitajika kwenda Hospital (*on call*), inakuwa usumbufu kwa kuwa anasumbua wenye nyumba uraiani na yeje ni mpangaji.

*Otherwise*, kazi mbele yetu ni kubwa, lakini naamini kwa ushirikiano mlionao kama Wizara na Sekta nyingine, mtaweza kutekeleza yote yaliyoazimiwa. Kila la kheri, nasi tupo pamoja kutoa ushirikiano kwa niaba ya Wantanzania. Nawatachia kazi njema.

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaunga mkono hoja hii ya Wizara ya Miundombinu. Aidha, ninapenda kuwapongeza kwanza, Mheshimiwa Dr. Kawambwa na pia Mheshimiwa Chibulunje, kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais, kuiongoza Wizara hii. Pia ninawapongeza Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Miundombinu, kwa kuandaa bajeti nzuri ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia majibu ya swalilouliza hapa Bungeni, lililohusu ujenzi wa daraja la Mto Lukwamba huko Mpombe katika Kata ya Napacho, Wilaya ya Nanyumbu, iliahidi kuwa ujenzi wa daraja hili ungeanza mwaka wa fedha 2007/08. Ujenzi ambao haujaanza hadi sasa; hivyo, Serikali kutosema ukweli kuhusu jambo hili. Ninatarajia kutoa shilingi wakati wa kupitisha vifungu mbalimbali vya Wizara, hivyo naitaka Wizara inipe maelezo ya dhati kwa nini ujenzi wa daraja hilo haujaanza kama ilivyoahidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujuu ujenzi wa kiungo cha barabara kati ya Tanzania na Msumbiji (Mangaka – Mtambaswala) utakamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa hotuba nzuri.

Pili, naomba nzungumzie barabara ya kutoka Mbande – Kibakwe – Malolo – Ruaha Mbuyuni. Barabara hii ni muhimu sana katika Maendeleo ya Wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa hasa Jimbo la Kibakwe – Wilaya ya Kilosa – Morogoro na Kilolo – Iringa. Wananchi wa maeneo hayo wapo *locked* na wanaendesha shughuli za kilimo cha umwagiliaji na ni wazalishaji wazuri wa mazao ya vitunguu, vaharagwe, viazi mviringo, mahindi na kadhalika. Umuhimu wa barabara hii ni mkubwa sana kwa maendeleo ya kiuchumi. Ninaomba yafuatayo:-

(a) Naomba barabara hii angalu iwe ya Mkoa (ipandishwe daraja), kwa sababu inakidhi vigezo vyote vilivyotajwa katika Sheria ya Barabara.

(b) Barabara niliyoitaja ukianzia Mbande – Mpwapwa hadi Gulwe ni ya Mkoa bali kuanzia Gulwe – Kibakwe – Malolo – Ruaha Mbuyuni siyo ya Mkoa. Nakuomba

kwa nafasi yako, Idara za barabara za Mkoa wa Morogoro, Dodoma na Iringa zikutanishwe kukubaliana juu ya upandishaji hadhi wa barabara hiyo muhimu.

(c) Kwa kuwa barabara hiyo itakuwa inaunganisha *Truck Road – to Truck Road*, lakini pia inakata katikati ya Wilaya/Jimbo la Mpwapwa na Jimbo la Kibakwe na kuunganishwa na Mikoa mitatu; Morogoro, Dodoma na Iringa; ni imani yangu kwamba utazingatia ombi langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami pia nichangie hoja hii muhimu iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, pamoja na Wataalam wote, walioandaa bajeti hii nzuri iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niipongeze Wizara ya Miundombinu kwa kukubali kukarabati barabara muhimu ya kutoka Mwabuki – Jojilo – Nyamilame – Mwankulwe - kuelekea Malampaka. Hivi sasa inapitika vizuri kabisa. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichangie kuhusu barabara ya Migumbi - Maswa – Bariadi - Lamadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoahidi Rais toka mwanzo kuwa, barabara hii itatengenezwa na kwa kuwa kauli hii amekuwa akiirudia mara kwa mara, lakini Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa hakuna dalili yoyote ya kuonyesha utengenezaji wa barabara hii. Nilikuwa naomba nipate maelezo ya ziada kama kweli bado azma ya kuitengeneza barabara hii ipo, kwa sababu wananchi wamekuwa wakituuliza mara kwa mara na sisi tunakosa majibu ya uhakika. Naomba maelezo ya uhakika tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua ni taratibu gani zinatumika ili kukagua vifusi vinavyokuwa vinamwagwa barabarani, kwani mara nyingi vifusi hivi vinakuwa vidogo sana kiasi kwamba, siyo *trip* nzima ya tipa. Ni kweli kwamba, kinachohesabiwa hapo ni marundo ya *trip*. Sasa kutokana na marundo machache hayo, Wizara haioni kuwa Wakandarasi hawa wanakuwa hawatoshelezi vifusi hivi na kusababisha hesabu nyingi ya vifusi visivyokuwa halali kuhesabiwa. Naomba Wizara ifuatilie suala hili; ni muhimu sana, linaiupunja sana Serikali kutokana na vifusi visivyokamilika kwa kuongeza idadi kubwa isiyo kuwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kusema, naunga mkono hoja ya Waziri wa Miundombinu, kwa kuwa inaonyesha wazi kuwa, dhamira ya dhati ya kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa ipo. Hata hivyo, naomba nielekeze mchango katika maeneo yafuatayo:-

Naipongeza sana Serikali kwa jitihada zinazoendelea za ujenzi wa Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongolosi. Tayari kipande cha Mbeya – Lwanjilo Mkandarasi yupo *site* na kazi inaendelea. Hata hivyo, kero kubwa katika barabara hii ni kutolipa fidia ya wahanga wa barabara, hasa wale ambao barabara iliposanifiwa tumewafuata. Si vyema kuanza ujenzi wa barabara, kabla ya kutoa fidia kwa wananchi hasa kwenye maeneo ya Isango, Iganzo na eneo la *Coffee Garden*.

Zoezi zima la kulipa fidia limechukua muda mrefu, fedha za awali ziliweza kulipa eneo la uhamishaji wa miundombinu lakini wananchi hawakulipwa. Sasa ni muda mrefu, kiasi ambacho wananchi wanaona ni kero na dhamana ya fedha ina shaka, itawawia vigumu kujenga na kupata makazi mapya. Naomba nipate maelezo ya lini fidia italipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Mbeya na wapiga kura wa Jimbo la Mbeya Mjini, napenda kuishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha za kumalizia ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe. Naamini Uwanja huu utasaidia sana kuibua fursa za kiuchumi ndani ya Mkoa wetu, pia nchi jirani kama vile DRC, Zambia na Malawi. Ninaamini pia sasa utekelezaji na ujenzi utanza mara moja ili gharama za ujenzi zisipande na hatimaye Uwanja uishe kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa tatu sasa, ninawaomba wataalam wa Wizara kuangalia upya uwezekano wa kufanya *design* upya kwenye eneo la Mafati. Eneo hili limekuwa kero mno kwa ajali za magari mwaka 2006/07 na 2007/08; zaidi ya watu 16 walipoteza maisha yao. Michoro iliyochorwa barabara huwa haionekani wakati wa usiku na mchana, pia eneo hili linawababaisha madereva. Hivi ni kweli kuwa Serikali imeshindwa ku-*redesign* eneo hili lisiendelee kuwa chanzo cha ajali? Hivi kwa nini hatujengi round about pale au kuweka taa za kuongozea magari? Katika mchangwo wangu wa mwaka jana, Serikali iliahdi kuzifikiria *options* zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo imani kubwa kuwa, Serikali italipa uzito unaostahili, tatizo la Mafati Jiji la Mbeya.

Barabara ya zamani kuanzia Mlima Nyoka kupitia Chuo cha Kilimo Uyole – Iyela – Iyuga – Kupima Mist, ipo haja kubwa ya kuiboresha kwa sababu hajabomoka sana. Katika Vikao vya *Road Board* Mbeya, ilikubalika kuwa, ukubwa wa Jiji la Mbeya unahitaji kuangalia upya katika eneo la msongamano wa magari yaingiyo katika Jiji la Mbeya.

Tunaomba Serikali iangalie namna ya kuitekeleza rai ya *RCC*. Kuwepo kwa barabara hii, itasaidia kupunguza msongamano wa magari, kwani magari yanayokwenda nje ya mji yatatakiwa kupita katika barabara hii ambayo itakuwa inaelekeza. Naomba sana Serikali iliangularie kwa uzito mkubwa ili kulinusuru Jiji la Mbeya na wananchi kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawatakia kila lililo jema Wizara hii, Mungu awape afya njema Mawaziri wetu watatu; Mheshimiwa Dr. Kawambwa, Mheshimiwa Chibulunje na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba maelezo kwa nini *crusher* la kokoto limeondolewa Kiwira ambako kuna kokoto; Daraja la kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hiyo.

Nawapongeza kwa hotuba nzuri na pia kwa mafanikio makubwa, yaliyopatikana kupitia Wizara yako kwenye miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio changu ni kile kile, watu wa Kagera wana uchu wa maendeleo. Miundombinu imara itaweza kuwakomboa, kwani itaufungua Mkoa wa Kagera na mikoa mingine, pamoja na nchi jirani za DRC Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya. Hivyo, Waziri ningependa nielezwe ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kupanua na kutengeneza Uwanja wa Ndege wa Bukoba kwa Kiwango cha lami? Miezi mitano imepita tangu Barabara ya Kagoma – Lusahunga mkandarasi wake kusimamishwa, kwani alishindwa kutekeleza kazi yake kwa muda. Je, sasa ni lini tutaletewa mkandarasi mwingine na ni kiasi gani cha pesa kimetengwa kwa ajili ya barabara hiyo kwenye bajeti hii ya mwaka 2008/09?

Mheshimiwa Rais, alipokuja Kagera aliahidi kuwa, Serikali itaijenga Barabara ya Kyaka – Kayanga kwa kiwango cha lami. Aliporudi mwaka huu ameahidi tena na kuwashakikishia watu wa Karagwe kuwa, barabara hiyo itajengwa. Je, ni kiasi gani kimetengwa kwenye bajeti hii kwa ajili ya barabara hiyo na ni lini ujenzi huo utakuwa umeanza?

**MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa ushirikiano walionipa wakati nikiwa Naibu Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maoni yafuatayo: Kituo cha Hali ya Hewa - Pemba, napenda kujua hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa kituo hicho; kuisaidia Zanzibar katika kupata ujenzi wa udhibiti na usimamizi wa Usalama wa Usafiri wa Majini; mchango wa Sekta ya Usafiri na Usafirishaji katika uchumi wa nchi yetu; umuhimu wa kuboresha/kujenga magati machache *strategically* yenye biashara katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, hii itafungua maeneo mengine ya nchi na kuboresha uchumi wetu; kuisimamia vyema *TRL* ili iweze kutoa na kuboresha huduma zake. Hasa Reli ya Dar es Salaam - Kigoma, ili tuweze *ku-tape* biashara ya Congo, Burundi na Rwanda; udhibiti na usimamizi wa ujenzi wa majengo ya ghorofa nchini ili kupunguza ajali

zinazoweza kuepukika; na Uwanja wa Ndenge Songwe upewe kipaumbele ili kazi iliyonza iweze kufikia hatima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza wote; Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi, kwa kazi nzuri. Roma haikujengwa kwa siku moja tutafika tu.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, kwa kuteuliwa na Rais wetu kuwa Waziri wa Wizara ya Miundombinu. Namtakia kazi njema za Ujenzi wa Taifa.

Ndani ya Jimbo la Kigamboni, tuna barabara ambayo *TANROAD* wameisahau na kutoishughulikia kwa muda mrefu sasa; barabara ya kutoka Kibada kwenda Tungi.

Barabara hii ni muhimu sana, hasa kwa kuzingatia sasa baada ya ujenzi wa Hospitali Ndogo ya Vijibweni iliyojengwa kwa msaada wa ndugu zetu wa Korea. Serikali kimsingi imekubali kuipandisha hadhi kutoka Hospitali Ndogo na kupewa hadhi ya Hospitali Wilaya. Hii ni kutokana na mazungumzo yetu na Viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda. Naomba kwa niaba ya wananchi, barabara hiyo ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono juhudzi za Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni takriban mwaka mmoja na miezi kadhaa imepita, kinyume na makubaliano ya awali ya ujenzi wa pantoni jipy. Wananchi wamekata tamaa; lini pantoli hili litaanza kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Jimbo la Kigamboni wanapenda kujuu hatua zilizochukuliwa na Wizara ya Miundombinu juu ya Agizo la Rais la kuiunganisha barabara inayojengwa sasa ya kutoka Rangi Tatu – Charamble hadi kona ya Kongowe kuelekeea Mjmwema. Agizo hili alilitoa wakati wa kuweka Jiwe la Msingi la Ujenzi wa Barabara ya Kilwa, kilomita 11 kutoka Bandarini – Mtoni (awamu ya kwanza). Naomba kauli ya Mheshimiwa Rais, iheshimiwe na ifanyiwe kazi.

Katika Kikao cha *RCC*, ultolewa ushauri wa kuweka uwiano wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami Dar es Salaam kwenye majimbo ya uchaguzi. Inasikitisha, kwa mara ya pili kupuuzwa kwa ushauri huo ni vyema mwaka ujao wa fedha, kuzingatia uwiano tuondoshe upendeleo.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda nipate ufanuzi wa kina; mimi pamoja na Wananchi wa Mkoa wa Kagera, kama unavyojua, kwa sasa usafiri ni wa shida sana, nitapenda kujua kuhusu meli tuliyohidiwa, sasa ni miaka kumi hatujaiona kulikoni?

Pili, kuhusu barabara zetu nitazitaja hapa niweze kupata majibu mazuri, barabara hizo ni Kyaka - Mrushaka – Mulongo na Mrushaka - Benako kwa ajili ya Kimisi -

Kyetema - Katoro - Kagoma - Rusahunga. Barabara hii ni muhimu sana kwa ajili ya majambazi Kasindaga - Kimisi pamoja na za mjini. Vichochoro vile havina barabara kwa sasa ama barabara inaonekana kama uchafu.

Naiomba sana Serikali tusiwe tunategemea wafadhili bila kutokuwa na akiba yoyote. Mtegemea cha nduguye hufa maskini, kama Uwanja wa Ndege Bukoba. Kuhusu mitandao, naomba mara kwa mara kusambaza mawasiliano sehemu zenyenye matatizo hasa ujambazi, mapori matatu Mleba, Biharamulo, Karagwe, Uzuri wa Kondoo, Karagwe, Benako. Naomba nipatiwe majibu nijue kuna tatizo gain? Nitashukuru sana.

Pamoja na Bandari za Bukoba Mjini na Kemondo kutokuwa na meli; je, Serikali haioni huu ndio wakati sasa wa kuzitengeneza bandari hizo? Nikisikia Serikali inatamka bandari nyingine, nasikitika sana; Kagera ina matatizo gani hata Viwanja vya Ndege vinatajwa vya sehemu nyingine cha Bukoba sikukisia; ni vipi ahadi tumechoka nazo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza, Waziri, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje na Watendaji wote wa Wizara hii, chini ya Katibu Mkuu, Ndugu Omary Chambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi, nitoe shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi nzuri ya kukamilisha barabara ya kiwango cha lami ile inayopita jimboni kwangu Shelui hadi Singida. Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, tumefarijika sana na juhudhi ambazo kwa makusudi zimefanywa na Mheshimiwa Rais, barabara hii ndani ya Jimbo langu Kata za Kyengege, Ulemo, Mto na Shelui zimefaidika na hali ya barabara hii, kimsingi naamini sasa milango ya kiuchumi imefunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi hiyo nzuri iliyofanyika, nashukuru sana yale majengo yaliyotumika kama Kambi (Kambi ya Shelui) na yale ya Kizaga – Ulemo sasa yamekabitihwa mikononi mwa Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Shelui na Ulemo, kwa ajili ya majukumu ya Shule ya Sekondari ya Shelui na Ulemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nisemee kidogo kazi ambayo imekamilika, ni dhahiri barabara imetengenezwa kwa viwango, lakini yapo matatizo madogo madogo ambayo kwa kiwango fulani, wananchi wanayalamikia baada ya kukamilika ni vivuko vya waenda kwa miguu kutokujengwa hasa maeneo ya Kyengege na Shelui. Kwa nafasi hii, ningeomba Wizara iiagize *TANROAD* Mkoa ili kazi hiyo ikamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kutoa changamoto kwa Wizara juu ya Matumizi ya fedha zinazotolewa/kutengwa kwa ajili ya bajeti ya Wizara kwa mwaka. Utaratibu wa sasa wa kutangaza *tender* na baadaye barabara za mikoa kuwa chini ya Mamlaka ya Bodi ya Barabara Mkoa (*TANROAD*) ni nzuri, tatizo lililopo ni

namna ya uchunguzi wa *contractors* ambao wanajenga barabara zetu. Tumeshuhudia *contractors* wengi kuwa hafifu, wakati wakitekeleza majukumu yao, utendaji wao wa kazi ni hafifu. Hapa usimamizi katika utekelezaji wa majukumu unaofanywa na *TANROAD* upo duni na ndio maana mwanya huu unajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe mapendekezo au rai kuhusu *Road Fund* kwenda Halmashauri ya Wilaya, Manispaa na kadhalika. Kimsingi suala hili lilikuwa zuri kwa maana Halmashauri yenyewe isimamie barabara zake, lakini tatizo lililojionyesha katika hizi Halmashauri ni *capacity* ndogo iliyopo, hasa ya wataalam ambao mara nyingi hushindwa kumudu utekelezaji wa jukumu la barabara kwa wilaya nzima. Katika suala hili, ningependekeza barabara zote ziendelee kuwa chini ya *TANROAD* na *TANROAD* Mkoa iendelee kubaki na Mfuko wa Barabara kwa barabara zote za Wilaya zilizopo katika mkoa husika. Ugumu wa halmashauri kutekeleza majukumu, unaotokana na Halmashauri (Watendaji) kuwa na mahusiano wa majukumu mengi, mbali na *TANROAD* ambao hubaki na jukumu moja la barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa nia njema, kutekeleza utengenezaji wa barabara ya Njia Panda ya Misigiri kuelekea Kiomboi (Makao Makuu ya Wilaya ya Iramba), kwa urefu wa kilomita kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge la Bajeti la mwaka 2005/06, Bunge hili Tukufu lilipitisha jumla ya shilinigi milioni mia tano kwa ajili ya barabara hii ili kuiwekea lami nyepesi (*otter seal*). Inashangaza tangu kipindi hicho, barabara hii imekuwa ikirukwa mwaka hadi mwaka. Katika hatua hii, kipindi hiki Serikali imeazimia kuanzia na km kumi. Ningeomba Wizara itoe kipaumbele kwa kuzingatia unyeti wa barabara hii ili kuikamilisha yote, kwa idadi ya kilomita 21. Kutokuikamilisha barabara hii katika kipindi kimoja, kutafanya ongezeko la gharama na hivyo kuna ugumu kukamilisha eneo liliosalia. Natoa rai kuzingatia wakati na kuepuka kurejea mradi mmoja mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru uangalizi wa mara kwa mara wa barabara ya Mkoa ile ya Kizaga – Ndago - Sepuka - Singida. Barabara hii sasa inahudumia watu wengi, naomba Wizara ione uzito wa mipango ya baadae kuiwekea lami. Eneo la Usure kwenye *drift* ni hatari sana, nyakati za mvua huzuia magari na watu kuvuka kutokana na maji mengi. Pia kona inayoingia eneo la mnadani (Usure), irekebishwe kwani mara kadhaa imesababisha ajali mbaya.

Naomba sasa Wizara iidhinishe ile barabara ya Shelui – Mto – Mtekente – Ndago kuwa ya Mkoa kama ambavyo Bodi ya Barabara Mkoa (*TANROAD*) tulivyopitisha. Naiomba *TANROAD* Mkoa ihakikishe barabara ya Mkoa ile ya Shelui - Mgongo – Sekenke - Nkonkilangi - Ntwike inatengenezwa na inapitika muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuteuliwa kwake kushika

Wizara hii. Pia nawapongeza wote; Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri walijotuandalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia chochote, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Wanawake na Wanaume wa Mkoa wa Pwani, kuipongeza Wizara kwa kututengenezea Kiwanja cha Ndege Mafia. Tunashukuru Mheshimiwa Rais Kikwete, kwa kusisitiza uharaka wa kukamilisha kiwanja hiki, pale alipokuja kwenye ziara Mafia. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri anaelelwa uwezo wa Wana-Pwani kwani na yeye ni katika hao; sio wengi wenye uwezo wa kupanda ndege kutokana na bei (nauli) za safari hizo. Hivyo, wengi tunategenea kwenda Mafia kuitia usafiri wa baharini. Tatizo sio tu vyombo tunavyotumia haviaminiki, lakini pia havina hata bima wala vifaa vya kujiokolea. Ili tutoke kwenye majanga haya ni muhimu tupate vyombo bora zaidi kama wanavyotumia wenzetu wa Visiwani Zanzibar, Pemba, Ukerewe na kadhalika; kwa nini tunavikosa? Jibu hatuna Gati.

Tunashukuru dalili zinaonekana za Ahadi ya Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete kwamba, Mafia atahakikisha tunapata Kiwanja na Gati. Mimi ni shahidi wa jinsi gani Wabunge wa Mafia waliopita na wa sasa walivyo na wanavyoendelea kuongelea juu ya suala hili la Gati. Miaka mingi imepita na ahadi mbalimbali za viongozi mbalimbali zimetolewa, sina hakika kama hii ya Rais wetu itatekelezeka. Nimeshudia eneo limetengewa, fidia zimelipwa na nyumba na miti (minazi na miembe) inang'olewa hapo Kilindoni. Tunashukuru, sasa tunataka tuone na huko baharini kunafanyika kitu.

Jamani hebu oneni aibu na muwe na huruma, bila kutafuta visingizio tupate Gati Mafia ndani ya muda mfupi iwezekanavyo. Kwa nini hili jambo linakuwa zito; mnataka watu wa Mafia wafanye nini? Tunahitaji maendeleo kama wengine.

Kwa sasa tunaiomba sana Serikali ihakikishe vyombo tunavyotumia (maboti), yawe na Bima, pia vyombo na vifaa vya kujiokolea wakati wa ajali. Tunakufa na tunapoteza mali bila malipo yoyote. *Why?* Kuishi Visiwani sio kosa; hivyo, hakustahili kuadhibiwa. Tunashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwa vile Waziri katika hotuba yake ametaja kuwa Makao yote ya Mikoa isipokuwa mine, imeunganishwa na Barabara na kwa kuwa katika Mikoa hiyo Arusha – Shinyanga haipo:-

(a) Je, Waziri anaweza kueleza lini Makao Makuu ya Mkoa wa Arusha – Shinyanga kupitia Makuyuni, Njia Panda (Oldeani), Mataala –Lalago Shinyanga itawekwa kwenye mpango wa utekelezaji ili barabara hiyo muhimu kwa uchumi wa mikoa hiyo na shughuli za jamii iweze kutekelezwa?

(b) Je, Waziri anafahamu kuwa barabara hiyo iliisha kufanyiwa upembuzi yakinifu na *beacon* kuwekwa na Bunge hili kuarifiwa mara kadhaa kuwa kazi iliyobaki ni kutafuta fedha, lakini Waziri katika hotuba yake siyo haelezi *progress* ya utafutaji fedha bali hazungumzii kabisa barabara hii. Naomba maelezo ya kina kwani kuna uwezekano barabara hii sasa ikasahaulika kabisa wakati Serikali imekwisha kutumia fedha.

(c) Barabara hii imetengewa mwaka huu shilingi milioni 80 tu, ambayo haitoshi kutengeneza hata kilomita moja ya changarawe. Serikali inatoa kauli gani kuhusu hali hii?

Nafurahi kuwa baada ya ahadi ya muda mrefu, Mpango wa Reli ya Tanga – Arusha – Musoma sasa imerudi kwenye Hotuba ya Waziri:-

(a) Reli hii hasa itapita maeneo gani kwa Wilaya ya Karatu?

(b) Je, upembuzi yakinifu umeshafanyika au bado, kama bado unategemewa kuanza lini ili wananchi sio tu waanze kuwa na matumaini, lakini pia kuanza kujiandaa kisaikolojia kwani ujenzi wa reli kwa vyovyote utahusisha wananchi kuhamishwa kwa kuachia njia ya Reli na pia Vituo vya Reli?

Katika hotuba yake uk. 74, Waziri anaeleza kuwa Bodi ya Mfuko wa Barabara (*RFB*), moja ya changamoto ni kucheleva kukamilika kwa taarifa za Ukaguzi wa Halmashauri kwa upande wa *CAG* wa Hesabu za Serikali. Je, Waziri na Bodi wanafahamu kuwa changamoto kubwa kwa *CAG* na kwa Kamati ya Bunge ya *LAAC* ni kucheleva kupelekwa fedha kwenye Halmashauri kiasi cha kufanya miradi siyo tu haitekelezwi katika mwaka husika wa fedha, bali pia fedha hizo zinazoonekana kutotumika, huleta *audit querry* kila mwaka. Hata kwa ukaguzi wa mwaka unaofuata, *Perfonance Audit* au *Value for Money Audit* inakuwa ngumu. Waziri anatoa kauli gani kurekebisha hali hii kwa fedha kupelekwa kwa wakati, ikizingatiwa nyakati za mvua utengenezaji wa barabara unakuwa mgumu na mara nyingi inakuwa uharibifu wa fedha?

Katika Bunge lililopita kulikuwa na Azimio la Bunge kusitisha mkataba wa nyongeza kwa Kampuni ya *TICTS*. Katika Hotuba yake, Mheshimiwa Waziri anaeleza au anatoa taarifa ya *TICTS* kupewa eneo hili, kwa mkataba wa miaka mingapi? Hotuba pia haielezi chochote kuhusu hatua za utekelezaji wa Azimio la Bunge. Je, Serikali inatoa kauli gani?

Hotuba ya Waziri katika ukurasa wa 64 – 66, inazungumzia uendeshaji wa Viwanja vya Ndege. Siku za karibuni, kumekuwa na taarifa kuhusu kukodishwa au kubinafishwa kwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam. Nilitegemea Hotuba ya Bajeti ni njia mwafaka ya kuliarifu Bunge kuhusu mpango

wowote wa ukodishaji wa Uwanja muhimu kama wa DIA ili Bunge liweze kutoa ushauri stahiki sasa:-

(a) Waziri anaweza kiliarifu Bunge hili kuhusu Taarifa hizo za kukodisha, nia au mchakato wa kukodisha au kubinafisha Uwanja wa DIA?

(b) Iwapo mchakato huo upo, ni taratibu zipi zimefuatwa; *Tender* zimetolewa lini, makampuni mangapi yamejitokeza hadi sasa na mchakato upo kwenye hatua gani hasa na unategemewa kukamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpngeza Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Chibulunje, Katibu Mkuu, Eng. Omari A. Chambo, Naibu Katibu Mkuu, Bibi Mapunjo na Wataalam wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha ya dharura ili kufungua Mkoa wa Tabora kwa njia ya Manyoni - Itigi – Tabora. Kwa kweli imewatia moyo wakazi wa mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imeonyesha mipango na matarajio ya kuongezwa ratiba ya treni ya abiria kwa kuongeza siku toka mbili hadi nne. Pamoja na hayo, ningeshauri utekelezaji wake uanze mapema, kwani huduma hiyo ni muhimu sana. Kutokana na kutokuwa na usafiri wa uhakika ni vyema Serikali ikasimamia kuliko kuiachia *TRL*.

Chakula cha ndani ya treni ni kibovu na hakifai kwa afya ya binadamu. Hata vyombo vyao ni vichafu na vichakavu. Huduma hiyo hujali sana mambo ya vilevi (pombe) kuliko chakula. Mtendaji huyo afuatiliwe.

Kwa kuwa Chuo cha Reli cha Mkoa wa Tabora kina historia ndefu ni vyema kikaimarishwa zaidi kama ilivyokuwa mwanzo. Chuo hicho asiachiwe mwekezaji ili tupate wataalam Watanzania ambao wana uchungu na nchi yao

Vituo vya njiani (*Gang*), tangu amefika mwekezaji amefunga makambi mengi ambayo yalikuwa yanasa idia usalama wa reli, hasa kwa ukarabati mdogo mdogo (pigilia), arudishe ili angalau mawasiliano yawepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hotuba imetamka Kiwanja cha Ndege cha Tabora, kwa kweli Serikali iangalie angalu ukarabati mdogo ili wakati wa masika ndege ziweze kutua kuliko ilivyo hivi sasa, kwani hutua kwa tabu. Wakati upembuzi yakinifu unaendelea, ningomba kiwanja kiwekwe kwa kiwango cha changarawe (kokoto).

Barabara ya Sikonge – Urambo kupitia Tutuo iangaliwe ili ichukuliwe na Serikali Kuu, kwani Halmashauri zetu haziwezi kutengeneza kutokana na kutokuwa na vyanzo vya mapato vya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Uyui inakabiliwa na tatizo la ujenzi wa nyumba za watumishi, ambao mpaka sasa unasua sua, kwani fedha inayotengwa ni kidogo kiasi kwamba, haiwezi kutosheleza kukamilisha ujenzi huo. Je, Serikali haionti sasa umefika wakati wa kugawa utekelezaji huo kwa mashirika ambayo yanaweza kujenga na kuwapangisha watumishi wadogo kwenye Wilaya ambazo ni mpya kama vile *NHC, PPF, NSSF* na kadhalika ili kukidhi mahitaji hayo na kusogeza huduma karibu na wananchi.

Kwa kuwa madaraja mengi hujengwa kwa kiwango cha chini na kwa ujanja na kusababisha ujenzi huo kurudia mara kwa mara; je, inapotokea Mkandarasi huyo kusababisha uharibifu huo Serikali inachkukua hatua gani ili iwe fundisho kwa wajenzi wa aina hiyo hapa nchini, hali hiyo hujitokeza wakati wa masika husombwa na maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN S. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ya kina. Mimi katika mchango wangu, ningependa kujikita katika mambo muhimu matatu:-

Kwanza, hivi sasa tatizo kubwa la miundombinu nchini ni Barabara Vijijini. Tatizo hilo, ndiyo linalochangia sana kufanya maendeleo vijijini kuwa duni. Upungufu huu huwalazimisha wananchi kusafiri maili nyingi kwa miguu na kufanya uwezo wa kuuza mazao kuwa kazi ngumu.

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, katika bajeti ijayo waongeze ruzuku kwa Serikali za Mitaa. Tusingahau karibu asilimia 80 ya wananchi wetu wapo vijijini. Ruzuku hizo zitolewe kwa wakati unaotakiwa ili ziweze kutumika wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kusemea Jimbo la Mtera. Katika Jimbo la Mtera, naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri, Wizara yake izifanyie ukarabari barabara zifuatazo ziwe za Mkoa ili zihudumiwe na *TANROAD*.

(a) Handali – Ng’hahelezi, Chinoje - Citamo - Gulwe hadi Mpwapwa. Hii itaunganisha Majimbo ya Mtera – Kibakwe na Mpwapwa. Barabara hii itapita katika sehemu yenye watu wengi ambao hulima Zao la Karanga kwa wingi, ambazo huhitaji kufikishwa kwenye masoko na pia kurahisisha mabasi kuhudumia sehemu hizi. Mkoa umekwishatoa mapendekezo ya barabara hii.

(b) Barabara ya kutoka Mpunguzi – Mwitikira – Nagulo – Huzi – Manda – Ilangali – Ruaha National Park, ikipandishwa hadhi itakuwa njia fupi kuliko zote kwenda Mbuga za Wanyama Ruaha. Hii italeta faida ya kuinua hadhi ya utalii Mkoa wa Dodoma na

Wananchi wa Tarafa za Mwitikira na Mpwayungu ambao sasa wana adha kubwa ya usafiri hasa wakati wa masika. Mkoa umetoa mapendekezo ya barabara hii.

(c) Barabara ya Fufu – Suli – Chiboli – Chamhumba, ikipandishwa hadhi ndio itakuwa njia ya ukakika kwa wengi wa wavuvi wa Bwawa la Mtera.

Sasa ningependa kusemea Miradi miwili ya Kitaifa Mkoa wa Dodoma; Barabara ya Minjingu - Babati - Kondoa - Dodoma hadi Iringa kujengwa kwa lami. Nataka nimkumbushe Waziri kuwa, ahadi ya kujenga Barabara hii kwa kiwango cha lami imekuwa ya tangu miaka ya sabini. Safari hii namwomba Waziri atoe ratiba ya uhakika, juu ya ujenzi wa barabara hii.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Dodoma (Chitelela); Mradi huu umeahidiwa tangu uamuzi wa kufanya maamuzi ya Dodoma kuwa Makao Makuu. Matokeo yake *CDA* ikapima na kugawa viwanja na kujengwa, kiasi kwamba hivi sasa kiwanja kidogo cha Dodoma ni hatari sana. Maana nyumba za wanachi zipo si zaidi ya mita 100 kutoka barabara (*runway*) ya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri atoe kauli thabiti kuhusu Mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nimpongeze Waziri wa Miundombinu kwa hotuba yake ya kina. Ninamtakia afya njema na maisha mrefu ili tundelee kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Kwanza, naipongeza Serikali kwa kumpata mkandarasi wa kujenga barabara kipande cha Ndunu - Somanga. Hongera sana.

Ningependa kujua mipango ya Serikali ya kujenga barabara ya lami kati ya Mtambawala hadi Mangaka. Daraja la Umoja (*Unity Bridge*), karibu litakamilika; je, ni sawa kweli kwa daraja lile kuunganishwa na barabara inayofanana na kichochoro?

Ni lini Serikali itajenga Daraja la Mto Kilombero? Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Kivuko cha Kilambo, kwani Mto Ruvuma ni mrefu sana? Daraja moja la Umoja halitoshi hivyo mipango ya kuboresha Kivuko cha Kilambo ni muhimu sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya lami ya Mangaka hadi Tunduru?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa mipango ya kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa iliyobaki kwa lami lakini, ifikirie kujenga reli kati ya Mtwara hadi Songea – Mbambabay.

**MHE. FRED T. MPENDAZOE:** Mheshimiwa Naibu Spika,, naomba niunge mkono hoja ya Miundombinu.

Nitachangia kwa kifupi eneo la barabara. Katika mwaka wa fedha 2007/08, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kufanya upembuzi wa kina, kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kolandotto – Lalago – Mwanuzi yenyen urefu wa kilomita 121.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2008/09, barabara ya kutoka Kolandotto – Lalago – Mwanuzi haikutajwa na haikupangiwa fedha yoyote (haiopo kwenye orodha ya miradi).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipoitembelea Wilaya ya Kishapu akiwa ameambatana na Waziri wa Miundombinu, Waziri huyo aliwahakikishia Wananchi wa Kishapu kwamba, barabara ya Kolandotto – Lalago kupitia Mlunze itaanza kujengwa. Aidha, wakati Mheshimiwa Rais, alipokuwa akiomba kura mwaka 2005, aliwaahidi Wananchi wa Kishapu kwamba, barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kutoka Kolandotto hadi Lalago ni muhimu sana kwa Wananchi wa Wilaya ya Kishapu, Maswa, Meatu na Bariadi. Hivyo, ninaomba Wizara ifanye *re-allocation* na ipewe kiasi cha fedha, upembuzi uendelee kufanyika ili hatimaye ujenzi uanze.

Katika Hotuba ya Bajeti, Mheshimiwa Waziri ameelza kwamba, upembuzi kwa barabara ya Maganzo – Maswa umekamilika, lakini hajaeleza ujenzi utaanza lini. Naomba Serikali itoe *commitment* kwa wananchi watakaonufaika na barabara hiyo ujenzi huo utaanza lini.

**MHE. EMMANUEL J. LUAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ulinzi wake ambao anaendelea kunipa na kuliongoza Bunge lake Tukufu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara, kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu upo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara Kuu ya Isaka – Kahama – Bukombe – Rusahunga, naomba Serikali iangalie kwa makini sana. Barabara hii imeharibika sana na kusababisha ajali kila wakati. Naomba Serikali itoe ufanuzi ni lini itaanza kujengwa upya?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ndiyo inayounganisha nchi ya Tanzania na nchi jirani za Rwanda, Burundi na Uganda. Katika Vikao vya Mkoa, *Road Board* waliahidi kuwa itafumuliwa upya, naomba iangaliwe kwani ni chanzo kizuri cha uchumi toka nchi jirani, pamoja na maeneo ya Isaka, Kahama, Bukonge na Rusumo.

Barabara ya Ushirombo (Bukombe) - Buseresere (Geita), wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Ushirombo tarehe 23 Agosti, 2007, aliahidi kuitengeneza kwa kiwango cha moramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa masikitiko yangu kutokana na barua ya tarehe 26 Juni, 2008 toka Wizara ya Miundombinu kuja au kwenda kwa Mbunge wa Bukombe, maelezo yaliyomo kwenye barua siyo sahihi. Mheshimiwa Rais katika ziara yake, wakati anaahidi kupitia kauli ya aliyekuwa Waziri wa Miundombinu, matengenezo hayo madogo madogo yalikuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Sheria ya Mfuko wa Barabara iliyopitishwa mwaka 2007, barabara hii haionekani mahali popote, halimo kwenye barabara za Wilaya, Mkoa wala Taifa. Naomba mfanye ufuatiliaji, kwani sisi Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe hatuihudumii barabara hii bali ni mali ya Mkoa.

Naomba Serikali iwaeleze Wananchi wa Bukombe ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha moramu kam ilivyoadhidi tarehe 23 Agosti, 2007, mbele ya Wananchi wa Bukombe?

Barabara ya Runzewe – Bwanga, ni barabara ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga kwa kiwango cha lami. Naipongeza Serikali katika barua yake ya tarehe 26 Juni, 2008, isiyokuwa na Kumbukumbu kwenda kwa Mbunge, wameendelea kuitambua. Naomba Serikali ifanye kila liwezekanalo ili mwakani (2009/2010), barabara hii itengenezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Iyogelo – Bugelenga – Nsanga – Iponya – Masumbwe – Lugunga – Bwelwa – Ivumwa, tumeitolea mapendeleko ya kuipandisha hadhi kuwa Barabara ya Mkoa, kwani Bukombe ina mfumo mkubwa sana wa barabara, lakini nyingi ni za Halmashauri za Wilaya. Tunaomba tupunguze mzigo kwenye Wilaya hiyo ili iweze kufanya mambo mengine ya maendeleo.

Naiomba Serikali iharakishe mchakato wa kujenga Reli ya Isaka - Kahama - Bukombe - Kigali, naamini itasaidia sana kuondoa uharibifu wa Barabara ya Isaka - Kahama - Bukombe - Rusahunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa jitihada ambazo inaendelea kuzifanya kwa ajili ya Baraba ya Dodoma – Manyoni – Singida – Shelui – Nzega. Naomba iendelee kumpatia msukumo Mkandarasi ili aweze kukamilisha kipande kidogo kilichobaki maeneo ya Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kati imekuwa kero kwa wananchi wa kanda ya kati, kwani hali ni mbaya sana na ninyi ni mashahidi wa hilo. Naomba Serikali iwe na usimamizi wa karibu ili kuboresha na kusaidia wasafiri wa Kanda ya Kati.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati wa hotuba yake, aliliahidi Bunge hili kuwa, Barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora - Kaliua - Kigoma itajengwa. Inasikitisha kuona barabara iliyohadiwa kwa dhati 2006/07, 2007/08, inakosa bajeti. Naamini barabara hizi zitakamilishwa kabla ya mchakato wa uchaguzi 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Serikali ifanye mgawanyo wa rasilimali vizuri katika Kanda zote, hii ndiyo inadumisha umoja wa Watanzania. Si vyema kila mara kutumia nguvu kutafuta haki ya wananchi. Ingawa mwandishi mmoja alisema nanukuu: *"The door of opportunity will not open, unless you do some push."* Tutumie uungwana ambao ni tunda la Watanzania.

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri aliyoitao leo asubuhi. Kwanza, naanza kuchangia suala la usafiri wa barabarani. Usafiri huu umekuwa ziraili mkubwa kwa Wananchi wa Tanzania, kwani kila siku ukisikiliza taarifa za habari, utasikia ajali za barabarani na wananchi wanakufa. Sababu kubwa ya ajali hizo ni magari mengi mabovu na wala hayafanyiwi ukaguzi.

Suala la pili ni mashimo yaliyokuwepo barabarani, yanakaa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo kwa wakati. Usafiri wa majini; bado usafiri wa maboti una matatizo ya kupakia mizigo na watu bila kukaguliwa na vyombo husika na mara zikiondoka kwenye bahari ajali hutokea na wananchi hupoteza maisha na mali kupotea.

Baada ya ajali kutokea, hakuna tena fidia wanayolipwa ndugu wa marehemu, waliopona wala fidia ya mali zao. Tuseme hizi boti hazina bima, lakini ningependa kutoa ushauri kwenye bahari zote zinazopakia abiria, kuwepo na wataalam wanaoweza kuwaleza makapteni wa vyombo hivyo, kutopakia abiria na mizigo kwa kiwango kilichozidi uwezo wa chombo hicho. Ili kuепusha ajali, kila chombo cha majini kinachopakia abiria kinatakiwa kiwe na vyombo vya kuokolea maisha, pia wawe na mabaharia waliopitia kwenye vyuo vinavyotambulika.

Madereva wa magari nao leseni zao ziwe zinakaguliwa, kwani kuna madereva wengine leseni zao huwa wanaletewa majumbani na kupelekwa kwa matajiri wa magari. Matajiri huwakabidhi magari hayo bila ufuatiliaji wowote na baada ya kusababisha ajali, ndio idara husika inashtuka na kuanza kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Dar es Salaam bado inawasumbua wananchi kutokana na mizigo kukawia. Hii inatokana na mizigo hiyo kuwa nusu kwa nusu (inaibiwa). Tatizo la Bandari yetu lichunguzwe kwa makini. Hawa wanaoiba mizigo inapokuwa bandarini ni akina nani, kwani sehemu ya bandari yote huwa

inalindwa na vikosi tofauti; leo ni ajabu kuona hata redio za magari yakiwa hapo bandarini huibowi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuliendesha Bunge kwa umahiri mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Miundombinu, kwa hotuba nzuri, yenye mvuto na iliyojaa matumaini kwa Chama cha Mapinduzi na Watanzania kwa ujumla. Hotuba ya Miundombinu imetuonyesha dira, kwa kutukumbusha tulikotoka, tulipo na mwelekeo wa tuendako.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha bajeti kwa ufasaha na umakini mkubwa, ikiwa ni pamoja na kutumia muda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri ameahidi kuwa mwaka 2008/09, Serikali kuititia Miundombinu, itanunua boti kwa ajili ya kuvusha wananchi katika Kivuko cha Mtwara – Msangamkuu. Je, suala hili limezingatiwa kwenye bajeti hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege Mtwara kimejengwa miaka mingi iliyopita, sasa hivi kwa kweli uwanja unahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara iwekeze kwenye Bandari ya Mtwara na iruhusu wafanyabiashara wanaoomba kuitumia bandari hiyo ili bandari itumike kikamilifu.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri sana, hasa ubunifu wa kuwianisha utekelezaji na malengo ya Ilani. Nilikuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuanzia mwaka 1995 hadi nilipostaafu kwa mujibu wa sheria.

Wizara ya Miundombinu ina umuhimu wa kipekee kwa ustawi wa nchi yetu; ni kubwa, ngumu na ina changamoto nyingi, lakini inaleta faraja kubwa kwa wananchi, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wahandisi, kila hatua ya ufanisi. Mimi binafsi, Mheshimiwa Anna Abdallah na Mheshimiwa Magufuli, tulifarijika sana kufanikisha ujenzi wa Daraja la Mkapa, Mto Rufiji mwaka 1998. Nawatakia Viongozi na Wataalam wa Wizara kila la heri na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Nashauri Wizara izingatie Maombi yafuatayo na kuyatolea tamko katika majumuisho:-

Kwanza, Barabara ya Mombo – Lushoto – Mlola ni nyembamba sana, ina *blind corners* nyingi na ina magari mengi makubwa. Tunaomba ipanuliwe na *blind corners* zirekebishwe ili barabara hii iwe salama.

Pili, Barabara ya Mombo – Doch – Lushoto ni muhimu sana kama barabara mbadala kati ya Mombo na Lushoto, hasa inapotokea ajali na Barabara ya Mombo – Soni – Lushoto kujifunga. Ni vyema barabara hii ya kilomita nane iwe ya Mkoa.

Tatu, Barabara ya Mlalo – Ngwelo – Mlola – Makanya ni kiungo muhimu kati ya Tarafa za Mlalo na Mlola. Ngwelo na Makanya ni *terminal* kwa mabasi makubwa yaendayo Arusha, Tanga na Dar es Salaam. Hivyo ni vyema zikawa za Mkoa chini ya *TANROAD*.

Nne, Nyumba za Watumishi wa Serikali Wilaya ya Lushoto kwa sasa hakuna hata moja, ukiacha ile ya DC; ni lini nyumba zitajengwa?

Tano, Reli ya Tanga - Dar es Salaam - Tanga - Arusha – Voi; je, itaanza kutoa huduma lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wataalam na Watendaji wao wote, kwa jitihada zao za kuifanya wizara hii iwe na uhai, utendaji mzuri na wenye matarajio mazuri ya baadae, kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ameelezea nia na jitihada za kuonyesha nia ya ujenzi wa Darala la Kigamboni, kwani ujenzi wa Daraja hilo ni siasa kwa wakazi wa eneo hilo.

Nilitegemea sana leo hii, angalau kwa kiasi wangelitoa uchambuzi wa hatua waliyoifikia katika mchakato mzima wa ujenzi wa Daraja hilo, kwani Watanzania wengi wana hamu ya kuelewa nini kinachoendelea katika ukimya mkubwa uliotawala kwenye ujenzi wa Daraja hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwenye Kitabu chake cha Hotuba alichokiwasilisha kwetu, kilichoishisha *NSSF* kama tegemeo la kwanza katika ujenzi huo; je, Serikali imejipanga vipi na kwa kiasi gani kuhusu kukamillisha ujenzi wa Daraja la Kigamboni?

Mheshimiwa Naibu Spika, pale *Ferry* Kigamboni kuna askari walioajiriwa na Wizara hii kwa ajili ya kupanga magari, kupokea tiketi na kufungua na kufunga mageti, hali zao sio nzuri. Watu hao niliowataja wanaofanya kazi ngumu bila kuajiriwa rasmi na

baadhi yao wako hapo kwa zaidi ya miaka sita bila kuajiriwa. Hali hii inawafanya wasijielewe na wasijue wanafanya nini, kwani wakati wowote wanaweza kuondolewa kwa kuwa pale wao wapo *temporary* tu, sio kazi ya kudumu. Naomba sana Wizara ione umuhimu wa watu hao ili wajijue, kwa kuwa na kazi yenye uhakika ambayo watafaidika kwa kupata mshahara kwa mwezi, kwenda likizo, kupata matibabu na mambo mengi mengine yanayomhusu mwajiriwa mwingine yejote ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya kuimarisha reli zetu pamoja na njia zake, kwani huduma za reli ni mbaya sana, tofauti na matengenezo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Shirika hili kubinafsishwa, tuligegemea kuona mabadiliko ya utendaji wa Shirika hili, lakini matokeo yake yamezidi kuwa mabaya kuliko hata ilivyokuwa hapo mwanzoni. Napenda kutumia nafasi hii, kumwomba sana Mheshimiwa Waziri, aliangalie sana Shirika hili ili watu wanaotumia reli hii, wafurahie huduma na wasilalamike kila siku kwa kukosa huduma nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ili nitoe mchango katika sekta muhimu ya kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitishwa na kutopewa pesa ya barabara yangu ya Misasi – Mbarika, ambayo imekuwa ikitengewa pesa kwa mwendelezo wa miaka mitatu. Katika taarifa ya Kamati iliyotolewa Dar es Salaam, ilionekana ikiwa imetengewa Sh. 60,000,000, cha ajabu katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ameifuta! Naomba sana Mheshimiwa Waziri, awafikirie wananchi wa maeneo hayo, wana matatizo makubwa na aruhusu pesa zilizokuwa zimetengwa. Naambatanisha kivuli cha mgao uliokuwa umenipa katika Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, haujaonyesha mkakati wa kutia moyo. Pesa zilizotengwa ni kiasi cha Sh. 1,000,000,000; hizi ni pamoja na Uwanja wa Kigoma. Serikali inapaswa kuona hali ilivyo na kutoa kipaumbele, kiasi kilichotengwa ni kidogo mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufanuzi hasa juu ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, umesema kuwa mchakato wa kumpata Mkandarasi kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanja hicho. Je, huyo Mkandarasi atapanua kiwanja hicho kwa Sh. 1,000,000,000 tu kwa kugawana na Kigoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Salawe – Misasi – Mwanangwa kupewa Sh. 60,000,000,000 ni kutoifanya isipitike mwaka mzima.

Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, aliwahi kuwa Waziri wa Maji na aliona tatizo linalowakabili wananchi hasa Mradi wa Maji toka Ihelele hadi Shinyanga na Kahama. Mheshimiwa Waziri, Mradi huo unakaribia kuzinduliwa lakini tatizo ni

Barabara ya Buhingo – Seeke – Nyamayinza – Mbalama – Isesa - Ihelele km kati ya 39. Barabara hii inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya lakini kwa sasa imekuwa ikipatiwa matengenezo ya sehemu korofii na Mradi tu; kuna hatari ya kutofikisha vifaa na dawa kwa ajili ya kutibu maji.

Tafadhli sana, Waziri kwa vile unafahamu umuhimu wa barabara hiyo, naomba ufanye yafuatayo: Hakikisha barabara hiyo inakuwa ya mkoa na iwe inapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahadi ya Serikali kupandisha baadhi ya barabara za Halmashauri kuwa za Mkoa ifanyike kwani baadhi ya barabara hazijatengenezwa muda mrefu, zinahitaji msaada wa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Barabara ni chombo ambacho kinaonyesha kuwakomboa Watanzania kwa kazi walizopanga kuzifanya 2008/09, iungwe mkono hasa pindi wanapofanya ziara ya kufutilia matumizi ya pesa waliyotoa. Ni jambo la ajabu, mtoa pesa hajui nini kimefanyika na kwa bahati Watendaji wa Mfuko baadhi ni Wahandisi; hivyo *value for money* itasaidia kufahamu kuliko kupoteza pesa; hivyo tunawaunga mkono wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ERB* na *CRB* ni vyombo vytaalam wa uhandisi ni vyema wakapewa kila kinachohusika ili kazi yao ifanyike kwa ufanisi. Suala la kuanguka kwa ghorofa la Dar es Salaam ni aibu kwa vyombo hivi. Usajili wa Wahandisi na Makandarasi usiwe na upendeleo, unatufanya tuaibike kwa kazi zinazofanywa na wazalendo hivyo kushusha taaluma yetu nzuri ya Watanzania tuliyonayo. Hali hii inafanya tuwaamini Wahandisi wa nje badala ya Wazalendo, kitendo ambacho si kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (*AQSEB*) ni chombo muhimu kipewe kipaumbele, baadhi ya kazi zake zinaingiliwa na Wahandisi wa Ujenzi hivyo, Serikali ione mipaka ya kila chombo ili tuweze kuitekeleza vyema Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ombi langu ni Misasi – Mbarika iliyotengewa leo milioni 60.

Pongezi kwa Serikali juu ya Kivuko cha Kigongo – Busisi, Mv Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri afafanue ujenzi wa Barabara ya Kissisa – Usagara – By pass; mbona kimya?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema Wizara na tupo pamoja.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba ya bajeti. Nampongeza vilevile Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote.

Kwanza, naishukuru Serikali kwa kutuma fedha za kukarabati Kivuko cha Pangani na *engine* mbili za kivuko hicho, lakini bado zinahitajika pesa za ziada kwa ajili ya kununua vipuli vipyta vya *Propulsion Unit* na *Gear Box* zake. Bila ya kutengemaa *Propulsion Unit* bado kivuko kinaweza kuhatarisha maisha ya wananchi na mali zao.

Pili, naishukuru Serikali kwa kuweka saini mkataba na kampuni ya Jons Gram Hanssen As kutoka Denmark kwa ajili ya kivuko kipyta. Ningependa kufahamu, kivuko hicho kinaundwa wapi ni hapa nchini au nchi gain? Ili niweze kufuatilia kwa karibu zaidi ni muhimu nijulishwe, nisipojibwa nitahoji kwenye vifungu vya kupitisha bajeti.

Naishukuru Serikali kwa hatua ya upembuzi yakinifu inayoendelea kwenye Barabara ya Bagamoyo – Pangani – Tanga ni matumaini mazuri kwa wananchi wa Ukanda huu, ili isaidie kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na kukuza uchumi wa nchi na hasa utalii katika Hifadhi ya Sadani.

Baada ya kujulikana gharama za ujenzi wa Barabara ya Bagamoyo Pangani – Tanga, kuna wasiwasi kuwa baada ya kukamilika barabara ya Tanga - Morogoro tutaathiri uchumi wa nchi, kwa maana mizigo mingi itakwenda Bandari ya Mombasa. Suluhisho ni kuanza ujenzi wa Bandari ya Tanga (Mwambani), ili kutoa ushindani wa Bandari ya Mombasa ama sivyo tutaua Bandari ya sasa ya Tanga na mizigo ya Bandari ya Dar es Salaam itapungua.

Mheshimiwa Waziri, naomba nipatiwe fedha kwa ajili ya barabara zifuatazo: Pangani Mjini – Kumba Mtoni Sh. 10,000,000; Mwembeni – Madanga – Bushini Sh. 15,000,000; na Masaika – Kigumisimba Sh. 15,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa, nitapewa maelezo mazuri juu ya hoja yangu. Naunga mkono hoja ya Wizara ya Miundombinu.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinnu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wao, kwa kazi nzuri. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuipa uzito Barabara ya Kagoma - Muleba – Biharamulo - Lusahunga (154 km).

Hatua ya Mheshimiwa Rais kueleza waziwazi kutoridhishwa na utendaji kazi wa Kandarasi wa Kichina, wakati wa ziara yake Muleba, aligusa moyo wangu na Wananchi wa Muleba Kusini. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Aidha, kila anapopata fursa ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara nchini, huwa hasahau kuitaja Barabara ya Kagoma – Muleba – Biharamulo – Lisahunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, atoe ufanuzi wa maelezo yake uk. 34, ibara ya 48 na 49. Barabara ya Kagoma – Muleba - Lusahunga haikutajwa katika Miradi ya Barabara Kuu ambayo utekelezaji wake unaendelea! Katika kiambatisho Na. 2 (Uk.154 code 4181), Barabara ya Kagoma – Muleba – Lusahunga inaonekana kutengewa Sh. 15,895,250; je, ukweli ni upi, itatengenezwa mwaka huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo kushusu madai ya fidia ya Wananchi wa Muleba waliovunjiwa nyumba zao. Naibu Waziri aliyepita, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, alitoa ahadi mbele ya Rais na Umma, mwanzoni mwa mwaka huu kwamba, yanafanyiwa kazi. Je, watalipwa lini tuondoe kero hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufanuzi kuhusu Sh. 1,000,000,000 zilizotengwa kukarabati Kiwanja cha Ndege cha Bukoba. Je, kitawekewa lami? Bukoba hupata mvua nyingi mfululizo karibu miezi kumi, kutoweka lami ni kupoteza fedha na kuhatarisha maisha ya wananchi na viongozi wao. Mheshimiwa Rais, ameteseka kutua Geita wakati wa kuingia kutoka Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo kwa nini Serikali haikuweka fedha za kununua meli kubwa ya abiria kwa ajili ya Ziwa Victoria? Aidha, kwa nini hakuna mpango wa kununua meli kubwa ya kubeba mabehewa (*Wagon Ferry*) kuisaidia MV Umoja? Je, Bandari ya Kemondo ambayo ina reli; uzito wake na umuhimu wake umeshushwa? Serikali inajua wawekezaji hawakujitokeza kuweka meli kubwa; ni hatari kwa maisha yetu, tuisahau ajali ya MV Bukoba. Nasubiri ufanuzi wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuendeleza miundombinu.

Naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuweka lami Barabara ya Katoma hadi Kanyigo ambayo ni ya Mkoa. Barabara hii ni muhimu sana hasa eneo la Kajai, ambalo limekuwa likisumbuliwa sana na mkondo wa maji. Eneo la Kajai lina tingatinga na linahitaji kuongezewa madaraja ya kuruhusu maji kupita. Hivi karibuni barabara hiyo ilifanyiwa matengenezo makubwa. Kwa kuwa tayari imefanyiwa matengezo makubwa, itakuwa jambo jema kuiwekea lami au lami nyepesi ili kuepuka kutumia fedha nyingi kila mwaka za ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isaidie kuwezesha ujenzi wa Daraja katika eneo la Kabingo. Wataalam kutoka *European Union* walishatembalea eneo hilo na walikubaliana na hoja ya kujenga daraja eneo la Kabingo ili kuweza kuunganisha Wilaya ya Missenyi, kwa kuunganisha Tarafa ya Kiziba na Tarafa ya Missenyi. Barabara niliyoieleza ya Katoma hadi Kanyigo na Daraja la Kabingo ipo katika Wilaya ya Missenyi, Jimbo la Nkenge.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu, kwa kazi nzuri ya kuandaa bajeti hii ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2008/09.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, ninapenda sasa nitumie fursa hii, kutoa maoni yangu kuhusiana na hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukio lingine la hivi karibuni la kuanguka kwa jengo lenye ghorofa kumi ni changamoto kwa Serikali ya kuangalia uwezekano wa kuzuia matukio kama hayo hasitokee kamwe.

Nchi yetu haina Sheria ya Majengo kwa sasa, hivyo kutungwa kwa Sheria hiyo kutasaidia sana kuwadhibiti wakandarasi wasiokuwa na uwezo, ikiwa ni pamoja na wenye majengo, kuwapa adhabu kali na hata kuwa na viwango vyta majengo vinavyokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakandarasi wetu hawawezi kuwa wazoefu na wenye uwezo na ujuzi wa kutosha, pasipokuwa na mikakati ya kuwawezesha kifedha ili wawze kununua vifaa vyta ujenzi wa barabara vyta kisasa. Hivi ule Mfuko wa Wakandarasi Serikali imechangia kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mikakati gani Serikali imepanga kuondoa upungufu wa makadarasi wenye uwezo, ujuzi, vifaa na uzoefu wa kutosha katika Sekta ya Ujenzi wa Miundombinu kama changamoto?

Kutokana na utaratibu huu wa Miradi Maalum ya Ujenzi wa Barabara, bila shaka kuna faida na hasara zilizojiteza tangu kuanza kwa miradi hiyo. Kama zipo ni zipi hizo kitaalam/kiufundi kwa kuzingatia gharama za ujenzi, muda wa kukamiliaka ujenzi na viwango kwa kulinganisha na ule utaratibu tuliouzoea? *Design, tendering and contract; je, Serikali itaendelea na uratibu huu au basi tena?*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikilipa fedha nyingi sana zinazotokana na adhabu ya ucheleweshaji wa malipo ya *Certificates* zinazowasilishwa na Wakandarasi kwa mujibu wa mikataba. Fedha hizo zinazotokana na *penalty* au *compensation*, kama *certificates* zingelipwa kwa muda muafaka wa makubaliano kimikataba, zingeweza kutumika kwa kuongezea urefu fulani wa angalau kilomita kumi za barabara hatua ya lami.

Ninashauri Serikali itenye fedha za miradi iliyosainiwa kwa kila mwezi kama ilivyokuwa Awamu ya Tatu ya Utawala. Vilevile kuanzishwe Mfuko wa Fedha za Miradi iliyosainiwa na inatekelezwa (*Road Implementation Fund Projects*). Serikali pia isiingie mikataba ya miradi ambayo upatikanaji wa fedha utakuwa si wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndege za Serikali zinakabiliwa na uhaba wa marubani kutokana na marubani wake kuijunga na mashirika mengine ya ndege, kwa kufuata mishahara mizuri. Pamoja na kwamba, kuna demand kubwa ya marubani nchini, hata hivyo, mishahara wanayolipwa na hata wahudumu wa ndege za Serikali ni ya chini mno ukilinganisha na mashirika binafsi ya ndege ya hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/09, Serikali hajatenga fedha za matengenezo ya Ndege za Serikali. Ninalotaka kujua ni kama ndege hizo zinaweza kutumika kwa mwaka mzima bila ya kufanyiwa matengenezo na kama Sheria za *ICAO* zinaruhusu? Kama sio, kuna mikakati gani mbadala ya kuzifanya matengenezo ndege hizo ili zitumike kwa mwaka mzima?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*), ndiyo Msimamizi Mkuu wa Viwanja vya Ndege Tanzania. Mamlaka hii haina vyanzo vya kutosha vya mapato kwa kuendesha shughuli zake. Pamoja na ufinyu wa vyanzo hivyo, Serikali bado inachukua mapato yake kwa asilimia kubwa, yanayotokana na *airport charges* na kupeleka Mfuko wa Hazina na kubakiwa na kiasi kidogo sana cha fedha, ambazo huwa hazikidhi mahitaji ya shuguli za majukumu makubwa iliyopangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili *TAA* ifanikishe majukumu yake iliyopangiwa na Serikali ni vyema fedha au mapato yatokanayo na *airport charges* zote zitumike kwa shughuli za *TAA*. Hata hivyo, pamoja na ufinyu wa fedha, *TAA* wanafanya kazi nzuri na kama watawezeshwa kwa kuachiwa mapato hayo, watafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahra midogo kwa Watendaji wa *TANROADS* ukilinganisha na wanayolipa Wahandisi na Wataalam wa *TANROADS* na wa Sekta nyingine ni midogo, pamoja na kwamba, sifa zao zinaweza kuwa sawa. Hivi kuna sababu zipi za msingi kwa Serikali kuwalipa wataalam wake wenye sifa linganifu mishahra inayotofautiana? Majukumu ya Watalam wetu wa *TANROADS* ni magumu sana na wao ndio Wasimamizi Wakuu wa Miradi ya Maendeleo ya mikoa yote nchini. Wataalam wetu tusiwavunje moyo, walipwe mishahara inayostahili ili kuwapa uwezo zaidi wa kusimamia miradi yetu vizuri, badala ya kuendelea kuwalaumu kuwa wanakula rushwa. Jambo la kula rushwa kwa wataalam wa *TANROADS* halipo kama wengi wanavyofikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha inayotengwa kwa ajili ya matengenezo ya Reli ya *TAZARA* kwa mwaka wa pili mfululizo (Sh. 100,000,000), hazitoshii wakati *TAZARA* inakabiliwa na ukata mkubwa. Serikali iangalie utaratibu wa kuiongezea *TAZARA* fedha zaidi angalau reli hiyo kwa upande wa Tanzania, iwe imeboreka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu, kunijalia uzima na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, napenda kujua au kupata maeleo kuhusu barabara ya kusini; Mikoa ya Lindi na Mtwara, kile kipande cha kilomita 60 cha Msitu wa Muhoro ambacho ni kibaya sana hasa wakati wa mvua huwa kinakuwa na tope jingi na isitoshe ni kwenye

msitu na hivyo hupata watu wabaya hupata nafasi ya kufanya vitu viovu. Hivyo, ninaiomba Serikali ikiangalie kipande hiki muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuchukua fursa hii, kuzungumzia Barabara ya Tanga – Horohoro. Barabara hii ni muhimu inaunganisha nchi ya Tanzania na Kenya, kila siku tunaambiwa ipo katika upembuzi yakinifu, upembuzi huo utamalizika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni kuhusu viwanja vya ndege hasa vile vya vumbi, ambavyo havina lami, kwa mfano, Uwanja wa Ndege wa Tabora na Viwanja vingine ambavyo havina lami, viwekwe lami kwani viwanja vya ndege sio vikubwa vya kuweza kuchukua lami nyingi.

**MHE. ABASS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa Hotuba nzuri ya Bajeti, pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Miundombinu. Nawatakia kila la heri katika kazi za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia uk. 13(B). Katika Hotuba ya Waziri Mkuu, nilichangia eneo la *TAZARA*, wakati Waziri Mkuu anajibu, alielekeza majibu yangu nitajibiwa na Wizara ya Miundombinu. Naomba nijibiwe maana Wananchi wa Kijiji cha Wavuvi Mtoni, Temeke, watafurahi sana wakipata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikumbushe maswali niliyouliza:-

Je, Tanzania bado tuna hisa *TAZARA*?

Kule Kurasini, *TAZARA* imeuza maeneo yote ya viwanja, hata sehemu za viwanja vya michezo kwa Shule ya Indiana ya Wa-Asia, matokeo yake wamejenga ukuta na kuzuia eneo hilo kukosa uwanja wa michezo. cha kusikitisha, walionunua maeneo hayo wamefunga hata njia za maji. Matokeo yake mvua kubwa zinapokuja, zinabomoa nyumba za wananchi. Pale Kijiji cha Wavuvi kuna nyumba 145; tano zimeshabomoka kutokana na njia za maji kuzibwa na waliouziwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi pale Kijiji cha Wavuvi kutokana na matatizo hayo yaliyosababishwa na *TAZARA*, wanaomba Serikali iwalipe fidia ili wahame eneo hilo. Naomba tusaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kusema kuwa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo ni kuhusu hatua ya Serikali ya kuamua kuifufua Bandari ya Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Kigoma ni kitovu muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa letu. Nchi yetu imekuwa ni tegemeo kwa nchi nyingi za Afrika ambazo ni *land locked*. Nchi hizo kwa muda mrefu zimekuwa zikitumia Bandari yetu ya Dar es Salaam kwa kupitishia mizigo mingi kwenda katika nchi mbalimbali. Kutokana na ufanisi uliopo katika bandari yetu, imeonekana kuwa mizigo mingi imekuwa ikichelewa kutoka kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuelemewa na wingi wa mizigo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuiuliza Serikali hasa Wizara hii ya Miundombinu; imefikia wapi kuhusu uamuzi wa kuifufua upya Bandari ya Kigoma kwa kuanza kutoa udongo katika bandari hiyo?

Nakumbuka Mheshimiwa Rais alitoa agizo kuwa, Bandari hiyo ifufuliwe kwa kuondoa udongo katika eneo hilo ili kuwepo na kina kinachofaa kwa meli kuweka gati. Kwa kufanya hivyo, itasaidia sana kupunguza msongamano wa mizigo hasa ya nchi za Rwanda, Burundi, Congo na kadhalika. Je, Serikali imefikia wapi kusu suala hilo?

Ni vyema kufanya maamuzi hayo mapema, kwani kuna habari kuwa, kuna athari zinazoweza kutokea kwa wananchi kama kusogezwa/kuvunjiwa. Hilo lifanyike mapema kabla ya mwaka 2010 wakati wa uchaguzi. Tukichelewa, itatuharibia katika uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza Wizara hii. Aidha, nampongeza Naibu Waziri, kwa kuhamishiwa katika Wizara hii. Wote wawili nawatakia mafanikio mema katika kuiongoza Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na iliyandalialiwa vizuri. Nawapongeza Watendaji wote wa Wizara hii, kuanzia Wizarani hadi Wilayani, kwa jitihada zao za kuiboresha Sekta ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia yafuatayo:-

Napenda kumrejesha Mheshimiwa Waziri, kwenye barua zangu za tarehe 21 Aprili, 2008 na 17 Juni, 2008, zote kuhusu Barabara ya kutoka Mpemba hadi Isongole. Naishukuru Wizara, kwa kukubali ombi letu la kuiwandisha hadhi barabara hiyo na kuiweka kwenye mpango wa kufanya upembuzi yakinifu, kwa lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami hapo baadaye. Nimetambua uwepo wa barabara hiyo kwenye Kiambatisho Na. 3 uk. wa 191.

Napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba, ombi letu la hapo juu, lilikuwa linahusisha pia uendelezaji wa kazi ya kutengeneza barabara za Mji wa Makao Makuu ya Wilaya (Itumba) kwa kiwango cha lami. Huu ni Mradi unaoendelea. Mwaka

wa 2007/08 zilitengwa Sh. 200m na kazi haijakamilika. Mwaka huu inaelekea hakuna fedha iliyotengwa. Tafadhali tazama Kiambatisho Na. 3 ukurasa wa 168 (*upgrading to DSD Itumba township roads - 8 km – Ileje District*). Naomba ufanuzi kwa kutokutenga fedha kwa mwaka huu.

Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza *TANROADS* kwa jitihada wanazofanya kwa barabara wanazozisimamia. Hata hivyo, ipo haja ya kufuatilia kwa karibu na kuchukua hatua za haraka za kutengeneza barabara zinapoharibika ili usafiri usikwame. Juhudi maalum, zielekezwe katika maeneo yenye mvua nyingi na madaraja mengi. Naomba *TANROAD* Mkoa wa Mbeya, wachukue hatua za haraka za kuyatengeneza madaraja ya mba yaliyoharibika sana katika Barabara ya Mpemba (Mbozi) hadi Isoko (Ileje). Ukarabari wa barabara uende sambamba na matengenezo ya madaraja ya mba. Kama inawezekana, kungekuwa na makandarasi pekee wa kushughulikia madaraja.

Natambua juhudzi za Serikali katika ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe. Naomba juhudzi ziendelee ili Mradi huu uweze kukamilika haraka ili kuongeza vichochoeo vya biashara endelevu na nchi jirani za Zambia, Malawi na Nchi za SADC kwa ujumla. Aidha, Serikali iendelee kushughulikia kwa ukamilifu, madai ya wananchi katika eneo hilo la Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kuwatachia mafanikio mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hobuta ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, imeonyesha nia njema ya Serikali ya kutaka kuondoa dhiki kwa Watanzania katika nyanja za usafiri ili kuiongezea Serikali pato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza ni vyema Serikali iwe na utaalami wa kijiografia wa miji yetu ili iepushe hasara isiyokuwa ya lazima. Maumbile ya miji yetu, mara nyingi hutokezea bomoabomoa, jambao ambalo husababisha manung’unico ya wananchi wetu kwa njia ya maneno na wakati mwingine wananchi wetu huwa tayari kukataa kwa vitendo kama vile kuwa tayari kupambana na dola. Ni vyema sasa Serikali iwe tayari kunusuru hili, pia kunusuru hasara kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri ya Wizara hii juu ya usimamizi wa miundombinu ya barabara, ipo haja ya makusudi ya Wizara yetu kuziangalia barabara za mitaa zilizopo Dar es Salaam. Hali ya baadhi ya barabara hizo sio nzuri, ukilinganisha na ukuaji wa mji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia usafirishaji wa mizigo mizito, ambayo mara nyingi inatia ubovu barabara zetu ni wakati muafaka wa Serikali kuhakikisha usafirishaji wa mizigo unatumia treni. Hili litanusuru barabara zetu. Pamoja na hilo, kuna udhia mkubwa juu ya wasafiri wetu kwa njia za reli, jambo ambalo kiwango cha wasafiri kwa eneo hupita idadi na ni hasara sana kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ongezeko la wasafiri wa ndege, ipo haja Serikali iondoe msongamano wa abiria viwanjani. Hili linasababishwa na mambo mawili muhimu; uhaba wa viwanja na muda wa utuaji wa ndege kuwa mmoja. Ni vyema sasa Serikali ituondelee dhiki katika hili ili nasi tuwe na usafiri mzuri kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi ndani ya Bunge hili, Wabunge husemea Daraja la Kigamboni. Daraja hili ni muda mrefu sana limo midomoni, jambo ambalo inaonekana Serikali haitilii maanani matatizo yanayowakabili watu wetu. Kwa kuzingatia muda na suala lenyewe, wakati umefika kwa Serikali kusikia kilio hicho, pamoa na ugumu wenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, nampongeza Waziri kwa usikivu wake pia na upole wake. Ahsante.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, kwa kuandaa bajeti nzuri kwa mwaka wa fedha wa 2008/09. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza Wizara kwa kuendelea kujenga barabara nchini kwa kasi kubwa. Hata hivyo, naomba nishauri kwamba, Barabara ya Mlowo – Kamsamba inayoendelea kujengwa na wakandarasi mbalimbali, bado kazi yake siyo kubwa sana. Nashauri kasi iongezwe na ubora wa ujenzi uzingatiwe. Aidha, vipande ambavyo havijapata wakandarasi, yaani Mlowo – Halungu na Itumbula – Kamsamba, jitihada zifanyike ili wakandarasi wapatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Barabara ya Zelezeta – Isansa – Magamba – Iporoto hadi Itaka, inahudumiwa na *TANROADS* vizuri sana. Hata hivyo, katika barabara hiyo, kipande cha kutoka Magamba hadi Iporoto hakina barabara kabisa. Naomba Waziri atoe tamko ni lini sasa kipande hicho kitatengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha pesa ambacho Reli ya Uhuru (*TAZARA*) inapewa cha Sh. 100 milioni ni kidogo sana. Je, kuna sababu gani za Wizara kufanya hivyo, ukizingatia kwamba, *TAZARA* hutozwa kodi kwenye mafuta (*fuel levy*), fedha ambazo kimsingi huenda kwenye ujenzi wa barabara? *TAZARA* hufaidika vipi? Aidha, naomba Mheshimiwa nifahamishwe, je, kuna mkakati gani wa dhati wa kuwakwamua wafanyakazi waonaostaifu ambao hawakulipwa haki zao kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Karakana ya *TAZARA* – Dar es Salaam, inasemekana ni ya pili kwa ukubwa Barani Afrika, lakini matumizi yake ni kama asilimia 25 tu ya uwezo wake! Je, Wizara ina mkakati gani wa kuitumia karakana hiyo kadiri ya uwezo wake? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna shaka kwamba, karibu sekta zote za uzalishaji na zisizo za uzalishaji, hutegemea hali nzuri ya hewa. Ukweli ni kwamba, sio wakati wote hali ya hewa huwa nzuri; kuna majanga mengi sana ambayo huleta athari katika uchumi wa nchi na shughuli mbalimbali za binadamu. Ili kukabiliana na majanga hayo,

mamlaka ya Hali ya Hewa, lazima iwezeshwe ili inunue vifaa vya kisasa zaidi, vya kupima na kufuatilia mwenendo wa hali ya hewa nchini.

Kubwa zaidi, mwaka wa fedha 2006/07, Serikali iliahidi kununua rada kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa hali ya hewa, hadi leo tunaenda mwaka 2008/09 bado rada haijanunuliwa. Naomba Waziri atoe maelezo, kulikoni?

Aidha, nchi hii ni kubwa sana rada moja haitoshi, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu, iwe na mpango wa kununua rada nytingine angalau tano hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha takriban miaka miwili, majengo mengi yamekuwa yakiporomoka au kuanguka na kusababisha maafa kwa maisha na mali za binadamu.

Naomba kujua Baraza la Ujenzi la Taifa, Bodi ya Usajili ya Makampuni ya Ukandarasi na Bodi ya Usajili ya Wahandisi wanafanya kazi gani katika kudhibiti makampuni yanayofanya kazi chini ya kiwango na wahandisi wasio na sifa za kusimamia kazi za ujenzi?

Kwa vyovyyote vile, kukosa sifa kwa Makampuni ya Uhandisi na Wahandisi wasio na sifa, ndio chanzo kikubwa cha kuperomoka kwa majengo marefu hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, naomba kujua hatua ambazo Wizara imechukua juu ya Makampuni ya Ukandarasi na Wahandisi waliojenga majengo ambayo yameporomoka na kusababisha vifo na hasara kwa mali za watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilete masikitiko yetu Wana-Mara kuhusiana na Hotuba ya Waziri wa Miundombinu. Ukweli kwetu sisi Wana-Mara tunao uhakika wa asilimia mia ya kwamba, utekelezaji wa Ilani kwa Mkoa huu bado upo nyuma sana na hasa kwa upande wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili ya nyuma, barabara yetu ya Musoma – Fort Ikoma ilikuwa tayari kwenye upembuzi yakinifu. Tulitegemea kwa mwaka huu wa fedha 2008/09, ujenzi ungeanza lakini cha kushangaza, hotuba inatuambia barabara hii bado ipo kwenye upembuzi yakinifu. Pia zipo Barabara zinazounganisha Tarime - Mugumu na barabara ya Bunda - Kisorya - Ukerewe ambapo tulitegemea ujenzi ungeanza kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wana-Mara tumesikitishwa na maelezo yasiyojitosheleza kuhusu Viwanja vya Ndege vya Musoma Mjini na ule wa Serengeti. Namwomba Waziri atupatia maelezo ya kutosha kuhusu lini ujenzi wa viwanja hivi utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea tungesikia habari njema kuhusu ukarabari wa Gati la Mwigobero na Gati la Kinesi, lakini Waziri pia ametoa maelezo yasiyojitosheleza. Kwetu wana Mara, Hotuba imekwenda pembeni na Ilani yetu ya

Uchaguzi. Tungependa tupate maelezo ya kina juu ya barabara hizo na magati niliyoyataja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema siungi mkono hoja hii mpaka nipaye maelezo ya kutosha kwani tumebakia na mwaka mmoja tu wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii, kwa kuizungumzia *TCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uk. 61, Waziri amezungumzia ufanisi wa *ATCL* kwa kusema kwamba, ndege zilifanikiwa kuondoka kwa wakati (*on time performance*), ikilinganishwa na mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni msafiri mzuri sana wa *ATCL*, kwani tangu mwaka 2006, Februari, niliacha kusafiri na Shirika la Ndege la Precision; hivyo, naomba niseme sentensi hiyo si kweli kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndege hizi zimekuwa kero kubwa kuliko hata zilipokuwa kwenye ubia na South Africa, kwani zimekuwa hazina uhakika hasa unapokuwa unataka kutoka Mwanza – Dar es Salaam, mara nyingi zimekuwa hazifuati muda na hivyo kugeuka kuwa kero kubwa kwa wasafiri. Leo hii Waziri anatuambia *on time performance* ni asilimia 80. Hii si kweli na kwa *statement* hii itakuwa vigumu kwa hawa *TCL* kujirekebisha!

Mheshimiwa Naibu Spika, kero nyingine ambayo haikuzungumziwa ni upatikanaji wa *tickets za ATC*. Pale ofisini kuna kero kubwa; foleni kubwa kwa ajili ya wafanyakazi kuwepo wachache. Namwomba Waziri, ajitahidi ili kero hiyo iondoke pale kwani inapelekea wasafiri wengi kuhamia Precision Air.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningombia tupate maelezo zaidi ni kwa nini shirika hili limekuwa na utendaji usioridhisha na kugeuka kuwa kero kwa wananchi, kwani ninaamini kabisa iwapo kungekuwa na *more alternatives*, basi *ATCL* isingepata wasafiri. Tulisaide Shirika letu kwa kulikosoa na si kulipa sifa ambazo halistahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya CCM ya 2005, kuna mambo muhimu mawili ambayo Mkoa wa Mara uliahidiwa. Haya mambo ni kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami toka Makutano – Natta- Mugumu – Loliondo - Mto wa Mbu hadi Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa hii barabara imefanyiwa *feasibility study* katika mwaka 2006/07 na 2007/08, inasikitisha kuwa katika Bajeti ya 2008/09 hata haitajwi kuwa ni barabara inayotarajiwa kujengwa. Badala yake, inayotajwa ni ile ya Makutano hadi Fort Ikoma, ambayo ilikataliwa na ikaamuliwa ipite Makutano Natta – Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu hadi Arusha.

Sasa kilichowekwa kwenye hotuba ya 2008/09 ni kichekesho, kwani hata Wizara hajui inafanya nini, wakati Mheshimiwa Rais amekuja Serengeti na kuwaahidi kuwa barabara itakayojengwa ni ile ya Makutano Natta – Mugumu - Loliondo hadi Arusha. Wananchi wa Serengeti wamenipigia simu kutaka kujua ukweli kuhusu barabara hii na lini ujenzi utaanza? Naomba jibu niwapelekee wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha pili, Wilaya ya Serengeti iliahidiwa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Mjini Mugumu. Hadi sasa *feasibility study* imefanyika. Aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Lowassa, alikuja kukagua Uwanja huu utakapo jengwa. Akaahidi umati wa watu kuwa, Uwanja huu utajengwa. Wakazi wa eneo hili wameshalipwa fidia, shule zimehamishwa; sasa inakuwaje katika Bajeti ya 2008/09 ujenzi wa uwanja huu hautajwi kama Serikali ilishawahamisha watu kutoka eneo hili, hivi tutawaambia nini mwaka 2010? Nataka jibu la kuwapelekea wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Wilaya ya Serengeti kama vile Silori Simba – Rung’abure - Mto Mara – Mugumu, Mugumu – Natta, Natta – Isenye, Mugumu - Fort Ikoma, zina hali mbaya. Kinachosikitisha ni kuwa, hazikuwekwa kwenye Bajeti ya 2008/09; hivi kweli Wananchi wa Serengeti wamekosa nini hadi kusahauliwa hivyo? Naomba majibu ya kuwapelekea wananchi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka mzima hadi muda huu ninapochangia.

Pili, natoa pongezi kwa Waziri wa Miundombinu, Naibu wake na Watendaji wake wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naomba nielekeze mchango wangu katika suala zima la usafiri na uchukuzi wa reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati hawa wawekezaji walipokodi toka *TRC* katika Jiji la Tanga Locoshed kulikuwa na mabehewa ambayo yalikuwa chakavu na yalikuwa pale takriban kwa kipindi cha miaka kumi na ushee.

Mara tu baada ya *TRC* kuwakodisha *TRL*, wawekezaji hawa mara moja wakayahamisha mabehewa hayo chakavu na kuyapeleka wanakojua wao wenyewe. Mheshimiwa Waziri, atueleze mabehewa hayo yamepelekwa wapi na yalikuwa *written off?* Napata wasiwasi hawa wawekezji isijekuwa wana biashara ya vyuma chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu hawa ni wajanja, ukichukulia wawekezaji huchukua michanga kutoka migodini na kwenda kupimwa nje na michanga hiyo inakuwa chini ya ulinzi mkali. Nao ni mchanga tu, kuna sababu zipi zinazopelekea hata mchanga kulindwa na wakati ni mchanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napata dhana ambayo inapelekea kuona mabehewa yale yamechukuliwa kwa ajili ya kufanya vyumba chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli baada ya Shirila la Reli (*TRC*), kusimamisha kazi zake kwa kweli hali ya reli imekuwa mbaya sana. Njia ya reli inaonyesha uchakavu, nyumba zimetelekezwa, chafu na nyingine zimeng'olewa vigae.

Mkoloni alipojenga reli alijenga na nyumba ili wafanyakazi wake wasipate tabu ya kutafuta makazi na iwe rahisi kwao kufika katika sehemu zao za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baya zaidi nyumba hizi baadhi yake zimeuzwa.

Mheshimiwa Waziri, atueleze ni sababu zipy zilizopelekea nyumba hizi zilizopo Kata ya Central, Jiji la Tanga kuuzwa; je, kukodishwa kwa Shirika la Reli ndio mwisho wa shughuli za reli hadi nyumba ziuzwe?

Mheshimiwa Waziri, naomba atueleze kila nyumba iliuzwa kwa bei gain? Inanishangaza mtu kuuziwa nyumba na yeye akawa anailipa kidogo kidogo. Mbona hatuendi dukani kutaka sukari kilo moja utalipa shilingi mia mbili na fedha iliyobaki ukalipa kidogo kidogo hadi hapo utakapomaliza deni. Je, Serikali haioni kuwa mtindo huu sio mzuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bandari ya Tanga; kwa kweli ni kitega uchumi kikubwa sana cha Taifa. Bandari ya Tanga kama itaendeshwa ipasavyo na kutokana na kulundikana kwa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, itasaidia kupunguza mizigo hiyo ambayo imekuwa ni kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboreshwa kwa Bandari ya Tanga kutasaidia biashara kati ya Tanga – Mombasa kushamiri vizuri. Nchi ya Uganda, Ruanda na Burundi, wangeweza kusafirisha mizigo yao kuititia Bandari ya Tanga na huweza kuwapatia ajira wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Tanga ni uwanja unaojengwa muda mrefu sana. Majengo yake yamekuwa chakavu sana. Naiomba Serikali, iitupie jicho la huruma Uwanja huu ili nao uonekane unaendana na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara, Serikali iangalie wale wakandarasi wasiofaa wasipewe nafasi ya ujenzi wa barabara. Kuna wakandarasi ambao hawatengenezi vizuri barabara zetu, kiasi ambacho baada ya muda mfupi barabara zetu zimekuwa mbovu kupita kiasi.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa tamko la Waziri Mkuu, kuipatia Barabara ya Itigi – Tabora shilingi bilioni kumi.

Kwa kuwa sijaona katika maelezo ya Wizara juu ya fedha hizi; je, pesa hizo zimetengwa kupitia *TANROADS* au kwa *RAS* (Tabora, Singida, Kigoma)?

*Design* ya Itigi – Tabora – Ipole ilishafanywa tangu 1994, kinachosubiriwa ni fedha za kujenga kwa kiwango cha lami. Je, ni shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Tabora iendelezwe lazima kuhakikisha miundombinu ya Barabara na Reli inamarishwa: Barabara ya Nzega – Tabora – Pole ijengwe kwa kiwango cha lami kwa fedha za ndani; Reli ya Kati, Dodoma – Tabora – Kigoma na Tabora – Mwanza ipanuliwe ili kuwa ni kiungo cha usafirishaji kufanikisha soko la nchi za *DRC*, Burundi, Rwanda na Zambia; kufungua Mikoa ya Magharibi, yaani Tabora, Kigoma na Rukwa ni kufanya miundombinu kuwafaidisha kupata masoko ya mazao yao kupeleka Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kati.

Duniani kote, Mataifa makini huwa na mashirika yao ya Ndege (*National Carrier*). Ukitaka kuimarisha utalii, lazima kuimarisha Shirika la Ndege (*ATCL*). Lipa madeni ya *ATCL* na kupata ndege mpya za kukodi. Zianzishwe safari za moja kwa moja (*direct flight*), kutoka sehemu watalii wanapotokea mfano, USA, UK, China via Dubai na kadhalika; kutegemea KQ au ET daima tutabaki nyuma. Air Tanzania iwe ni *image* ya Tanzania. Serikali iipe mtaji wa kutosha ili ifikie hadhi ya kutambulika Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa viwanja vya ndege ni muhimu ukienda sambamba na kuimarisha Shirika la Ndege. Hatima ya Kiwanja cha KIA kubinafishwa kwa KADCO ifikie mahali Serikali ikimiliki. Mwekezaji aliyepo sasa hana nguvu ya kukifanya kiwanja hicho kuwa cha kisasa.

Napendekeza Mwanza Airport iwe ni *hub* ya Maziwa Makuu, kukifanya kiwanja hicho kuwa kiunganishi cha Kigali, Bujumbura, Entebbe, Nairobi na hata kwenda DRC. Tuandae mazingira ya kuvuna biashara ya Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, msukumo wa kutaka kupata watalii wengi ni lazima Viwanja vya Dar es Salaam na KIA viimarishwe zaidi. Lakini kwa ajili ya ku-diversify fursa ya utalii katika maeneo mengine, lazima Viwanja vya Tabora, Kigoma na Songea viimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema, msiisahau barabara yangu ya Nzega – Tabora km 120, mwaka 2009 ijengwe kwa lami.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kiimarishwe as a matter of urgency, maana kama tunataka nchi ichukue fursa ya huduma za usafiri kwa nchi za Maziwa Makuu. Lazima kuwa na wataalamu wa kutosha wa usafiri ili waweze kuishauri vyema nchi kuiendeleza sekta ya hii. Chuo sasa

kitoe wachumi usafiri wengi na pia kijikite katika kada ya *logistics*, kwani kutokana na ukuaji wa sekta wanahitajika wataalamu wengi.

Ninaomba Waziri afuutilie kwa karibu sana, tatizo la mgogoro unaofukuta ndani ya *TANROAD*, kwani wafanyakazi wanalamika kuhusu kuhamishiwa katika ajira za mikataba. Hivi punde imetokea kutoelewana kati ya *NORCONSULT* na *TANROADS*. *NORCONSULT* wameondoka na miradi iliyokuwa chini yao inakwama. Suala hili liangaliwe sana na ninapenda nimwonye *CEO* wa *TANROAD*, apunguze kugombana na wakandarasi na badala yake afanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati akichangia Mbunge wa Viti Maalum Sijapata Nkayamba, alisema kuwa Kampuni ya MWAPI Kigoma (Bandarini) imeajiri Warundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuletea orodha ya waajiriwa wa kampuni hii inayoendesha Bandari ya Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni Ushauri:-

(1) Wabunge waepuke kutoa “*Sweeping Statement*” humu Bungeni bila ushahidi. Mbunge huyu alitaka apewe ajira kwa watu wake pale Bandarini. Akakataliwa, akakasirika.

(2) Fanya uchunguzi kuhusu suala hili. Nitakusaidia ili tubaini ukweli kuhusu suala hili kwa lengo la kujenga.

- *If need be, you can ask Kigoma District Mps to make follow up on this and resolve whatever problem to be realised.*

*I wish you all the best.*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri aelezee wazi juu ya Babaraba ya Marangu – Mwika – Mkuu na Mwika – Kilacha. Barabara hii alipewa *contractor* baadaye akanyang’anywa. Napenda Wananchi wa Vunjo wajue kama amepatikana mjenzi mwingine na ataanza kazi lini na barabara itamalizika lini?

Pili, barabara ya Ahadi ya Rais kutoka Marangu - Mtoni - Kilema hadi Kawawa Road - Kirua Vunjo. Barabara hii Mheshimiwa Rais, aliahidi mara tatu kuwa itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Mtakumbuka Ndugu Agustino Mrema alipeleka lami kwa ajili ya barabara hiyo, lakini ilitelekezwa hadi ikaharibika. Baada ya Jimbo kurudi CCM, wananchi wanangojea Ahadi ya Rais kutekelezwa. Naomba Waziri atoe tamko.

Tatu, Barabara ya Himo – Mandaka – Maua, inapitia Mandaka Chuo cha Ualimu, St. James Seminary, Shule ya Sekondati Sita na Hospitali kubwa ya Kilema hadi Maua Seminary. Naiomba Serikali iipandishe daraja barabara hii iwe inahudumiwa na *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni ununuzi wa magari ya Serikali. Naishauri Serikali ianze utaratibu wa kuachana na mashangingi. Kama mfanyakazi anataka shangingi, anunue kwa mkopo. Idara zinunuliwe mabasi. Pia kuwe na aina mbili ama tatu za magari ya Serikali na yawe yamenunuliwa kwa mkupuo, kama wanavyofanya Umoja wa Mataifa. Ni hasara kubwa mno kununua magari ya Serikali kwa *open tender*. Utaratibu ufanyike wa kununua moja kwa moja kiwandani, kwani bei itakuwa ndogo ikinunua magari mengi kwa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATCL* kama tunataka tuwe na Shirika la Ndege imara ni lazima Serikali ilipe fedha ama iliwezeshe kukopa. Hakuna maendeleo, bila kutumia fedha wala hakuna miujiza. Fedha zikiwepo pamoja na uongozi bora, maendeleo yatapatikana.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza mchango wangu kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja. Hata hivyo, ninayo machache ya kuchangia, ambayo ni Miundombinu ya Barabara katika Wilaya ya Kahama na hususan Jimbo la Kahama.

Wilaya ya Kahama, ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Mkoa wa Shinyanga. Wilaya hii ndio inayozalisha mazao mengi ya chakula na kilimo kuliko wilaya nyingine katika mkoa. Inazalisha kwa wingi mazao ya chakula kama mahindi, mpunga na mihogo. Aidha, inazalisha kwa wingi mazao ya pamba na tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia karibu 60 ya mazao haya inatoka na Kata za Ulowa, Usheta, Uyogo, Kisuke, Ukune, Nyandekwa hadi Kahama Mjini. Kata hizi zinaunganishwa na barabara moja inayotoka Kahama Mjini hadi Ulowa, umbali wa km 120. Barabara hii ni ya Halmashauri na muda wote imekuwa mbovu. Kwa kuzingatia umuhimu wake, Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ilikwisha azimia ipandishwe hadhi kuwa ya *TANROAD*, jambo ambalo limeridhiwa na *RCC*. Bahati mbaya, hadi leo ni kimya hivyo, nguvu za wananchi zimeendelea kupotea bure kutokana na mazao yao kushindwa kusafirishwa.

Barabara hii ni muhimu, tunaomba Serikali kwenye mchakato unaoendelea wa tathmini ya kupandisha hadhi barabara za aina hii, ione umuhimu wa kuipandisha hadhi barabara ya Kahama - Nyandekwa - Ulowa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Oktoba, 2005, Mheshimiwa Rais, wakati akiwahutubia Wananchi wa Mji wa Kahama, aliwaahidi kwamba, Mji wa Kahama una hadhi kubwa na hivyo, inatakiwa kuwa na barabara ya lami. Aliahidi kufanya hivyo kama watamchagua kuwa Rais na walifanya hivyo.

Mheshimiwa Rais alirudia kauli yake ya 2005 mwaka jana, alipotembelea tena Kahama. Wakati akizungumzia ahadi hiyo, alimsimamisha Waziri wa Miundombinu wakati huo, kuwahakikishia Wana-Kahama kwamba, Ahadi ya Rais itatekelezwa. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hotuba yake, anifafanulie utekelezaji wa ahadi hii umefikia wapi? Wananchi wanasumbua kwamba wamedanganywa. Ninaomba sana nipate ufanuzi.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa na Wasaidizi wake, kuanzia Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Eng. Omar Abdallah Chambo na Bi. Joyce Mapunjo na Wataalam wote wa Wizara ya Miundombinu, kwa utekelezaji wa asilimia kubwa ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005. Kwa kifupi naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nina mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Uwanja wa Ndege wa Mtwara, hutua ndege zinazotoka na kuingia kutoka Nchi za Comoro na Msumbiji. Aidha, Uwanja huu una historia ya Uhuru wa nchi nyingi za Kusini mwa Afrika. Nilidhani bajeti hii, baada ya uwanja huo kuwepo kwa muda mrefu ukitambuliwa kama *National Airport*, sasa ungetengewa fedha na kutangazwa kuwa Uwanja wa Kimataifa, hasa kwa kuwa Mtwara ina Miundombinu yote ya Bandari na Barabara inayokaribia kukamilika. Ningependa nipate maelezo, kwa nini Serikali ina kigugumizi katika kufanya uamuzi wa msingi wa Uwanja huo?

Pili, ningependa nipate maelezo kwa nini Barabara ya Mtwara - Tandahimba - Newala – Masasi, ambayo *RCC* Mtwara ilipitisha kuwa ya lami haipo kwenye Bajeti hii? Baada ya Baraza la Ushauri Mtwara kuipitisha, nilidhani bajeti hii ingetenga angalau bajeti ya upembuzi yakinifu. Kimya kilichopo ni lazima Waziri atoe maelezo ni lini utaratibu wa hatua za kuiwekea lami barabara hiyo utaanza? Ikumbukwe kwamba, asilimia 90 ya uchumi wa Mtwara hutegemea Barabara hiyo.

Tatu, mwaka 1990/91 yalitokea mafuriko makubwa yaliyobomoa Daraja la Nangoo na hivyo kusababisha tatizo kubwa la mawasiliano kati ya Mtama - Ndanda. kwa nini basi tangu wakati huo hadi leo hakuna mpango (bajeti), yenyе lengo la kurejesha daraja hilo katika hali yake ya awali?

Nne, ukitoka Mtwara kuelekea Tandahimba na Newala, unakutana na Mlima wa Kinolombo. Mlima huo umekuwa chanzo cha hasara kwa magari, mali na vifo kwa binadamu. Kwa nini Wizara ya Miundombinu haioni haja ya kuitengea bajeti, angalau tu sehemu ile ya mlima (km 7), ili iondoe athari na hasara za mali na binadamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashindwa kufahamu kiini na ukubwa wa Wizara kushindwa kutengeneza Barabara ya Malamba – Namikufa – Maundo, ambayo nayo inapitia milimani lakini Wananchi wa Tandahimba huitumia sana kwa kilimo cha mazao ya chakula na mboga, kwani huenda pembezoni mwa Mto Ruvuma.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ya Waziri wa Miundombinu kama ifuatavyo:-

Barabara ya Murugalama – Rulonge – Keza – Kamubuga - Mizani. Wananchi wa Ngara, wanaomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami kwa sababu ni muhimu sana katika kuleta maendeleo ya Wilaya ya Ngara. Barabara hii ni kiungo muhimu katika kuunganisha sehemu mbili za Wilaya ya Ngara. Wakati wa ukoloni, *Ngara District* ilikuwa na tarafa mbili; Tarafa ya Bugufi ambayo sasa ina tarafa mbili, yaani Mabawe na Kanazi; na Tarafa ya Bushubi ambayo sasa ina Tarafa mbili, yaani Tarafa ya Relenge na Murusagamba. Kisiasa barabara hii ndiyo kiungo muhimu, kuunganisha sehemu hizi muhimu za Wilaya ya Ngara.

Kwa hiyo, Wananchi wa Wilaya ya Ngara na hasa wale wa Tarafa za Rulenge na Murusagamba wameanza kuona ya kwamba, wametengwa na ndiyo sababu hawapati maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa Kabanga Nickel ndiyo utakuwa mkubwa wa kuchimba nickel katika Afrika. Mgodi huu unahitaji umeme wa mega watts 45. Umeme wa ukubwa huu hauwezi kupatikana kwa sasa katika Wilaya ya Ngara. Wananchi wa Wilaya ya Ngara, wanaomba umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Shinyanga kuititia Bukombe mpaka Kabanga Nickel Ngara. Huu umeme utawezesha Mgodi wa Kabanga Nickel kuanza na kuleta ajira kwa Wakazi wa Wilaya ya Ngara.

Barabara ya Kabanga Nickel – Relenge – Keza mpaka Mizani ni muhimu sana hasa ukihusisha hii baraba na usafirishaji wa *concentrate* za Nickel kusafirishwa kutoka Kambanga Nickel Mine kwenda Mizani, Isaka ili yaweze kupelekwa nchi za nje kwa ajili ya kutengeneza *finished products* za Nickel. Haiwezekani kuwa na Mgodi wa Kambanga Nickel bila kuwepo barabara hii. Hivyo basi, Wananchi wa Ngara wanaomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kabanga Border - Mabawe – Muruvyagira – Mukikomero – Kasange – Mugoma – Ntobeye – Rusumo Border ni ya ulinzi na inaambaa mpakani mwa Wilaya ya Ngara na nchi za Burundi na Rwanda. Barabara hii ni muhimu sana, hasa wakati wa kuwasaka majambazi wanaoingia Ngara kutoka Burundi. Wananchi wa Ngara, wanaomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Ngara wanaomba Uwanja wa Ruganzo – Ngara uwe wa kisasa ili ndege kubwa ziweze kutua hapo. Huu ni Uwanja muhimu kwa ajili ya ulinzi na usalama wa Wilaya ya Ngara.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kutuletea Bajeti inayotia matumaini kwa wananchi wake. Aidha,

tunaipongeza Wizara kwa kudiriki kugharimia Bajeti ya Maendeleo kwa asilimia 60 Fedha za Serikali. Kwa hiyo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Naomba kuikumbusha Serikali kutekeleza Ahadi za Rais juu ya barabara zifuatazo:-

(a)Kibiti – Mkongo – Utete - Kivukoni (*Ferry*) – UTETE (Bomani) – Nyamwage km 77. Barabara hii inapangiwa fedha ya utekelezaji km 9 tu. Wananchi wanaiomba Wizara, iongeze fedha angalau kutoka Kibiti – Utete ijengwe na kumaliza kazi hiyo. Serikali iheshimu Ahadi za Rais Kikwete, kwa kweli ni aibu kubwa kwa Wizara kutengeneza km 9 tu badala ya angalau km 40 katika km77. Wzara itenye fedha zaidi na kipande korofi ni kutoka Kibiti – Mkongo – Utete Kivukoni (*Utete Ferry*). Wizara ijjitahidi kumaliza na kutimiza ahadi hii ya Rais.

(b)Hoja ya ununuzi wa Kivuko kipy cha Utete (*Utete Ferry*) ni Ahadi ya Rais Kikwete, yaani kufungua barabara toka Kibiti – Mkongo – Utete Ferry – Utete. Katika Bunge liliopita, Serikali ilitueleza kuwa ununuzi wa kivuko (Pantoni) Utete upo katika hatua ya zabuni. Tunaomba Wizara itoe kauli juu ya ununuzi wa pantoni mpya ya Kivuko cha Utete katika kikao hiki cha Bunge.

(c)Katika zirara ya Rais Kikwete Wilayani Rufiji, Mheshimiwa Dr. Kawambwa alishiriki, Serikali (Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Andrew Chenge), alitoa ahadi baada ya Mheshimiwa Rais kusema kuwa, anataka kuwapata watalii kutoka Msumbiji waje mpaka Mloka (Selous) kutoka Ikwiriri. Kwa kauli yake, alitamka kuwa, watalii wakivuka Daraja la Umoja kati ya Msumbiji na Tanzania, waje mpaka Daraja la Mkapa. Wakifika Ikwiriri (Rufiji), watumie barabara toka Ikwiriri – Mkongo – Mloka (Selous Game Reserve). Ndipo aliyekuwa Waziri, akaahidi kuwa, barabara hii itachukuliwa na *TANROAD* Mkoa wa Pwani. Aidha, Barabara hii inaunganisha Wilaya za Mkoa wa Pwani, yaani Ikwiriri – Mkongo – Mloka – Vikumburu – Kisarawe – Kibaha – Bagamoyo. Hii kweli ni Barabara ya Mkoa wa Pwani? Kati ya Vijijij vya Mbunju na Ruwe kuna Daraja la Mbambe linalohitaji kujengwa upya haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iisimamie barabara hii na ipate fedha ya ujenzi wake na ianze ujenzi wa barabaraba kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rufiji ina viwanja vya ndege vidogo (*airstrips*) zifuatazo: Kiwanja cha Utete (Bomani), Mtemela (Mloka Selous) na Kiwanja cha Kingupira (Selous). Viwanja vya Mtemela na Kingupira vinatunzwa na Idara ya Wanyamapor, lakini Kiwanja cha Utete (*airstrip*) ni mali ya Serikali. Kilikuwa kinafanya kazi tangu enzi za ukoloni. Ni kiwanja chenye *high strategy*, sasa kiwanja hicho kipo katika hali mbaya sana (*poor state of repair*), tunaomba Serikali ikikarabati kiwanja hiki mara moja.

Tunaishukuru Wizara kutia saini Mkataba wa kumaliza ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Ndunu – Malendego. Tunawaomba Wizara ihmize ili Mkandarasi aimalize kwa kiwango cha juu cha ufanisi na kazi imalizike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naitakia Wizara mafanikio makubwa katika shughuli zake. Ahsante.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu yao yote, kwa kazi nzuri mwaka huu licha ya ugumu wa kupatikana fedha. Nawapongeza pia kwa hotuba fasaha na murua.

Pili, naishukuru Wizara imezingatia umuhimu wa kuweka lami katika Barabara ya Dodoma hadi Iringa. Nafahamu kwamba, Wizara itakamilisha *final design* na *tender papers* mnamo Agosti, 2008. Napenda kusisitiza umuhimu wa kuharakisha mchakato wa Mradi huu muhimu.

Tatu, tuna uwanja wa ndege pale Nduli, jirani na Mji wa Iringa. Upo tangu enzi ya ukoloni, lakini hautumiki kikamilifu.

Mkoa wa Iringa umepania kukuza uchumi kwa njia ya utalii na uwanja huu ungekuwa ni kichocheo kikubwa cha azma hiyo. Hili halina mjadala na kwa hiyo, naomba Wizara ihakikishe kasoro zozote kama zipo, ziharakishwe. Pili, Wizara itusaidie Uwanja huo uanze kutumika kwa usafiri wa abiria na mizigo.

Nashukuru sana kwamba, Barabara ya Iringa – Msembe imewekwa lami kilomita chache mwaka jana. Hivi sasa nusu kilomita imewekwa lami. Utakubaliana nami kwamba, kwa kasi hiyo 70km za barabara hiyo zitachukua zaidi ya karne moja. Naomba kusisitiza mambo mawili: Barabara hiyo ipandishwe hadhi kuwa ya Taifa kwa vile inakwenda Ruaha National Park, ambako ndiyo kitovu cha utalili tunaojaribu kuujenga; na kasi ya sasa ya uwekaji lami ni ndogo mno, naomba iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja na naitakia kheri na mafanikio katika utekelezaji mwaka 2008/09.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kibaha Mjini mpaka hivi sasa hakuna Barabara ya Mkoa. Barabara ya Morogoro imepita Kibaha si kwa matakwa ya watu wa Kibaha, ila watu wa kibaha wamejikuta barabara hii inapita kwa sababu ya Kitaifa; sisi tunashukuru.

Hivi sasa watu wa Kibaha wameona umuhimu wa kuwa na Barabara ya Mkoa. Tangu nimekuwa Mbunge mwaka 2006, nimezungumzia Barabara ya TAMCO Mapinga, mpaka sasa bado mahitaji ya watu wa Kibaha hayatekelezwi. Je, sababu ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya zote za Mkoa wa Pwani, wametengewa pesa za kutengeneza barabara mbalimbali na Wilaya nyingine ndani ya Mkoa wa Pwani, zimetengewa pesa za barabara zaidi ya moja. Wabunge wenzangu wote wa Mkoa wa Pwani, wanarudi na furaha kwa wapiga kura wao, mimi peke yangu ambaye wananchi wangu wameomba barabara moja tu, hawakupewa. Huku nataka kuwaambia wajivune eti kwa sababu Mji wa Kibaha ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani, wakati mji

wenyewe upo porini, hakuna hata barabara ya lami. Je, mnawadanganya kwa kuwaambia sura zenu ni nzuri mnafanana kama manyani au mnawaadhibu watu wa Mji wa Kibaha kwa sababu ya kumchagua Mbunge asiyetakiwa na wakubwa? Kama si hivyo; je, Serikali itasema kwa nini haitaki kuuendeleza Mji wa Kibaha?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Mbunge, Mkurugenzi wa Mji wa Kibaha na *CO* wa Nyumbu, tulimwona Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati akiwa Waziri wa TAMISEMI. Tulionana naye kwa ajili ya Barabara ya kwa Mathias – Nyumbu – Msangoni, yenyе urefu wa kilomita 12.6, ili itengenezwe kwa sababu imeharibika sana. Barabara hiyo ilitengenezwa kwa sababu ya matumizi ya Kiwanda cha Nyumbu. Hivi sasa barabara hiyo ina matumizi makubwa; kuna vijiji vingi vimeanzishwa na watu wengi wanatumia hiyo barabara.

Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema, kwa wakati huo kuwa anawasiliana na Waziri Mkuu. Akasema haiwezekani pesa zinazotakiwa kuijenga barabara hiyo zichangwe na wananchi. Alionyesha (Mheshimiwa Pinda), umuhimu wa barabara hiyo. Bahati mbaya, sijaona bajeti imetengwa kwa ajili ya barabara hii. Barabara ya km. 4 inayotoka Sheli kuelekea Magereza Mkoani, Maili Moja na kutoka Mkoani kuelekea kwa Mkuu wa Mkoa, tuliomba na tukaahidiwa. Waziri Mkuu, aliahidi barabara hiyo itatengenezwa, watatoa pesa kidogo kidogo. Kwenye *RCC* tuliambiwa tumetengewa shilingi milioni 300. Sisi tuliona kuwa hiyo ndiyo Ahadi ya Waziri Mkuu, kuitengeneza barabara hiyo kwa kuitengea pesa kidogo kidogo. Kwa mshangao, sijaona pesa iliyotengwa katika vitabu vya bajeti. Hii ina maana gain?

Mheshimiwa Waziri, nakuomba uutazame Mji wa Kibaha kwa jicho la huruma. Tayari kuna watu wanaoonyesha nia ya kugombea Ubunge 2010, wameanza kusambaza sumu mbaya kuwa Mji wa Kibaha hautengenezwi kwa sababu Mheshimiwa Dr. Zainab Gama hatakiwi na wakubwa na wala Serikali. Ndio maana Mji wa Kibaha utakaa porini mpaka Dr. Zainab Gama atakapoangushwa. Kwa hiyo, 2010 akipatikana Mbunge mwingine, Mji utajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Serikali kuondoa uvumi huu, naomba Mji wa Kibaha utengenezwe ili ufanane na Miji Mikuu mingine ya Mikoa ya Tanzania.

**MHE. MWADINI ABABAS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upungufu na uchakavu wa vyombo vya usafiri hasa Baharini na kwenye Maziwa, kumekuwa kunatokea ajali mara kwa mara na kusababisha watu kupoteza maisha na mali zao.

Pamoja na kwamba, Serikali inajitahidi katika upatikanaji wa vivuko, lakini vivuko hivi kwa upande wa usafiri wa baharini ni vichache mno, hali inayopelekea wananchi kutumia vyombo vyao vya usafiri kama vile mashua, madau, ngalawa na majahazi.

Vyombo hivi vinakuwa si salama hasa pale hali ya bahari inapochafuka na kusababisha upemo na mawimbi makali katika hali kama hii inapotokea ajali. Uokoaji wa

wananchi na mali zao, unakuwa mgumu mno kwa kutumia boti za uokoaji. Kwa hiyo, matayarisho ya uokoaji huchukua muda mrefu na ufanisi kuwa mdogo. Ningependa kuishauri Serikali iweke helikopta maalumu kwa ajili ya uokozi wa ajali zinazotokea baraharini na ziwani ili kulinda uhai wa binadamu na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni wakati wa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Wabunge wa Bungu lako Tukufu, baada ya kupokea na kujadili hoja binafsi ya Mheshimiwa Zambi, hatimaye Maazimio kadhaa yalipitishwa kwa ajili kuchukuliwa hatua na Serikali. Mionganoni mwa Azimio la Bunge kuhusu hoja hiyo ni kuhusu suala la Mkataba wenye utata wa *TICTS*. Ninataka kujuu mpaka sasa ni hatua gani Wizara imechukua, kuhusu Mkataba huu wa Serikali na *TICTS* wa suala la kushughulikia makontena Bandari ya Dar es Salaam? Aidha, Serikali imechukua hatua gani katika kusitisha nyongeza ya miaka 15 zaidi ya ule Mkataba wa awali wa miaka kumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Serikali kwa kuvunja mahusiano ya kibiashara na Shirika la Ndege la Afrika Kusini na sasa *ATCL* imerudi mikononi mwa wananchi wenyewe. La kushangaza sana ni kwamba, Shirika hili lina matatizo makubwa ya kifedha. Aidha, hata Menejimenti ya Shirika hili inaonekana imepwaya sana.

Ningelipenda kuishauri Serikali, kuliimarisha Shirika hili la *ATCL* kifedha ili liweze kupata ndege za kutosha, kubwa na za kisasa. Liweze kufungua safari zake nchi mbalimbali duniani na kuweza kushindana kibiashara na Mashirika ya Ndege ya Ethiopia na Kenya, ambayo yanaonekana yamepiga hatua sana kibiashara na kuweza kuhimili ushindani.

Kadhalika ni vyema basi na Menejimenti ya *ATCL* ifanyiwe marekebisho makubwa ili kuweza kuliendesha Shirika letu hili kwa ufanisi zaidi.

Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni mikakati gani Serikali itaitekeleza, kuhakikisha kwamba Shirika la Ndege *ATCL* linaboreka kiufanisi na kuweza kuwashudumia abiria wake ndani na nje ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamekuwa wanalamia kila sana kuhusu huduma ya usafiri wa reli, ikiwemo njia ya reli, mabehewa, injini, pamoja na majengo mbalimbali. Bahati mbaya, dhuhuni hili linaonekana linachelewa kutimizwa, hali inayopelekea huduma wenyewe kudorora. Aidha, nauli zimepanda sana, mabehewa ya mizigo au ng'ombe ndiyo yanayotumika kusafirisha abiria. Mbaya zaidi, idadi ya abiria ndani ya behewa moja ni zaidi ya uwezo wa mabehewa wenyewe mara kumi. Hii ni hali ya hatari kwa uhai wa wananchi na mali zao.

Naiomba Serikali, kama vile ambavyo askari wa barabarani wanasimamia mienendo ya mabasi na idadi ya abiria wanaochukuliwa na mabasi hayo, basi ni vyema iandae utaratibu wa kusimamia idadi ya abiria wanaopakiwa katika mabehewa ya reli ili kuepusha wananchi wetu kuhatarishiwa maisha yao. Naomba kujuu ni mkakati gani Serikali imejiwekea kusimamia tatizo hilo?

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kusema naunga mkono hoja hii, kwa vile Wizara hii kupitia bajeti hii imeonyesha mwelekeo wenyewe kutia matumaini ya utekelezaji wa ahadi za Ilani ya uchaguzi ya CCM. Hata hivyo, ninayo mawaidha yafuatayo:-

(a) Matengenezo ya barabara ya Dodoma – Manyoni; tunaishukuru Serikali kwa kuanza kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Awali ilipangwa kukamilika 2007, lakini hadi hivi sasa haijaisha na mara kwa mara Mkandarasi husimamisha kazi kutokana na kutolipwa. Tunaiomba Serikali imlipe madai yake KONOIKE (mkandarasi), ili barabara hii ikamilike. Tunarudia ombi letu la awali kwamba, kwa vile barabara hii inapita nje kidogo ya Mji wa Manyoni, tunaomba barabara ya sasa inayopita katikati ya mji iwekwe lami hata kama ni ile lami nyepesi.

(b) Bodi ya Barabara ya Mkoa, ilishaipitisha Barabara ya Chikuyu – Chibumungwe – Majiri – Ikasi (120 km); ipandishwe daraja iwe ya Mkoa. Barabara hii inapita katika eneo lenye viwanda vidogo vidogo vya chumvi, eneo la kilimo cha mazao ya biashara ya ufuta/karanga, eneo lenye wafugaji wengi na kadhalika. Hii ndiyo barabara pekee inayohudumia vijiji vyote katika bonde la ufa.

(c) Barabara ya Chunya – Itigi – Mkiwa imeanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami kutoka Mbeya kwenda Chunya, lakini kutoka Chunya kwenda Itigi hadi Mkiwa, maandalizi yake hayaleti matumaini na wala Wizara katika hotuba yake haikueleza ni lini hasa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Singida; hivyo, ina umuhimu mkubwa.

(d) Tunaishukuru Serikali kwa kumpata mkandarasi wa kuitengeneza Barabara ya Manyoni - Isume (53km). Lakini makisio ya kazi hii ni miezi 36, yaani miaka mitatu; eneo hilo halima milima wala mito (madaraja) ni tambarare; vipi ujenzi uchelewe muda mrefu hivi? Wizara isimamie mkandarasi amalize kazi hii katika muda mfupi kuliko miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Baada ya hapo naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza na kumshurukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa juhudhi zake alizofanya mpaka kufanikisha Serikali ya China, kusamehe mkopo wa Serikali ya Tanzania na Zambia wa ujenzi wa reli TAZARA. Sasa naiomba Serikali, ifanye haraka mchakato wa kutafuta wawekezaji ili waiendeshe reli hii kwa ufanisi. Serikali ikisinzia, tutapoteza biashara ya Zambia, Malawi na Congo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeamua kuondoa Kitengo cha Manunuzi toka Wizara hii na kukipeleka Wizara ya Fedha, basi naomba na NBMM nayo, pamoja na *Government Stores* ziende Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Bandari iliweka *flow meters* Bandarini Dar es Salaam na Tanga mwaka 2006. Baada ya kufunga mita hizi, mapato ya Serikali kwa kodi ya mafuta yamepanda kutoka shilingi bilioni saba kwa mwezi mpaka shilingi bilioni 29 kwa mwezi. Mita hizi zimefanya kazi miezi sita tu na kuharibika. Mwaka jana mzima na mpaka sasa mita hizi, hazifanyi kazi. Naomba maelezo toka kwa Waziri, maana mimi ni nahisi *foul play* toka kwa wafanyabiashara ya mafuta kuhusu mita hizi na naona mapato ya Serikali yanavuja sana hapa.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Kwanza, nashukuru na kuipongeza Serikali kwa kuanza kuijenga Barabara ya Mbalizi - Mkwajuni - Makongolosi, pamoja na ile ya Galula - Magamba - Muheza - Namkukwe. Tatizo, kazi inakwenda polepole sana. Nashauri jitihada ziongezeke kukamilisha ujenzi huo.

Serikali iliahidi kutengeneza sehemu korofî tatu kwa kiwango cha lami kwenye barabara ya Mbalizi – Mkwajuni - Makongolosi. Sehemu hizo zina wastani wa kilomita moja na nusu. Nashauri ahadi hiyo itekelezwe.

Vilevile nashauri vifusi vilivyorundikwa kwenye Mlima wa Mbala, Barabara ya Mbalizi – Makongolosi, visambazwe haraka maana vifusi hivyo vimeanza kupeperushwa na upepo.

Serikali ianze kufikiria kurudisha utaratibu wa kuwepo na vituo vinavyojulikana kama magenge, vitakavyotumika kuhudumia sehemu korofî za barabara.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa; Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje; Katibu Mkuu, Brg. Omari Chambo na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Joyce Mapunjo, pamoja na wataalam na watumishi wote wa Wizara. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Magharibi na kwa niaba yangu, ninaipongeza Wizara kwa maamuzi ya kuanza kutekeleza Miradi ya Ujenzi wa Madaraja ya Mto Kilombero na Mwatisi. Daraja la Mto Kilombero ni faraja, siyo tu kwa wananchi wa Jimbo langu, bali pia kwa wakazi wa Wilaya nzima ya Ulanga, Wilaya ya Kilombero na Wilaya ya Namtumbo iliyopo Mkoa wa Ruvuma. Aidha, Daraja la Mwatisi ni kiungo muhimu ndani ya Tarafa ya Malinyi, ambayo kijiji chake cha mwisho cha Kilosa kwa Mpepo, ndani ya Wilaya ya Ulanga na pia kuingia na Wilaya ya Namtumbo na Mkoa wa Ruvuma. Hivyo, ujenzi wa madaraja haya ya Kilombero na Mwatisi, utakuwa mkombozi wa Wana-Morogoro na Wana-Ruvuma hasa Wana-Ulanga na Wana-Namtumbo. Nahimiza Wizara kukamilisha ujenzi wa madaraja haya kwa ari, nguvu na kasi mpya.

Naiomba Serikali itazame kwa makini, barabara ya sasa ya Mkoa ya Lupiro – Malinyi - Kilosa Mpepo, kilometra 164 (yaani Kilomita 112 Lupiro – Malinyi na kilomita 52 Malinyi hadi Kilosa kwa Mpepo). Barabara hii ni sehemu ya Barabara ya Mikumi – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kitanda (Namtumbo/Songea). Kwa maneno mengine, hii ni *truck road* (Barabara Kuu), inayotarajia kuunganisha Wilaya za Ulanga na Mamtumbo, yaani Mikoa ya Morogoro na Ruvuma. Nimesikitishwa na kiwango kidogo cha fedha kilichotengwa kwa matengenezo ya Barabara ya Lupiro – Kilosa kwa Mpepo (km 164), Sh. 62 milioni eti *gravelling 3.76 km only*. Barabara ina sehemu korofi nyingi; kwanza, sehemu za Milima ya Msitu Nambiga (km 15), sehemu ya Nakafulu hadi Namhanga (km 10), sehemu ya Mlima Mnyambwe, Bonde la Ifungila na Lupambo, kwa pamoja zaidi ya kilometra 20.

Aidha, sehemu ya Mwembeni (Malinyi) hadi Ihowanja zaidi ya kilometra 20. Sehemu hii hupitika wakati wa Kiangazi tu, lakini yakijengwa matuta na kuwekwa changarawe, barabara hii inaweza kupitika mwaka mzima. Hii ndio sababu ya ujenzi na madaraja ya Furuwa au maarufu kwa Daraja la Ngasongwa, kwa kutambua juhudzi za Mbunge wao ya ujenzi wa Barabara ya Ulanga (Malinyi) hadi Namtumbo, Songea (Kitanda) (Ukurasa wa 128, Mkoa wa Morogoro, Hotuba ya Waziri wa Miundombinu).

Katika Hotuba ya Msemaji wa Upinzani katika Wizara hii, Mheshimiwa Kabwe Zitto, kuhusu *Rural Road Agency (RRA)*, wazo hili lilishatolewa na aliyekuwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kabla ya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri Februari, 2008. Waziri huyu aliandaa makala iliyojenga hoja ya kuanzisha Wakala wa Barabara Vijiji na Mfuko wa Barabara Vijiji (*Rural Road Agency* na *Rural Road Fund*). Makala hii ilitumwa kwa Mheshimiwa Rais, nakala kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambaye sasa ndiye Waziri Mkuu wetu mpendwa, Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki na Waziri wa Miundombinu wakati huo, Mheshimiwa Andrew Chenge. Natumaini nakala hiyo bado ipo ofisini kwako Mheshimiwa Waziri.

Aidha, makala yote iliyochapishwa katika Jarida la “*Construction*,” hoja za makala hii ni nyingi, lakini kubwa ni *focus* na miliki ya wadau. *RRA/RRF* itaendeshwa na kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na *District Engineer* (Ujenzi) wa Halmashauri, Manispaa na Jiji, ndiye mwakilishi wa *RRS*. Lengo ni kuwawezesha Madiwani (Halmashauri, Manispaa na Jiji), kuwa wasimamizi wa shughuli na utendaji wa Wakala wa Barabara Vijiji na Mfuko wa Barabara Vijiji.

Hoja ya *economics of scale* ni sahihi pia, lakini hoja ya udhibiti wa wadau ni muhimu sana. Kwa kuwa nchi yetu ni kubwa mno na ina barabara zaidi ya kilometra 85,000, ambazo zaidi ya kilometra 55,000 ni Barabara za Wilaya na Vijiji, ambazo kwa kweli hazina mwenyewe au fedha za uhakika licha ya kutosha kujenga, kuzitengeneza, kuzikarabati wala kuzitunza. Hii ni moja ya sababu za Waheshimiwa Wabunge, kudai baadhi ya barabara zao ziwe za Mkoa au Barabara Kuu. Katika mashauriano niliyoyafanya na Maofisa wa Benki ya Dunia na *NORAD*, kuna uwezekano mkubwa wa kupata msaada moja kwa moja za Barabara za *RRA/RRF*. Isitoshe, suala maendeleo vijiji, litapata msukumo ikiwa barabara vijiji katika mfumo huu zitapewa kipaumbele.

Suala hili pia ni la uwezeshaji kiuchumi wananchi hasa wa vijiji. Kampuni ndogo za vijiji zitapata fursa ya kandarasi za barabara na madaraja, ambazo zitaajiri wanawake na vijana kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia suala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Katika Sekta ya Ujenzi hasa wa Barabara na Madaraja, Sera ya uwezeshaji na Sheria Na. 24 ya 2004, zinafafanua vizuri suala hili. Nakuomba urejee maandishi haya Mheshimiwa Waziri.

Kimsingi Sekta hii inatawaliwa sana na wageni kama ilivyo ya ushauri wa kitaalam. Nakuomba uanzishaji mapinduzi katika sekta yako, kwa kunufaisha zaidi Watanzania wazawa. Faida nyingi zitapatikana kwa hatua ya aina hii. Mojawapo ni *retention* ya fedha, itakuwa kubwa zaidi. Tutapambana na umaskini wa kipato kwa uhakika zaidi na hatimaye kuboresha maisha ya Watanzania wengi zaidi.

Kwa maoni na imani sekta hii na zile za Viwanda na Biashara, Madini, Kilimo cha kisasa (kwa tafsiri pana Kilimo), (kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi) na Maliasili (uvunaji wa rasilimali asili, misitu na wanyamapori hasa uwindaji wa kiitalii).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa shukrani na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Timu yake yote Wizarani.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujiunga na wenzangu katika kuchangia hoja hii muhimu ya Wizara ya Miundombinu.

Kwanza kabisa, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wao, kwa kazi nzuri na juhudhi kubwa wanayofanya katika kuhakikisha kwamba, Serikali inajaribu kwa kadiri inavyoweza, kuhakikisha kwamba inapunguza kero zinazohusiana na miundombinu hasa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri yote yanayofanywa na Wizara hii, lakini bado wapo watendaji ambao wanakatisha tamaa katika kuharakisha maendeleo. Nazungumza haya kwa sababu pale kwenye Jimbo langu la Morogoro Mjini, tunalo daraja moja tu katikati ya mjini, ambalo ni kiunganishi cha kuwafanya wananchi wavuke kupata huduma kutoka kila upande. Daraja hili tayari limeshaweka ufa mkubwa tu na lipo chini ya *TANROADS*.

Sasa kutokana na tatizo hili, tumeonelea tujaribu kujenga daraja lingine mbadala ili kupunguza msongamano na uzito mkubwa, liweze kuishi kwa muda mrefu zaidi. Kama daraja hili litavunjika kabisa, maana yake itaigharimu Serikali fedha nyingi sana ambazo hazipo. Hivyo basi, tumeonelea kuanzia mchakato wa kujenga daraja mbadala; ambalo gharama yake si kubwa sana kulinganisha na hili kubwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kinachonisikitisha ni kwamba, upembuzi yakinifu umefanywa na wataalam wa *TANROAD* karibu miaka miwili iliyopita na tukaambiwa michoro inafanywa na inakamilishwa Wizarani. Toka tuambiwe michoro inakamilishwa, hivi sasa ni zaidi ya mwaka mmoja na nusu; hivi kweli michoro ya daraja la kawaida

hukuchua muda wote huo? Kwa mtindo huu kweli tunategemea kupata maendeleo ya haraka? Maana kila nikiulizia naambiwa subiri baada ya wiki moja au mbili, kila mara naambiwa hivyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, sina nia ya kuzuia shilingi ya mshahara wa Waziri, kwa sababu naamini kosa hili sio la Mheshimiwa Waziri, bali Watendaji wake; hivyo, basi namwomba afuutilie jambo hili ili ajue uzembe huo unafanywa na nani, ambaye anajiona ni mkubwa sana ambaye hawezi kuhojiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, afuutilie kwa karibu sana kitengo hiki cha uchoraji. Wafanye kazi sasa kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Wajaribu kusahau kule kulikotoka, maana tunahitaji maendeleo ya haraka sana. Bado naamini jambo hili litarekebishwa kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia heri sana, wapate nguvu za kuwashudumia Watanzania ambao wanahitaji maendeleo. Naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake ya Bajeti vizuri sana. Ni dhahiri kwamba kuna kazi nyingi na kubwa zinazofanyika katika kupanua mtandao wetu wa barabara, viwanja vya ndege na vivuko. Naipongeza sana Serikali za awamu ya tatu na nne kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na matatizo makubwa sana ya barabara. Maeneo mengi hayana barabara au barabara zilizopo ni mbaya sana. Katika mwaka uliopita, tuliahidiwa kwamba zinajengwa *ring-roads* na barabara kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara kuu. Hakuna dalili za kutekelezwa kwa ahadi hizo na wala hakuna maelezo kwa nini ahadi hizo zimepuuzwa. Hali hiii linatutia wasiwasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Ubungo kuna ulazima wa kujenga *a fly-over* ili kuondoa msongamano wa magari kwenye makutano hayo ya barabara wakati wa asubuhi au jioni. Mtu anaweza kukwama kwenye msururu wa magari pale Ubungo kwa saa mbili hadi tatu. Muda unaopotea ni hasara kwa uchumi wa nchi.

Aidha, magari yanayokwama kwenye msongamano huo yanachoma mafuta yanayonunuliwa kwa fedha nyingi kutoka nje ya nchi na yanatoa moshi unaochafua sana mazingira. Inabidi Serikali ikubali kuondoa kero hii mapema sana. Kwa maoni yangu, kinachokosekana ni ujasiri wa kuamua. Kwa vyovoyote vile, usanifu wa *fly-over* hiyo unapaswa kukamilishwa mwaka 2008/2009 na ujenzi ufanywe 2009/2010 bila kukosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi dakika za mwisho za mchakato wa kuandaa makisio haya, barabara ya “*round about*” ya Kawawa – Kigogo – Mabibo – Maziwa – Ubungo na Maziwa - External ilikuwamo na Mheshimiwa Waziri Mkuu alihimiza sana

ipewe fedha ili ijengwe. Barabara hiyo ni muhimu sana katika kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara za Morogoro na Mandela. Inashangaza kwamba barabara hiyo imepewa Sh. 30 milioni tu! Kiasi hiki ni kidogo sana na hakitoshi kuitilia barabara hii lami.

Katika miaka miwili iliyopita, Serikali imeahidiwa, zaidi ya mara tatu, kwamba barabara ya Tangibovu – Mbezi – Luis – Kinyerezi ingejengwa kwa kiwango cha lami kwa kuwa ni *ring road* katika mwaka wa fedha 2007/2008 barabara hiyo ilifanyiwa usanifu lakini haikutengewa fedha katika mwaka 2008/2009. Kiasi cha Shilingi milioni 100 kilichowekwa kwa barabara ya Tangibovu – Goba – Mbezi Luis ni kidogo sana kisichotosha hata kutilia kifusi. Kipande cha Mbezi -Malamba Mawili – Kinyerezi kimepewa Shilingi milioni 20 tu hiki ni kiasi kidogo sana cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba Chuo cha Usafirishaji kimepewa fedha za kujenga Mkataba. Chuo hiki ni muhimu sana kwa Taifa letu kuwa ndiyo Chuo pekee kinachoandaa wataalam wa usafirishaji. Tunaiomba Wizara ihakikishe kwamba Chuo hiki kinatumika kikamilifu kwa kuchukua wanafunzi wa kutosha kujaza nafasi zote zilizopo. Aidha, utaratibu wa kuandaa madereva uendelezwe na iwe ni lazima kwa madereva wote wa mabasi kupitia kwenye Chuo hiki ili kupunguza ajali na vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. RAPHAEL MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya CCM ya mwaka 2005 inaadhi kuwa barabara zote nchini ziwe za lami na zile zinazounganisha Makao Makuu ya Wilaya zipitike mwaka mzima kwa kuwekewa lami nyepesi (Kifungu 37, Uk. 24 wa hotuba). Vile vile barabara ya Itoni – Ludewa – Manda ni barabara kuu na inayounganisha Makao Makuu ya Ludewa na Njombe.

Zaidi ya hapo, barabara za Itoni – Mkiwu – Ludewa – Manda na Itoni Mkiwu – Liganga ni za kiuchumi mkubwa kuelekea migodi ya Mchuchuma na Liganga. Kadhalika, Serikali imepanga kuanza uchimbaji chuma, Liganga na ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha *Sponge iron* kwa kutumia chuma (Ligonga) na makaa ya mawe Mchuchuma mwaka huu.

Kwa vile barabara hizi za Ludewa zinazingatia vigezo vya kiuchumi na Ilani ya CCM, kwa nini barabara hizi hazizungumziwi kujengwa kwa kiwango cha lami?

Uimarishaji wa gati ya Manda pamoja na *Mbambabay* ultengewa Shilingi milioni 100 mwaka 2006/2007, Shilingi milioni 50 mwaka 2007/2008 na Shilingi milioni 50 mwaka 2008/2009. Nataka maelezo kwa nini Bandari ya Manda yai kujengwa kwa miaka miwili mfululizo wakati fedha ilitengwa.

Kuna mawazo yanayopingana kuhusu reli itakayotoka Liganga/Mchuchuma kwenda Mtwara au Dar es Salaam. Je, uamu ni kutumia *alternative* ipi kati ya hizi mbili na maandalizi yake yamefikia wapi?

**MHE. MARIA IBESHI HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa hotuba yake kwa kufafanua utekelezaji utakavyokuwa kwa kufuata Ilani ya Chama Tawala

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Uwanja wa Ndege Mwanza, tunashukuru upanuzi wa uwanja huo, lakini nyumba, majengo, Ofisi, hazilingani kabisa na hadhi ya uwanja huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba, utafutwe mkopo kwa ajili ya kubadili/ kuboresha majengo hayo na bajeti ijayo ya mwaka 2009/2010 iwe kipaumbele katika majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Reli ya Kati, usanifu huu Mheshimiwa upo, lakini haufai kabisa. Mabehewa hayatoshi na ni machafu sana na ratiba haifuatwi ili kupunguza msongamano mkubwa wa wasafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni moja kwa ajili ya viwanja vya ndege, Mwanza na Kigoma, tunaipokea. Ombi ni kwamba itumike ipasavyo.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Matumizi ya fedha mwaka 2008/2009 kwa ajili ya Wizara ya Miundombinu. Aidha, nawapongeza Watendaji wote wa Wizara hiyo kwa maandalizi mazuri ya hotuba nzuri iliyosheheneza taarifa na takwimu za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuona umuhimu na kwa hiyo, kutenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba. Ni matumaini yangu kuwa kazi zilizopangwa kufanyika zitafanyika ili kukifanya kiwanja hicho kiweze kutumika wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri wa reli ya kati, Mheshimiwa Waziri ameelleza mipango mingi ya kurekebisha usafiri wa Reli ya Kati lakini inavyoolekea ni mipango ya muda mrefu. Namshauri Mheshimiwa Waziri aangalie/afuatilie kwa haraka suala zima la hali mbaya na matatizo yanayowakumba wasafiri wa treni ya Dar es Salaam – Dodoma – Tabora – Kigoma na Mwanza. Kuna matatizo makubwa sana. Je, Waheshimiwa Wabunge wanafikiri wanasema uongo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya mwekezaji kulikuwa na utaratibu wa kila treni kuwa na behewa/mabehewa machache ili kubeba mizigo ambayo wasafiri hawawezi kusafiri nayo katika mabehewa ya wasafiri, pia mizigo ambayo haiwezi kukidhi haja ya kukodi behewa. Sasa hivi utaratibu huo haupo, hivyo mtu mwenye mizigo michache au asiye na uwezo wa kukodi behewa hawezি kusafirisha mizigo yake. Namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie hili na utaratibu wa zamani urejee.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaelekea Mkoa wa Kagera una barabaraba, chache za Mkoa, lakini tunashukuru kwa namna ya barabara hizo zinavyohudumiwa na kwa hiyo,

kuweza kupitika mwaka mzima. Kuna barabara ya Kabanga – Mabawe – Mukikomero-Kirushya – Ntobeye – Nyakiziba hadi Ruvubu na kuvuka kwenda Rusumo *Customs*. Barabara hii inaambaa mpaka wa nchi yetu na nchi ya Burundi na Rwanda, hivyo, kwa kweli inastahili kuitwa Barabara ya Ulinzi. Nashauri barabara hiyo ipandishwe hadhi na kuwa ya Mkoa pindi sheria husika itakapopitishwa. Lakini nauliza, ni lini Sheria italetwa Bungeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika barabara niliyoitaja hapo kuna kivuko (ili kuvuka kwenda Rusumo *Customs*) ambacho ni kichakavu kinachotembea kwa kuvuta kamba. Ni lini Serikali itaweka kivuko kipyta ili hata magari yaweze kupita? Hii ni njia fupi ya kwenda Ngara kutoka Rusumo badala ya kuzunguka kupitia Nyakasanza Benako/Kasullo hadi Rusumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa ambapo tunasubiri Uwanja wa Ndege wa Bukoba kutengenezwa, tunaomba Serikali ione umuhimu wa kuboresha usafiri wa meli ndani ya ziwa Victoria. Ni njia nyepesi na rahisi kwa kusafiri na kusafirisha mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE MATUMBO SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Waziri, nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Wizara hii nyeti na muhimu, sio tu kwa uchumi wetu, bali pia kwa maendeleo ya nchi yetu.

Aidha, nichukue fursa hii kumpongenza Naibu wake (kaka yangu), Mheshimiwa Chibulunje, kwa kuteuliwa kwake. Pia niwapongeze Katibu Mkuu - Ndugu Chambo na Naibu Katibu Mkuu – Ndugu J. Mapunjo (*Iron lady*) kwa kazi nzuri waifanyayo. Naamini kutokana na timu hii tutapata mafanikio mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitaifa, napongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mundombinu ila ninayo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa na Wataalam, ni kwa nini barabara zikianza kuharibika, tunaendelea kuziangalia mpaka zinakuwa mahandaki ambapo gharama ya matengenezo inakuwa kubwa sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, tuliwahi kuona Wachina wakiwa wamepewa tenda kubwa ya kukarabati *sewage system Dar es Salaam*? Tuliwahisini kuwa walikuwa bora kuliko wengine walijitokeza, matokeo yake maji yamekuwa yakijaa zaidi na kuleta usumbufu mkubwa katika Jiji la Dar es Salaam. Je, Wizara ina mkakati gani na *weighbridge* zinazohamishika kuwekwa ovyo ovyo kiasi cha kusababisha usumbufu mkubwa kwa magari pale wanaposimamishwa ovyo ovyo, hakuna utaratibu?

Je mna utaratibu gani wa kutengeneza *traffic lights* zinapoharibika au kugongwa au kuugua *bulbs*? *Who is responsible? Are you satisfied with performance ya ATC inayopata ruzuku compared to Precision isiyopata?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mkoa, naomba maelezo kuhusu matengenezo ya Bandari, Tanga kule Mwambani mwaka jana lilisomeka hivyo hivyo. Je, pengine niulize ni lini kazi hiyo itakamilika hasa ukizingatia ndiyo itafufua uchumi wa Mkoa wa Tanga, kwa kiwango kikubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mbona barabara yetu muhimu Handeni /Mkata haina pesa kwa 2008/2009? Aidha, barabara ya Korogwe – Handeni – Mzihi – Mikumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango gani wa kuagiza karakana (Mikoa) kutupatia *grader* kwenye Wilaya bila kututoza, sisi tugharamie mafuta na posho ya dereva ili kukarabari barabara ziendazo vijiji kabla ya mavuno?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Makao Makuu ya Wilaya, kulingana Ilani, tunaomba lami nyepesi, kwingine imewezekana: Je, Kilindi kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 71 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia nyumba tano za viongozi wa Kilindi, lini zitaanza na kukamilika na kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Songe – Kikunde ilipangwa kuingia *TANROADS*, mbona haipo (toka Makao Makuu Kilindi hadi Gairo)?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya *DC* inahitaji ukarabati, wataalam mbalimbali wamekuja kuiona. Kulikoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baada ya yote hayo, naendelea kutoa shukrani zangu kwa wananchi wa Kilindi, wana imani na Wizara yako ila shida haziishi, mtuvumilie. Mungu ibariki Tanzania.

**MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeelezea wazi namna Ilani ya Uchaguzi inavyotekelozwa na Serikali yetu Tukufu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utekelezaji wa Ilani hiyo inatupa faraja Watanzania kuwa Serikali ipo imara kuhakikisha kuwa kinachoandikwa kwenye Ilani ya Chama tawala kinatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutekelezeka kwa ilani hiyo, ningependa kuikumbusha Serikali kuwa, baadhi ya ahadi alizotoa Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni mwaka 2005 bado hazijaanza kutekelezeka. Miiongoni mwa ahadi hizo ni pamoja na barabara ya Kibiti – Ruaruke – Nyamisati. Barabara hii hadi sasa ujenzi wake kwa kiwango cha changarawe bado haujaanza wananchi wanaendelea kuhoji juu ya utekelezwaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika kwenye kikao cha *RCC* – Pwani, hapo Juni mwaka huu, Meneja wa *Tanroads* Mkoa, alieleza kuwa katika bajeti ya mwaka huu, Mkoa umepewaa Shilingi milioni 150 kwa kujenga barabara hiyo kwa kilometra 10 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa hizi ni ndogo sana ukilinganisha na urefu wa barabara ya kilometra 41. Kama Serikali itatoa kiwango hicho kila mwaka, barabara hiyo itaishia mwaka 2012. Hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu aongeze fedha kwa barabara hii ili iweze kukamilika haraka iwezekanavyo na kuwapa imani wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo barabara hiyo inapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuunganisha wananchi wa maeneo ya Delta, kuna barabara mbili muhimu sana. Barabara hizi ni barabara Mohoro – Mtanga – Ruma yenye urefu wa kilometra 19. Barabara hii ni ya Wilaya, lakini ndiyo pekee ambayo inaunganisha wananchi wa Delta Kusini (Tarafa ya Mbweru) yenye wakazi zaidi ya 25,000 pamoja na kusafiri kwa mitumbwi kwa masaa hadi 12 wananchi hao hulazimika tena kutembea kilometra 19 kwa miguu ndipo wafike Mohoro ambako watapanda magari kuelekea maeneo mengine ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutowatendea mema wananchi wa Delta. Naiomba Serikali iweze kuunga mkono jithada za Wilaya kwa kuitengeneza barabara hii ambayo imeshafanya upembuzi yakinifu na Wilaya inagharimu shilingi milioni 600 ili uweze kukamilika. Halmashauri ya Wilaya inajitahidi sana kuifanyia matengenezo madogo madogo (*spot maintenance*) lakini kutokana na ufinyu wa fedha za *Road Fund* zinazopelekwa Wilayani Rufiji. Mchanganuo upo na nitauwasilisha kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya pili kuelekea Delta ni ile ya Mohoro – Kipoka – Mbuchi hadi Mbwena. Barabara hii ni muhimu sana kwa wakazi wa Mbweru. Matengenezo ya barabara hii yanahitaji fedha nyingi sana ukilinganisha na ile ya Mohoro – Mtanga – Ruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inapita kwenye mito minne, naishauri Serikali iweze kusaidia Wilaya angalau kujenga madaraja kwanza wakati ujenzi wa barabara ukisubiri fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya ya Delta hadi sasa Serikali haijatoa kipaumbele katika kuwapatia huduma wananchi wake (*underserved*). Namwomba Mheshimiwa Waziri tushirikiane kwa pamoja ili kuboresha miundombinu hatimaye wananchi hao wanufaikie na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM HEZEKIA SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dk. Shukuru J. Kawambwa (Mb),

Waziri wa Miundombinu kwa hotuba yake nzuri sana yenyе maelezo ya wazi, yenyе takwimu muhimu na aliyoisoma kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Chibulunje (Mb) - Naibu Waziri, Katibu Mkuu - Bwana Chambo, Naibu Katibu Mkuu - Bi. Joyce Mapunjo, watendaji wakuu wa Taasisi chini ya Wizara hiyo pamoja na Wasaidizi wao kwa jinsi wanavyomsaidia Waziri katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nina hoja chache ambazo zinahitaji maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira ambayo imepewa fedha za *EU (STABEX ya Kahawa)* na Mkandarasi *BECCO* akapewa barabara hiyo na utendaji wake kuwa mbovu. Je, ni nini hatima ya barabara ya Mkoa wa Tanga? Ilikwishapendekezwa tangu mwaka 2000.

**MHE. GERTRUDE RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, natoa pongezi kwa hotuba nzuri iliyoandalowiwa kwa makini. Naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri wa ndege, ghamama za uendeshaji *Airport* ni kubwa. Kwa nini *Trafic* ya Ndege katika *Airport* zetu ni ndogo! Serikali iongeze ndege iinue heshima kwa Tanzania. Ni aibu *Presecion* kuwa na ndege nyingi na kufanya vizuri zaidi ya *Air Tanzania*. Serikali ikope, inunue ndege nyingine za kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakandarasi wa barabara wa Kichina, hawana uzoefu kabisa. Wanachukua muda mwingi kufanya kazi dhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama barabara ya Sam Nujoma, kutoka Ubungo kwenda Mwenge imechukua muda mrefu kuliko kawaida. Hawana utaratibu. Ingefaa wanyang'anywe na barabara nyingi ambazo ziko chini ya Wachina hazijakwisha na hazina viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu usafiri wa mabasi. Tabia ya kuchimba dawa njiani ni tabia mbaya na inadhalilisha wanawake. Serikali iimarishe wenye mabasi kujenga vyoo kwenye vituo muhimu ili watu wajisaidie kwa heshima. Imewezekana katika nchi nyingi za jirani na hata zilizoendelea zimeweza. Serikali itoe amri na wenye mabasi watajenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la usafiri wa Ziwa Victoria, Serikali inunue meli mpya kwa wasafiri wa Ziwa Victoria. Maisha ya watu wengi yamo hatarini isije ikatokea yale ya *MV Bukoba*. Mungu alaze roho za Marehemu waliofariki katika ajali ya *MV Bukoba*, mahali pema Peponi. Amen.

**MHE. JUMA SAID OMARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ni moja katika sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Barabara za vijijini ziko katika hali mbaya kiasi kwamba usafirishaji wa mazao mbalimbali ya wakulima yanawawia vigumu kuyasafirisha kupeleka mjini au kwenye masoko. Mazao mengi hususan matunda kama vile nyanya, machungwa, mananasi, ndizi na kadhalika huoza yakiwa mashambani kabla hayajafikishwa kwenye masoko kutokana na ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanja vya ndege ni sehemu nyingine muhimu katika sekta ya Miundombinu ambayo watalii na wageni mbalimbali wanaokuja hapa nchini hupendelea zaidi kuliko usafiri wa barabara. Kwa hiyo, viwanja vyetu vya ndege katika Mikoa mbalimbali vinahitaji kuimariswa ili ndege ziweze kutua bila ya matatizo. Hii itasaidia kuongeza pato la Taifa la hivyo kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa majini hasa katika Maziwa Makuu, Victoria, Nyasa, Tanganyika na kadhalika, unahitaji kuimariswa kwa kupatiwa vyombo vya uhakika kama vile boti zinazokwenda kwa kasi (*speed boats*) ili kupunguza ajali pamoja na vifo kwa wananchi wanaosafiri katika maeneo hayo

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano kwa njia ya simu ni mojawapo wa Sekta ya Miundombinu ambayo sasa hivi imepanuka sana, kwani wananchi wengi wa mijini na vijijini wanawasiliana kwa kutumia simu za mkononi. Pamoja na umuhimu wa njia hii ya mawasiliano, lakini għarama yake imekuwa kubwa kiasi kwamba wananchi wengi hawaimudu. Pamoja na Makampuni mengi ya simu yaliyopo hapa nchini, lakini bado utumiaji wa simu za mikononi unawagħarim u tħalli pese nyingi. Ni vyema makampuni ya simu yakaliona jambo hili na hivyo kupunguza ughali wa utumiaji wa simu za mkononi.

**MHE. GOSBERT BEGUMISA BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Karagwe, napenda kuishukuru Serikali kwa kukumbuka ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara ya Kyaka – Bugene kwa kiwango cha lami. Barabara ya Kyaka – Bugene ni kilometra 58, cha ajabu, fedha iliyotengwa ni Shilingi milioni 550 kwa ajili ya kujenga kilometra tatu tu. Kwa kuwa ahadi ya Rais ni kujenga barabara hiyo kilometra 58 hadi mwaka 2010: Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuhakikisha barabara hiyo ya Kyaka – Bugene inakamilika kabla ya miaka mitano (2005 – 2010) ya uchaguzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ujenzi wa barabara hii uanzie Bugene kuelekeea Kyaka katika Jimbo la Uchaguzi Karagwe, kwani ujenzi ukianzia Kyaka utakuwa umeanzia Jimbo la Nkenge wakati ahadi ya Rais ilitolewa kwa wananchi wa Jimbo la Karagwe.

Pili, naomba Serikali wakati iaanza ujenzi huo, ijjitahidi kutafuta fedha za kujenga barabara hiyo ili wananchi wa Jimbo la Karagwe wafaidike na ahadi ya Rais, barabara hiyo iishe kabla ya mwaka 2010. Kinyume na hapo Mheshimiwa Rais ataonekana aliwadanganya wananchi wa Jimbo la Karagwe. Nina imani na Wizara ya Miundombinu

kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake zote. Naomba msimuangushe Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli ya *MV Bukoba*, ilizama tangu mwaka 1996 na madhara yaliyotokea wote tunayaafahamu. *Mv Victoria* ni nzee, imechoka na haifai kwa usafiri wa majini kwani sio salama. Naisihi Serikali ijitahidi kununua meli mpya ili kuwasaidia wananchi wa Kagera na Mikoa jirani kwa ajili ya usafiri wa uhakika na kuzuia ajali nyingine mbaya inayoweza kujitokeza. Wananchi wa Kagera wanataabika sana kwa kukosa meli hiyo.

Mheshimiwa naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni nzuri, sina matatizo nayo. Napenda Serikali inifahamishe kwa nini inasuasua kutengeneza barabara ya Kamachumu – Nyakahama – Rubale – Izimbya – Omubeya – Karagwe? Hii barabara inatoka Muleba, inapitia Bukoba vijijini hadi Karagwe. Lakini wakati wote ni mashimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi barabara hii inanihu sana, maana ili niende kijiji cha Rutoro mpakani mwa Muleba na Karagwe, napita barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika,, naomba kesho Mheshimiwa Waziri anapotoa majibu kwa ujumla, anieleze kama ametuma watu wake kule *TANROAD* Kagera na wana mpango gani kama Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maandishi, naunga mkono hoja. Yale niliyochangia kwa kuzungumza yanabaki pale pale, nasubiri maelezo ya Serikali.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wote wa mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya hoja hii muhimu katika uchumi wa nchi hii na pili, kwa kuelezea utekelezaji a Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niaomba Mheshimiwa Waziri alisaidie Bunge hili, nini hatma ya barabara zilizotajwa kuwa zitaghamariwa na fedha za Afrika ya Mashariki, kwa kuwa zimependekezwa na nchi za *E.A.* Kwa mfano barabara toka Tunduma - Sumbawanga - Mtukula Mpakani na Uganda. Hivi kuna utaratibu gani kwa barabara hizi kuanza kupata fedha ili zisaidiane na zile zinazopangwa na Serikali yetu? Je, hatuna Kamati inayoratibu mipango hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kutumia fedha zetu badala ya kushirikiana na fedha za *World Bank* zinazotarajiwa kuombwa kwa hizi barabar tano zilizopendekezwa na *East Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe pia maelezo, kwa nini fedha za *MCC* ziko chini ya Wizara ya Fedha (Hazina) badala ya kuwa chini ya Wizara ya Miundombinu, kama wafanyakyo wahisani wengine? Tuna wasiwasi kuwa kunaweza kuwa na masharti tofauti sana na wahisani wengine na hivyo kusababisha utekelezaji wa miradi mingi inayofadhiliwa na *MCC* ikasuasua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sasa Mheshimiwa Waziri alelezee wana Rukwa, kama sasa taratibu za kuanza kutangaza zabuni za kutengeneza barabara hii zianze. Pili, namwomba Mheshimiwa Waziri akubali pendekoz la uongozi wa Mkoa wa Rukwa na wananchi ili ujenzi wa barabara hii upate makandarasi zaidi ya watatu, maana hata baadhi ya wataalam wenye wa *MCC* waliotembelea Mkoa wa Rukwa hivi majuzi, wameona ukweli wa hali ya barabara hii na urefu huo wa kilometra 230.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri pia, chini ya uongozi wake asaidie kuwapanga makandarasi waanzie wengine Sumbawanga kuelekea Lacha ili baadaye tusije tukakumbana na vipande vyta barabara kuishia njiani lakini angalau, wana Sumbawanga wanaamini barabara inajengwa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine Mheshimiwa Waziri amekwishawasilisha kwenye hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. MATILDA SALHA BURIAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa dhati ya moyo wangu niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dk. Shukuru Kawambwa (Mb) - Waziri wa Miundombinu kwa hotoba yake nzuri iliyosheni takwimu na vielelezo kuonyesha majoribio ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Ezekiel Chibulunje - Naibu Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu pamoja na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, kwa kazi kubwa na nzuri wanayoendelea kufanya katika kuendeleza Sekta hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ya bajeti imechangiwa vizuri na kwa ujumla imepokelewa vizuri na Waheshimiwa Wabunge walio wengi. Mimi, kwa upande wangu nitapenda kuchangia hotuba hii kwa kujielekeza zaidi katika kuboresha uratibu wa masuala ya mazingira kama eneo Mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 90 ameelezea maeneo matatu ya Mtambuka, ambayo ni rushwa, jinsia na Ukimwi. Hata hivyo, eneo moja muhimu lilisahaulika. Naomba masuala ya mazingira yaonekane kwa dhati, kama mojawapo ya eneo muhimu sana katika masuala mtambuka.

Kwa ujumla, kuna maeneo mengi sana katika Sekta hii ambayo yanahuksika kwa karibu sana na masuala ya mazingira. Kwa mfano, huduma za hali ya hewa. Kitengo

hiki ni muhimu sana hasa katika kipindi hiki tunachokabiliana na mabadiliko makubwa ya hali ya hewa (*climate change*). Pamoja na kuwa tumekuwa na ushirikiano kiutendaji, ni vizuri – mahusiano hayo yakahuishwa (*mainstreamed*).

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mikataba ya kimataifa inayosimamia uthibiti wa usafirishaji wa taka hasa taka za sumu toka nchi moja kwenda nyingine (*Basel convention*) inazitaka taasisi zinazosimamia huduma za Bandari (*TPA*) na Mamlaka ya Uthibiti (*SUMATRA*) kuhakikisha kuwa sheria hii haivunjwi na pia meli chakavu haziletwi na kutelekezwa kwenye bandari zetu. Kimsingi, kuna mambo mengi sana, hivyo basi, nashauri kama inavyoolekeza kwenye sera na sheria ya mazingira kuanzisha Dawati la Mazingira katika Wizara ili waweze kusaidia kufuatilia masula haya kwa karibu zaidi na hivyo kurahisisha shughuli za uratibu wa masuala ya mazingira ambayo inafanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kutoa pongezi zangu tena nyingi kwa Waziri na Naibu Waziri. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa kwa hotuba nzuri sana. Wote ametupa ufumbuzi wa kuelezea utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Hongera sana. Hotuba imeelezea kwa kina jinsi ambavyo Serikali imetekeleza kwa uhakika Ilani ya CCM ya mwaka 2005 katika Sekta ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiografia ya Wilaya ya Mwanga ina milima ya Upare Kaskazini iliyopo katikati ya Wilaya, tambarare ya Mashariki ya milima sambamba na Ziwa Jipe na tambarare ya Magharibi iliyosambamba na Bwawa la Nyumba ya Mungu. Watu walio wengi na shughuli nyingi za kiuchumi zinafanyika katika eneo la Mlimani katika tarafa za Ugweno na Usangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara inayofika milimani inatokea Mwanga na kupitia *Mwanga Escarpment* mpaka Kikweni. Barabara hii ndiyo inapitisha magari mengi kuliko barabara zote za Mikoa katika Mkoaa wa Kilimanjaro. Barabara ya *Mwanga Escarpment* ni korofii sana, ina mawe, makubwa. Bahati nzuri Wizara ilikubali kuiwekea lami barabara ya *Mwanga Escarpment* kwa kilomita 11 kutoka Mwanga hadi Kikweni. Tangu mwaka 2006, 2007 na 2008 barabara imewekwa lami kidogo sana. Aidha, kwa miaka yote mitatu imewekwa urefu wa kilometra 1.2 tu kwa maana ya kilometra 0.4 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Mwanga, naomba mwaka huu, Serikali ituwekee angalau lami ya kilometra nne tu ili tufike angalau urefu wa kilometra 5.2. Hili naomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tumekuwa tunajenga barabara ya Mwanga *Bypass* tangu mwaka 1995. Katika mwaka wa 2002 aliyekuwa Waziri wa Ujenzi - Mheshimiwa John Pombe Magufuli (Mb) aliahidi kutupatia *Bailey Bridges* mbili ili

tukamilishe kazi hii. *Bailey Bridges* hizo tuliahidiwa kuwa zitatoka kwenye daraja za zamani zinazojengwa upya katika barabara ya Kusini. Naomba Wizara ikumbuke na itusaidie hizi *Bailey Bridges*.

Napenda tena kutoa pongozi zangu za dhati kwa hotuba nzuri sana. Asante sana.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri na Naibu kwa utulivu wanaouonyesha katika utendaji wao wa kazi. Naomba watendaji wa Wizara wakaongozwe na Katibu Mkuu, waonyeshe uadilifu na imani ya utendaji wa kazi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo naomba maelezo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya mkopo kutoka America alioelekezwa Rais atekelze mambo kadhaa ili apewe mkopo wa zaidi ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya ukarabati wa reli ya kati, maelekezo hayakukamilika kuanzia mwezi Septemba, 2007 hadi Mwezi Mei, 2008 ndiyo wakakamilisha watendaji wa Wizara hii. Sasa uzembe huo wa kukawia kutimiza yanayoelekezwa, fedha hizo zitapatikana kweli na kazi ianz? Nani alizembea na hatua gani imechukuliwa kwa Maafisa hao wanaoshindwa kutimiza wajibu wao? Suala hili nilieleza kwenye Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu apotoa hoja yake na mimi nikalieleza. Naomba jibu kwamba, ni lini tunapata fedha hizo? Lini fedha hizo zitapelekwa kwenye ukarabati wa reli hii ya kati?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipokwenda India mwezi Mei, 2008 na akatueleza tatizo la reli ya kati, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisikia ombi hilo na Mheshimiwa Rais aliahidiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu huyo wa India kuwa, Mheshimiwa Rais arudi Tanzania apelike ombi rasmi la kuomba mkopo na India itakuwa tayari kutoa mkopo nafuu wa dola milioni 43 ili zisaidie kuendesha reli hii. Hadi nilipochangia tarehe 27 Juni, 2008, Serikali ilikuwa haijafanya chochote. Je, ni vipi? Reli hii itakuwa imara na salama kwa wananchi kutumia ikiwa fedha za ndani hazipo na za mikopo hazichangamkiwi? Naomba maelezo ya fedha hizi, mtazipataje kama Serikali inaelekezwa cha kufanya lakini utekelezaji hakuna? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatari kwa wananchi wanaotumia reli hii, kwa sasa hivi ni kifo kwa watu. Wakati Serikali imejipanga, niliomba msitishe au mwongeze ratiba ya treni irudi mara nne kwa wiki. Je, ratiba hii itatekelezwa? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Itigi – Tabora, upembuzi ulikwisha siku nyingi. Serikali ielete lini inaanza ujenzi? Naomba maelezo.

**MHE. DR. LUKE J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii nimpongeze Waziri wa Miundombinu – Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa (Mb), kwa hotuba mahiri yenyе kuelezea kwa upana utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2005 hadi sasa na shughuli zitakazotekelzwa kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Pia napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Hezekia Chibulunje (Mb) - Naibu Waziri wa Miundombinu, Katibu Mkuu - Dr. Omari Chambo, Naibu Katibu Mkuu - Bi. Joyce Mapunjo, Wakuu wa Idara na Watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu na Taasisi zake kwa kazi kubwa ya utayarishaji wa hotuba hii na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara hii.

Baada ya kusema hivyo, napenda kusema, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kutokana na jinsi ilivyozingatia. Kwa kiwango kikubwa, uwiano mzuri wa mgawanyo wa usambazaji wa huduma za miundmbinu kwa nchi nzima, hususan miundombinu ya barabara. Naomba niungane na Waheshimiwa wenzangu katika kusisitiza umuhimu wa kuwa na barabara zinazopitika kwa mwaka mzima katika kusukuma mbele maendeleo ya jamii katika maeneo husika kutokana na kurahisisha usafiri na usafirishaji ambayo ni chacchu katika kufungua njia kwa maeneo husika kuendesha shughuli mbalimbali kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi lenye ukubwa wa eneo la Kilomita za mraba 6275 kati ya eneo la kilomita za mraba 9,679 za Wilaya ya Mbozi, lakini kwa bahati mbaya sana, zaidi ya asilimia 85 ya vijiji vya Jimbo hili havifikiki kwa njia yoyote ile kwa takriban miezi nane kwa mwaka, yaani kuanzia mwezi Novemba hadi Juni, kutokana na ama kutokuwepo kabisa kwa barabara ama kwa ubovu wa barabara hizo pale ambapo zipo. Kwa hakika, Jimbo hili ni moja ya maeneo ya pembezoni mwa nchi hii na hivyo kuwa na hali mbaya kiuchumi, uduni wa huduma za afya, elimu na nyinginezo ambazo ni za msingi katika kuleta maisha bora kwa wanachini hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya uhuru kulikuwapo barabara ambazo zilikuwa zinaunganisha vijiji vya Jimbo hili na maeneo mengineyo ya nchi hii na hata nchi jirani za Malawi na Zambia. Kwa bahati mbaya, nyingi ya barabara hizo ama zimetoweka kabisa kwenye ramani ama zimeharibika sana na hivyo kutopitika kwa zaidi ya miezi nane kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufungua maendeleo ya Jimbo la Mbozi Magharibi ukarabati na ujenzi wa barabara zinazopitika kwa mwaka mzima ni muhimu upewe upendeleo maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda nichukue fursa hii kuishukuru kwa dhati Serikali kwa kuitikia maombi ya wananchi wa Mbozi, hususan wala wa Jimbo la Mbozi Magharibi, nikianzia na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Bodi ya barabara ya Mkoa wa Mbeya na Kurugenzi ya Barabara ya Wizara ya Miundombinu ambayo kupitia *TANROADS* Mkoa wa Mbeya iliweza kutekeleza haraka ombi lao na kufanya makisio ya matengenezo ya barabara zifuatazo na kuziombea Wizarani kupandishwa hadhi kuwa za Mkoa kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Chapwa – Chiwezi – Chidi – Msangano – Chitete – Chilulumo – Mkulwe – Kamsamba yenyе urefu wa Kilometra 123, ambayo

Serikali imepanga kufanya matengenezo ya kilomita 66 kuanzia Chapwa hadi Chitete kwa awamu ya kwanza. Barabara hii itaunganisha Kata saba kati ya 11 za Jimbo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kakozi – Chisitu – Kapele – Kasinde – Ilonga yeny urefu na kilometri 54 ambayo Serikali imepanga kuitengeneza yote na hivyo baada ya muda sio mrefu usafirishaji kutoka Tunduma hadi Bandari ya Kasanga, Ziwa Tanganyika itarahisishwa kutoka siku nne za sasa hadi tatu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe shukrani za dhati kwa Serikali kwa kutenga fedha za matengenezo ya barabara za Mlowo – Igamba – Itumbula – Kamsamba yeny urefu wa Kilometri 130 ambayo itaunganishwa na barabara ya Chilyamatundu – Ntendo – Mpanda mkoani Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Igamba – Msangano – Utambalila yeny urefu wa kilometri 86, utengenezwaji wa barabara hizi kwa hakika utaleta mapinduzi makubwa kwa maendeleo ya Jimbo la Mbozi Magharibi, Wilaya ya Mbozi na Mkoa wa Mbeya kwa jumla, kwani Jimbo hili lina hazina ya utajiri iliyolala kwa mfano, kilimo, ufugaji, uvuvi, madini na misitu mbali ya vivutio vyta utalii kama nyayo za binadamu wa kale kwenye jiwe lililopo Kata ya Nkangamo na Kimondo kilichopo Kata ya Ivuma ambacho ni mbali kilie Kimondo maarufu kiiitwacho Mbozi *Meterorite*. Kinachohitajika zaidi ni ujenzi wa barabara imara.

Napenda pia, kwa heshima na taadhima, Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani zangu za dhati kwa uamuzi wa kujenga barabara ya Tunduma – Sumbawanga yeny urefu wa kilometri 231 kwa kiwango cha lami ambapo kilometri 114 ziko Jimbo la Mbozi Magharibi katika Kata nne.

Ombi la Wananchi wa Mbozi na kwa hakika wale wa Mkoa wa Rukwa ni barabara hii kujengwa haraka iwezekanavyo kwa kutumia Wakandarasi wawili tofauti, mmoja akianzia Tunduma hadi Laela na mwengine akianzia Sumbawanga hadi Laela. Umuhimu wa barabara hii umekwisheselezewa na wachangiaji waliotangulia, hivyo sina maelezo tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu, Naibu wake, Katibu Mkuu wa Wizara, Wasaidizi wake na Wakuu wa Taasisi chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa kwa hotuba nzuri iliyozingatia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM wa 2005. Nawapa hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu yanalenga katika maeneo makuu matatu. Mgano wa Mfuko wa barabara na barabara za vijiji; hali ya barabara za Wilaya ya Kisarawe na usafirishaji kwenda nchi za jirani na hali ya Bandari zetu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mfuko wa Barabara ya mwaka 1985 na marekebisho yake ya miaka 1998 na 2006 zinagawa makusanyo ya Mfuko wa Barabara kwa barabara kuu na za vijijini kwa uwiano wa asilimia 70 kwa 30 katika mpangilio huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo huo ulifaa kwa miaka ya nyuma. Sasa panahitajika mabadiliko ili kuongeza hisa ya barabara vijijini angalau ifikie asilimia 40. Nina sababu zifuatazo:-

- (i) Kwenye miaka ya 80 hali ya barabara kuu ilikuwa mbaya sana, sasa kuna afueni;
- (ii) Barabara kuu zina nafasi ya kupata wahisani toka taasisi za fedha za kimataifa na nchi wahisani;
- (iii) Barabara hizo zinaweza kuvutia wawekezaji binafsi kwa mtindo wa “Jenga, Tekeleza na Jilipe” (*BOT*) kwa barabara kuu zina uwezo wa kujilipa wakati sababu barabara za vijijini hazileti faida;
- (iv) Barabara za vijijini ni nyingi. Hivyo mgao kidogo hautakidhi haja;
- (v) Halmashauri ambazo ndizo zenye jukumu la kuzijenga barabara za vijijini hazina uwezo kifedha; na
- (vi) Makusanyo ya mfuko wa barabara kama mlivyoonyesha katika ibara ya 99 yamekuwa yakiongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya barabara za Wilaya ya Kisarawe inasikitisha na inahitaji kupewa upendeleo ili barabara hizo zikaribie sura za barabara nyingine nchini. Katika Ibara ya 8.7 ya Kamati ya Miundombinu, taarifa inashauri Serikali kuendeleza miundombinu iliyopo katika Mikoa ya pembenzoni. Nakubaliana na rai hii, lakini yapo maeneo ambayo kijiografia yako katikati ya nchi, lakini kimaendeleo ni ya pembezoni. Kisarawe ni moja ya maeneo hayo. Kisarawe ina Tarafa nne. Kati ya hizo, Tarafa mbili za Chole na Mzenga nyakati za mvua hazipitiki kabisa. Kwa hiyo, nusu ya Wilaya haina miundombinu ya kuaminika.

Licha ya jitihada zilizofanywa na Halmashauri kuutumia vizuri Mfuko wa Barabara, maeneo yafuatayo hayana barabara na hayapitiki hata nyakati za kiangazi. Gwata – Mzenga; Mafizi Gwata – Kimalamisalie, Marui – chole na Vikumburu; Vikumburu – *Selous* – Mloka (Rufiji); Chole – Mafumbi – Gwata – Dololo; Msanga – Kibukilu – Kimanzechana(Mkuranga) na Masanganya.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zifuatazo hazipitiki nyakati za mvua. Kisarawe – Mzenga – Mafizi; Msanga – Chole – Vikumbulu; Msanga – Marui; Mzenga – Maneromango.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Mkoa ziko mbili. Pugu – Kisarawe – Masaki – Maneromango- Msanga – Vikumburu. Barabara hii nimeipigia kelele tangu mwaka 1996 hadi leo ni kilometra sita tu ndiyo zimejengwa wa lami mwaka 2001/2002. Lakini leo Serikali inapiga debe kuwa imejengwa. Kati ya kilometra 105, unajenga sita tena baada ya Mkuu wa nchi kuagiza. Hivyo ni jambo la kujisifu?

Mlandizi – Mzenga – Manerumango. Hali ni mbaya sana. Kwa msaada wa *DANIDA*, Mlandizi – Mzenga imewekewa changarawe. Sehemu iliyobaki ni nzee! Hali hii inaonyesha kuwa ukaribu wetu na Dar unatuponza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu usafirishaji kwenda nchi za jirani na hali ya bandari zetu. Usafirishaji wa bidhaa toka na kwenda nchi sita za jirani Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kongo, Zambia na Malawi ni moja ya njia kuu zinazoipatia Tanzania fedha za Kigeni. Njia nyingine zikiwa mazao ya Kilimo, Utalii, Madini na Maliasili. Lakini bado nchi yetu haijafaidika vizuri na usafirishaji huo kwa sababu zifuatazo: Kwanza, uwezo mdogo wa bandari zetu kuu wa kuhudumia bidhaa hizo na pili, urasimu katika kushughulikia usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwezo wa bandari zetu: Bandari kuu za Tanzania ni Dar es Salaam, Tanga Mtware na Zanzibar. Zote zina matatizo ya kutomudu uwingi wa shehena zinazopitia katika bandari hizo. Kwa ujumla, sababu kuu ni pamoja na zifuatazo:-

- (i) Tija ndogo katika bandari zenyewe (*low productivity*);
- (ii) Miundombinu finyu, mibovu ya usafirishaji nchi kavu zikiwemo reli na barabara; na
- (iii) Uwezo mdogo wa wahudumiaji bandari (*port operator*) wakiwemo maajenti wa kutoa mizigo bandarini, *TRA* na Maajenti wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo makubwa ya Bandari ya Dar es Salaam ni kulundikana kwa mizigo hasa makontena katika eneo la *TICTS*, kuchelewa kuondoa mizigo bandarini na kuchelewesha uondoaji wa meli kutoka bandarini kwa sababu ya kushindwa kuteremsha na kupakia mizigo melini.

Haya yote yanababishwa na upungufu wa zana kwa sababu ya uwekezaji mdogo, kasi ndogo ya utendaji, urasimu wa *TRA* kuititia maajenti wao, gharama kubwa za ushuru wa *TRA* na *TPA* na uwezo mdogo wa reli na barabara kuondoa shehena bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kwa Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

- Kuangalia upya mkataba wa *TICTS* hasa kwa kuweka viwango vyatowekezaji;
- Kufuta mkataba wa nyongeza;
- Kuitisha zabuni kwa maeneo nje ya mkataba wa awali wa *TICTS* ili pawe na ushindani;
- *TRA* iangalie uwezekano wa kuwaondoa maajenti wao wanaosimamia ushuru wa forodha ili kuondoa urasimu, bugudha kwa wateja na kupunguza gharama. Usimamizi huo sasa ufanywe na *TRA* yenye;
- Zoezi linaloendelea la kujenga barabara kwenda mipaka ya Tanzania liongezwe kasi, kwani nchi nyingi ulimwenguni zinasafirisha makontena zaidi kwa barabara kuliko reli ambazo ni ghali na inahitaji mwekezaji wa mabilioni;
- *SUMATRA* isimamie vizuri utendaji wa bandari, reli na barabara ili kuhakikisha kwa uzembe unatokomezwu;
- Serikali badala ya kuweka mkazo kwenye maeneo ya kuhifadhi makontena ndani na nje ya bandari kama inavyoshauriwa katika Ibara ya 30 ya hotuba, ijenge magati mapya na ikodishe kwa waendeshaji mbalimbali ili kuimarisha ushindani utakaoleta tija.
- Matatizo makubwa ni kina kifupi katika Bandari ya Tanga, hivyo meli kushindwa kuegesha kwenye magati, miamba katika ufukwe na nje baharini, reli mbovu, barabara isiyotosheleza na ukame wa shehena. Kwa kuwa zipo tafiti (*studies*) za kuhamisha bandari kwenda eneo la Mwambani lenye kina kirefu na ujenzi wa reli tokea Arusha hadi Ziwa Victoria ili kupitisha shehena toka Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kongo, vile vile Uganda iko tayari kushiriki katika miradi hiyo na hapa Tanzania wapo wawekezaji walio tayari kushirikiana na wa nje ya nchi, Serikali ichangamkiele changamoto hizi ili matatizo ya Bandari ya Tanga yatatuliwe. Niko tayari kutoa ushauri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Mtwara ina kina kirefu na tatizo ni ukosefu wa usafiri wa nchi kavu, tuta kwenye lango la bahari na kuongezwa magati, nashauri Serikali iyafuatilie haya na iondoe urasimu wa *TRA* kukataa kufungua ofisi Mtwara kwa ajili ya Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Zanzibar ni ndogo, inahitaji kuongezwa magari na kufatilia suala la bandari huru ambalo limesahaulika baada ya kuondoka *Dr. Salmini* kwenye Urais. Kwa kuwa mawasiliano siyo suala la Muungano, Mheshimiwa Waziri anachowea kufanya ni kumshauri mwenzake wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY FIDELIS OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara za *TANROAD*, ningependa kujua ni kigezo gani kinachotumika kupata Mkandarasi? Kama tenda inayochukuliwa ni ile yenye bei nafuu, basi hapa ndiko matatizo yanakoanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, akishamaliza kutengerneza barabara, kwa hakika lazima anaikabidhi na kuwa na aidha Mhandisi wa Kitanzania au aliyoeta *tender* anakabidhiwa barabara ile. Cha kujiuliza: Je, barabara hizi wanapokabidhi huwa wanatoa *guarantee* barabara ile itatumika kwa muda gani kabla haijaharibika?

Kwa mfano barabara kuu ya kile kipande kutoka Mlandizi mpaka Chalinze, ilie barabara ina mawimbi na inasababisha *accidents* za mara kwa mara katika barabara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili: Je, ile barabara pale Dar es Salaam ya Sam Nujoma itamalizika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika Shirika la Ndege la *ATC* ni jambo la kusikitisha kwa jinsi Shirika hili linavyofilisika tukiona kwa macho yetu. Niliuliza swalii Na.168 hapa Bungeni kuhusu umuhimu au kigezo gani kilichotumia kwa *ATC* kwenda kukodisha ndege ya *Airbus*. Majibu yaliyotolewa ambayo sikubaliana nayo, *ATC* siku zote imekuwa ikitumia ndege aina za *Boeing* kulikuwa na tatizo gani la kuendeleza hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, *Air Bus* hii inakodishwa kwa dola 325,000 kwa mwezi, bado *Insurance* na watu wa kufanya *maintenance* wanatoka *Mauritius* wanalipwa dola 225,000 kama sikosei. Malipo kwa ndege hii yanahitaji karibu dola 800,000 kwa mwezi. Kwa njia hii, kweli shirika hili litafufuka?

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu. Kuna zile ndege mbili zilizonunuliwa na *ATC* kwa karibia dola 800,000 wakati kwenye mtandao ndege aina hiyo hiyo ipo kwenye soko. Kwa bei ya dola 500,000. Swalii la kujiuliza, wanunuzi hawakufanyia utafiti? Naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika la *Presicion Air* wanakodi ndege ya *Boeing 737 – 300* ambayo inatumia mafuta madogo zaidi na kukodi ndege ile wanakodi kwa dola 125,000 chini (zaidi ya nusu) ya kurudi ile *Air Bus* ambayo *ATC* wameikodisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua *ATC* wameshalipa kiasi gani kwa kurudisha ile *Air bus*? Kwa nini ndege yenye bei ya juu kiasi hiki isirudishwe ilikotoka na wakakodisha ndege ya bei nafuu zaidi ili tunusuru shirika?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona katika vyombo vya habari kwamba *ATC* wanadaiwa mafuta na *BP* hawajalipa. Ningeshauri Serikali iingilie kati ili inusuru Shirika hili. Naamini kabisa kuna fedha za dharura. Serikali kama tuliweza kupata fedha nyingi tu za kufadhili mkutano wa Leon Sulvan, kwa nini tusilinusuru Shirika letu ili sisi tuwe na ndege inayobeba Bendera ya Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za vijijini, wanapewa makandarasi wasiokuwa na uwezo, hawazitengenezi barabara hizi kwa hali nzuri, hata mitaro ya maji hawayachimbi vizuri, barabara zinakuwa mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya *Old Moshi* kuanzia Kiboriloni mpaka Kidia ni mbaya, mbovu kabisa! Kwa nini barabara hizi wasipewe *TANROADS*?

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara hii kwa matayarisho mazuri ya Hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwe na mpango Kabambe wa kutumia nafasi ya nchi yetu Kijiografia ili kuliongezea Taifa letu kipato cha fedha za Kigeni, kuongeza ajira na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu kwa matumizi mazuri ya bandari zetu zote kwenye Bahari ya Hindi – kupokea na kusafirisha mizigo mingi zaidi iendayo na itokayo nchi za Maziwa Makuu.

Tutaweza kufanya hivyo kama tutawekeza zaidi katika bandari zetu na njia (Barabara na Reli) zetu toka Mashariki kwenda Magharibi. Tufanye hivyo kwa kutafuta fedha kwa njia *Sovereign Bonds* pamoja na kukaribisha Wajenzi/Wawekezaji kwa utaratibu wa Jenga – Endesha – Kabidhi (*BOT*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma upewe kipaumbele. Naishukuru Serikali kukubali kutenga fedha, kiasi cha Shilingi bilioni 10 kwenye Bajeti ya mwaka 2008/2009 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Ili kuharakisha ujenzi wa barabara yote mwaka ujao napendekeza Serikali ianzishe mchakato wa kuwapata Wakandarasi mapema (mwaka huu) tena wawe zaidi ya mmoja ili kuharakisha utekelezaji wa ujenzi kwa kipindi kifupi (miaka miwili).

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha usanifu wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege Tabora kwa kiwango cha lami chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Je, Serikali inatarajia kazi ya ujenzi wa Kiwanja hiki itaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nzega – Tabora – Mbeya ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Tabora na nchi nzima. Hivi sasa usanifu wa kipande cha Nzega – Tabora umekamilika chini ya ufadhili wa Denmark. Je, ujenzi wake utaanza lini? Kwa kuwa kipande hiki ni kifupi, takriban kilometra 115 tu, kwa nini Serikali isigharamie ujenzi wa kipande hiki kwa fedha zetu za ndani kama hatujapata wafadhili?

Mheshimiwa Naibu Spika, nini hatima ya ujenzi wa sehemu ya Tabora Sikunge – Mbeya? Aidha, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa Kiwango cha asilimia mia moja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya hotuba inayoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba sasa kutoa mchango wangu katika lugha ya maswali kwenye sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais akiwa kwenye harakati za kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2005, aliahidi kuwa barabara ya Uru (Rau) mlimani itajengwa kwa kiwango cha lami kabla ya mwaka 2010. Je, ni lini sasa barabara hiyo itajengwa? Kwani siku zinaisha! Wananchi wanaisubiri kwa hamu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mizani zilizo barabarani zina sababisha msongamano wa magari hususani nyakati za jioni, mfano mizani iliyoko Kibaha na ile ilio nja panda Himo: Je, *TANROADS* haiwezi kurekebisha hali hiyo kwa kuweka mizani kila upande wa barabara? Hapa nina maana, mizani mbili kwa *direction* zote za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ina nia nzuri ya kuboresha viwanja vya ndege hususani vile vya kimataifa: Je, Serikali haionti kuwa ni vyema pia vikaboresha baadhi ya vya Mikoa na vile vidogo vya mbuga za wanyama ambavyo vinatuingizia mapato kutoka kwa watalii?

Mhashimiwa Naibu Spika, hapa ninaomba nitoe mfano wa kiwanja cha Arusha/Dodoma na Iringa. Kwa kuwa *route* ya Arusha/Manyara/Dodoma/Ruaha iko *busy* sana na wale wenye ndege binafsi wanufaika kimya kimya. Je, Serikali haionti kuwa vikiboreshwa itakuwa kwa manufaa ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote zinazoendelea duniani zinaimarisha usafiri wa reli kwa kuwa reli ni rahisi kusafirisha mizigo na kwa kuwa reli inapunguza ajali barabarani na kwa kuwa nauli ya treni ni nafuu ukilinganisha na ile ya basi: Je, ni kwanini reli ya Dar es Salaam – Moshi – Arusha haitiliwi mkazo kufufuliwa? Je, Serikali haionti kuwa reli hiyo ya Kaskazini ilikuwa inatuunganisha na jirani zetu Kenya? Hivi ninajiuliza, vita ikitokea, madaraja yakavunjwa, silaha tutasafirisha vipi? Wizi wa mataruma sasa umeshamiri na zile nyumba za kusimamia vituo mfano Makanya, Hedaru na kwingineko zinabomolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu *TBA*. Nyumba za kisasa Dodoma ni kero kubwa kwa wapangaji wote, nami naomba kuorodhesha:-

- (1) Uzio – Nyumba hizo ziwekwe uzio;
- (2) Bati linaloua macho, tafadhali lipigwe rangi ya Kijani au nyekundu; na
- (3) Kodi iko juu sana kupita hizi yenye hadi *Area 'D' Sight 'E'*. Tafadhali hali hii irekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza urasimishaji wazalendo, eneo moja ambalo lingeweza kupunguza gharama za ujenzi, kuwaunganisha wananchi wetu na kujijengea uwezo makampuni yetu ya ndani hatua zifuatazo ni muhimu.

- a) Kujua kwa undani uwezo wa kila kampuni kitaaluma, vifaa, uongozi na ufani na kumua msaada wa mahitaji;
- b) Kuanza kupunguza orodha ya Makampuni ya nje ambayo hayafanyi vizuri katika ujenzi wa barabara; na
- c) Kutumia fedha ambazo zingetumika kwa *mobilization* – kuongeza uwezo wa makampuni yetu na kuongeza urefu wa ujenzi wa miundombinu,

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali (Wizara) ikaainisha miundombinu ambayo imehitaji kujengwa kwa njia ya *BOTI PPP* na kadhalika ili wawekezaji wasiendelee kusumbuka. Ni vyema Wizara ikaeleza ni barabara za urefu wa kilomita ngapi nchi yetu inahitaji, ngapi za Mkoa na Vijiji. Aidha, kuelewa vipaumbele katika ujenzi wa barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Wizara sikuona hata mahali pamoja panapozungumzia Bohari Kuu la Serikali. Je, halipo chini ya Wizara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, *SINOTA*: Katika hotuba pia sikuona takwimu zinazoonyesha mafanikio au hasara ya ubia wa Tanzania na China katika meli za mizigo. Ni vyema Mheshimiwa Waziri akaelezea ikiwa iko kwenye Wizara hii.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, yaliyofanywa na Serikali yetu sio haba kuhusu miundombinu japo kwa bajeti finyu. Naipongeza Serikali kwa tozo la mafuta lililoongeza mapato ya mfuko kwa ajili ya matumizi endelevu ya barabara. Najua watu walipiga kelele hasa wapinzani wa Serikali yetu. Lakini ukitaka kuendelea, lazima kuumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali imefanya kazi nzuri ya kukamilisha ujenzi wa barabara nyingi nchini, tunaomba basi Serikali iangalie uwezekano wa barabara ya lami toka Tunduma – Nyakanazi haraka iwezekanavyo ili kuiondolea Rukwa umasikini. Watu wa Rukwa wamevuta subira ya kutosha na Serikali yetu yenye huruma inafahamu hilo. Haipendezi kiwango kilichofikiwa cha viongozi kuzomewa kwa ajili ya barabara. Ni changamoto hii! Fedha ya *MCC* ipo, tunaomba utekelezaji wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoandikwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ya Julai, 2008 ukurasa wa 6(e) kuhusu Barabara: “Kuendelea

kuimarisha barabara nchini zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani kwa barabara ya lami". Kwa kigezo hicho, naomba barabara ya Kaengesa – Mwimbi – Mozi (Zambia) ijengwe kwa kiwango cha lami na barabara hiyo inatoka Mwimbi kwenda Mambwekenya. Kabla ya kufika Mambwe Kenya inapiga kona kuingia Zambia kupitia kijiji kinachoitwa Mnamba. Hivyo ni barabara ya Mwimbi – Mnamba. Naiarifu Serikali kuwa hali ya barabara hizi mbili inaitia aibu sana nchi yetu. Naomba sana ziwekwe lami kwa sifa ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sumbawanga imepiga hatua mpya ya kujenga viwanda. Mfano ni Kiwanda cha Nyama Safi na kiwacha cha kusaga Unga - *Energy Milling*. Kwa kutumia barabara hizo vingeweza kusafirisha unga Zambia. Hiyo ndiyo njia fupi kwa biashara (*shortcut*). Sio hayo tu Mpenda wanajenga Kiwanda cha Kukamua *bio-diesel*, wawekezaji wa *PROKON*. Barabara hizo mbili zikiwekwa lami ni mkombozi wa Rukwa. Sambamba na hayo, Ufipa na Rukwa kwa ujumla ni wakulima wakubwa wa nafaka na alizeti. Tunazihitaji barabara hizo kwa kiwango cha lami kwa maendeleo ya Rukwa na nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na viwanda na kilimo, Rukwa ina madini, mazao ya misitu na mbuga za wanyama. Tunahitaji wawekezaji na bila barabara za lami, yote ni bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja cha ndege cha Kigoma ni muhimu sana kwa wananchi waishio maeneo yale. Lakini katika karne ya leo, naomba sana Serikali iweke mashine za kisasa za kupakulia kama ilivyo katika viwanja vyta Dar es Salaam, Arusha na Mwanza. Nakumbushia kwamba kule ni mpakani na pia mtu ni afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudhi za Serikali kuhusu reli ya kati hazijafanikiwa. Reli yetu iliyokuwa fahari ya Tanzania sasa imekuwa aibu ya Tanzania. Hata kama kuna makosa katika kuingia mkataba inafaa mkataba huo ufutwe, kwa sababu:-

- (1) Kukodi *engine* yake *Rites* moja kwa siku Sh. 600,000/= ni ghali sana kwetu. *Engine* zenye we glass 89 badala ya class 73, 86, 87 na 88. Tunajiuliza kama yeze anatukodishia *engine* zake: Je, *engine* zetu 25 anatulipa nini? Wakati *engine* za *Rites* hulipiwa hata kama haitembe;
- (2) *Rites* ambaye aliingia mkataba yuko India, hivyo *TRL* ndiyo wapo hapa kutenda kazi tena kwa ubabaishaji tu;
- (3) Reli haijaongeza wafanyakazi, badala yake imepunguza ajira kutoka 1,800 mpaka 6,000.
- (4) *Board* ni wahindi 20;
- (5) Pesa zinazopatikana hupelekwa Benki ya Baroda, kwa sababu hiyo wafanyakazi wakilipwa mfano Sh. 1,000/= inabidi Sh. 25/= ikatwe na Benki zetu za *CRDB* na *NMB*;

- (6) Kitengo cha *catering* kimevunjwa na baadaye kupewa mtu binafsi aitwaye *Trust Service Groups* ambaye kulipa mishahara ni kazi. Wafanyakazi wengine hawajalipwa zaidi ya miezi mitatu. Hawana likizo, wakihamishwa hawalipwi na mishahara yao ni Sh. 60,000/= kwa mwezi. Hawana *PPR* wala *NSSF*. Behewa hilo la *Catering* halifiki Mpanda na Kigoma, huenda Mwanza tu. Wengine tule mihogo tu njani.
- (7) Mabehewa hayatoshi, yaani hajaonyesha kuwa anatusaidia. Watu hubanana mno hatu vifo hutoke. Nilishuhudia mtu akianguka na kufa hapo tarehe 1 Mei, 2008 baada ya mtu huyo kupanda kwenye *engine* ya treni iliyokuwa inakwenda Kigoma na ndugu zake walilazimika kubaki Ngenge 60 kwa ajili ya ndugu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Magenge zimeachwa tu kuharibiwa, naishauri Serikali nyumba hizo wapewe wananchi wazitumie ili zilindwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi treni inasimama hovyo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashindwa kufahamu, huyu mwekezaji *Rites* ni kwa manufaa ya nchi hii? Kwani hivi sasa wako hoi wanangojea mkopo wa dola milioni 14 kuongeza huduma. Sio hilo tu, Serikali ilijikuta ikienda kulipa mishahara ya wafanyakazi wa Reli na kwa fedha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika tufike mahali tuiokoe nchi yetu ambayo inaitegemea reli ya kati kwa kusafirisha mazao yao na mizigo mbalimbali hususan Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Mwanza, Tabora na hata nchi jirani za Zambia, *DRC* na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED ABDUL AZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mitatu iliyopita Serikali ilitoa ahadi kuwa inafanya utafiti wa kujua chanzo cha Bandari ya Lindi kujaa mchanga.

Katika eneo la maegesho ya meli, ningependa kujua kama utafiti huo umeshafanyika. Kama bado, kwa nini? Kazi hiyo itafanyika lini? Kama tayari, nini matokeo ya ufatifi huo? Ukosefu wa Bandari ya Lindi unaongoza gharama za maisha. Aidha, *TPA* imelipa fedha kwa eneo kubwa la jirani na bandari hiyo. Je, *TPA* ina mpango gani na eneo lililolipwa fidia?

Uwanja wa Ndege wa Kikwetu ulijengwa mwaka 1939, ni miongoni mwa viwanja vyatamani ni uwanja ambaa una njia nne za kurukia tofauti na viwanja vingi hapo nchini. Aidha, hivi sasa uwanja huo unatumika sana na Mheshimiwa Rais na *First Lady* ambaye amekuwa na safari nyingi za Lindi. Naomba kuelewa mpango wa Wizara kuhusu uboreshaji wa uwanja huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria ya ununuzi, mwenye bei ya chini ndio huwa mshindi wa Tenda. Kwa upande wa Manunuzi inawezekana ikawa sahihi lakini kwa upande wa ujenzi lipo tatizo. Mkandarasi akipewa kazi ya ujenzi kwa vile tu *bid* yake ni chini, tunaweza kujikuta tunatoa kazi kwa kufuata bei, lakini utekelezaji ukawa dhaifu jambo ambalo ni hasara.

Napendekeza sheria hiyo ibadilishwe ili wananchi wa ujenzi wapewe uwezo wa kuteuliwa Mkandarasi kwa kuangalia uwezo wa Mkandarasi kuhusu ujuzi, uzoefu, vifaa na uwezo wa kufanya kazi husika. Kuendelea kutoa kazi kwa kigezo cha *Lowest Bid* ni kujiletea hasara katika miradi yetu.

Bandari Bandari ya Tanga ni muhimu sana. Ni bandari hiyo itakayosaidiana na Bandari ya Dar es Salaam ambayo inaonekana kuzidiwa na hasa vile *TPA* haikupewa uwezo wa kufanya *heavy investment*. Ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro, haukuwa na faida kwa nchi yetu kama hatutakuwa na Bandari ya Tanga badala yake itanufaisha zaidi *Mombasa Port* kuliko nchi yetu. Naomba Serikali ifanye haraka ili agenda ya *Tanga Port* ikamilishwe kwa haraka.

Barabara ya Tanga – Horohoro inatazamiwa kujengwa na fedha za *MCC* lakini hadi sasa haijulikani itaanza lini. Hadi leo – *Resettlement Action Plan. (RAP)* bado haijakubalika na wafadhili. Kwa hiyo, inawezekana mwaka mmoja au miwili ikapita kabla kazi haijaanza na baya zaidi ni kwamba Wizara. Haikutenga fedha zozote kwa ajili ya *sport improvement* na *periodic maintenance*. Barabara hii ni muhimu sana kwa vile ndio inatuunganisha na nchi ya Kenya. Kwa kukosa fedha za matengenezo hayo. Mwaka huu barabara hiyo itaharibika kiasi cha kushindwa kupitika kama ilivyotokea mwezi uliopita. Naomba Wizara itafute fedha kwa ajili ya barabara hii.

Naipongeza Bodi ya Wakandarasi chini ya uongozi wa *Eng. Mohegi* kwa kazi nzuri wanayoifanya. Semina za mafunzo wanazozienthesa zimekuwa na faida kubwa kwa Wakandarasi wadogo na pia ufuutiliaji wa kazi zao ni nzuri bila malalamiko ya rushwa. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DANIEL NICODEM NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo yafuatayo ni vyema yafanyiwe kazi kwa haraka na dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Kigoma – Kidahwe, Kidahwe – Uvinza na Uvinza – Ilunde, pamoja na kuanza ujenzi, *package* ya kwanza Kigoma/Kidahwe kilometra 35.7 ni vizuri *package* ya pili nay a tatu zifuate haraka au kwa kukopa au kufanya *commitment* ya fedha zetu za ndani. Kujenga kidogo kidogo ni hasara *in terms of time and economies of scales*. Tafadhali naomba *system* hii ibadilishwe. Baadaye *packages* hizo zitakuwa ghali *source* kifedha na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu sisi wana – Kigoma – *this is a historic Budget*. Ujenzi wa Barabara za Mwandiga – Manyovu, Kigoma Kidahwe; Daraja la Malagarasi na kilometra 48 za Bonde la Malagarasi. Usimamizi ni Kitu cha muhimu sana. Kujenga ni jambo moja, lakini usimamizi wa kimanejimenti ni jambo *basic*. Hii itatusaidia kuepuka *bad experiences* kwa baadhi ya barabara ambazo zimekuwa na matatizo mengi, i.e. Singida - Manyoni na hata Ubungo - Mwenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, *transfer of technology*. Je, Wizara yako ina mpango mahususi wa vijana wetu wahandisi kujifunza au hata kufanya ukachero wa kitaaluma ili baadaye miradi hii mikubwa ya ujenzi wa barabara na madaraja ije ifanywe na Wahandisi Wazalendo. *This is what Chinese did, this is what Jananes did after 2nd World War.*

Endapo sera hii ipo, vijana wangapi Wahandisi wetu wamenufaika na kufanya kazi na Makapuni hayo makubwa ya nje? Endapo sera hiyo hakuna, tunasubiri nini kuanzisha? Mfano ujenzi wa daraja la Mkapa kule Rufiji ni *Local engineers* Wangapi walikuwa *attached* kwenye mradi?

Mheshimiwa Naibu Spika, uchafu katika vituo vya Reli/treni umekithiri. Je, kufanya usafi katika maeneo ya vituo hivyo, tunahitaji fedha za kigeni? *TRL* na Wizara kaeni (jana) ili tatizo hilo liondolewe haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa abiria, msongamano ndani ya treni, haya ni mambo ya uendeshaji. Serikali isishangae tu, ichukue hatua sasa. Adha za majeruhi na vifo, sasa basi! Watumiaji wa reli tumechoka na sasa hakuna lugha nyingine ya kulisemea jambo hili la aibu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtandao wa barabara za Mkoa wa Kigoma ni mdogo ukilinganisha na Mikoa mingine. Tumeleta maombi ya kuongeza mtandao huo, sasa ni miaka mitatu, *what is happening?* Tusubiri hadi lini kupata majibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kidahwe – Kanyani/Kasulu – Kibondo – Nyakanazi ndio inayounganisha Wilaya za Mkoa wa Kigoma. Nimepata taarifa kwamba *design* yake imekamilika. Kama taarifa hizi ni za kweli, basi tuipe kipaumbele, ni barabara ya ulinzi, ni uchumi na ndiyo itakayotuunganisha na ile ya Kagoma – Lusahunga kutokea Mleba – Mtukura, fedha ziko wapi? Fedha ziko *EADB, EU, WB* na hata wale marafiki wa Mheshimiwa Rais wetu. Tusiope kukopa. Deni hili baada ya miaka 20 gharama yake itakuwa imelipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa *TANROADS* Kigoma ni mzuri sana ni Wahandisi vijana, wenye ari na hakika mwaka 2007, pamoja na mvua nyingi, barabara zetu nyingi zilipika vizuri. *Engineer Senkuku* na timu yake msiwahamishe kwa sasa acha vijana hawa wafanye kazi. Waongezeni vitendea kazi na sisi Wabunge tutawapa kila aina ya *support*.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri alivyowasilisha hotuba wa Wizara yake kwa umahiri

mkubwa (*setting new standards*). Pongezi vile vile ziende kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wake na watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kuchangia hoja kwa matatizo ya Mkoa wa Kagera yanayohusu Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege Bukoba, nashukuru kuwa Wizara imeliona hili na kulichukulia hatua. Ilikuwa aibu kwa Mkoa wa Kagera wakati Mheshimiwa Rais alilazimika kutumia uwanja wa Wilaya ya Geita alipofanya ziara ya Mkoa wa Kagera kwa kuwa uwanja wa Mkoa (Bukoba) ulikuwa sio salama.

Nafikiri Mheshimiwa Waziri ana taarifa kuwa hata *Presicion Air* wamesitisha huduma yao ya ndege ya Mwanza – Bukoba kwa sababu hiyo ya usalama wa kiwanja na viwango ambavyo wanatakiwa kuvifiki.

Mheshimia Naibu Spika, kuhusu suala la usafiri wa majini (watu na Mizigo), Mkoa wa Kagera ulikuwa unahudumiwa na Meli za Victoria, *MV Bukoba* na *MV Serengeti*. Baada ya Meli ya *MV Bukoba* kuzama, huduma kwa abiria, ikabaki meli ya *MV Victoria* peke yake. Hata hivyo, meli ya Victoria inasuasua kwa matengenezo ya mara kwa mara.

Hivyo, Mheshimiwa Waziri, usafiri kuunganisha Mkoa wa Kagera ni wa mashaka. Mizigo iliyosafirishwa kwa treni kwa njia ya Makontena inachukua muda mrefu wa kuweza kuisafirisha toka Mwanza kuja *Kemondo Bay*, Bukoba. Hili husababisha upungufu wa mara kwa mara wa bidhaa zinazosafirishwa toka Dar es Salaam kwa njia ya treni mpaka Mwanza na kusababisha ongezeko la bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kuna barabara zinazolenga kuunganisha Mkoa wa Kagera na Mikoa mingine. Kama Mwanza na Shinyanga ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji, tunasikitika kuwa mkandarasi aliyepewa kipande cha barabara ya Kagoma – Rusaunga amefukuzwa kwa vile kashindwa kutekeleza wajibu wake.

Ushauri ni kuwa, Mkandarasi mwingine apatikane haraka iwezekanavyo na ikibidi igawanywe mara mbili na kupewa wakandarasi wenye uwezo wawili ili barabara hiyo ikamilike kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Kemondo Bay* ni bandari ilijoengwa kwa ajili ya kuhudumia mizigo ya Kagera, lakini vile vile nchi za jirani za Uganda, Rwanda, na Burundi. Nashauri bandari hii ipewe kipaumbele katika mkakati mzima wa kujiimarisha kibiashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupandishwa hadhi barabara Kafunjo – Rubale – Izimbya – Kabwashu na kuunganisha Wilaya ya Misenyi. Barabara hii tumeizungumza kwa muda mrefu katika vikao vya Hal mashauri na *RCC*. Hii barabara ambayo iko Jimboni kwangu inaunganisha zaidi ya Kata 13 ambazo ndio chimbuko kubwa la chakula kinacholisha Bukoba Mjini na mazao ya kibiashara. Inatumika sana kwa magari ya abiria

na mizigo na imekuwa mzigzo mkuwa kwa Halmashauri ya Bukoba Vijijini ambayo inashindwa kuihudumia. Ni matarajio yangu kuwa wakati taratibu za kukamilisha sheria ya barabara tulioipitisha hapa Bungeni, barabara nilioitaja hapo juu nayo itaunganishwa katika barabara zitakazopandishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumponeza Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Dk. Shukuru J. Kawambwa, Naibu Waziri - Mheshimiwa Hezekia Chibulunje, Katibu Mkuu - Eng. Omar Abdallah Chambo, Naibu Katibu Mkuu – Bi. Joyce K.G. Mapunjo, pamoja na watendaji wao wote ambao kwa namna moja au nyingine wamewezesha utayarishaji wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie masuala ya ujenzi wa nyumba za viongozi na za wananchi. Katika hotoba yake Mheshimiwa Waziri amezungumzia maneneo mengi ya Mikoa mbalimbali ambayo Wizara yake kupitia Idara yake ya Majengo inajenga nyumba mbalimbali. Leo nazungumzia nyunga zilizojengwa hapa Dodoma katika maeneo ya Kisasa ambazo zimejengwa na vikosi vyetu *JKT* vikisimamiwa na Idara ya Majengo ya hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ukiziangalia nyumba zile, kwa nje utaziona ni nzuri sana, lakini nyumba zimejengwa kwa kiwango cha chini mno. Miundombinu yake hasa ya maji kuanzia vifaa vyake ni vya hali ya chini sana kiubora, kwani mara kwa mara vinapasuka au kukatika kabisa jambo ambalo linawasababishia, hasa kubwa sana wakazi wa nyumba zile nikiwemo mimi mwenyewe.

Mheshimiwea Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ikiwezekana aunde TUME japo ya watu wachache waende kutembelea majengo yale ya kisasa. Yapo katika hali mbaya japokuwa ni mapya. Madirisha yake yanadondoka ovyo, rangi za ukutani za nje zinabanduka ovyo, vifaa vingine havikukamilika kuwekwa na mpangaji analazimika kuweka mwenyewe na bila ya kulipwa gharama zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ipo haja kubwa Mheshimiwa Waziri kuunda Tume na kupata maoni ya wapangaji wenye na atabaini ni nini kilitendeka katika majengo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nazungumzia barabara, wachangiaji wenzangu wengi wameshachangia kuhusu umuhimu wa barabara na sote tunaelewa hivyo. Hivyo mimi ningombia Serikali ielekeze nguvu zake fulani zijengwe zimalizike na mwaka mwingine zielekezwe nguvu kwengine na hatimaye tuzimalize kulikoni kuzigawa fedha kidogo kidogo kwa kutaka kugusa kila barabara na hatimaye zote hazimaliziki na wananchi wanabaki na matatizo yao pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DK. HARRISON MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Dk. Shukuru Kawambwa kwa ufasaha mkubwa.

Ukurasa wa 46 wa hotuba ya Waziri unatamka kwamba *TPA* ilifanikiwa katika mwaka 2007/2008 kukamililisha ukarabati wa barabara ya Kajunjumele hadi Bandari ndogo ya Kiwira. Hii ni sahihi kabisa, lakini kutokana na mvua kubwa zilizonyesha Nyanda za juu Kusini kati ya mwezi Machi na Aprili, 2008 barabara hiyo haipo tena. Kwa maneno mengine haiwezi kabisa kuitisha magari ya aina yoyote kutokana na uharibifu mkubwa uliotokea kwenye barabara hiyo.

Kutokana na umuhimu wa kipande hicho cha barabara chenye urefu wa kilometra  $6\frac{1}{2}$  hivi, Serikali haina budi kuikarabati barabara hiyo haraka iwezekanavyo. Kuanzia mwezi wa nane kila mwaka, Bandari ya Itungi haitumiki kutokana na wingi wa mchanga unaosukumwa na mawimbi makubwa ya msimu. Hivyo, bandari ndogo ya Kiwira hutumika hadi mvua zinapoanza mwezi Desemba na milima ya mchanga Bandari ya Itungi kusambazwa na mawimbi makubwa.

Hivyo basi, kipande hicho cha barabara hakuna budi kukanabatiwa mapema iwezekanavyo ama sivyo tutangaze mapema kufungwa kwa Bandari za Itungi na Kiwira hadi mwakani. Ushauri wangu wa ziada ni kuwa ukarabati wowote utakofanywa kwenye barabara hiyo uwe wa kuweka lami kutokana na wingi wa mvua maeneo hayo.

Pili, ukurasa wa 49, Waziri anaongelea bandari kama za Isaka na Mbeya ilikupunguza msongomano wa mizigo bandari ya Dar es Salaam. Naishauri Serikali kuanzisha bandari kavu mbili Mikoani Mbeya, moja iwe Tunduma kuhudumia mizigo iendayo Zambia na ya pili iwe Kasumulu, Kyela kuhudumia mizigo iendayo Malawi. Uamuzi huo utawavutia wafanyabiashara wote wa Malawi kuachana na Bandari ya Beira wanayoitumia sana kutokana na huduma zisizoridhisha Bandari ya Dar es Salaam. Tatu na Mwisho, Serikali imetenga shilingi milioni 200 kwa ujenzi wa Daraja la Lusungo ukurasa 148 kati ya shilingi milioni 350 zinazohitajika.

Ombi langu kwa Serikali, fedha hiyo yote yaani shilingi milioni 350 na shilingi milioni 50 zilikwishatengwa kwa upembuzi yakinifu, ipelekwe Jeshini wanunulie daraja jipya la vyuma ili lile lililopo Lusungo, lililojengwa na Jeshi mapema mwaka huu, liachwe hapo hapo. Naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika bajeti ya Miundombinu. Kwanza, napenda kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa hotuba yao ya Bajeti ya Miundombinu kwani ni wajibu wao kutoa mpango wa kazi zao. Kwa umuhimu wa Wizara hii nami pia napenda kuchangia kuhusu mawasiliano ya barabara. Napenda kuongelea barabara ya Sasa – Saba – Kayenze. Katika halmashauri ya Jiji la Mwanza, upande wa Wilaya ya Ilemela, barabara iendayo

kayenze kupitia Uwanja wa Ndege, ilisemekana itapitia Sabasaba. Kwani huko mbele inapita katika Kambi ya Jeshi na sasa itahamia Sabasaba. Naomba kuuliza ni lini itaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami? Kwani barabara hiyo itapunguza matatizo wakati wa masika kwa kukatika kwa barabara hiyo na madaraja kwa pamoja.

Pili napenda kujua, katika safari za Mahujaji mwaka jana *ATC* ilichukua tenda ya kusafirisha Mahujaji na usafirishaji huo ulikwama na kusumbua sana Mahujaji pia kuitia Serikali hasara kubwa, sasa basi kwa kuwa shirika hilo liko katika Wizara hiyo ya Miundombinu, ni lazima tatizo hili liliwagusa na kuweza kuisaidia Serikali kwa karibu sana.

Napenda kujua katika tatizo hilo Serikali ilitumia kiasi gani katika kuhudumia Mahujaji hao? Pia nilisikia tetesi kuwa Mahujaji hao watafidiwa gharama fulani, kwani baadhi yao hawakumaliza suna zao kwa kucheleweshwa kusafirishwa na Shirika la Ndege la Tanzania (*ATC*). Pia, kama siyo hivyo, Wizara ilichukua hatua gani kwa Bodi ya *ATC* kwa tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchangia kuhusu suala la barabara za Wilaya ya Ilemela ambazo zinashughulikiwa na *TANROAD* kwani Wilaya hiyo ni mpya na barabara zake karibu zote ni za vumbi, hivyo tunaiomba Wizara kuptia kwa wakala wake kuziangalia barabara hizo kwa jicho la huruma

Uwanja wa Ndege wa Mwanza katika uwanja huu ni tatizo, kwani kwanza *VIP* yake haina hadhi. Pili, *VIP* hiyo hakuna mitambo wa ukaguzi na wahudumu wa uwanja hufungulisha mikoba ya mkono kwa ukaguzi. Mbona Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam hatufungulishwi mikoba? Huwa tunakaguliwa na mitambo ya ukaguzi. Tunaomba iwe hivyo kama Dar es Salaam.

Pili, upanuzi wa uwanja huo pia tunaomba majengo yapanuliwe na yawe ya kisasa. Uchukuzi wa kutupa masanduku ya watu sio ya kufumbiwa macho, nasi tunaomba utaratibu wa mkanda wa mizigo ili kuweka usalama katika masanduku na mizigo ya watu. Masanduku hurundikwa na watu kusukumana na mwenye nguvu ndiyo ataanza kutoa mizigo yake na kukandamizwa mizigo ya wasiokuwa na nguvu. Tunaomba upanuzi wa uwanja uendane na ujenzi wa Majengo ya Kisasa na vifaa vyta kisasa pia. Hapo tutaimarisha uwanja huo wa ndege na kuwa na mandhari ya kisasa na tulivu. Ahsante.

**MHE. CLEMENCE BEATUS LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia hoja hii. Naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri - Mheshimiwa H. Chibulunje na wataalam katika Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri sana. Uzuri wa hotuba hii ni kuwa mtiririko wake wa maelezo umepangwa vizuri sana kwa kuainisha ahadi za Ilani ya Uchaguzi ya CCM – 2005 na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miundombinu, napenda Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako, Serikali imehamasika kwa kiasi gani Mwekezaji - *TRL* kufufua

matumizi ya reli ya kati ya Kilosa na Kidatu, vilivyopo viwanda viwili vikubwa vya sukari ya Kilombero ili kupunguza gharama kubwa ya kusafirisha sukari nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa zaidi ya tani 100,000 za sukari inayozalishwa Kilombero husafirishwa kwa magari kwa gharama inayofikia asilimia 20 zaidi ya gharama ya kusafirisha sukari hiyo kwa njia ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuzingatia ratiba ya mipango ya ujenzi wa barabara ya lami kutoka Mikumi hadi Kilosa na hadi Mziha/Korogwe. Pamoja na kuzingatia ratiba, napenda kumkumbusha, Mheshimiwa Waziri awahimize, kuititia wataalam washauri (*consultants*), wasisahau kuyajumuisha jumla ya madaraja manne kwene *feeder roads* katika Kata za Ulaya na Zombo katika mradi huu kama ilivyofikiwa awali na Wizara ya Miundombinu, kuititia Mawaziri waliotangulia. Kugharamiwa madaraja tajwa katika mradi huu, ulizingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, kutaongeza *financial na economic viability* ya ujenzi wa barabara hii, kwa kuwa mashamba makumbwa yanayozalisha mazao ya biashara na chakula kwa wingi yako ng'ambo ya madaraja hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umadhubuti au uimara wa kudumu wa madaraja yanayotakiwa kujengwa hautaweza kugharamiwa kwa fedha chache za Halmashauri kutokana na mafuriko makubwa ambayo hutokea kila mwaka, yanayosababishwa na mto Miyombo, amba ni korofi, hautabiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napenda Mheshimiwa Waziri anijulisse kama madaraja niliyoyaeleza, yamo katika *detailed designs* zinazoendelea hivi sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata ufanuzi ufuatao kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa barabara inayotoka Mikumi hadi Kilosa hivi sasa ina daraja moja kubwa linalovuka mto Mkondo, amba ni mji Kilosa. Daraja hili pekee, kwa sasa linatumika na watu waendao kwa mguu, waendesha baiskeli, pikipiki, magari, treni na mifugo. Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza kuliarifu Bunge lako iwapo daraja jipya litajengwa sehemu nyingine itakayotenganisha watumiaji niliowataja hapa juu? Naomba wananchi washirikishwe kushauri sehemu inayofaa kujengwa daraja hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwisho ni ushauri kwa Serikali. Kwa kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara hustawi sana katika maeneo maalumu yenye rutuba nzuri. Naishauri Serikali iyabaini maeneo haya na kuyapanga matengenezo ya barabara, zinazouganisha maeneo hayo na barabara za Mikoa zihudumiwe na *TANROAD* ili kuhakikisha ubora wa barabara na kuwezesha kuyasafirisha mazao hayo kwene maeneo yenye uhaba au masoko ya bidhaa hizo. Kwa njia hii, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja, nikiamini ufanuzi niliouomba nitaelezwa wakati wa kuitisha Bajeti leo jioni.

**MHE. LUHAGA JOELSON MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itaipandisha barabara ya kutoka Bariadi – Gambasingu – Kisesa – Mwandoya – Nghaboko JC kuwa ya Mkoa (*TANROAD*)?

Ni lini ujenzi wa barabara ya Mwingumbi – Maswa – Bariadi- Lamadi itaanza kujengwa? Kwani fedha zilizotengwa katika bajeti 2008/2009 shilingi milioni 80 ni mzaha kwa wananchi waliongoja kwa muda mrefu?

Katika bajeti ya mwaka 2007/2008, Serikali ilitenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa barabara ya Kalandotto – Lalago – *Mwanhuzi road* (121 km) & Lalago – Maswa (34 km) katika bajeti 2008/2009 hakuna fedha iliyotengwa. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliwaahidi wana Meatu na wanachi wa Shinyanga kuwa barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami, ni lini ujenzi utaanza?

Sambamba na upandishaji wa barabara ya Bariadi – Gambasingu – Kisesa – Mwandsosy – Nghoboko JC kuwa ya Mkoa. Ujenzi wa daraja la mto Simayu utakamilika Oktoba, 2008. Je, ujenzi wa daraja la mto Lubiga utaanza lini ili kuruhusu mawasiliano ya Jimbo la Kisesa na Makao Makuu ya Wilaya pamoja na sehemu nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini fedha za ujenzi wa daraja la mto Sibiti litatengwa? Kwani wananchi wamechoshwa na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, natoa pongezi kwa Wizara ya Miundombinu kwa kuweza kuifikisha barabara ya Kibiti – Lindi hapo ulipofikia.

Vile vile, kwa kuweza kupata migao ya fedha kwa matengenezo ya barabara zetu za Mikoa na Wilaya: Nimeona katika hotuba ya Wizara kuhusiana na Kipande cha barabara ya Kibiti – Lindi chenyé kilometra 60 (Ndundu – Somanga) kwa kiwango cha lami na Nyamwage – Malendego kwa matengenezo maalum. Eneo hili lote limeelezwa kwamba litaaanza kazi kipindi cha mwaka 2008/2009. Je, ni lini matengenezo maalum yataanza kufanyika na ni lini, hasa, mwezi, tarehe ambayo eneo hili tajwa la kilometra 60 litaaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Liwale hutumia gharama kubwa na mzunguko mkubwa ili fika Liwale. Huanza safari Dar es Salaam – Lindi – Nachingwea hadi Liwale, wakati ipo njia ya mkato yenye kilometra chache toka Nangurukuru hadi Liwale. Ni lini Wizara itafikiria barabara hii, ukizingatia kwamba barabara hii inaunganisha Wilaya ya Kilwa na Wilaya ya Liwale?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la Nangurukuru na Liwale lina vitega uchumi vingi, ikiwemo *Selous* na watalii, lakini haipitiki kwa kipindi chote cha mwaka. Naomba barabara hii ifikiriwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Dk. Shukuru Jumanne Kawambwa kwa hotuba nzuri iliyoendana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Pia nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje kwa utendaji mzuri bega kwa bega na Mheshimiwa Waziri.

Naanza kuzungumzia upande wa Viwanja vya Ndege, ni ukarabati wa *JNIA*, uwanja huu uliendelea na ukarabati ni pamoja na matengenezo ya maegesho ya ndege, upanuzi wa barabara pili ya kuruka na kutua ndege, mfumo wa umeme, pamoja uboreshaji wa mazingira kama hotuba iliyojieleza.

Kwa upande wa Abiria wanaoondoka na upande wa abiria wanaowasili kwa kweli hali sio nzuri. Nafasi imekuwa haitoshi, kuna mlundikano wa abiria kwa pande zote mbili ukizingatia ni *International Airport*, wageni wetu toka nje ya nchi na hapa nchini wamelalamikia sana hali hii. Serikali ijaribu kuliona hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni pande wa maegesho ya magari (*car park*), kuna mlundikano mkubwa wa magari, kwani *car park* haitoshi, pamekuwa padogo sana kwani baadhi ya wasafiri na wanaopokea wageni wote wanaegesha magari yao hapo *Terminal two*.

Mwisho, naomba kuingia upande wa wale mavu. Wale mavu wanahitaji msaada kwenye kuvuka barabara, nao ni wenye ulemavu wa miguu, viziri na wasioona. Pia wenye ulemavu wa viungo, miguu wanahitaji wapatiwe msaada kwenye kupanda ghorofa, ni tatizo kubwa kwao. Serikali ilione hilo, kwani ni tatizo kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu na pia naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALIM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kivuli - Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa mchango wake, naamini kwa usiku vuwa Mheshimiwa Waziri ataifanya kazi. Vile vile nawashukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wake wote wa Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu nyumba za kisasa. Nyumba za kisasa kwa kweli vifaa vyake kama vya umeme na mabomba havina viwango na kila siku vinaharibika, ni hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri kwa nyumba za Kisasa waheshimiwa Wabunge tujengewe geti kwa sababu nyumba za Waheshimiwa Mahakimu, nyumba zao zote wamejengwa mageti, nasi sisi hatukai, kwa hivyo tutaepukana na wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu *ATCL*, kwa kweli naiomba Serikali ipange mkakati madhubuti kuhusu *ATCL* kwani sijui kwa nini Shirika hili bado halijaboreka kila wakati ndege zake zinakuwa *cancelled*. Hii ni aibu kwa Taifa letu, kwani iweje ndege za binafsi ziweze sisi tusiweze? Naiomba Serikali isimamie *ATCL* ili isiweze kuitia Serikali kwenye hasara kama ilivyofanya mwaka jana wakati wa Hijja, kwa kuwakosesha Mahujaji ibada muhimu kutokana na uzembe wa *ATCL* pia kuitia aibu nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wanaiomba Serikali ipange mpango madhubuti wa kuruhusu Bandari ya Mtwara kuweza kugunga gati meli za kutoka nje za mizigo ili kupunguza msongamano wa mizigo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Miundombinu inapoingia mikataba waweke maslahi ya Watanzania mwanzo. Mkataba wa *TRL* unasikitisha sana, kwani Serikali imeingia mikataba na mwekezaji hana hata senti moja, ametumia Shirika letu kujipatia mikopo. Sasa Mheshimiwa, kwa nini asipewe Mtanzania akawenza kuliendesha Shirika hilo? Leo Watanzania wanapata taabu sana kuhusu mwekezaji huyu ambaye hana huruma na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *airport*, kwa kweli inasikitisha, msongamano ni mkubwa. Naiomba Serikali ipange mpango mahsuswa kuiongoza *airport* ili iweze kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kuleta bajeti ambayo ni nzuri na inakidhi matakwa ya Watanzania, lakini pia ni bajeti ambayo inatekeleza Ilani ya Chama cha CCM ya mwaka 2005 ambayo inazungumzia sekta ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iendelee kuzingatia mikataba mbalimbali ya kimataifa inayosimamia usafiri wa majini (*International Maritime Organization*). Kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wamiliki wa vyombo vyao majini kutumia vyombo vyao ambavyo huwa havikidhi vigezo kwa kusafirisha watu kupitia majini na kusababisha usumbufu kwa abiria hao.

Mfano, kuna baadhi ya maboti yanayosafirisha watu kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar, baadhi ya vyombo hivyo huwa zinakata moto na baaadhi ha vyombo huwa havina hata viroza hewa na kusababisha usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kusimamia usalama wa kusafiri majini pamoja na ukaguzi wa vyombo vyao majini ili kuweza kuvisimamisha vyombo ambavyo havina ubora wa viwango na kuwasumbua abiria hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sheria na kanuni zitumike kuwabana wamiliki wa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. ZULEKHA Y. HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa katika Wizara hii, nampongeza kwa hotuba yake nzuri, yeye pamoja na wasaidizi wake wote.

Pamoja na yote yaliyoelezwa, mikakati, mipango, lakini bado nasisitiza suala la watu wenye ulemavu hasa kwa upande wa viwanja vya ndege na bandarini, ni vigumu kwa watu wenye ulemavu. Tunapata matatizo sana na hakuna njia nyingine na sisi tunatumia kwa matatizo.

Pia kwa upande wa majengo tunashindwa kutumia kama vile Benki na ofisi mbalimbali. Mabasi yanatarajiwa kuletwa tunaomba japo moja liletwe ili na sisi watu wenye ulemavu tuweze kulitumia. Hata barabara zinazojengwa ziwekwe sehemu za waenda kwa miguu pamoja na walemvu waweze kuzitumia bila matatizo. Hivyo, naomba lifikiriwe na lipewe kipaumbele kwa utekelezaji. Nawataakia kila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana bajeti ya Kambi ya Upinzani kama ilivyowasilishwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto. Natambua vile vile juhudzi za Serikali katika kujenga barabara, lakini kwa kazi hii haiwezekani kufikia malengo. Kwa umuhimu wa suala hili, lazima pawepo na mjadala wa pamoja hapa Bungeni ili hatimaye tuwe na azimio litakaloifanya Serikali kulifanyia kazi azimio hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Sekta ya kilimo ipate maendeleo, barabara ni muhimu ili kwanza kuweza kuwafikishia wakulima na wafugaji pembejeo zote. Ni muhimu pia pawe na barabara zinazopitika ili wakulima na wafugaji waweze kusafirisha mazao yao ya kilimo na mifugo. Hali ilivyo sasa, ni ngumu sana kiasi kwamba wakulima na wafugaji waishio pembezoni mwa nchi yetu wanalahazimika kuuza mazao yao nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri wa nchi Kavu (barabara): Watanzania walio wengi ni wale wa Kipato cha chini. Usafiri wao huwa ni wa treni au mabasi. Reli sasa, hasa reli ya kati imekuwa ni Jehanama. Ni mateso, ni aibu kwa Tanzania, baada ya miaka 45 ya uhuru tumerudi nyuma kwa mwaka 45. Serikali, tena kwa haraka lazima iwe na reli inayolingana na hadhi ya nchi yetu, reli safi, salama ya uhakika ambayo kila mtu atapenda kuitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sekta binafsi kujitahidi kuwa na vyombo bora vya usafiri kuliko reli bado kuna matatizo ya usalama wa abiria na mali zao. Tatizo kubwa ni kuwa inapotokea ajali hakuna vyombo vya kuokolea maisha. La kusikitisha

zaidi ni kuwa hata pale vyombo vyaya dola kama Polisi vinapopewa taarifa havichukuwi hatua yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa anga ni muhimu kwa Watanzania wenye vipato nya kati na juu. Wawekezaji wapo japo hawatoshelezi, lakini tatizo kubwa ni viwanja vyetu nya ndege, ambayo havina hadhi, havina ubora, vingine havifanyi kazi wakati wa mvua kwa sababu havina lami. Usafiri wa anga unaongezeka kwa sababu wasafiri wa ndani na nje wameongezeka sana. Serikali basi ivikarabati viwanja vyote nya ndege.

**MHE. HERBERT JAMES MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nahofia kukosa nafasi ya kuchangia kwa mdomo, basi nitangulize mchango wa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Muheza – Amani – Kwamkoro ni ya Mkoa. Kuanzia Novemba, 2007 barabara hii imeharibika vibaya sana na haipitiki, hivyo kukwamisha usafirishaji wa chai, miwa, ndizi, madini, utalii na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ni udhaifu wa Mkandarasi pamoja na mvua. Mkandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi wa Daraja la Ziggi amefanya kazi hafifu licha ya kwamba ameshalipwa na kukabidhi kazi. Mhandisi wa pili, amepewa miradi mingi (Mitatu) na hana uwezo wa kuitekeleza. Amepewa barabara za Tanga – Pangani, Boza – Muheza na Muheza Amani, Kwamkoro, hajafanya lolote kipande cha barabara ya Boza – Muheza upande wa Muheza, hajajenga mifereji barabara ya Muheza – Amani, hajajenga barabara hiyo ya Muenza – amani – Kwamkoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya jitihada za kufanya mukutano, hivi karibuni kati ya Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mbunge, Madiwani wa Taratfa ya Amani, Mhandisi wa ujenzi Muheza *TANROADS* Mkoa na Mwakilishi wa Mamlaka ya Hifadhi ya msitu wa Amani, kujadili matatizo ya barabara hiyo, Mkandarasi huyo hakuhudhuria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapendekezo. Mkandarasi huyo ambaye viongozi wote wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, Mkurugenzi wa Halmashauri, Wahandisi wa Wilaya na hata Mbunge hatumfahamu hana ushirikiano na ameshindwa kutekeleza kazi ndani ya muda wa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mitatu, barabara ambayo ilipewa ahadi ya kuwekwa lami (Vielelezo vyote viro kama ifuatavyo):-

- (i) Barua ya bodi ya barabara ya Mkoa (2004);
- (ii) Majibu ya Waziri wa ujenzi ndani ya Bunge (2004) na kadhalika;

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda wote huo tumetengewa fedha kwa lami kilometra 1.5 tu toka barabara kuu hadi Mbaramo! Fedha zilizotengwa 2007/2008,

zimekusudiwa kuweka zege maeneo 11 ya kona hatari. Wote tumeridhika, lakini Mhandisi ameshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Muheza - Mkuzi – Boza (Pangani) Kwa upendeleo tu, mkandarasi ametengeneza eneo la Wilaya ya Pangani hadi mwisho wa mpaka wa Muheza Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkandarasi mwingine alipewa na kukamilisha kazi eneo dogo la kutoka Muheza Mjini kuelekea Kalulu, (Barabara hiyo ya Muheza Boza – Pangani). Hata hivyo, amepewa fedha kujenga mfereji wastani wa mita 700, lakini kwa upande mmoja tu wa barabara kutoka eneo la *TANESCO* hadi barabara kuu – Muheza – Tanga. Huu ni utaalam hafifu. Nashauri mfereji upande wa pili ujengwe.

Muheza sasa imepata hadhi ya kuwa mji mdogo tangu mwaka 2006/2007. Tunaomba angalau kilometu tatu za lami kwa barabara hii ya Mkoa – Muheza – Mkuzi – Boza (Pangani) ili kuupa mji mdogo wa Muheza hadhi katika barabara za mji mdogo kwa mwaka 2008/2009. Lengo kuu ni kupendekeza barabara hii kuingizwa katika mpango wa kuwekwa lami kuunganisha Wilaya za Pangani, Muheza na Mkinga.

Mwisho, nawaomba *TANROADS* Mkoa wa Tanga wafuatilie utekelezaji wa kupunguza miti (kivuli) katika barabara ya Muheza – Amani – Kwamkoro kama tulivyokubaliana katika Mkutano wa pamoja niliotaja hapo juu. Chini ya Mkuu wa Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa (MB), kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuongoza Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamini W. Mkapa, kwa kutumia mamlaka aliyopewa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aligawa uliokuwa Mkoa wa Arusha na kuwa Mikoa miwili ya Arusha na Manyara.

Aidha, iliamuliwa kuwa Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara yatakuwa Babati na kwa kuzingatia jiografia na ukweli kuwa hakuna barabara inayounganisha Babati na Makao Makuu ya Wilaya za Simanjiro (Orkesumet) na Makao Makuu ya Wilaya ya Kiteto (Kibaya), Rais aliahidi kutengwa kwa fedha za kutosha na kwa haraka ili kuunganisha Wilaya hiyo na Makao Makuu ya Mkoa. Ilibainika kuwa kwa kutenga kiwango cha TSh.1bln (bilion moja) kwa mwaka, utahitaji si chini ya miaka kumi na tano (15) kuunganisha miji hiyo. Mwaka uliopita, Wizara yako, ilitenga Sh.900,000,000/= na mwaka huu umetenga Sh.335,430,000/= tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali ya Awamu ya Nne kuititia Wizara hii kufahamu kuwa mwananchi wa Simanjiro akitaka kwenda Babati, analazimika kuititia Mikoa miwili ya Kilimanjaro na Arusha. Umbali kati ya km.450 na 600km kutegemea wapi alikoanzia safari yake ya kuelekea Babati. Naomba maelezo na iwapo Serikali haina fedha ni vizuri Serikali itazame upya uamuzi wake wa kuunda Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya ufanuzi kuhusu Sh.60mln zilizotengwa kwa ajili ya “*Feasibility Study and Detailed Design of KIA – Mererani Road*”, kama zitatosha. Aidha, ni vizuri ieleweke kuwa ahadi ya kutengeneza barabara hii ya Mererani – KIA, ni ya Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin Mkapa na pia ni ahadi ya Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, alipotembelea Mererani na wote walisema barabara itatengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuungana na Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kuomba Serikali itoe ufanuzi wa fidia kwa wananchi wa Kamwangi waliovunjiwa nyumba zao kwa ahadi ya kujengewa barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbushia barabara ya Wilaya yangu ya Samanjiro tulizoomba zipandishwe hadhi mwaka 2007, sasa ni vizuri tuelewe zipi zimekubalika na zipi hazijakubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasubiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuhusu barabara ya Babati – Orkesumet kabla sijaunga mkono hoja.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa hongera Mheshimiwa Waziri, kwa bajeti iliyogusa maeneo yote ya nchi. Nilitegemea nitachangia kwa kusema lakini nikakosa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, bandari. Uchumi wa nchi yetu unakua, bandari ya Dar es Salaam, ingepaswa kukua mara kumi zaidi ili kubeba uchumi unaokua kwa haraka sana. Serikali itafute eneo kubwa kwa mfano *Ruvu Railway Station*, iitwe bandari ya nchi kavu. Reli iongezewe uzito na ziwe mbili Dar es Salaam na Ruvu. *Containers* zote zikipakuliwa, zipelekwe huko. *Clearance* zote zikafanyike hapo kwa ajili ya kwenda Uganda, Burundi, Rwanda na Mikoa ya Magharibi hadi Congo. Faida yake, malori yote yanayokwenda Mjini Dar es Salaam yatazuiwa yasiingie mjini na kwa kufanya hivyo, tutapunguza msongamano wa magari Dar es Salaam. Mafuta yaendayo Bara nayo tufanye hivyo hivyo. Ufanisi utaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ujenzi wa barabara zetu kwa fedha za ndani, tuendelee na utaratibu huo kwa sababu ni ukombozi thabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, bandari za Kigoma, Kipili na Kasanga, zipanuliwe ili tuchume mzigo wa Kongo tani milioni tatu. Tuongeze ubora wa reli,

tujenge na reli ya Tazara (Tunduma, Kasanga, Mpanda, Karema) ili tuongeze uwezo wa kuchuma toka Congo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Mkoa wa Rukwa, unashukuru bajeti hii lakini fedha zikichelewa kutoka kero itaongezeka mara dufu. Fedha itoke mapema ili barabara zetu za Tunduma, Sumbawanga, Mpanda zianze. Barabara ya Sumbawanga, Matai Kasesya na Matai Kasanga ianze haraka. Wakandarasi wachunguzwe sana na kuhakikisha hawachezei fedha hizi tunazopata kwa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hongera kwa kufuata Ilani ya Uchaguzi, hii ndiyo njia pekee ya kuondoa kero ya upendeleo wa Mikoa fulani fulani tu. Hili tulizingatie.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeza Waziri wa Wizara hii, Naibu wake pamoja na wataalamu wake wote, kwa kuandaa bajeti hii ambayo imesomwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora, ni Mkoa wa wakulima na wafugaji. Wananchi wake ni maskini sana kutokana na kutokuwa na miundombinu mizuri. Wakulima hawafaidiki na kilimo hicho kutokana na kushindwa kusafirisha mazao yao ili kupata masoko mazuri ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe barabara ya Urambo – Songambele – Ulyankulu, Uyowa hadi Kashishi, yenye kilometra 134, inapandishwa hadhi ili Serikali iweze kuisimamia ijengwe kwa sababu wakati wa mvua haipitiki kabisa. Wananchi wanatembea kwa miguu kilometra zote hizo wakati wa mvua hakuna gari linalopita. Hii sio adhabu kwa wananchi wale?

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara nydingine inayoanzia kata ya Kaliua-Uyumbu – Kangeme – Umbe hadi Ukumbi Kakoko hadi Wilaya ya Rukwa. Barabara hii ina kilometra 119. Barabara hii, ni chafu kabisa kuona kila anayepita njia hii anatafuta pa kupita porini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali angalau barabara hii kongwe itengenezwe kwa kokoto wakati inaandaa utaratibu wa kuitengeza kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Tabora, kinahitaji kupanuliwa ili kuweza kupokea ndege zaidi kwenda sambamba na ukuzaji wa utalii kwenye Kanda ya Kusini.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kuwapa hongera, Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wa Wizara ya Miundombinu, kwa hotuma nzuri sana ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii, inajibu hoja na ahadi za Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Chama cha Mapinduzi (CCM), kilitangaza ahadi zake juu ya Miundombinu katika nchi. Pamoja na ahadi hizo, ndani ya Ilani, zipo pia ahadi za Rais

wakati alipokuwa kwenye kampeni. Ni jambo la kuliwadha kuona kwamba imezingatia ahadi hizo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ya Wizara ya Miundombinu, inazingatia sana maendeleo ya barabara katika upande wa Magharibi wa nchi yetu. Kwa kutengeneza barabara hizo kwa kiwango cha lami, kutakamilisha nia ya CCM kuunganisha Mikoa yote kwa barabara za lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninapenda kuzungumzia barabara za Wilaya ya Morogoro Vijiji. Barabara hizi zipo za aina mbili. Barabara za Mikoa na barabara za Wilaya na Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais wakati alipokuwa kwenye kampeni, alitembelea Wilaya ya Morogoro Vijiji. Alianza safari yake toka Morogoro akipitia Matombo, Mvuha hadi Kisaki. Alipokuwa anarudi alipitia Mvuha, Magogoni – Kiganila (ambapo alivukia chini Mto Ruvu ili kuwahi kufika Ngerengere ikiwa ni *shortcut* badala ya kurudi tena hadi Morogoro na kwenda Ngerengere kufanya mkutano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kisaki aliahidi kuwa, barabara ya Morogoro hadi Kisaki itakuwa kwa kiwango cha changarawe ili ipitike kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale uwanja wa Jamhuri – Morogoro Mjini, wakati wa kushukuru, alitamka na kuahidi kuwa pale alipovuka chini (Kijiji cha Kiganila) atajenga daraja na barabara ya Ubenazomozi, Ngerengere, Tununguo, Kiganila (kupitia daraja la Kikwete – Kiganila) hadi Mvuha na kukutana na barabara ya Morogoro – Kisaki, kuwa ya changarawe na kupidika wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais kwa kuweka ahadi yake hiyo alipokutana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania pale Ngerengere alitoa Sh.300,000,000/= kutengeneza barabara kuanzia Ubenazomozi hadi Ngerengere. Tunashukuru sana kwa msaada huu na sasa barabara hii inapitika.

Bajeti ya mwaka jana, yaani 2007/08, Wizara ilipanga pesa kwa barabara hii ambayo iliwezesha *TANROAD* kufanya *Lightgrading* toka Ngerengere hadi Tununguo. Bahati mbaya pesa haikutosha kuendelea toka Tununguo kwenda Kiganila (18 km.) hadi Mkulazi (22 kms.)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali nilimwandikia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu, nikimwomba Sh.300,000,000/= kwa Kms.40 hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kubadilisha bajeti iliyopo, naomba nishauri yafuatayo: -

Katika ukurasa wa 166 wa Bajeti kuna Sh.60/= millioni za barabara ya Ubenazamozi – Ngerengere. Hapa ninamuomba Mheshimiwa Waziri kutenga milioni

30/= na milioni 30/= kwenda sehemu ya barabara hiyo kuanzia Tununguo – Kiganila – Mkulazi. Kitendo hiki hakibadilishi bajeti ya barabara hii ingawa ingekuwa jambo la maana sana kama Mheshimiwa Waziri angeweza kupata hizo 30/= milioni kuwa nyongeza ya Sh.60/= milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 166 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, barabara inayoitwa Duthumi – Kolelo – Lukange – Kasanga, 35 Kms haikupata pesa. Tafadhalii Mheshimiwa Waziri barabara hii ni ya milima mirefu sana na mvua ni nyingi mno. Barabara za milimani ni ngumu sana kuzitunza, kwa bahati mbaya sana barabara hii haikupata hata senti moja. Mheshimiwa, Waziri uhai wa barabara hii, ni uhai wa watu wake kuweza kusafirisha mazao yao kwenye soko la Mvuha na hatimaye aidha Dar es Salaam au kwenda Dodoma. Mheshimiwa Waziri, hapa nakuomba Sh.30,000,000/= kwa kukarabati barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi kubwa na ngumu sana ya kupanga bajeti, Mheshimiwa Waziri, naomba akubali kuiokoa barabara hii ya Mkoa ya Kiswira – Tawa (R.669) Km.12, ukurasa wa 140. Barabara hii imekosa huduma kwa miaka miwili sasa. Hivyo, Sh.3,000,000/= iliyopangwa, haitasaidia hata kwa kuziba mashimo tu. Angalau Mheshimiwa Waziri, ili soko kubwa la mazao la Tawa kuweza kufikiwa na malori yaweze kuteremka na mizigo mizito ya mazao aina kwa aina, naomba kuongezewa ifikie angalau milioni 20/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa barabara hii ni mkubwa sana ikiwa ni kiungo cha kata tatu kubwa za milimani, yaani Kibungo Juu, Kibogwa na Tawa yenewe na kuiunganisha na Kata ya Kisemu, katika Tarafa ya Matombo.

Daraja la Kiganila, hii ni ahadi ya Rais, Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete. Sikuona pesa yoyote. Labda Mheshimiwa Waziri analo kwenye mpango wa Wizara, ninapenda kujua juu ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa matayarisho na mawasilisho mahiri. Nawatakia majadiliano mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Wilaya ya Hanang, ina barabara nyingi chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Hanang na kwa kuwa fedha za barabara zinazotengwa kwa Wilaya ni kidogo sana, hivyo Wilaya imebaki na barabara mbovu. Kutokana na hali hiyo, tuliomba Mkoa uwasilishe orodha ya barabara ambazo zimefikia vigezo viwe barabara za Mkoa. Napenda kujua ni lini barabara zifuatazo zitakuwa za Mkoa:-

(1) Barabara ya Katesh Balang'ada, Murumba kuititia  
hadi Mkoa wa Singida hususani Wilaya ya Mureru  
Singida Kusini;

(2) Barabara ya Endagaw Gidohobabieg kwenda Gidas  
ya Babati Vijijini; katika Wilaya

- (3) Barabara ya Basodesh, Gawidu, Langanga kuelekea  
Singida; na
- (4) Zile ambazo zimekwishawasilishwa Mkoani na bila shaka  
zimefikishwa kwa Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, muda umefika sasa wa kuunda Mamlaka au Wakala wa Barabara za Vijijini ili kuongezea nguvu za Halmashauri katika ujenzi wa Barabara Vijijini na Wilayani, jambo ambalo au jukumu ambalo linapita kimo Wilaya zetu.

Mfano ujenzi wa Daraja la Mto Bubu linalounganisha Wilaya ya Hanang na Babati, daraja ambalo Mheshimiwa Damas Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini amekuwa akiuuliza Wizara ya Miundombinu mara nyingi ili lijengwe kutokana na matatizo yanayokabili wananchi kuvuka hasa watoto wa shule na wafanyabiashara pamoja na watu wanapohemea kutokana na ukosefu wa chakula upande mmoja wa mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano, kwanza, kwa vile mawasiliano ya simu ya mkononi (*Celtel, Vodacom etc*), hazisikiki katika Makao Makuu ya Tarafa ya Balangda na Kataza Maskta, Masgarodo katika tarafa ya Endasak na Tarafa ya Simbay zote zikiwa Wilaya ya Hanang. Wizara itasaidiaje kujua tatizo ni nini? Vile vile kuona kuwa tatizo hilo la mawasiliano katika maeneo niliyoyataja, linaondolewa mapema ili wananchi wawe na mawasiliano na kuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nawapongeza sana na nawatachia mema katika kupitisha hoja ya Wizara yenu.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakupongeza Mheshimiwa Waziri na timu yako kwa kutayarisha na kuwasilisha bajeti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, barabara ya Mugakorongo – Kigarama – Murungo. Hii ni barabara ya Kilomita 120 na inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe. Ni ndefu mno. Tulishaeleza sana, inaunganisha Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Rais mwezi February mwaka huu alitembelea Karagwe na akapita barabara hiyo kilomita zote 120, akawaahidi wananchi hadharani kwamba Serikali Kuu, inachukua barabara hiyo. Naibu Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Makongoro, alikuwa kwenye msafara. Baada ya kauli hiyo ya Serikali, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, inategemea barabara hii ihudumiwe na Serikali Kuu. Sioni bajeti yake kwenye bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, barabara ya Kyaka – Karagwe. Ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kuitengeneza kwa kiwango cha lami. Ahadi hii aliirudia Mheshimiwa

Rais alipotutembelea Karagwe mwezi February mwaka huu. Okoa heshima ya Mheshimiwa Rais.

Nne, Rwabunuka *Escarment*, Barabara ya Bugene – Nkwenda-Murongo, inayounganisha Tanzania na Uganda na inayohudumiwa na Mkoa, ina kilima kibaya sana kwa jina hilo. Walikipitia Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu. Tunaomba kama ambavyo huwa inafanyika, kilima hiki cha kilomita nne kiwekwe lami ili kupunguza ajali. Itakuwa vizuri Mkandarasi wa Kyaka – Bugene akiunganisha kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Uwanja wa Ndege Bukoba, tunashukuru kwa hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa “*infrastructure*” katika maendeleo ya nchi, Tanzania tumepakana na nchi nane (8). Uchumi wa Jiografia, maamuzi yetu lazima yazingatie umuhimu na sisi kuwepo katika “*position*” yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida, ni kama zifuatazo:-

- Kilimo kitakua;
- Utalii;
- *Transit trade*;
- Biashara ya ndani;
- *Cost of doing business*; na
- *Attraction of investors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Infrastructure Bonds*, hii ni muhimu sana lakini itawezekana iwapo tu sheria yetu itadilishwa. Sheria ya Mikopo ya Nje ya 1974, inasema mkopo wowote ule lazima uwe na *element* ya *grant* kwa asilimia 50% au zaidi. Sheria hii lazima ibadilishwe bila hivyo *Sovereignty Bonds*, haiwezekani, ije Bungeni tuibadilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *contractors*, naomba Serikali ije na mpango mahususi wa kusaidia *Local Contractors* kwa kuwapatia *Government guarantee* ili waweze kununua vifaa vya ujenzi, tuchague wachache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *ATC*, naomba Serikali iwekeze kwenye kampuni hii, sioni pesa za *ATC*, naomba maelezo katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara, naomba Serikali inieleze ni kwa nini wanagawa pesa kidogo kidogo? Hii inafanya barabara zetu ziwe na gharama kubwa, ‘*no economy of scale price advantage, time wastage*’, naomba maelezo ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Road Fund Board*, Sheria ibadilishwe.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika ninampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri na ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi, ninaomba nichangie maeneo machache katika hotuba ya Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ujenzi wa miundombinu ya barabara ya reli inahitaji fedha nyingi sana lakini Wizara hii imepewa bajeti ndogo sana hivyo kusababisha miradi mingi kukwama kwa muda mrefu. Katika hili, ninaungana na maoni ya Kamati ya Miundombinu, kuisihi Serikali kutafuta vyanzo mbadala vya kupata fedha za kuharakisha ujenzi wa barabara na reli kama *BOT*, *BOOT* na ule wa PPP. Aidha, serikali itafute mikopo katika taasisi za kifedha za kimataifa kwa lengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niipongeze Serikali kwa ujumla pamoja na ufinyu wa bajeti, kwa kazi nzuri ya uimarishaji wa barabara nchini, zikiwemo barabara za kiwango cha lami na zile za changarawe. Kutokana na juhud hizi, barabara nyingi nchini hivi sasa zinapitika kwa wakati wote wa mwaka. Pamoja na kazi hiyo nzuri, ziko barabara chache pamoja na umuhimu wake zimesahaulika kwa muda mrefu nazo ni:-

(a) Barabara ya Babati - Kondoa – Dodoma – Iringa. Pamoja na barabara hii kuwa kiungo muhimu kati ya Makao Makuu ya nchi (Dodoma) na Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Arusha), barabara hii haipewi kipaumbele chochote. Tukumbuke kuwa nchi wanachama, waanzilishi wote (Uganda na Kenya) wameunganishwa na barabara za lami kutoka Makao Makuu yao isipokuwa Tanzania peke yake. Tanzania ni nchi pekee ambayo Makao Makuu ya nchi, imeunganishwa na barabara ya vumbi na Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali iondoe aibu hii kwa kujenga barabara ya Iringa-Dodoma – Kondoa - Babati kwa kiwango cha lami.

(b) Barabara ya Zamahelo – Kwamtoro – Kinyamshindo – Singida. Baada ya kuanza ujenzi barabara ya lami kutoka Dodoma - Manyoni - Singida, barabara ya Zamahelo – Kwamtoro – Kinyamshindo hadi Singida ambayo ni sehemu muhimu ya barabara fupi kati ya Dodoma na Singida imeanza kupuuzwa.

Mheshimiwa Spika, ninaisihi na kuishauri Serikali iendelee kuimarissha barabara hii kwa sababu ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa Tarafa za Farkwa na Kwamtoro Wilayani Kondoa.

(c) Barabara ya Kondoa – Goima – Mrijo Chini/Olboloti. Barabara hii ni ya Mkoa na inapita katika maeneo muhimu ya uzalishaji wa mazao ya kilimo yakiwemo

mahindi, ulezi, ufuta, mbaazi na alizeti. Pamoja na umuhimu wake barabara hii haijapata matengenezo makubwa kwa muda mrefu na kufanya ipitike kwa shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba barabara hii ifanyiwe matengenezo makubwa haraka ili mazao ya wananchi yaweze kusafirishwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ujenzi wa nyumba za viongozi na watumishi wa umma, ninaipongeza Wakala wa Majengo ya Serikali (*TBA*), kwa kuendelea na ujenzi wa makazi ya viongozi, watumishi wa umma na ofisi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa Serikali ina nia dhati ya kuhamia Dodoma, ninaomba Wakala wa Majengo ya Serikali, iweke mkakati maalum wa kujenga nyumba za viongozi wakuu, watumishi wa Serikali na ofisi za Serikali Dodoma badala ya kuendelea kujenga Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, upandishwaji wa barabara ya Kondo – Kwamtoro hadi Mpendo. Wilaya ya Kondo ilipendekeza barabara iliyotajwa hapo juu kupandishwa daraja kutoka barabara ya Wilaya kuwa barabara ya Mkoa. Ninaomba kufahamu maombi hayo yamefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, baada ya kuchangia haya machache, ninaomba kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Miundombinu.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwa makini sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini kwa kifupi siridhiki nayo kwa sababu daraja la Mto Sibiti halikutengewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naandika hivyo kwa sababu TSh.80m zilizotengwa, haziwezi kufanya kitu chochote kulinganisha na mafuriko ya huo mto unavyojaa wakati wa masika na ifahamike kwamba mafuriko haya husambaa Iramba Mashariki ambako ndiko barabara ya Mkoa inayotoka Ulemo, Gumanga, Sibiti, nayo kwa urefu wote huo imetengewa TSh.50m tu ambapo kipande cha barabara ya Ulemo Msingi na Gumanga Mkalama vimeoza kabisa, sehemu ya chemchem Sibiti ambamo ndilo eneo la mafuriko hupita imetengewa TSh.50m tu, fedha ambazo hazitoshi kuinua tuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi hata mwaka jana zilitengwa, barabara hiyo inatengenezwa chini ya kiwango kwa hiyo fedha hizi ni kama zinatupwa tu. Maana mafuriko yakianza, barabara hiyo huwa haipitiki kwa miezi kati ya minne na mitano kwa ajili ya mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ikumbukwe kwamba daraja hili ni sehemu ya barabara ambayo tulipendekeza itoke Arusha kuitia Karatu/Mbulu Haydom, Kidorata, Ibaga, Mto Sibiti, Meatu, Bariadi na hatimaye ifike Musoma. Wananchi wa Mikoa ya Shinyanga, Singida, Manyara na Arusha, wanashangaa sana barabara hii inaachwa kienyeji na sasa inapendekezwa ijengwe barabara ya Musomo, Mgumu, Loliondo, Monduli hatimaye Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mkono, Mbunge wa MusomoVijijini alipochangia jana tarehe 02/07/2008, alikuambia wazi ya kwamba wahifadhi kote duniani wanapiga kelele na kukataa barabara hiyo isikatishe ndani ya hifadhi ya Serengeti tena kwenye eneo ambalo ndiyo njia finyu inayotumiwa na wanyama wanaohama kutoka Serengeti kwenda Masai Mara Game Reserve (Kenya).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambayo tunaomba daraja la Sibiti lijengwe, inaunganisha Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Singida, Shinyanga, Mwanza, Mara na nchi jirani za Uganda, Rwanda, Burundi na Zaire. Wakati wa kiangazi, magari makubwa na madogo hutumia njia hii mto ukikauka. Hii ni barabara inayopita kwa wakulima, wafugaji wachimba madini, wavuvi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuambie tu au nikukumbushe kwamba darala la Mto Sibiti litaungana na darala la Mto Simiyu (Bariadi) ambalo tayari limeishajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana fedha kwa kazi hii zitolewe ili kukamilisha ujenzi wa daraja la Mto Sibiti. Naomba hata kama Serikali haitakuwa na fedha za kutosheleza kazi hii itakuwa vizuri zaidi ikitekelezwa na Jeshi la Ulinzi (JWTZ).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Bonde la Ziwa Eyasi (Shinyanga, Singida, Manyara na Arusha), nina imani kwamba Serikali itatafuta fedha kwa kazi hii mwaka huu wa 2008/09.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja hii pale tu utakaponithibitishia kwamba fedha zitapatikana kwa ujenzi wa darala hilo hata kwa fedha za mkopo. Ninao mpango wa kukamata shilingi.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, barabara ya Minjingu – Babati – Singida, kwa niaba ya wananchi wa Babati Mjini, naipongeza Serikali kwa uamuhi wake wa kutenga fedha bilioni 17.7 kwa ajili ya kujenga barabara hii muhimu kwa uchumi wa nchi hii. Nimefarijika kuona Serikali imetenga fedha za ndani TSh.1.9bn.

- Naomba Serikali itoe fedha hizi zote mara tu mradi ukianza ili kuondoa kuchelewa kwa mradi;

- Nashauri Mkandarasi/Wakandarasi wenye uzoefu na sifa, ndio wateuliwe ili kuondokana na tuliojifunza kwenye barabara za Manyoni – Singida na kadhalika; na

- Mkandarasi wa kipande kati ya Minjingu na Babati, azingatie historia ya mafuriko na kutitia kwa ardhi katika maeneo ya Mdori, Mwada, Matufa/Mawemairo na Babati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, barabara ya Dodoma – Babati, barabara hii imetengewa TShs.12bil lakini bado inaelezwa kuwa kuna upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara. Kwa kuwa sasa zimepatikana kwa kuweza kuanza ujenzi, nashauri ujenzi uanze kwa eneo la Babati – Dodoma ambapo bila shaka upembuzi na usanifu umefanyika ili upembuzi na usanifu ufanyike katika eneo la Dodoma – Iringa ambayo umepata fedha kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifahamike kuwa barabara hii imewekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi 2005 ya CCM, Kifungu cha 125, kuhamia Makao Makuu na imeelezwa kuwa hatua moja kubwa ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma – Babati na Dodoma – Iringa. Hii ni hoja kubwa sana kwa Mikoa mikubwa ya Manyara, Dodoma na Iringa lakini kwa Watanzania wote, tuanze ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Babati – Orkesmet/Kibaya, wananchi walifiki kuanzishwa kwa Mkoa wa Manyara kwa Serikali kuunganisha Wilaya ya Simanjiro na Kiteto kwa barabara ya kudumu. Tangu Mkoa wa Manyara uanzishwe, Serikali imekuwa ikitoa fedha ili walau barabara ifunguke lakini tatizo sasa ni Mkandarasi – *Weasons* ambaye ameshindwa kukamilisha kazi kwa sababu zake mwenyewe hasa madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa *Road Board Meeting* ya Manyara, ilitolewa taarifa kuwa Mkandarasi anakatwa TSh.Mil.1.3 kila siku hadi siku 100. Ni wazi kuwa fedha anazokatwa hazitafidia hasara ambayo tayari tumeipata na hasa ya kiuchumi.

Nilichojifunza ni kwamba Mkandarasi huyu sasa amejiingiza kwenye shughuli zingine za kijamii na za kisiasa. Inaonekana kuwa amekaa muda mrefu sana kwenye eneo hilo na kwa kuwa amelipwa fedha zake, sasa ana kiburi na wala hata kusogezwa kambi yake kwenye eneo husika, halifanyiki. Kambi ya sasa ipo kwenye *Road Reserve* – eneo la Kambarage – karibu na *Songea Secondary School*. Ameambiwa aondoe kambi hiyo ambayo imekuwa kero kwa wananchi wanaofanyiwa vitendo vya kupigwa mara kwa mara wanapopita eneo hilo ambalo lipo barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkandarasi huyu anaendelea kututia hasara, naomba kutoa ushauri ufuatao:-

- (1) Mheshimiwa Waziri ufanye ziara rasmi kuitembelea barabara hii ili upate kwa kina tabia na mwenendo wa Mkandarasi huyo;
- (2) Mkandarasi huyu asipewe kazi yoyote katika eneo la Mkoa wa Manyara au hata pengine kama hawezি kudhitiwa, tungependa kujua historia yake;
- (3) Naomba nipate *list* ya miradi anayotekeleza Mkandarasi huyo sehemu zingine za nchi na tujuu viwango vyake; na
- (4) Ni muhimu Wabunge wapate majina ya Wakandarasi kila mmoja ana miradi mingapi kwa barabara kuu na za Mikoa.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Tanzamia inajaribu kutangaza vivutio vya utalii ili watalii waje kwa wingi hapa nchini. Hata Mkutano wa Nane wa Leon Sylvian, sehemu moja imefanya kazi hiyo ya kutangaza nchi yetu. Watalii watakapohamasika na kutaka kuja nchini, watahitaji usafiri wa kuwafikisha hapa nchini, usafiri wenyewe sehemu kubwa ni ndege. Inashangaza sana na *ATCL*, juhudhi hizo zinazofanywa lakini bado shirika letu la ndege katika bajeti hii, halikupewa uzito unaostahili katika kuliimarishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kukuza utalii nchini kiasi kikubwa bila kuwa na shirika la ndege letu kubwa ili tuweze kuwachukua watalii moja kwa moja huko wanakotoka mfano Asia, Amerika na Europe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la msongamano kwa wasafiri wanaokwenda Zanzibar kwa kutumia boti zinazokwenda kasi. Licha ya wasafiri kuwepo mapema eneo hilo kwa kutaka kusafiri lakini huzuiliwa nje ya lango kuu (*gate*) mpaka unapobakia muda mfupi boti kuondoka ndio wananchi huruhusiwa kwenda kuingia kwenye boti. Hali hiyo husababisha msongamano na tabu kubwa kwa wasafiri hao. Ipo haja serikali kulitatua suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya juhudhi ya kujenga barabara lakini baadhi ya barabara hizo kwa kuwa ujenzi wake uko chini ya viwango wakati wa mvua hubomolewa na mvua hizo. Wizara katika hotuba yake, haikueleza ni barabara zifi hizo na Serikali imepata hasara ya kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara hii na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia yafuatayo:-

(1) Daraja La Mto Kilombero. Katika mkutano wa nne, kikao cha 41, cha tarehe 11/08/2006, Waziri wa Miundombinu alipokuwa anajibu Swali langu Na.393, juu ya ujenzi wa daraja la Mto Kilombero alisema na naomba kunukuu:-

*"Katika mwaka wa fedha 2005/06, Serikali ilitenga jumla ya Shilling milioni 50 kwa ajili ya kufanya upembizi wa awali wa daraja la Mto Kilombero na pia katika mwaka wa fedha 2006/2007, jumla ya Shilingi 70 milioni zimetengwa kwa ajili ya upembizi na usanifu. Baada ya kazi hizi za awali, Serikali itaendelea na juhudhi zake za kupata fedha za ujenzi wa daraja hilo kama alivyoahidi Mheshimwa Rais."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu aliyejita aliliambia Bunge kuwa mwaka wa fedha uliopita 2007/2008, shughuli ambayo ilikuwa ifanyike ni kufanya upembuzi yakinifu wa kina (*detailed feasibility study*).

Mwaka huu Mheshimiwa Waziri anasema kazi ya upembuzi yakinifu wa daraja la Mto Kilombero imekamilika. Hatua inayoendelea ni usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni za ujenzi wa daraja. Je, usanifu wa kina unaendelea mwaka huu wa fedha 2008/2009, ni mwendelezo wa kazi ya mwaka 2007/2008? Je ni shirika gani linafanya upembuzi huo au ni Serikali yenyewe?

(2) Barabara ya Kidatu – Ifakara – Mahenge. Akijibu Swalii hilo hilo, Na.393, la tarehe 11.08.2006 kuhusu barabara hiyo, Waziri alisema:-

*“Mheshimiwa Spika, barabara ya Kidatu – Ifakara – Mahenge, ni sehemu ya barabara kuu ya Mikumi – Kidatu – Ifakara – Mahenge yenyе urefu wa kilometra 175. Sehemu ya Mikumi – Kidatu, kilometra 35, ilishajengwa na kukamilishwa kwa kiwango cha lami. Aidha sehemu ya barabara hiyo kutoka Kidatu – Ifakara – Mahenge, ni mojawapo ya barabara iliyopo kwenye mpango kabambe wa Transport Sector Investment Programme wa kujenga kwa kiwango cha lami kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007 hadi 2010/2011”. Mwisho wa kunukuu”.*

Je, serikali katika kipindi hiki cha miaka mitano ni lini hasa kazi katika barabara hii itaanza? Huu mpango kabambe wa *Transport Sector Investment Programme*, umeanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ikiijengwa pamoja na daraja, itafungua fursa nyingi za uwekezaji kwenye kilimo kwa sababu maeneo ambayo barabara hii inapita kuna ardhi nzuri.

(3) Barabara ya Ifakara – Taweta - Madeke (Njombe). Wilaya yangu ina barabara moja kubwa ambayo ni (*TRUNK ROAD*), barabara kuu ya Kidatu-Ifakara (km 75) na kutoka Ifakara – Taweta – Madeke (Km 250) ambayo ni barabara ya Mkao chini ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiuchumi barabara hii, ni kama ulivyo mshipa wa *AORTA* katika mwili wa binadamu. Kwa siku, barabara hii hupitisha magari zaidi ya 100 yenyе kusheheni mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkao wa Morogoro, umebainishwa kuwa mojawapo ya Mikoa ambayo itazalisha chakula kwa wingi na kulisha nchi na ziada kuuzwa nje ya Mkao na hata nje ya nchi, kwa maana halisi ya kuwa Ghala la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongezaji wa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara bila kwenda sambamba na uimarishaji wa miundo mbinu ya barabara, kutaathiri kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa masoko kwa mazao yanayozalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na hoja kwamba barabara zijengwe kwa kufuata fursa za uchumi kuliko kuzijenga kwa vigezo vya siasa. Sidhani kuwa Serikali itaweza kujenga barabara ghali kwa sababu ya kusafirisha watu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara chache za lami zilizojengwa wakati wa Mkoloni kwenye miji yetu, fedha zake zilikopwa kwa kutumia “*Sovereign Bonds*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nchi hii sasa inakopesheka basi hamna njia ya kuweka miundombinu nchi nzima ili kufungua uchumi. Kwa njia ya “*Sovereign Bonds*”, Serikali ikope kwa makusudi. Hilo lifanyiwe kazi bila “*laxity*” yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maoni ya Kamati ya Miundombinu, kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2008/2009, kuhusu ujenzi wa Daraja la Kilombero, Kamati inasema (Daraja la Kilombero lijengwe kutoka Mfuko wa Barabara).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Waziri, Mfuko wa Barabara unaweza kufanya kazi hii kubwa? Ikiwa barabara za kawaida haziwezi kujengwa na Mfuko huu, je mfuko huu utaweza kujenga barabara hiyo? Naomba ufanuzi kwani kauli hii inapingana na tamko hilo. (Tazama taarifa yako ukurasa 10 & 11 na ufananishe na taarifa ya Kamati Ukurasa wa 7 kipengele 5.3).

(4) Barabara mpya kuunganisha Taweta (*Kilombero District*) na Madeke (*Njombe District*). Barabara hii ni muhimu katika kuwafungulia wananchi wa Taweta na Tanganyika, Kata ya Masagati amba ni wakulima wa mpunga na machungwa na soko la mazao hayo liko katika mji wa Njombe ambako ni maarufu kwa mazao ya viazi mviringo, mbao na mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana, barabara hii ilitengewa Sh.70 milioni. Ni juzi tu Mhandisi wa Mkoa alinipigia simu kuwa anapeleka *bull dozer* kwa ajili ya kazi ya kutoboa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walishaelezwa juu ya utoboaji wa barabara hii ambayo ina urefu wa km.30 tu. Mwaka mzima 2007/2008, kazi haikufanyika jambo ambalo limeniletea lawama miye Mbunge wao ambaye niliwapa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika majumuisho nielezwe juu ya barabara hii ambayo pia niliiombea iingizwe kama barabara ya Mkao kwa vile kutoka Ifakara-Mlimba-Taweta, ni barabara ya Mkao.

(5) Barabara zisigawanywe kisiasa. Rasilimali tulizonazo ni chache. Fedha zilizotengwa Wizara ya Miundombinu, ni kidogo na haziwezi kukidhi matakwa ya kila Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hufuata bidhaa kama tunataka kuwa wa kweli katika jambo hili, basi itabidi kabla ya kuweka barabara, lazima kujibu maswali ya msingi ya kiuchumi, kwa mfano:-

- Tutafungua fursa gani za kiuchumi kama barabara hii itajengwa.
- Je, tutaibua viwanda gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kujenga barabara, ghali za lami ili tu kwenda kuchukua watu (siasi).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba daraja la Kilombero kwa sababu maeneo ya Malinyi hadi Kilosa kwa Mpepo yana mabonde makubwa ya kuweza kuanzisha mashamba makubwa (*plantation*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba barabara ya Kidatu –Ifakara – Taweta kwa sababu tunajenga Kiwanda cha Sukari Ruipa na kulima mpunga shamba la *KATOCO*.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Miundombinu na timu yake kwa ujumla kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa umahiri kuandaa bajeti yao ya 2008/2009, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia kwa kuishukuru Serikali kwa kutekeleza Ilani ya CCM kwa vitendo hasa kwa kuweza kusaini mkataba wa kilomita 60 za Ndundu – Somanga, mahali ambapo ni korofi na ndiyo sehemu pekee ilikuwa korofi sana kwa barabara ya Kibiti-Lindi. Tunaomba barabara hii, Serikali iwajibike kwa kutoa pesa kwa wakati na kumsimamia Mkandarasi ili atende kazi yake kwa viwango na umahiri ili barabara hii imalizike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishukuru Serikali kwa kuridhia matumizi ya Bandari ya Mtwara ili kupunguza msongamano uliopo Bandari ya Dar es Salaam. Huu ni uamuzi wa busara na vilevile itasaidia kuongeza ajira kwa wananchi na kuwapunguzia umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, sina budi pia kuishukuru Serikali kwa kuanza matengenezo ya barabara itokayo Masasi-Nanyumbu-Tunduru-Namtumtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, mara itakapomalizika, itakuwa ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Kusini na nchi yetu na nchi za jirani. Pia itawenza kuunganisha nchi za jirani kama Msumbiji, Malawi na Bandari yetu ya Mtwara, hivyo kapanua uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, bado naiomba Wizara yako inipe ufanuzi wa kina juu ya barabara itokayo Mangaka-Mtambaswala endapo

itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuweza kuunganisha na daraja linalotarajia kumalizika hivi karibuni linalounganisha Tanzania na Msumbiji, ni lini hasa barabara hiyo itanza kujengwa na endapo Serikali imeshatenga pesa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Serikali ianzé kufikiria kutenga pesa kwa ajili ya barabara itokayo Mtwara - Tandahimba-Newala - Masasi. Kwani barabara hii ni muhimu sana kiuchumi kwani ikikamilika itawarahisishia wananchi kutumia bandari ya Mtwara kikamilifu na kuweza kupata wawekezaji hasa umeme wa gesi ya Mnazibay utakapopita katika Wilaya hizo, ninaomba Serikali kuandaa mazingira hayo mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada zote zinazofanywa kuondoa kero za muda mrefu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwish, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Nkenge, Wilaya ya Missenyi, eneo la Kajunguti, kwa muda mrefu kuna mpango wa Serikali wa kuwezesha kujenga Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa *Kajunguti International Airport*. Mara ya mwisho nilielezwa kwamba jitihada za kutafuta mwekezaji wa kujenga uwanja huo, zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja huo ni muhimu sana, utasaidia kuongeza kasi ya uchumi wa Mkoa wa Kagera na eneo lote la Maziwa Makuu kama vile Rwanda, Burundi na Uganda. Naomba Wizara yake isaidie kuharakisha ujenzi wa uwanja huo kwa sababu ndio utakuwa ufumbuzi wa kudumu wa Mkoa wa Kagera kuondokana na tatizo la ndege kubwa kushindwa kwenda Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuitumia fursa hii, kwanza kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hii kwa jinsi walivyoshirikiana kwa pamoja kuandaa hotuba hii inayoendana kwa hakika na uwezo na mazingira ya uchumi wa nchi yetu ulivyo sasa. Ni hotuba nzuri sana na inaonesha waandaaji wanaona walikolenga si katika fikra tu bali kwa macho pia. Ninawatachia kila la kheri ili mipango iliyoainishwa katika hotuba itekelezwe kwa kiwango kikubwa kama si kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi ninayo machache ya kuongeza kwa kuomba na kushauri kwa Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa reli, naipongeza sana Serikali kuptitia Wizara hii kuahidi kuongeza safari za abiria za gari moshi kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma na Mwanza kutoka safari mbili hadi nne kwa wiki.

Aidha, kwa niaba ya watumiaji wa njia hii ya usafiri, nazidi kuipongeza Serikali kwa kuahidi kuboresha huduma kwa watumiaji wa usafiri huu ambao hivi sasa unatisha na unaitia aibu Serikali mbele ya mwekezaji mwenyewe. Mto huduma anajali kuwatoa abiria wake toka mahali pamoja na kuwafikisha wateja wake kituo kingine na kupokea ujira kwa kazi hiyo kama msafirishaji wa mizigo. Haiwezekani kutofautisha kati ya mizigo kama magunia ya pamba na mbaa na kusafirisha binadamu. Siamini kuwa pamoja na matatizo yaliyojiteza kama Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu alivyotoa taarifa, mwekezaji huyu anaweza kutoa huduma inayofanana na hii kwa watu wake huko atokako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, pamoja na nia njema ya Serikali kutaka kuongeza idadi ya safari, kama kampuni hii haijajiandaa vyema kutokana na uwezo kifedha, uwezo uliopo, uanzo kwanza na kuboresha huduma kwa wasafiri na safari ziongezwe hadi tatu badala ya nne. Hii italeta heshima kwa Mtanzania na mwekezaji ataoneshwa kuwa watumiaji wa usafiri huu wana mwenyewe nayo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba sana Serikali iliangalie suala hili, ni vema mwekezaji na wengine wajao katika nchi yetu tuwapatie picha (*first impression*), kuwa nchi yetu na Serikali yake inajali kwa dhati watu wake. Ni muhimu wakalijua hili mapema na wakadumu katika hili, huduma bora itangulie kabla ya faida. Ni bora nauli ikapanda kidogo ili huduma za msingi kwa wasafiri zipatikane.

Aidha, katika kuhitimisha, namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anahitimisha, atoe kauli, ni lini ongezeko la idadi ya safari na kuboreshwa hadi kufikia kiwango cha msingi, maji, vyoo na nafasi na chakula litaanza kuonekana kwa wasafiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara, naipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu na kuendeleza juhudzi za kujenga barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Mkoa na Kitaifa, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri ambaye katika Hotuba yake ametoa mipango mingi mizuri ya ujenzi wa barabara hususani zilizopo pembezoni mwa nchi yetu. Ninaamini barabara hizi si tu zitarahisisha usafiri katika maeneo hayo bali pia ni muhimu sana kwa ulinzi na usalama wa nchi yetu. Naomba sana zikamilishwe kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Meneja wa *Tanroad*, Mwanza, Eng. Kadashi na Mhandisi wa Ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya Kwimba, Ndugu Paulo Selemani, kwa kazi nzuri kama matokeo ya ubunifu na mipango mizuri katika maeneo yao. Tangu *waingie* katika maeneo yao, hali ya barabara za Mkoa wa Mwanza na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, zimebadilika sana. Kila mwananchi barabara hizo zinakopitia, anafarrijika na utendaji kazi wa Wahandisi hawa. Ninawaomba wasije wakalegeza katika juhudzi zao hizi wanazozonesha.

Napenda vile vile niipongeze Serikali kwa hatimaye kuanza utekelezaji wa mradi wa *PMMR* ambao katika Wilaya ya Kwimba na Jimbo la Kwimba ziko barabara mbili (a) Mabuki – Malampaka na (b) Jojiro – Magu. Naipongeza sana Serikali kwa kuanza kuitekeleza ahadi hii ya muda mrefu – ahadi ambayo sasa ilikuwa imeanza kugeuka mwiba wa kisiasa dhidi ya CCM katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, katika majumuisho Mheshimiwa Waziri, licha ya kueleza kuwa ni mpango wa miaka mitano ni vyema akaeleza vile vile ni kwa kiwango gani barabara hizi zitakuwa zinatengenezwa? Je, pamoja na kuwa sasa hivi barabara husika zinajengwa kwa kiwango cha changarawe, ni lini barabara hizi zitaanza kuwekewa lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na utata wa siku nyingi katika kauli ya Mheshimiwa Rais katika kipindi cha Kampeni. Mheshimiwa Rais akiwa mgombea Urais, alipokuwa akiongea na wananchi wa Mjini Ngudu, alitumia maneno haya:

*“Serikali kadri ya uwezo wa kifedha utakaovyokuwa ukipatikana itajenga barabara la Ngudu – Magu.”*

Kwa wananchi karibu wote waliokuwa hapa ikaeleweka kuwa Serikali ikipata uwezo, itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa kuwa barabara hii tayari imekuwepo kwa muda mrefu na imekuwa ikijengwa na kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Hivyo, kwa kuwa barabara tayari ilikuwepo na uhitaji wa kujenga tena haukuwepo, wakaamini Mgombea Urais wakati ule alikuwa na maana kujenga kwa kiwango cha lami. Ninaomba sana ufanuzi kwa mara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utata wa tafsiri hiyo, ombi la wakazi wa Ngudu (Makao Makuu ya Kwimba) na Kwimba kwa jumla bado wanahitaji sana barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami. Aidha, katika ujenzi huu ujumuushe kipande cha Ngudu, Nyamilama hadi Hungunalwa. Barabara hii Magu, Ngudu, Nyamilama, Hungunalwa, ina faida nyingi. Nazo ni:-

- Ni njia fupi kati ya Shinyanga na Musoma.
- Inaufungua mji wa Ngudu na kuimarisha uchumi kati ya Wilaya ya Kwimba na mji wa Ngudu wenyewe.
- Inapunguza msongamano wa magari mjini Mwanza kwa magari kutoka/kwenda Shinyanga na kwenda na kutoka Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Tanroad* Mwanza wanaitembelea barabara hii na wanawenza kuthibitisha ukweli huu. Barabara hii ikiachiwa Halmashauri ya Wilaya peke yake, haitaiweza. Halmashauri ya Wilaya inahitaji msaada wa ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa ndege, Kiwanja cha Ndege kiko mjini sana, litafutwe eneo la kutosha nje ya Jiji, kiwanja kipyka kabisa kijengwe. Napendekeza kijengwe Wilayani Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

**MHE.JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, vipande vya barabara vya Sengerema hadi Ngoma (Wilaya ya Sengerema) na Nyang'holongo hadi Segese (Wilaya ya Geita/Kahama), vinahudumiwa na Halmashauri husika. Tayari vikao vya Halmashauri hizo pamoja na RCC, vimeomba barabara hizo zipandishwe hadhi ili ziwe chini ya TANROADS. Je, Waziri wa Miundombinu, kwa mamlaka aliyopewa na sheria, anaweza kutekeleza hilo angalau kabla ya mwaka ujao wa fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingi za *Road Reserve* za barabara za Mikoa na Kitaifa zimewekewa alama na TANROADS. Tatizo, wananchi wanalima katika maeneo hayo na hakuna anayechukua hatua kuanzia mamlaka ya Wilaya, wa Mkoa, Serikali inasemaje juu ya tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi wa barabara ya Geita – Usagara (lami), kumekuwa na maombi ya kujenga vituo vya Polisi pale Busisi na Kigongo ambavyo vitawezesha Jeshi la Polisi kuweka “Armery”, Radio na kadhalika ili kulinda kivuko, mali za wasafiri pamoja na usalama wao. Je, hilo limezingatiwa?

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuchangia kwa maandishi hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri na watendaji walioandaa hotuba hii kama itatekelezwa kama ilivyo basi itakuwa imepiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naishukuru Serikali kwa kufuta mkataba wa Dowans, ni jambo la kufurahisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naanza kuchangia kuhusu barabara. Barabara ndio uti wa maendeleo ya nchi hii na ndio inayochangia uchumi wa Taifa letu. Serikali ni lazima itoe kipaumbele kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingi za vijijini bado ni mbovu zinahitaji kujengwa na kupanuliwa ili tupate maendeleo. Kwa kweli wakati wa mvua vijijini kuna tatizo la usafiri kutokana na ubovu wa barabara hawawezi kupeleka mazao yao sokoni, magari yanakwama kupelekea kupata ajali mara kwa mara, mazao yanaharibikia njiani wanapata hasara na kukosa faida na kupelekea kupanda bei za chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Madereva wanaotumia barabara waliokuwa hawana sifa, nao wanachangia kuleta ajali. Kwa hiyo, Serikali isimamie kikamilifu na

wakibainika wapelekwe Mahakamani na kufutiwa leseni na adhabu ifuatie. Nakuomba Waziri ulizungumze hilo wakati wa majumuisho ili Madereva wasikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miundombinu ya viwanja vya ndege, viwanja vingi ni vichakavu vinahitaji ukarabati na kupanuliwa kwa usalama wa ndege zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uwanja wa Ndege, Dodoma, ni mdogo na upo katikati ya mji na hauridhishi hasa kutokana na lengo la kutaka kuwa Makao Makuu ya nchi. Kwa hiyo, kama Serikali ina nia kutafuta kiwanja kingine ni vizuri, lakini ujengwe uwanja wa Kimataifa ule haufai kuwa uwanja wa Makao Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nakushukuru Waziri na Naibu Waziri, nawaombea kila la kheri na Mungu awape afya njema, mtuongoze Watanzania.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu pamoja na Manaibu Mawaziri na Watalaamu wote, kwa bajeti iliyopangiliwa vizuri kufuata matakwa ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyangi zimejengwa kwa kiwango cha lami. Sengerema hadi Kivuko cha Busisi, baraba hii iko mbioni kutengenezwa pamoja na *ferry* mpya ya Busisi, bado ingekuwa bora ile *ferry* ya zamani ya Sengerema ingekarabatiwa ili kupunguza *traffic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara fupi ya kutoka Sengerema hadi Kamanga kwenye *ferry* ya Geji inayochukua mizigo na abiria kwenda Mwanza na inachukua dakika 25 tu kuvuka. Barabara hii ya Segerema mpaka Kamanga ni fupi na ni mbaya sana. Ingefaa kama Serikali ingekarabati na kujenga barabara hii fupi kwa kiwango cha lami ili eneo hili la muhimu lenye kuzalisha vyakula, pamba na dhahabu, lipate barabara za lami za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi sana iwapo Serikali itafkiria zaidi suala la kuibua meli ya M.V. Bukoka, najua kuwa ni gharama. Serikali ifikirie sana suala hili kwani kuikarabati meli hiyo kutasaidia sana tena sana katika kuwezesha usafiri wa Ziwa Victoria. Iwapo kama haitawezekana, basi meli hiyo iwekwe kama maonyesho pembezoni mwa Ziwa au hata *Museim* (Jumba la Makumbusho).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha meli zote, naomba Serikali ifikirie sana uwezekano wa kuinua sehemu za *station (platfarms)* pale ambapo treni inasimama ili kuwawezesha wazee, wanawake, wajawazito na walemavu kuweza kupanda ngazi na kuingia ndani ya treni bila shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa hotuba mbili za Wazira ya Miundombinu na Waziri Kivuli wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ni roho ya uchumi kwa nchi yoyote ile, ni muhimu kujadili kwa kina ni jinsi gani tunaboresha miundombinu ya barabara na reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka nimeingia katika Bunge hili na hata kabla sijaingia Bungeni, Wabunge wote wanaochangia huongelea kwa kina kuhusu barabara za Majimbo yao. Kelele hizi, zitaisha lini? Cha kushangaza, unakuta bajeti kuu imeshapita sasa tunataka Waziri husika atoe wapi fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini ni muhimu tujadili ni jinsi gani tunapata fedha za ujenzi wa miundombinu (*financing infrastructure*). Ni lazima tukope hakuna njia nyingine kwani Tanzania ni nchi yenye amani na historia yetu inajulikana kwa demokrasia na kadhalika. Sasa tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mramba ambaye amekuwa Serikalini na kushika nyadhifa mbalimbali ikiwemo fedha na miundombinu, aliliambia Bunge kuwa China, wana fedha nyingi sana za kusaidia miundombinu kwa utaratibvu wa mkopo nafuu sana, kigugumizi cha Serikali kiko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna rasilimali nyingi ikiwemo bahari na maziwa. Singapore ni nchi isiyokuwa na rasilimali yoyote zaidi ya bahari ambapo bandari yake hupokea na kusafirisha shehena za mizigo kwa kasi ya ajabu na imetajwa kuwa nchi ya kwanza duniani kwa kukua kwa uchumi kwa kasi ya ajabu mwaka 2007/08. Tatizo letu ni nini? Naomba Serikali itume wataalamu kule wajifunze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina bahati ya kuzungukwa na *landlocked countries* kama Malawi, Rwanda, Burundi, Zambia, DRC na Uganda, lakini ni jambo la kusikitisha kuona jinsi tunavyoshindwa kuwa na reli madhubuti ya kusafirisha shehena. Ileweke kuwa bandari ni mahali pa kupokelea mizigo tu na si pa kuhifadhi. Pamoja na reli ya kati na ile ya TAZARA kusuasua bado barabara tunazotumia kusafirisha mizigo tunaziharibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa *landlocked countries*, ilikuwa ni njia pekee ya Watanzania kupata fedha nyingi mno toka nchi hizi. Wataalamu wa uchumi tunao tele tena *Professors* lakini hakuna kinachoendelea au ni siasa tu? Ni lazima tujenge *Inland Ports* pale Isaka –Shinyanga na Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo makubwa sana ya ujenzi wa barabara kutokumalizika kwa wakati. Barabara nyingi hazimaliziki kwa wakati na mfano ni ile ya Ubungo – Mwenge (Sam Nujoma). Ilikuwa ikamilike Novemba, 2006 wakati Mlimani City inazinduliwa. Hivi tatizo ni Mkandarasi au Wizara? Suala la *value for money* linaangaliwa vipi hasa tukizingatia *inflation rate*? Naamini ni Serikali kwa kuwa ingekuwa ni Mkandarasi basi Serikali ingemfukuza. Lakini cha ajabu Mkandarasi yule

anatumia vifaa vichovu na hasa *manpower* zaidi ya *machine*. Katika zama hizi za teknolojia, ni hatari kwa watu kutumia shoka, jembe na nyundo kutengeneza barabara kubwa kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani alisema mwaka 2007 bandari ya Dar es Salaam ilihudumia tani 5,703 milioni ikilinganishwa na tani 6.320 milioni mwaka 2006. Hili ni punguzo la 9.8% wakati nilitegemea mizigo ingezidi, tatizo ni nini au Mombasa wametuzidi kete? Punguzo hilo pia ni kwa bandari ya Mtwara na Tanga, kulikoni? Lakini kingine kinachojitokeza ni ukosefu wa reli kutoka bandari ya Mtwara kwenda Mikoa ya Kusini, shehena hizi zinabebwa vipi?

Pamoja na fedha kidogo zinazotengwa bado barabara nyingi zinajengwa chini ya viwango na ndio maana baraba nyingi mara baada ya kujengwa, huharibika, hivi huu nao si ufisadi? Au ni ule mchakato wa kupata Mkandarasi ambapo huchukuliwa the *lowest bidder* hata kama hana ubora?

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa majini ni kero sana kwa wananchi wanaotumia. Ni lazima Serikali ielewé kuwa wananchi wanaokaa maeneo ya maji kama Kanda ya Ziwa Nyanza, Nyasa, Tanganyika na mwambao wa bahari ya Hindi na Zanzibar ni wengi na wanachangia sana pato la Taifa. Hivyo, ni jukumu la Serikali kuwajali kwa usalama wao. Kila siku tunasikia vyombo vimezama lakini hata uokoaji unachukua muda mrefu sana lakini kibaya zaidi vyombo vyenyewe ni chakavu sana. Tunaitaka Serikali iseme ni lini itaboresha sekta hii ya majini?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mizani nalo ni kero, kwanza kuna mantiki gani ya kupima zaidi ya mara moja kwa safari moja? Je, hilo la kushusha abiria ili gari i-*balance* ni sayansi ya wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara tatu Dar es Salaam, inakera sana kwani hili lilikuwa ni tamko la Waziri Mkuu bila kutunga sheria. Hivi ni nchi gani duniani yenye utaratibu wa 3 *lines* lakini kwenye *junctions* hakuna njia tatu hali inayosababisha misongamano ya ajabu pamoja na ajali. Lakini kibaya zaidi hata ajali ikitokea linakuwa si kosa la *ki-traffic* bali ni uzembe. Mbaya zaidi hata bima hailipi. Kama utaratibu huu unakubalika, ni lazima Askari wafanye kazi yao. Inawezekanaje njia tatu ziwe hata mchana wa saa 6 – 7? Hii ni kero!

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Kigamboni, umuhimu wa daraja la Kigamboni unajulikana kwa maendeleo ya uchumi wetu. Kila leo tumeambiwa litajengwa lakini wapi. *Beaches* za Kigamboni ni nzuri sana lakini hakuna njia ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi holela – *substandards*, mwaka juzi ghorofa lilipoanguka kule Temeke, Tume iliundwa na hatujua matokeo yalikuwa vipi lakini leo ghorofa nyingine imeanguka pale Kariakoo, laiti ripoti ingekuwa hadharani labda mambo yasingekuwa hivyo. Hivi sasa Serikali inatuambia nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, *SUMATRA* inapongezwa katika hotuba kwa mambo mengi lakini cha ajabu nauli zinapanda kiholela na magari maarufu kama vipanya ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Hali ya Hewa bado hakina vitendea kazi vizuri ikiwemo kutokutoa taarifa sahihi na kwa wakati. Lakini hata rada yetu nadhani haitoi taarifa vizuri na ndio maana tukiwa kwenye ndege tunapoingia mpaka wa Kenya, Rubani hutangaza kulikuwa hakuna mawasiliano mazuri. Hii ni ishara kuwa rada yetu ina matatizo. Hii ni hatari sana na hivyo ni muhimu Serikali kuona umuhimu wa kuwa na rada mpya.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunashukuru kupewa kivuko kipyga cha Ruhuhu ambacho ni kwa ajili ya Ludewa na Mbinga. Kwa bahati mbaya, kumekuwa na mikasa miwili iliyotokea kuhusiana na kivuko kipyga. Kuanzia Dereva wa kivuko aliyeletwa alitoroka kwa vile hakuwa mwenyeji wa Ludewa wala Mbinga. Halafu alipoletwa Dereva mwengine, alikigongesha kivuko kisifanye kazi muda mrefu pengine kwa kutofahamu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itoe mafunzo kwa Madereva wenyeji wa Manda (Ludewa) au Lituhi (Mbinga), ili wanapokosa kazi za kuendesha kivuko wanawenza kufanya shughuli zao binafsi vijijini kwao badala ya Madereva wageni ambao hujsikia uvivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kivuko kitengenezwe ili kiendelee kutoa huduma iliyotegemewa.

**MHE. FELIX N. KIJKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa ushauri wangu kwa kuisaidia Wizara ya Miundombinu, napenda kutamka rasmi kuwa naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Baada ya maelezo yangu hayo, napenda kumpongeza Waziri wa Miundombinu na wataalamu wake kwa kuandaa taarifa ambayo inakwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Pia napongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na wajumbe wake kwa taarifa nzuri waliyoandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongozi zangu za dhati, napenda kutoa hoja kwamba majukumu ya Wizara ya Miundombinu ni makubwa kwa sababu ni Wizara inayotegemewa kutekeleza mengi yaliyoahidiwa na hasa kwa upande wa barabara katika Ilani ya Uchaguzi. Ni kwa mantiki hii, naiomba Serikali iwe inaipangia fedha za kutosha Wizara hii ili kuiwezesha kukamilisha majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa la usafiri wa gari moshi kwa reli ya kati. Kabla ya ubinafsishaji wa reli ya kati, kulikuwa na usafiri wa kila siku kutoka Dar es Salaam – Mwanza hadi Kigoma. Baada ya ubinafsishaji na kubadilika na kuwa *TRL*, utaratibu wa safari za gari moshi umebadilika na kuwa mara mbili kwa wiki badala ya

kila siku. Hali hii inaleta usumbufu kwa wananchi. Ninashauri Serikali kuingilia kati ili kuhakikisha wananchi wanaipata huduma kama ratiba ya awali ilivyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumeshuhudia kuanguka kwa ndege ya Jeshi la Wananchi na kupoteza maisha ya wananchi wasio na hatia. Kumekuwa na matukio kadhaa ya ndege za *Precision Air* na *ATCL* kuharibika mara kwa mara na kuathiri ratiba za safari.

Ninashauri mafundi ndege wote wa maeneo yenyne ndege wapelekwe kuhudhuria mafunzo ya utendaji wa kiufundi kwa sababu inaonyesha kuwa hawana utalaamu wa kutosha. Hali kadhalika kuwepo na usimamizi mkubwa na kuhakikisha kuwa mishahara ya watumishi kwenye makampuni ya ndege inaboreshwa kuliko hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na hali ya kupanda kwa nauli za ndege hali inayowashinda wananchi kuimudu. Mfano hai ni kupanda kwa nauli ya ndege kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma. Nauli imepanda kwa kiwango kikubwa. Ninashauri kuwepo na ratiba ya Ndege ya *ATCL* ili kutokutegemea ndege moja tu ya kampuni ya mtu binafsi ya *Precision Air*.

Baada ya ushauri huu, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sioni barabara ya Mkiwa – Itigi - Rungwa. Mwaka jana ilitengewa fedha ikaanza kukarabatiwa kwa ujenzi wa madaraja madogo madogo sehemu korofi. Sasa sielewi mwaka huu unaokuja 2008/2009, itakuwaje wakati mliahidi kuwa mntaendelea na ukarabati wa barabara hiyo wakati tunasubiri lami kutoka Makongorosi.

**BARABARA YA MKIWA - ITIGI – RUNGWA.** Kwa kuwa mwaka 1998 barabara hii iliharibiwa vibaya na mvua za *Elnino* na serikali kuona umuhimu mkubwa wa kutenga fedha za kutisha chini ya mradi maalum wa *Elnino Project* na kwa kuwa mkandarasi aliyeuleliwa *M/S Badri East Africa*, alishindwa kukamilisha ujenzi wa barabara hii kwa kutokuwa makini na uzembe; na kuifanya serikali kumsimamisha na fedha za mradi huo kurejeshwa lazima.

Naishauri serikali irejeshe/ihuishe mradi huo ITIGI – RUANGWA *Elnino Project* ili barabara hiyo muhimu iweze kujengwa kikamilifu na kurejea katika kiwango chake kama ilivyokuwa nyakati za *East African Road Services*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa fedha 2007/2008 serikali ilitenga Sh. 500m/= kwenye *development vote* kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii lakini fedha hizi hazikufua dafu ni kiduchu mno. Sasa mwaka ujao 2008/2009 zimetengwa Sh. 400 m/= tu – *shortfall* ya Shs.100 m/= za mwaka jana. Wakati serikali inafikiria kurejesha Mradi wa *Elnino Project* kama nilivyoshauri, napendekeza walau Sh Billioni moja zitengwe safari hii badala ya Shs.400 m/= ili ujenzi wa maana kama ukamilishaji wa madaraja madogo madogo kwenye sehemu korofi.

(2) BARABARA YA MANYONI–HEKA–HIKOLA–NKONKO–SANZA. Barabara hii ni muhimu sana sana kwa maendeleo ya wananchi wa majimbo yote mawili ya Mashariki na Magharibi. Lakini ni “*periodic*” na “*Spot maintenance*” tu ndiyo hufanyika kwa fedha kiduchu mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali sana tunaomba serikali itenye fedha za kutosha walau Shs. 500 m/= mwaka 2008/2009 ili barabara hii iweze kukarabatiwa kwa kiwango kinachoridhisha. Tarehe 2 Mei, 2008 Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete, alipita barabara hii na alijionea maendeleo makubwa ya wananchi. Marekebisho kidogo yalifanywa kwenye barabara hii, sasa wananchi wasije fikiria kwamba barabara zinakarabatiwa wakati wa ziara za viongozi tu. Barabara hii sasa iangaliwe. *Regional Tanroads Manager* wa sasa ni makini na mwadilifu asaidiwe kukamilisha barabara hizi mbili nilizozitaja.

(3) Naunga mkono Hoja asilimia mia moja (100%) kwa sababu mto hoja na msaidizi wake ni watu makini na waadilifu na malengo ya wizara kwenye hoja hii yanaonyesha kutukomboa siku si nyingi zijazo kwenye miundombinu yetu vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jibu.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala hili kama nyongeza ya mchango wangu wa maandishi

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nimekuwa nikifuatilia kwa karibu sana barabara zinazojengwa hapa Dodoma. *Style* inayotumiwa na ndugu zetu Wakandarasi wa barabara za Dodoma sidhani kama inafaa. Barabara hizi zinazojengwa zipo chini ya kiwango kwa asilimia kubwa mno. Mfano barabara itokayo NAM ikikatisha katikati ya Area C kupitia Mpepo Bar, barabara ile ilmwagwa kokoto ambazo tulidhani ingemwagwa lami kwa juu ya kokoto hizo lakini cha ajabu kokoto hizo ziliachwa kama zilivyo jambo ambalo zilitusababishia matatizo makubwa kwa wapitaji kwa magari, kwani kokoto hizo huruka na kupasua *wind screen*!

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mfano mmoja tu wa barabara zetu za hapa Dodoma lakini karibia zote zinajengwa kwa *style* hii. Mimi nahoji iko wapi *value for money*, kwenye barabara hizi za Dodoma. Namwomba Waziri anifafanunulie ni kwa nini barabara zinazojengwa hapa Dodoma – Mji Mkuu ziwe na ubora wa chini kiasi hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuliko kujenga barabara za Dodoma kwa kiwango kisichoridhisha, ni bora ikajengwa moja nzuri na yenye ubora unaofaa kuliko kutawanya nguvu bila kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri anifafanulie ni kwa vipi barabara za Dodoma zimwagiwe kokoto na kuachwa kama zilivyo. Mfano mwengine ni kutoka “*keep left*” mjini mpaka “*keep left*” ya kuelekea Arusha – Singida ambapo zinasababisha kero kubwa kwa wapitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAYNAB MATITU VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza wizara ya Miundombinu kwa hotuba yake yenyenye matumaini kwa taifa letu.

Baada ya pongezi hizo nina mambo mawili ya kuchangia, wilaya ya Kisarawe ina umri zaidi ya miaka mia moja (100) lakini ina barabara ya lami yenyenye urefu wa km 6 tu. Tena mradi huu ni wa mwaka 2001. Je ni lini kutakuwa na mwendelezo wa Barabara hiyo kwa Kiwango cha Lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vile hiyo haitoshi barabara zote zinazokwenda kwenye Makao Makuu ya mkoa au wilaya hakuna hata barabara moja ya kiwango cha lami. Je lini Serikali itafikiria kuanza ujenzi huo

Mheshimiwa Naibu Spika, Suala la pili, Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa haotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonyesha ujenzi wa madaraja 33 kwa Mkoa wa pwani. Wilaya ya Kisarawe ina kata moja (Mafizi) ukitaka kufika ni lazima uvuke mto Ruvu au upite kwanza Mkoa wa Dar es Salaam, Kibaha mjini, Kibaha vijijini, jimbo la Bagamoyo uingie tena Kibaha vijijini ndio uingie kwenye Kata hiyo ya Mafizi na uingie Kimalamisale.

Ombi langu tunaomba Serikali ijenje daraja (Mafizi – Kimalamisale) au itupatié pantoni ili kuokoa maisha ya wananchi wa maeneo hayo. Safari hii (nyakati za mvua) Kimalamisale ilikuwa haifiki kote hii ni kutokana na Miundombinu mibovu.

Je Serikali inasaidiaje katika kuleta ufumbuzi wa tatizo hilo kwani wananchi huliwa na mamba na kupoteza maisha au kupoteza viungo vyao na hata kuzorotesha Maendeleo yao. Naomba nipatiwe majibu.

Naunga mkono hoja.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba ya Maendeleo kwa Watanzania, mimi mchango wangu ni uelekeze Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ya Dar es Salaam eneo ambalo abiria wakishuka au wakiteremka kwenye boti wanapita eneo hilo ndipo wapandishe juu na kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ninalolizungumzia sio kubwa sana lakini ni bovu sana kwani hili eneo limeshaanza kuachia na kutengeneza nyufa na ukipita eneo hili linatikisika au kunepa ni hatari kwa maisha ya Watanzania walio wengi ambaao wanapita eneo hilo kila siku, hivi Serikali haoni kwa wakati wowote inaweza kutokea maafa katika eneo hilo hivi kuna utaratibu wowote wa dharura unaweza kuchukuliwa ili kuepusha maafa yasitokee.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hilo zamani magari yalikuwa yanafika na kupaki lakini sasa kumewekwa uzio kwa kukata pande la eneo hilo kuacha na kuwa ni hatari. Mimi niiulize Serikali inieleze ni hatua gani za makusu zitachukuliwa ili eneo hilo lifanyiwe ukarabari au wananchi wasipitishwe kwenye eneo hilo. Baada ya kusema hayo ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Pongezi sana kwako Waziri pamoja na timu ya Wizara ya Miundombinu. Wizara yenu ni ngumu sana kwani macho ya Wabunge wote na wananchi yanaelekezwa kwenu.

Mheshimiwa Waziri, napenda kukuarifu juu ya matumaini ya wananchi kufuatia ahadi ya Serikali kwa wilaya ya Tunduru.

(1) Kwa niaba ya wananchi wa Tunduru bado tuna imani na juhudzi za Serikali za kutafuta fedha za ujenzi wa barabara kutoka Manyaka hadi Tunduru na Tunduru – Namtumbo.

(2) kama wananchi wa Tunduru wangeulizwa leo juu kipaumbele katika zoezi zima la utengenezaji wa barabara, bila shaka yoyote, wangesema Serikali ingeanza kutengeneza barabara ya Mangaka – Tunduru badala ya kuanza ujenzi wa barabara ya Tunduru – Namtumbo sababu kubwa kwa chaguo hilo ni umuhimu wa barabara iendayo bandari ya Mtwara. Uchumi wa wananchi wa Tunduru unategemea zaidi ukanda wa Mashariki kuliko Magharibi. Hivyo bandari ya Mtwara, Mikoa ya Lindi na Mtwara ndiyo soko kubwa kwa bidhaa zinazozalishwa Tunduru.

Tunduru kwa kuamini kuwa ahadi zimetolewa na utekelezaji wake ni miaka mitano na hivi sasa ni nusu ya safari. Hivyo hatuna sababu ya kuhamanika kwamba Serikali hajatekeleza ahadi zake kwa jimbo letu la Tunduru. Nitachukua muda wangu kuwaelimisha wananchi wote waelewe hilo.

Nawatakieni kila la kheri.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara yako kwa Bajeti nzuri walioitoa hapa Bungeni, kwa maana hiyoninatanguliza kauli ya kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami upande wangu ninaomba kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

(1) Mheshimiwa Naibu Spika Gati za Bandari zetu ni muhimili mkubwa wa uchumi wa nchi yetu na endapo tutaziwekeza vizuri nina uhakika tutapata fedha nyingi na kunyanya uchumi wa nchi yetu. Ninashauri sana hebu tuelekeze nguvu zetu katika kuimarisha Bandari ya Tanga, Zanzibar, Dar es Salaam na Mtwara kwa upande wa bahari ya hindi. Aidha tuimairishe bandari zetu zote za katika maziwa makuu.

(2) Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ni mtaji mkuu wa kujenga uchumi, utajenga mawasiliano mazuri kati ya mikoa kwa mikoa aidha tutaunganisha nchi zetu za jirani zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya hivyo tutafanya biashara kati ya nchi kwa nchi lakini zaidi itavutia wawekezaji kuja nchini kwa kuwekeza lakini zaidi suala la utalii litaongeza nguvu kuu na kuimarisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa ni kuhusu Viwanja vya Ndege umefika wakati sasa lazima tuimarishe viwanja vyetu vya ndege, ni njia moja kuu ya kuimarisha uchumi wetu, Mheshimiwa Spika, Shirikisho la Afrika Mashariki liko jirani sana yaani sasa limepiga hodi. Muungano wa Bara la Afrika linakuja kwa mwendo wa kasi sana. Tukiangalia nchi za wenzetu zimepanda katika fani zote. Kwa kweli wameshajiandaa katika ushindani wa utandawazi wa biashara na mambo kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, lazima tuchangamke kweli kweli vinginevyo tutaachwa nyuma sana. Ninaomba sana sana lazima tujipime kulingana na mwendo wa kazi zinavyokwenda nchi za wenzetu. Lazima tukimbie ili tuweze kwenda nao sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha mchango wangu huu mchache na ninaomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. STEPHEN M. WASIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu yanahusu barabara mbili zifuatazo:-

(1) Barabara ya Makutano – Nyamswa – Bunda – Natta – Mugumu – Longido – Mto wa Mbu.

(2) Barabara ya Makutano – Natta ilikwishafanyiwa upembuzi yakinifu. Na sehemu ya Natta Mugumu hadi Mto wa Mbu ilikuwa inaendelea, ningependa kujua upembuzi yakinifu huo umefikia wapi na ujenzi wa barabari hii utanza lini?

(3) Bodi ya barabara ya Moa iliwasilisha ombi la kuunganisha barabara ya Bunda – Nyamswa km 24 ambayo inaunganisha barabara itokayo Mwanza kwenda Musoma, kupitia Butiama wizara ilishakubali ombi hili na iliniandikia kukubali ombi hili. Aidha wakati wa Kampeni 2005, Rais aliahidi sehemu hii ya barabara iunganishwe na barabara ya Makutano – Butiama – Nyamswa - Nata kuelekea Mto wa Mbu. Naomba kujua utekelezaji wa ahadi uko katika hatua gani.

(4) Kupandishwa Daraja barabara ya Bariri - Bunda – Mugeta – Manchmweru hadi Gusuhi Wilaya ya Serengeti. Hii ni barabara muhimu sana kwa kilimo, ufugaji na utalii.

Kwa sasa barabara hii inasimamiwa na halimashauri ya wilaya ambapo imeshindwa kabisa kutokana na ufinyu wa Bajeti na utaalal hafifu. Barabara hii inapakana na *Grumet Game Reserve*.

Naiomba Wizara ipandishe daraja ili kuwa barabara ya mkoa ili ishughulikiwe na *TANROADS*. Nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpungeza Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa Waziri wa Miundombinu na Naibu wake kwa Hotuba nzuri aliyoiwasilisha hapa Bungeni. Pamoja na hayo naomba kuchangia kwa ushauri kama ifuatavyo:-

(1) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni usafiri wa majini – (Ziwa Nyasa). Hali ya usafiri katika Ziwa hili hasa kwa wananchi wanaoishi katika vijiji kandokando ya Ziwa nyasa hasa watokao wilaya za Kyela na Ludewa ni mbaya sana.

Kutokana na kuzungukwa na milima mirefu ya Livingstone, hakuna barabara iendayo kwenye vijiji hivyo, hata kama zikifanyika juhudhi na halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kuchimba barabara hiyo yaitaweza kutokana na gherama kubwa sana za madaraja na miteremko mikali sana kutokana na hali hiyo napenda kutoa ushauri ufuatao:-

(a) Kwamba kwa kuwa uwekezaji wa usafiri katika Nyasa haupo, Serikali ianze kufikiria kutafuta fedha za kununua meli mpya kwa ajili ya usafiri kwa wananchi waishio kandokando mwa ziwa kwani meli ndogo zilizopo ni za zamani sana na zimechoka. Ni hatari sana kwa usalama wa wasafiri.

(b) Serikali ifikirie kuisaidia halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kukamilisha ujenzi wa barabara inayochimbwa kwa ubia wa wananchi wa halmashauri ya Ludewa ili kuwapatia usafiri wananchi hao.

Kuhusu bandari ya Itungi, kina cha Bandari ili kimepotea kabisa kutokana na mchanga uliofukia eneo lote la Bandari. Serikali ifikirie kutafuta fedha ili kufukua mchanga wote ili meli zote hata za Malawi zisimame pale kwani kuna miundmbinu ya kutosha badala ya bandari ndogo ya Kiwira.

Naipongeza Serikali sasa kwa kuvalia njuga suala la ujenzi wa Kiwanja cha ndege Songwe. Ni vizuri sasa ujenzi usisimame tena kwani wanachi wamejiandaa kuzalisha mazao mengi.

Fedha za barabara – wilaya ya Rungwe. Wilaya ya Rungwe ina mvua nyingi sana kwa mwaka na udongo ni *volcano*. Nashauri Serikali inapotoa fedha izingatie hilo kwa kuziongezea fedha barabara zote zinazotengenezwa. Ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

**MHE. SAID ARFI:** Mheshimiwa Spika, Hakika Wahenga walisema, penye miti hakuna Wajenzi na kweli wapo wenye macho lakini hawaoni na masikio lakini hawasikii kama alivyosema Mheshimiwa Kingunge hapa bungeni.

Mheshimiwa Spika, hivi malalamiko, ushauru, adha na taabu wanazopata wasafiri wa reli, hawasikii wala kuona? Hebu tuambieni hii *TRL NI NANI?* *NANI ANAMBEBA TRL?* Haiwezekani kuendelea kukaa kimya bila maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza *TANESCO* na wizara ya Madini na Nishati kwa hatua waliyochukua ya kuisimamisha *DOWANUS/(RICHMOND)*. Hongera hatua hii ni stahiki sasa kuchukuliwa kwa mkataba wa *RITES/GOT*.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli tunajenga uwezo wa nchi kujitegemea au kuliwa?

Mheshimiwa Spika, tuangalie mpango kazi wa TRL ni wa kukodi *engines* na mabehewa toka kwao *RITES* ya India na tunalipa kodi ya kukodisha kwa muda wote ya takayokuwepo nchini ama yanafanya kazi au laa! Ulaji ule ule wa *IPTL/Richmond* na hatimaye tunarudisha *engine*/Behewa India ni kweli tunajenga Kampuni kwa maslahi ya nchi?

Mheshimiwa Spika, *TRL* walishindwa hata kulipa mishahara baada ya ongezeko hadi Serikali ikaingilia kati na kutoa zaidi ya mahitaji yao ya tofauti ya mishahara tunakwenda wapi? Menejimenti pamoja na agizo la *WAZIRI MKUU* bado hakuna hatua iliyochukuliwa ya kurekebisha dosari hii *KULIKONI*? Wanaendelea kukaidi hata ushauri wa Waziri Mkuu.

Ukisoma taarifa ya Menejimenti ya TRL wanakiri kwamba zinahitajika engines za *Class 88* na si *Class 73* ambazo tayari *TRL* wamekodi toka *RITES* (India) matokeo yake ni kuongeza gharama kwa Kampuni, leo ni lazima watumie *engines* mbili za *73 class* badala ya engine moja *88 class* mafuta kwa ajili ya *engine 2* za *73 class* kwenda Kigoma toka Tabora na kurudi ni *Lts 6600* za Dizeli na engine za *88 class* hutumia kiasi cha lita 4000 kwa safari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata kusikia kwamba hata ukiangalia performance Report ya *TRC* miezi 6 kabla ya kukodishwa na miezi 6 baada ya kukodisha inadhihirisha wazi kabisa *TRL* ni tatizo kuliko ilivyokuwa *TRC* pamoja na kupandisha gharama za Uchukuzi muda mfupi tu baada ya kukodisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo kadhaa na mengi lakini hawayaoni wala kusikia. Umuhimu wa kuimarisha hduma na ubora wa Reli sina sababu ya kurudia. Tujitegemee, tukope tuendeshe wenyewe, vinginevyo hata soko la *DRC*, Burundi/Rwanda litahama tunapaswa kuijangalia, kujitathmini na kujisahihisha katika Bandari na Reli mbona bandari (*TPA*) inasimamiwa na Watanzania na inafanya vema?

Tunaweza tukijipanga vizuri. UMASKINI isiwe sababu ya kukubali masharti ya wakubwa *WB//IMF*, tukope tukope tuiweke uhuru wetu rehani.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua mtasema kelele za mlango hazimzuii mwenye nyumba kulala. Basi hata madofo mfanye kwa kuongeza Behewa za abiria kwa njia ya Mpanda. Inasikitisha Wabunge wengi wametaja adha ya usafiri lakini pia hatarishi kwa sababu chakula kinapikwa katika vyumba vyta kulala abiria ama 1st or 2nd class inategemea behewa ambalo linakwenda Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha wasimamizi walioteuliwa kusimamia mali za Reli (*RAHCO*) naomba wawe waangalifu katika kuuza mali za iliyokuwa *TRC*.

Mwisho, katika eneo hili la Reli nimalizie kusema ipo haja ya haraka na makusudi ya kutengeneza daraja karibu na *Katumba Station* nadhani *km 170* wamejenga *cluster* leo ni zaidi ya miaka 2, leo gari ya abiria/mizigo ukipita ni lazima isimame, dereva aweke sahihi katika kitabu cha *Keyman* na apite *at a speed*. Sasa mnangoja hadi ajali itokee na wananchi kupoteza maisha? Na kuunda tume? Tuondokane na tabia hizo. Waswahili husema uspoziba ufa utajenga ukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nipate tu ufanuzi kwa hotuba ya Waziri juu ya barabara. Lakini sina budi kuwapongeza kwa kutenga fedha kwa barabara ya Manyoni/Itigi/Tabora, pia Sumbawanga/Mpanda/Kanyani na nyinginezo nawapongeza, lakini naomba ufanuzi.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa hotuba iliyosheheni maelezo ya kina – *a lot of valuable information – for the whole sector*.

(2) Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa mahitaji ya fedha ya wizara hii ni makubwa sana na hayawezi kukabiliwa na mfumo wa bajeti tulionao sasa. Maombi ya wabunge ya barabara, reli, meli eti ni ushahidi tosha na kuelelezo cha hali halisi ya wizara hii - *The unsatisfied wish – list is probably the bigger challenge of the Ministry*.

(3) Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo ya Bajeti kidogo kilichopo hakitumiwi kikamilifu. Mfano uko katika pg 9 para ya 11. na nukuu: “Barabara zilizokamilisha upembuzi yakinifu ni 2 ambazo ni Maganzo – Maswa - Bariadi – Mkula – Lamadi km 191 na Bagamoyo – Saadan – Tanga (km 150)” mwisho wa kunukuu. Kama Serikali imetumia fedha kukamilisha upembuzi yakinifu, ni vipi ikose fedha ya kuanza ujenzi. Kama ujenzi utachelewa basi fedha za upembuzi zitakuwa zimepotea. Haya si matumizi yenye tija kwa Bajeti ndogo.

Nashauri fedha itafutwe nje ya Bajeti hii ili barabara ambazo zimekamilisha upembuzi yakinifu zianze kujengwa.

(4) Mheshimiwa Naibu Spika suala lingine la matumizi mabaya ya Bajeti ndogo ni umaskini katika kumeneji miradi. Haieleweki hata kidogo – kuchelewesha malipo kwa wakandarasi halafu baadaye unalipa fedha nyingi zaidi ya gharama iliyokubaliwa kwenye *contract* na pamoja na kucheleweshwa kumalizika kwa miradi. Barabara - Dodoma – Manyoni – Singida ni mfano wa matumizi mabaya ya Bajeti finyu na miradi ya namna hii ni mingi tu. Nashauri wizara ifanye utafiti na itueleze fedha tunazopoteza kwa mtindo huu wa kimeneji wa miradi.

(5) Mheshimiwa Spika na shauri Serikali ifanye uchunguzi wa matumizi na maptao halisi ya mfuko wa barabara. Haieleweki kwa nini fedha inakadirwa kupelekwa wilayani haiji kwa wakati na inakuja pungufu. Mfano Bariadi tuliahidiwa milioni 384.55 tumepokea milioni 183.05 mpaka tarehe 15 Mei, 2008.

(6) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ikope kutoka internation market tujenge miundo mbinu kwani maendeleo ni Miundombinu.

**MHE. FUYA GODWIN KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika,nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wengine wote Wizarani kwa kutuletea Hotuba nzuri sana yenye mwelekeo kutokana na yale yaliyokusudiwa katika Ilani ya CCM. Pia kutokana na kiasi cha pesa tulichokuwa nacho kwa Bajeti ya mwaka huu.Nitoe maoni/ushauri katika maeneo machache yafuatayo:-

Sasa Barabara. Nipongeze juhudi zinazofanyika kwenye barabara kuu zote na azma iliyopo ya kuza wekeza lami zote. Hapa ninashauri umuhimu wa kwenda kukopa nije ya nchi pamoja na kuhimiza utaratibu wa 'BOT' ili tuweze kufikia azma yetu mapema na hivyo kukuza uchumi mapema na kuweza kulipia hayo madeni.

Barabara za mikoa nako ni muhimu sana tukaziboresha na kuinua uchumi wa mikoa yetu kipaumbele kikiwa ni nguvu za kiuchumi. Ahadi za Mheshimiwa Rais katika Sekta ya barabara.

Ninaomba kuuliza na nipatiwe majibu ya uhakika kuhusu utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuijenga kwa kiwango cha Lami barabara ya kutoka Kwasadala – Masama Mboreny Masama Some (12.5 km) wakati wa kampeni hapo 2005 na tukizingatia uhumimu wa barabara hii kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuwa route mpya ya Utalii wa Mlima Kilimanjaro pia kusafirisha mazao ya kilimo hasa Kahawa na kufikiwa kwa Taasisi nyingi zilizopo uwanda huo wa milimani.

Pia ninaomba kupatiwa majibu ya upandishaji madaraja (up grading) wa barabara ambazo tumeshazipitisha katika hatua zote zinazohusika mkoani Kilimanjaro katika kikao cha Road Board na RCC na zina viwango/qualification zinazohitajika.

Sasa ni kuhusu viwanja vya Ndege: ninashauri tuviimarishe viwanja vyetu vya ndege vyote navyo tunaweza kukopa kutoka nije ya nchi pia pamoja na kutoa huduma

bora katika viwanja vyetu. Usafiri wa reli ni muhimu sana lakini jitihada zaidi zinahitajika. Bandari: Tuache kuzungumza sana, tufanye kwa matendo sasa katika kujenga Bandari zetu. Tuanzishe mifuko ya barabara vijijini sasa. Naunga hoja mkono.

**MHE. THOMAS ABSON MWANG'ONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo yangu niyaelekeze hususan katika maeneo manne.

- (1) Uwanja wa Ndege wa Songwe, Mbeya;
- (2) Shirika la Ndege la Taifa (*ATC*);
- (3) Shirika la Reli la Taifa (*TRL*); na
- (4) Msongamano wa magari.

Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Kawambwa kwa hotuba yake nzuri, yeye pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Chibulunje. Pamoja na pongezi hizi Mheshimiwa Spika, mkoa wa Mbeya unahisi unashaaulika! Mkoa wa Mbeya una mwamko mkubwa wa kisiasa, unafuatilia sana utendaji wa Serikali na wa msukumo mkubwa katika kutengeneza “maoni ya nchi” suala la Uwanja wa Ndege wa Songwe, ni kero kubwa kwa Mkoa huu na inaweza hata kuwa kikwazo kwa CCM kupata kura 2010!

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wakazi wa Mkoa wa Mbeya, tumeahidiwa na yamekuwa ni mategemeo yetu kwamba ujenzi wake ungekamilika mwaka jana mwezi Novemba, Ikumbukwe kwa Mbeya ni kiungo muhimu sana katika uchumi wa Tanzania. Mbeya ni kiungo cha Tanzania na Malawi, Zambia na Kusini wa Afrika. Mbeya pia ni mojawapo wa mikoa iliyojaliwa kuwa neema ya Madini na mazao ya chakula na biashara. Kukamilika kwa ujenzi wa uwanja huu kutaleta ufanisi mkubwa katika biashara na usafirishaji kiujuimla ndani ya nchi yetu na baina ya nchi yetu na nchi ngeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la Shirika letu la ndege, *ATCL*. Shirika hili liki “*HEAVILY UNDERFUNDED*” Hili shirika ni sawasawa na mtoto anaetambaa. Bado halijaweza kutembea lenyewe. Kukosekana kwa fedha kunaathiri sana huduma za shirika hili. Kwa hivi sasa ndege zinachelewa na kuna sehemu nyingine hata hazifiki mfanoMkoani Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali ilipatie fedha shirika hili angalau lipate ndege 6 mpya. Hili litasaidia sana kwa shirika kuongeza ufanisi wake na hata kuweza kufanya biashara kiushindani zaidi. *Re-financing* ya Shirika hili, itasaidia pia kuleta mvuto kwa aidha wawekezaji thabiti au washiriki wa biashara wakubwa kama vile *BRITISH Airways*, *KLN* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRL* inanikera sana. Tangu Shirika hili limebinafishwa bado hatujaona mabadiliko yoyote ya msingi. Kwa mfano, bado kuna mlundikano wa abiria usiofaa. Mimi najuliza, India abiria wanapandaje treni mpaka kwenye paa la treni imekuwaje leo hii ndio wawekeze kwetu? Naomba wizara ikae nao upya kuangalia tena namna wanavyotoa huduma kwa wananchi wetu.

Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MAGALLE JOHN SHIBUDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Awali ya yote napongeza maelezo yote yaliyotolewa kuhusu dhamira ya kutengeneza miundo mbinu katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia Bajeti ya Taifa ya mapato na matumizi ya fedha nilielezea kuhusu adha ya BARABARA.

Vile vile wakati nachangia hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu nilielezea adha ya barabara katika Jimbo la Maswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu apambanue juhudhi gani zipo kuondoa ubovu wa barabara ambao ni wa jumla ya Km.291.7. Naomba kufafanua kwa kusema:-

- Wakati wa uongozi wa Waziri wa Mheshimiwa Basil Mramba (MB) Serikali iliahidi kutatua tatizo la maeneo korofii ambayo yanatasababisha kupoteza maisha ya wananchi kwa kutopata mapitio ya magari ya kubeba wagonjwa.
- Watoto wa shule wakati wa masika wanakwama kwenda shule.
- Wakati wa masika wakulima hawapelekewi viua wadudu hivyo zao la pamba huwa linaathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa naiomba serikali iseme mwaka huu inatoa gawio gani la kuanza kutatua maeneo ya kutengeneza maeneo yote mabovu.

- Vile vile naomba serikali itamke ni lini barabara ya kutoka Mwigumbi – Maswa – Bariadi hadi Lamadi itaanza kujengwa.
- Vile vile naomba kufahamu ni mpango gani upo wa matumizi ya pesa kidogo za gawio la Shs. Millioni 80 badala ya gawio la mwaka 2007/2008 la Shs. Millioni 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka wa fedha wa 2007/2008 Barabara ya Kolandoto – Lalago-Mwanuzi na Lalago hadi Maswa ilipangiwa Shs.Million 200.Mwaka huu wa fedha sioni pana gawio la fedha pesa. Je pana maelezo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri apokee viambatanisho vya kufafanua shida zilizopo na maeneo ya adha za ubovu wa barabara.

Naomba Mheshimiwa Waziri anipatie majibu sahihi kwa sababu taarifa tangulizi zilishapkelewa toka Desemba mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaomba majibu mema. Ahsante sana.

**MHE. JANETH MORICE MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza napenda kumpongeza Waziri na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa wizara hii kwa kushiriki kuandaa hotuba hii ya Makadirio ya Bajeti 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Miundombinu ya barabara, na mifereji hapa nchini ni tatizo kubwa ambalo linaathiri uchumi wa wananchi, kwa kusababisha wananchi kuchelewa kufika kwa wakati sehemu mbalimblai za kazi. Pia kutofikika kwa urahisi kwa wakulima/wasafirishaji wa mazao mbalimbali katika maeneo ya vijijini. Hali hii inapunguza muda mwangi wa kuzalisha mali. Mfereji wa Majumbasita kuelekea banana ni kero kubwa sana kwa wananchi wa maeneo hayo. Wananchi hao wanaomba wizara iangalie.

Kwa mfano:- Wafanyakazi huchukua muda mwangi wakiwa kwenye foleni za magari na hasa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo asilimia 80% ya mapato hupatikana katika mkoa huo.

Kwa upande wa wakulima hali ya kutokuwa na Miundombinu ya barabara vijijini inasababisha wakulima wetu kuzalisha mazao yao kidogo na p engine hukata tamaa na kukimbilia mjini. Hali hii pia hutoa fursa kwa madalali kwenda mashambani kununua mazao kwa bei ndogo isiyokuwa ya ubinadamu, sababu kubwa ni miundombinu mibaya ya barabara vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, (*Municipal Bond*), Naomba serikali iangalie uwezekano wa kuziruhusu Manispaa ili ziweze kuchukua (*Municipal Bond*) kwa ajili ya Miundombinu ya baraba zake. Na pia serikali Kuu iangalie uwezekano wa kukopa fedha kwa ajili ya Miundombinu ya barabara. Nchi nyingi duniani hukopa kwa ajili ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara za Nyerere, barabara ya Tabata/Kinyerezi/Banana. Serikali iangalie uwezekano wa kupanua barabara hizo kutokana na wingi wa magari ambayo hutumia njia hizo, ili kupunguza msongamano wa magari barabarani. Kwa hiyo, naiomba serikali ipanue barabari hii ya Nyerere kuanzia Majumbasita kuelekea Pugu. Baraba hii inaongezeko wa magari kutokana na wananchi wengi kuhamia katika maeneo ya Pugu, Chanika, Kisarawe na pia *Dampo* kuhamishiwa Pugu.

Kwa upande wa barabara ya Tabata/Kinyerezi ni nyembamba na idadi ya magari ni mengi sana na makandarasi anayefanya matengenezo hana uwezo na haendi kwa kasi inayotakiwa. Wananchi wengi hatulaumu sisi wanasiasa tunaomba wizara ifuatilie kwa karibu zaidi katika barabara hii ya Tabata/Kinyerezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivuko vya watembea kwa miguu (*Flyovers*). Naiomba serikali yenye vivuko kwa ajili ya watembea kwa miguu katika maeneo yafuatayo:-

Buguruni (*Petrol Station*), Vingunguti (*Nyerere Road*), Ubungo, Kimara, Magomeni/*Kawawa Road*, Mbagala, Chang'ombe (*Machinjioni*), Kanisani, Tabata/*Madela Road*.

Maeneo haya ni hatari sana yanababisha vifo na ulemavu kwa wavukao barabara katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanja vya Ndege na Usafiri wa Anga. Viwanja vya Ndege ni kichocheo kikubwa cha Maendeleo ya Biashara na Utalii hapa nchini. Viwanja vya ndege kama Mwanza, Kagera, Musoma, Sumbawanga, Kigoma, Mtwara, Dodoma, Songea, Iringa, ni maeneo muhimu sana iwapo yakiboreshwa, yataleta manufaa makubwa sana na uchumi wa wananchi na nchi itapata maendeleo kwa haraka.

Maeneo hayo yana hifadhi za Taifa, misitu ya mbao, maziwa kama Ziwa Tanganyika, Nyasa, Victoria na kadhalika. Pia mikoa hii iko mpakani na nchi jirani wakazi wengi hutumia njia zilizopo katika mikoa hiyo. Na itakuwa rahisi kwa wawekezaji katika kilimo kufika kirahisi katika mikoa hiyo ambayo huzalisha mazao mengi kama Rukwa, Ruvuma na kadhalika.

Kwa mkoa wa Kigoma kuna mazao kama michikichi, uvuvi na biashara nyingine. Pia mkoa uko mpakani na Burundi, Rwanda na *DRC*. Kwa Musoma kuna Ziwa Victoria, madini mengi tu, kilimo cha pamba, na kadhalika.

Iringa kuna hifadhi ya Kitulo na mazao ya mbao na mazao ya aina mbalimbali, makaa ya mawe na rasilimali nyingine nyingi.

Kagera kuna Ziwa, madini ya aina mbalimbali, mazao ya biashara na chakula na pia iko mpakani na nchi ya Uganda. Usafiri wa Anga (*Air Tanzania*). Naiomba serikali ipatie uwezo *ATC* ili iweze kushindana na mashirika mengine. Uwezo wa viongozi wa *ATC* ni mkubwa, ni wabunifu na ni wazalendo. Kinachohitajika ni UTASHI na maamuzi ya makusudi ikiwezekana hata kwa kukopa katika taasisi zozote duniani. Shirika la serikali haliwezi kila siku linaaibika kwa kukosa fedha za uendeshaji na ukosefu wa ndege. Wakati umefika tuamue. Baadhi ya watendaji hawana maamuzi ya msingi katika maeneo ya msingi ya uchumi wan nchi. Naunga mkono asilimia mia moja (100%).

**MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naunga mkono hoja na kwa maandalizi mazuri ya hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimwambie Mheshimiwa Waziri kuwa *TAZARA* imetelekezwa na serikali ya Tanzania na serikali ya Zambia.

Hali ya *TAZARA* ni mbaya sana. *TAZARA* ikiboreshwa ni mkombozi si kwa Tanzania tu bali ni kwa Zambia, *DRC* na nchi zingine kusini mwa Afrika.

Tatizo kubwa ni “*Lomotives*” kuna mizigo mingi sana bandarini inayohitaji *TAZARA* kuisafirisha. Vivyo hivyo Zambia na nchi ya *DRC* kuna mizigo mingi.

Naomba serikali ya Zambia na Tanzania waangalie upya suala la *TAZARA*. Tukumbuke juhudhi za waasisi wetu, Rais Mstaafu wa Zambia Mheshimiwa Kaunda, Nyerere na Mao wa China.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TAZARA* ni *investment* muhimu kwa nchi yetu. Milioni 100 haitoshi kitu. Wachina pekee hawawezi kutusaidia kuendeleza reli hii muhimu sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGALLE JOHN SHIBUDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kuwasilisha taarifa ya nyongeza kuhusu mawasiliano muhimu ambayo yametendeka kati yangu Mbunge wa Jimbo la Maswa na serikali.

Hii ni kuhusu kuhabarisha juu ya matatizo na mapokeo ya maelezo ya serikali. Na kwa kuwa maelezo niliyopokea ni ya serikali ile ile ya chama chetu cha CCM.

Sasa naomba kuwasilishwa maelezo ya fafanuzi ili yaboreshe uharaka wa maamuzi. Viambatanisho ni nyaraka zifuatazo:-

(a) “*Note*” ya Mheshimiwa Waziri Basil Pesambili Mramba ya kuahidi hatua za serikali.

(b) Barua ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu kuhusu ahadi ya serikali.

(c) Barua yangu ya kuomba serikali inipatie maelezo kuhusu utekelezaji wa hatua za serikali.

(d) Adha ya matatizo kama inavyoonekana katika picha.

Naomba kuwasilisha na ninaomba majibu ya mdomo na maandishi. Ahsante sana.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 9 ya hotuba ya waziri anasema juu ya barabara zinazofanyiwa upembuzi yakinifu ni pamoja na:-

Sumbawanga – Kigoma – Nyakanazi (Kms.829). Ipole – Mpanda – Kigoma (Kms.582) ni barabara mbili tofauti ambayo ile ya Sumbawanga-Kigoma-Nyakanazi haipiti Mpanda, kama barabara zote zinapita Mpanda inakuwaje ifanyiwe upembuzi kwa miradi miwili tofauti?

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nahitaji maelezo juu barabara ya Sumbawanga – Mpanda ambayo ni zaidi ya Km. 240 itajengwa toka Sumbawanga – Chala (60 kms) ukurasa wa 34 wa hotuba kipande hicho cha kilomita 60 kinajengwa kwa kiwango cha lami?

Sehemu nyingine ya kilomita 180 kuna mpango gani wa eneo hilo ambalo pia lina maeneo korofî itashughulikiwa vipi? Maana katika ukurasa 178 miradi ya *PMMR* hakuna fedha iliyotolewa kwa mwaka huu barabara hii ni nyinginezo ambazo zilikuwa katika mradi huu itakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie pesa za mfuko wa barabara (*Road Fund*) ni vyema pesa za ziada zikatengwa kwa ajili ya mifereji ya maji ya mvua katika barabara lakini hazidumu kwa sababu hakuna mifereji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Miundombinu, Mheshimiwa Chibulunje.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia hoja yetu hii ya Makadirio ya Wizara ya Miundombinu ambayo napenda nianze kwa kutangulia kusema kabisa kwamba naunga mkono hoja hii, lakini pia naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote tuiunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwanza kwa kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani kubwa ambayo ameendelea kuwa nayo juu yangu kwa kunitfea hivi karibuni tena nitumikie katika Wizara hii ya Miundombinu kama Naibu Waziri, nikitokea Wizara ya Kazi. Naomba niendelee kumuahidi ya kuwa nitajitahidi kutekeleza majukumu aliyonipa kwa uwezo wangu wote na kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa uongozi na maelekezo yake ya mara kwa mara kwangu katika utekelezaji wa majukumu yangu niliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile namshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika majukumu ya kuiongoza Wizara hii ambayo mimi na yeze tumejiunga nayo hivi karibuni. Naomba pia niwashukuru watendaji wakuu wa Wizara hii wakiwemo Wakurugenzi wa Idara mbalimbali, Wakuu wa Taasisi chini ya Wizara hii kwa umoja wao wakiongozwa na Katibu Mkuu – Eng. Omar Chambo kwa jinsi walivyotupokea Wizarani na kuendelea kutupa msaada na ushirikiano katika kutekeleza majukumu yetu katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nimshukuru kwa dhati kabisa mke wangu mpendwa – Vaiolet, kwa kuwa msaada mkubwa kwangu kwa kunitunza na kuwa karibu sana siku zote katika mambo yote magumu na mepesi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie shukurani zangu kwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Chilonwa kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa na uvumilivu wao kwangu na hasa wanaponikosa kwa shughuli mbalimbali. Naomba waendelee na moyo huo, nami naahidi kuendelea kushirikiana nao na kuwawakilisha hapa Bungeni na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa nianze kuchangia hoja kwa kujibu baadhi hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia kwa kusema hapa Bungeni au kwa maandishi, lakini natangulia kusema kwamba mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atawatambua rasmi kwa kuwataja majina mmoja mmoja kama ilivyo desturi yetu. Lakini kwa ujumla wao wote tunawashukuru sana kwa michango yao, tunaithamini michango hiyo na tutaendelea kuifanyia kazi. Niseme tu kwamba michango ni mingi sana na yote tumeitolea majibu ila kwa sababu ya ufinyu wa muda, hatutaweza kuisoma yote katika kipindi hiki ila tumeiweka kwa maandishi ambayo Waheshimiwa Wabunge watapatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kila Mbunge aliyesimama kusema, kwa kutoa maombi ya barabara au kero nyingine ye yeyote katika sekta ya miundombinu tumehakikisha kwamba tumemjibu na atapata majibu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia katika eneo la barabara. Wachangiaji walikuwa wengi kama nilivyokwishatangulia kusema hapo awali, lakini niseme tu kwamba katika eneo hili tulipata mchango wa kutoka kwa Mheshimiwa Mohamed Khamis Missanga - Mbunge wa Singida Kusini ambaye aliongelea suala la kulipa madeni ya Makandarasi wa barabara ya Dodoma - Manyoni - Singida ili ujenzi ukamilike kwa wakati na hoja hii pia ilizungumziwa na Mheshimiwa Fatma Maghimbii.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ni kwamba, Serikali katika bajeti ya mwaka huu wa 2008/2009 imetenga fedha za kutosha kwa ajili ya madeni ya Makandarasi. Mkandarasi wa Konoike ameshalipwa sehemu ya deni hilo na kazi zimeanza katika barabara hiyo tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Ofisi ya Waziri Mkuu itumie baadhi ya Mabenki hapa nchini kuwa *facility* ambayo itatumia na *TANROAD* kulipa *certificates* ambazo zimeiva kwa malipo ili kupunguza riba na adhabu. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Andrew Chenge - Mbunge wa Bariadi Magharibi. Ushauri umepokelewa na tutaendelea kuufanya kazi kama alivyoshauri Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ilichangiwa kwenye eneo hili la barabara ni kwamba Serikali ihakikishe ujenzi wa barabara ya Ndunu mpaka Somanga kilometra 60 unakamilika. Nadhani Waheshiwa Wabunge wote hapa tuliwatangazia hapa

juzi na wale wa kutoka Mikoa ya kusini ni mashahidi kwamba mkataba wa ujenzi wa barabara hii tuliuufanya tarehe 30 Juni, kwa hiyo, hili limeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Wizara zote kusaidia mkataba wa mafanikio ya kilimo na hoja hii ililetwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga - Mbunge wa Viti Maalum na hili tumesema kwamba kwa kweli sekta ya barabara na uchukuzi kwa ujumla inasaidia sana katika kuendeleza kilimo na uchumi kwa ujumla. Tumetoa mifano kama vile mradi wa *STABEX* pamoja na *RUSMU* ambayo imekuwa ni kielelezo katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni barabara ya Njombe kupitia Itoni mpaka Manda ambayo ni barabara kuu na barabara hii imezungumzwa na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi - Mbunge wa Ludewa kwamba barabara hii imesahaulika na sisi tumesema kwamba sehemu hii ya barabara haikufanyiwa kazi wakati ule na mradi wa *RUSMU* kutokana na upungufu wa fedha za wafadhili, lakini katika mwaka huu wa fedha 2007/2008 sehemu ya barabara hii ilikosa Mkandarasi. Katika mwaka wa fedha huu unaokuja, *TANROAD* Mkoa wa Iringa imeagizwa kuhakikisha kuwa sehemu ya barabara kati ya Ludewa - Manda imefanywa matengenezo na inapitika.

Mchango mwingine ambao ultoka kwa Mheshimiwa Clemence Lyamba - Mbunge wa Mikumi ni kuwa kuna matatizo ya barabara katika maeneo yenye uzalishaji wa chakula katika Wilaya ya Kilosa na kwingineko nchini, kwa hiyo, walikuwa wanahimiza kwamba matatizo haya yaangaliwe na hii ndiyo azma ya Serikali katika matengenezo ya barabara zote na uimarishaji wa miundombinu kuhakikisha kwamba barabara zinapitika ili kuendelea kuimarisha kilimo na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dr. Charles Mlingwa - Mbunge wa Shinyanga Mjini amezungumzia habari ya barabara ya Mwingumbi, Maswa, Bariadi, Lamadi ijengwe kabla ya mwaka 2010. Tumemtaarifu ya kwamba, maandalizi ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami yanaendelea na upembuzi yakinifu umekamilika, kwa hiyo, utaratibu umekwishaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ambayo imeongeleta na Wabunge wengi kidogo na mimi nikiwa ni mdau ni barabara ya Dodoma - Kondo - Babati na ile ya Dodoma - Iringa, barabara hii imeongeleta na Waheshimiwa Wabunge wengi, lakini kwa kweli vinara wamekuwa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma, Iringa na Manyara, wakiongozwa na Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Felister Bura, Mchango wa maandishi wa Mheshimiwa John Malecela, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Degera, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Omar Kwaang' na Mheshimiwa Steven Galinoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona barabara hii ilipata wachangiaji wengi kwa sababu ya umuhimu wake, lakini wameuliza kwamba barabara hii upembuzi yakinifu umeanza siku nyingi na lini sasa itanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu yetu ni kwamba kipande cha Dodoma - Kondo - Babati hadi Mijingu usanifu wa kina ulishakamilika na ujenzi unatarajiwa

kuanza katika mwaka huu wa 2008/2009 kwa sababu zimetengwa shilingi bilioni 12.1 kwa ajili ya kuanza ujenzi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, barabara ya Dodoma, Iringa usanifu na upembuzi yakinifu nao unaendelea. Ukishakamilika, mfadhibili atatafutwa ili nayo ianze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika eneo la vivuko. Mheshimiwa Mohamed Missanga katika eneo hili alishauri kwamba Wizara itenye fedha za kutosha kukamilisha ujenzi wa vivuko vya Utete, Ukerewe, Kisorya na Musoma Kinesi. Ushauri umepokelewa na kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vivuko vipyta vya utete, Ukerewe, Kisorya na Musoma Kinesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili vilevile Serikali ina mkakati gani kuhusu matengenezo ya Kivuko cha Ilagala? Hoja hii ililetwa na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhanywa - Mbunge wa Viti Maalum. Kivuko cha Ilagala kinafanyiwa kazi kwa kutumia injini mbili baada ya injini nyingine mbili kuharibika.

Wakala wa ufundi wa umeme ana mpango wa kufanya matengenezo injini mbili na mitambo ya uendeshaji wa kivuko hicho. Aidha, Serikali inategemea fedha za kununua kivuko kipyta kwenye bajeti ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala kwamba Serikali inunue samani za ofisi kutoka Magereza ambao wamepata ushindi. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Ruth Msafiri asubuhi hii. Wizara imepokea ushauri na itaendelea kuufanya kazi.

Mheshimiwa Zainabu Vullu – Mbunge wa Viti Maalumu pamoja na Mheshimiwa Idrissa Mtulya, habari ya kivuko cha Utete, mkataba wa kuleta kivuko kipyta cha utete ulisainiwa Juni, 2008 kati ya Wizara na kampuni ya *NN Cheap Builders Engineers* ya India na kwa mujibu wa Mkandarasi, kivuko kinatarajiwa kukamilika Juni, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kwamba utengenezaji wa kivuko kipyta cha Kigamboni uharakishwe, hoja hii imezungumzwa na Wabunge kadhaa pamoja na Mheshimiwa Zainabu Vullu, Prof. Mtullya na Mheshimiwa Mwinchoum. Tumepokea ushauri, ujenzi wa kivuko kipyta cha kigamboni unaendelea vizuri na kwa sasa asilimia 70 zimekamilika na kivuko hiki kinategemea kukamilika mwezi Septemba mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kivuko cha Kigamboni, ni abiria wangapi wanavuka kwa mara moja na mapato yanapatikana yanatumikaje? Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliouliza katika eneo hili ni kwamba, kutokana na uwezo wa kivuko cha *MV Kigamboni* kinabeba abiria 800 na *MV Alina* abiria 400. Mapato yanayopatikana, yanatumika kuendesha Kivuko kama kununulia mafuta, vipuli, tiketi na kulipia mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Rished Abdallah - Mbunge wa Pangani, ameuliza kile kivuko tutakachokijenga Pangani kitajengewa wapi? Kivuko kile kitajengewa pale pale Pangani baada ya vifaa kufika kutoka Denmark.

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie katika eneo la reli. Nayapitia maeneo haya kama nilivyokuwa nimesema pale mwanzo kwamba baadhi tu, kwa sababu Mheshimiwa mtoa hoja atakapokuja atajielekeza katika hoja nyingine mahsusni ambazo zinastahili zipate majibu kwa uzito wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Damas Nakei - Mbunge wa Babati Vijiji, ameuliza kwamba Serikali ina mpango gani wa baadaye wa kuunganisha Mikoa yote ya Tanzania kwa njia ya reli, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki inatayarisha mpango kabambe wa uendelezaji wa reli katika nchi za Jumuiya ambazo utazingatia umuhimu wa kuunganisha nchi yetu kwa njia ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusimamia vyema *TRL* ili iweze kutoa na kuboresha huduma zao hapa nchini, Dar es Salaam, Kigoma, ili kupata mizigo ya Rwanda, Burundi na *DRC*, hoja imeletwa na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula wa Bukombe.

Serikali kwa kupitia *RACO* na *SUMATRA* inasimamia Makandarasi kwa karibu zaidi ili kutekeleza mpango wa Kiti Mtu, kuwa na vyoo safi na kuwepo kwa maji kwenye mabehewa na kuhakikisha kuwa *Corridor* za mabehewa ya daraja la kwanza na la pili zinakuwa wazi. Kusema kweli, katika hoja hii, ndiyo inajibu hoja zote ambazo zilikuwa zinazungumzia habari ya msongamano katika treni yetu ya reli ya kati kutoka Dar es Salaam - Morogoro Dodoma - Kigoma mpaka Mwanza. Hii ndiyo mikakati ambayo inaandaliwa ili kuhakikisha tunaondokana na msongamano katika shirika letu la reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TAZARA* imetelekezwa na Serikali za Tanzania na Zambia na inakabiliwa na upungufu mkubwa wa injini na treni, kwa hiyo, shilingi milioni mia moja zilizotengwa kwenye reli ya *TAZARA*, hazitosh, hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba – Mbunge wa Busanda, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi - Mbunge wa Mbozi Mashariki. Ni kweli fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya Wizara kiasi cha shilingi milioni mia moja ni kidogo. Hata hivyo kiasi hiki ni kwa ajili ya ukarabati wa eneo korofii la Mpanga – Uchindire, siyo ununuzi wa injini. Mikakati ya Serikali kufadhili *TAZARA* ni kupitia Serikali ya China ambayo hutoa mikopo ya kuifadhili (*technical support*) kwa wastani wa shilingi bilioni kwa kila miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine katika eneo hili ni ujenzi wa barabara na reli ufanikiwe. Ni vyema ziunganishwe na ujenzi wa bandari na hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama - Mbunge wa Lushoto, ushauri wa Mheshimiwa Balozi Mshangama umezingatiwa na Serikali kwenye mpango wa sekta ya uchukuzi wa miaka kumi (*Ten year Transport Sector Investment Programme*) ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni nauli zinazopandishwa bila mpangilio. Nashauri Wizara husika iangalie suala hili. Mheshimiwa Magdalena Sakaya ndiye mleta hoja hii. Ushauri wa Mheshimiwa Sakaya unazingatiwa na Serikali kuitia mamlaka ya udhibiti yaani *SUMATRA*, itaendelea kuyafanya tathmini na wadau kushirikishwa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo - Mbunge wa Moshi Mjini anashauri Serikali ifufue reli ya kati ya Moshi na Mpakani mwa Kenya kuelekea Mombasa ili kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji kati ya Moshi na Mombasa. Reli ya Kahe na Taveta Mpakani mwa Kenya, itaendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida na *TRL* baada ya kubaini mahitaji ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha - Mbunge wa Morogoro Kusini anaelezea habari ya Stesheni za *TAZARA* ziweze kusaidia kugawa umeme kwa wananchi kwa malipo. Viongozi wa *TAZARA* waliposikia hili, wameondoa *generator* kubwa, wameleta *generator* ndogo. Hii hoja ilichangiwa wakati wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kulikuwa na *generator* mbili kwenye Stesheni ya Kisaki. *Generator* zote hizi mbili ni mbovu na *generator* moja limepelekwa karakana ya Dar es Salaam kwa matengenezo. Matengenezo hayo yameshindikana kwa sababu *model* zake ni za zamani na vipuri vyake havipatikani hadi sasa. *Generator* hiyo bado iko karakana ya *TAZARA* Dar es Salam, *repair* zikishakamilika litarudishwa Kisaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni Serikali ifikirie njia mbadala ya kwenda Kigamboni kama vile *over head trains*. Huu ni mpango wa muda mrefu, Serikali itaendelea kuutafakari kadri uwezo wa fedha utakavyokuwa unapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jackson Makweta, anapendekeza Serikali ifufue na kuimarisha usafiri wa reli. Hilo nalo tumelizingatia kama tulivyokuwa tumeeleza huko nyuma.

Mheshimiwa Diana Chilolo kusimama kufanya kazi kwa treni ya Dodoma - Singida na kutojali huduma muhimu, Serikali inawaomba radhi wananchi wa Singida kwa kusimamishwa kwa muda huduma hii muhimu kutokana na ajali. Hata hivyo, mkandarasi ameahidi kwamba huduma ya treni ya abiria ya Dodoma na Singida itaanza tarehe 9 Julai, 2008. Kwa hiyo, huduma hii itarejeshwa na sisi kama Serikali tutahakikisha tunasimamia ahadi hii kama Mkandarasi alivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwanne Mchemba alizungumzia juu ya utekelezaji wa ahadi wa kuongeza huduma ya treni kutoka mbili hadi nne utekelezwe haraka na Serikali isimamie. Hili nalo tunaahidi tu kwamba totalisimamia kadri ambavyo Mheshimiwa ameshauri. Vilevile amezungumzia habari ya chakula kwenye treni; hizi huduma zote ndani ya treni nataka tu tuwahakikishie kwamba kwa sababu Serikali sasa hivi ipo karibu sana na usimamizi wa Shirika la Reli na huduma nyingine zote za usafiri

tutaendelea kuzisimamia kwa karibu na kuhakikisha kwamba wananchi wanapunguziwa kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabehewa chakavu yalikuwa yamehifadhiwa karakana, yaani *local ferry* ya Tanga, hayaonekani na hayajulikani yalipo: Je, *TRL* imeyapeleka wapi? Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Bafadhili - Mbunge wa Viti Maalum. Mabehewa hayo yaliyokuwa mabovu katika karakana ya reli ya Tanga yamekarabatiwa mengine wakati wa *TRC* na mengine yalipokelewa karakana kuu ya Dar es Salaam ambayo yamefanyiwa marekebisho ili yaweze kubebea *Klinker* na kukokota na kujenga matuta ya reli. Lakini mabehewa hayo yapo siyo kwamba yamepotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika eneo la usafiri wa anga. Hoja imetolewa katika eneo hili kwamba kiwanja cha ndege cha Tanga kilijengwa muda mrefu sana na majengo yamechakaa, Serikali iboreshe kiwanja cha Tanga ili kionekane kinakwenda na wakati. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Nuru Bafadhili. Serikali kupitia mamlaka ya viwanja vya ndege itaboresha majengo ya viwanja vya ndege, itaboresha majengo ya kiwanja cha ndege cha Tanga katika mwaka huu wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Prof. Philipo Banyikwa, alichangia kwamba wananchi wa Ngara wanaomba uwanja wa ndege wa Ruguzu kule Ngara, upanuzi wa miundombinu ya kiwanja utatokana na mahitaji ya wananchi huko Ngara. Eneo lingine, ni kwa nini *traffic* ya ndege kwenye viwanja vyetu ni ndogo?

Mheshimiwa Mch. Getrude Rwakatare alisema ongezeko la abiria na mizigo katika sekta ya usafirishaji inategemea mahitaji na uwezo wa watumiaji wa huduma. Kwa upande wa usafiri wa anga hapa nchini huduma hii bado ni ghalii kilinganishwa na uwezo wa watumiaji wengi, wengi wanatumia usafiri wa aina nyingine ambaa ni nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Deodoras Kamala alichangia kuhusu kujenga kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Umukwanjukuti kwamba, Serikali isaidie kuharakisha ujenzi wa kiwanja hicho. Umukwanjukuti, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea na taratibu za kupata miliki za eneo la ujenzi wa kiwanja hicho na taratibu na mipango na mchakato utaendelea kutazamwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge zaidi ya mmoja ambaa ni Mheshimiwa Jadi Kadika - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mariam Mfaki - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Felister Bura - Mbunge wa Viti Maalum ni juu ya kiwanja cha ndege cha Dodoma kwamba ni kidogo na kipo katikati ya Mji na hakiridhishi. Kama Serikali ina nia ya kutafuta kiwanja kingine, ni vizuri, lakini ujengwe uwanja mkubwa. Vile vile, hapa limeulizwa swali juu ya fedha shilingi bilioni 1.6 zilizotolewa, ni kwa ajili gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kiwanja cha Dodoma ni kidogo na kipo katikati ya Mji. Serikali kwa kuona hivyo, imeamua kujenga kiwanja kikubwa katika eneo la Msalato. Benki ya *BADDA* imetoa msaada wa dola 440,000 kwa ajili ya upembizi yakinifu na usanifu wa awali. Kazi inategemewa kumalizika mwisho wa

mwaka huu. Aidha, shilingi bilioni 1.6 zimetengwa kwa ajili ya fidia katika mwaka huu wa 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja cha Kigoma ni muhimu. Hili limeongelewa na Mheshimiwa Switi pamoja na Mheshimiwa Kilonsti Mporogomyi na Mheshimiwa Switi alikuwa ameshauri kwamba ni muhimu kuweka mashine za kisasa kuchunguza mizingo kama ilivyo katika viwanja vingine. Mashine za *X-Ray* zimenunuliwa na hivi sasa ziko njiani kupelekwa Kigoma tayari kwa kutumika kwa kupekulia abiria na mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga pamoja na Mheshimiwa Teddy Kasela Bantu wameongelea habari ya uwanja wa Tabora na umuhimu wake. Tumejibu tu kwamba uwanja huu uko katika msaada wa *World Bank* na utaendelea kujengwa, upembuzi yakinifu utakamilika Oktoba, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu niseme kwa ujumla kwamba, kama nilivyokuwa nimesema pale mwanzo kwamba hoja zilizokuja ni nyingi na karibu zote zinalenga kero mbalimbali ambazo zinasibu wananchi katika sekta hii ya Miundombinu na kama nilivyokuwa nimesema, tutajitahidi kwa kadri itakavyowezekana kwa yale ambayo yapo chini ya uwezo wetu kifedha yaweze kupatiwa ufumbuzi. Lakini ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwa na uhakika wa yale tuliyoyasema, kama nilivyosema, kwa sababu ya ufinyu wa muda, basi yale yote tutayaandika na kuwawasilishia ili hata kama ni kufuatailia iwe ni rahisi kwa kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naomba niishie hapa na nirudie tena kusema kwamba naunga mkono hoja na ninaomba na wenzangu wote tuiunge mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwako wewe mwenyewe pamoja na Mwenyekiti - Mheshimiwa Jenister Mhagama kwa jinsi mlivyo simamia majadiliano ya Wizara ya Miundombinu kwa siku hizi mbili. Pia nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu - Mheshimiwa Mohamed Missanga kwa maoni aliyoyatoa ambayo yatasaidia kwa kiasi kuboresha sekta hii katika siku zijazo. Aidha, namshukuru kiongozi wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa maoni na mapendekezo yake kuhusu bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa majadiliano ya hotuba ya Waziri wa fedha na uchumi, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 50 walitoa michango yao kuhusiana na sekta ya Miundombinu. Aidha, wakati wa majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge 52 walichangia hoja hiyo kuhusu sekta ya miundombinu. Kwa ujumla michango ya Waheshimiwa Wabunge kwa bajeti hizi mbili ililenga maeneo makuu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la barabara Wabunge 77, Viwanja vya Ndege, Waheshimiwa Wabunge 10; eneo la Bandari, Waheshimiwa Wabunge tisa; Reli,

Waheshimiwa watatu; Vivuko, Mheshimiwa Mbunge mmoja; *SUMATRA*, Mheshimiwa Mbunge mmoja na *ATCL*, Mheshimiwa Mbunge mmoja.

Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa tutazingatia sana ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nitatoa ufanuzi kwa yale ambayo nitamudu kuyatolea ufanunuzi ndani ya muda wa majumuisho ya hoja yangu hii. Michango ya Waheshiiwa Wabunge, iliyotolewa kwa ajili ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa ile ambayo sitawenza kuitolea ufanuzi hapa, basi niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba ufanuzi wa hoja zote hizo tutawakilisha Bungeni kwa maandishi ili kila aliyechangia aweze kupata majibu ya hoja yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao waliyotoa kwa maandishi na kuzungumza hapa Bungeni wakati wakijadili hoja ya Wizara yangu. Michango hii ni mizuri na itatusaidia sana katika usimamiaji wa bajeti hii pamoja na kuboresha sekta hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge, ambao wamechangia kwa kuzungumza hapa Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa *Capt.* John D. Komba, Mheshimiwa Abdulkarim I. Shah, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa *Brig.* Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Florence S. Kyendesya, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanywa, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Dr. Zabein M. Mhita, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Dr. Lucas J. Siyame, Mheshimiwa Benito Malangalila na Mheshimiwa Felister A. Bura. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Teddy L. Kasella - Bantu, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Kilontsi M. Mpologomyi, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Athumanji S. Janguo, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa John M. Cheyo na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwatambue waliochangia kwa maandishi katika hoja yangu hii, nao ni kama ifuatavyo na baadhi ya hao waliochangia kwa maandishi walichangia pia kwa kuzungumza. Nao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Mercy Emmanuel, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa *Dr.* Maua Daftari, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa *Dr.* Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Mwanne Mcemba,

Mheshimiwa John Malecela, Mheshimiwa Fred Mpandazoe, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Fatma Ali, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama na Mheshimiwa Mohamed Soud. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Dr. Deodorus Kamala, Mheshimiwa Shoka J. Khamis, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Hemed Hemed, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Lucas Selelili, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Aloyce Kimaro na Mheshimiwa James Lembeli. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Omar Nibuka, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Magalle Shibuda, Mheshimiwa Profesa J. Maghembe, Mheshimiwa Tom Ntimizi, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Juma Omar, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa John Chiligati, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Kabuzi Rwiomba, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Dr. Getrude Lwakatare, Mheshimiwa Profesa Feetham Banyakwa, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa na Mheshimiwa John Shibuda. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Hamad Mohamed Rashid, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Silaju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Ali Seif, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Mohamed Aziz na Mheshimiwa Hamad Mohamed Rashid. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Mkiwa Kimwaga, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Paschal Degera. Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Mgeni Kadika, Mheshimiwa Al-Shymaa J. Kwegyir, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy na Mheshimiwa Ussi Pandu. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Zuleikha Haji, Mheshimiwa Salim Khamis, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Bahati Abeid, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Col. Feteh Mgeni, Mheshimiwa Stephen M. Wasira, Mheshimiwa

Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Thomas Mwang'onda, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani nimemsahau Mheshimiwa Diana M. Chilolo dada yangu mpendwa.

Naomba nichukue nafasi hii kusema kama nitakuwa nimemsahau Mheshimiwa Mbunge yejote ambaye alichangia, basi aniletee tu tutakapomaliza nitawataja majina yao, ilikuwa kidogo kazi ndefu na ngumu kwangu mimi pamoja na wenzangu watalaan katika kuyaweka majina haya sawa na pia niombe radhi kwa wale ambaa sikutamka majina yao vilivyo au kwa usahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wabunge wengi walivyokwishaelekeza nyanja za barabara, reli, usafiri wa majina vivuko na usafiri wa anga, ni nguzo muhimu sana katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta maisha bora kwa wananchi wote. Hiyo ndiyo maana michango ya Wabunge, imekuwa mingi katika hoja hii ya bajeti ya Wizara yangu.

Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imepokea kwa moyo mkunjufu na tutalifanya kazi michango yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na itakuwa dira yetu katika utendaji wa kazi wa kila siku. Nina imani kwamba tutaendelea kushirikiana vizuri na Bunge lako Tukufu kuititia Kamati ya Bunge ya Miundombinu na hata baada ya vikao hivi vya Bunge katika kuboresha na kuimarisha sekta hii muhimu ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ufanuzi kidogo katika maoni ya Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu wakati wakiwasilisha maoni ya Kamati yako alisitisiza utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ulipaji wa madeni ya makandarasi, kufungua sehemu za Kusini Magharibi kwa barabara za kudumu, kukamilisha sera ya ushirikishaji sekta binafsi ama *PPP*, kujenga barabara za Manyoni, Itigi na Tabora, ujenzi wa barabara chini ya *MCC* uharakishwe, fedha za barabara zitolewe kabla ya mvua kunyesha, zoezi la bomoa bomoa liendeshwe kwa umakini, wakandarasi wazalendo wapewe upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwa niaba ya Kamati, ameshauri kwamba hatua zichukuliwe kwa watendaji wanaoingia mikataba mibovu na mishahara na marupurupu ya *TANROADS* yaboreshwe. Nakulibana kabisa na ushauri wa Kamati ya Miundombinu na kama nilivyoeleza katika hotuba yangu sehemu (b) ukurasa wa 3 hadi wa 11 pamoja na ufinyu wa bajeti, Wizara yangu itajitahidi kutekeleza kwa ukamilifu Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kama nilivyozungumzia changamoto za kukamilishwa sera ya ushirikishwaji wa sekta binafsi ama *PPP*. Wizara itasimamia na kuharakisha sera hii ambayo itatoa mchango mkubwa katika ujenzi wa barabara na njia nyingine za usafiri kama ambavyo tutajitahidi ikamilishwa ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sera ya ushirikishwaji sera binafsi Serikali itabuni mikakati mbalimbali ya kusaidia sekta kuhakikisha kwamba tunatekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya makandarasi ushauri huu tumeuzingatia na bajeti yetu ya mwaka 2008/2009 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 190 kwa ajili ya kulipa madeni hayo. Tuondokane na madeni haya tuingie katika mwaka mpya wa fedha 2008/2009 tukiwa na ukurasa mpya kufanya kazi na makandarasi kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya ili tuweze kuweka miundombinu mizuri kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itaendelea kuwa makini katika zoezi zima la bomoa bomoa na kwamba tutaandaa nyumba za wananchi, mali za wananchi, zilizo kwenye hifadhi za barabara kwa kuzingatia taratibu na kanuni na sheria zilizopo. Pia Wizara imeshaanza kushughulikia mishahara na marupurupu ya watumishi wa *TANROADS* kama vile ambavyo kamati imeshauri.

Kwa upande wa reli ya kati, Kamati ilizungumzia kuhusu kujenga Reli ya Tanga hadi Musoma na kufufua reli ya Dar es Salaam Tanga hadi Arusha. Mpango uliopo ni kuongeza uzito wa reli ya Tanga hadi Arusha kufikia ratili 95 kwa yadi moja na upana wa *1,435 mm* kutoka upana wa sasa wa *1,000 mm*. Aidha, ujenzi wa reli ya kutoka Arusha hadi Musoma ni moja kati ya miradi iliyomo kwenye mipango kabambe wa reli ya Afrika Mashariki. Serikali pia inatarajia kujenga reli ya Arusha hadi Wosiwosi - Arusha hadi Minjingu, kwa ajili ya usafirishaji wa mbolea ya *Phosphate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu reli ya *TAZARA* Kamati imeshauri Serikali kuunganisha reli kutoka Tunduma hadi Bandari ya Kasanga na kwamba Serikali ifanye rejea ya makubaliano ya sheria ili uongozi wa juu wa *TAZARA* uwe wa mzunguko. Ni kweli kuwa uongozi wa juu wa *TAZARA* unatokana na sheria iliyounda *TAZARA* sheria Na. 4 ya mwaka 1995 kifungu namba 14(1) sheria hiyo itafanyiwa mapitio na tutafanya hivyo kabla utaratibu wa ukodishwaji wa *TAZARA* kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu aliongea pia kuhusu masuala muhimu mawili yanayohusu usafiri wa majini na uendelezaji wa bandari nchini. Serikali kupitia *SUMATRA* inaendelea kutekeleza sheria ya usafiri majini ama *Merchant Shipping Act* ya mwaka 2003 inayosimamia usalama wa vyombo majini, kanuni mbalimbali zimeendelea kutengenezwa na kutekelezwa katika kukabiliana na tatizo la ajali. Ukaguzi wa vyombo vya majini umeendelea kufanyika na vyombo visivyokidhi ubora utakaotakiwa vitachukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria na vimeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria. Ofisi za *SUMATRA* kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa majini sasa vimeanzishwa kwenye Mikoa mingi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine katika sekta ya majini ambalo Mwenyekiti wa Kamati aliligusia ni lile eneo la kuboresha bandari zetu. Bandari ni moja ya maeneo muhimu katika kuendeleza uchumi wa nchi kwa ujumla, katika kuzingatia hili

Serikali kupitia mamlaka ya Bandari inatekeleza mpango kabambe wa maendeleo ya bandari ama *Ports Master Plan Study* kwa ajili ya bandari za mwambao na zile bandari za maziwa. Utafiti huu utakamilika mwezi Desemba, 2008 na utekelezaji wake utaanza rasmi Januari, 2009.

Tanga ni moja ya Bandari zilizomo kwenye mpango huo na ili kuimarisha zaidi Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kujenga bandari mpya yenye kina kirefu sehemu za Mwambani huko Tanga ili kukidhi ongezeko la mizigo na pia itumike na meli kubwa zitakazohudumia biashara ya ndani na biashara ya nje ya nchi.

Kuhusu uendelezaji wa bandari ya Bagamoyo, Serikali kupitia mamlaka ya Bandari Tanzania imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bandari mpya ya Bagamoyo kwa hatua za awali. Hatua iliyofikia ni kukamilisha *GO technical survey* kwa lengo la kubaini eneo zuri kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo. Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ni sehemu ya upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na tunalichukulia katika mtazamo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitaka Serikali itoe fedha za kutosha ili kujenga viwanja vya ndege hapa nchini, kuandaa mpango wa muda mfupi na muda mrefu wa kujenga viwanja vya ndege nchini pia kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kiimarishe ili *Terminal Two* iwe kwa usafiri wa kimataifa na *Terminal One* iwe kwa usafiri wa ndani. Serikali iandae mazingira mazuri ya kuwezesha huduma ya viwanja zinapatikana kwa ushindani baada ya ukiritimba wa *Swiss Port* kumalizika mwishoni mwa mwaka 2008.

Serikali pia itoe fedha za fidia kwa wananchi wa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila. Serikali tayari imeandaa mpango wa miaka kumi wa kuendeleza miundombinu na viwanja vya ndege, ni moja kati ya miundombinu muhimu ambayo imewekwa katika mpango huo. Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mpango wa Serikali ni kuimarisha kiwanja cha ndege hicho kwa kujenga *Terminal Two* na kujenga jengo jipya la abiria la *Terminal Three*. Baada ya kukamilika *Terminal Three* itakuwa ni matumizi ya safari za kimataifa, ama *international flights* na *Terminal Two* itakuwa ni kwa matumizi ya safari za ndani ama *domestic flights*. *Terminal One* itatumika kwa ajili ya *general aviation and low cost carriers* ni matumizi ya usafiri wa anga wa kawaida na wasafiri wa gharama nafuu.

Katika mwaka 2008/2009 Serikali haikuweza kutenga fedha kwa ajili ya fidia kwa wananchi wa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila. Lakini Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hili ili fedha zipatikane. Moja ya njia ya kupata fedha ni kuishirikisha sekta binafsi na hivyo tutalifuatilia kwa karibu na kwa umakini. Tayari tuna maongezi na sekta binafsi ambayo imejitokeza au mashirika machache ambayo yamejitokeza kuonyesha nia ya kufanya hivyo. Baadhi yao hawakuonyesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya kulipa fidia, lakini pengine wangependa kuingia moja kwa moja katika ujenzi wa miundombinu. Hili ni gumu kwa vile hatutaweza kuingia katika ujenzi kabla hatujaweza kulipa fidia.

Kuhusu ukiritimba wa huduma, Serikali kupitia mamlaka ya usafiri wa anga, *TCAA* imemwajiri mtaalam ama *consultant* ambaye anafanya tathimini ya kuondoa ukiritimba katika huduma za ndege (*ground handling*). Kazi hii tunaitegemea itakamilika Septemba, 2008 na itaainisha mahitaji ya kukamilika kuondoa ukiritimba katika viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia iliitaka Serikali iangalie upya mishahara na marupurupu ya marubani na wahandisi wa ndege ili kuondoa tatizo la kuwaacha ama kuondoka kwa marubani na wahandisi wa ndege na Serikali itoe fedha shilingi bilioni tano kwa ajili ya matengenezo ya ndege za Serikali ili kuimarisha usalama wa viongozi wetu. Serikali imekuwa ikipitia marupurupu ya watumishi wa Wakala wa Ndege za Serikali na kuzifanyia marekebisho kwa kadri ya uwezo wa Serikali. Mishahara na marupurupu ya watumishi wa Wakala wa Ndege za Serikali yamerekeblishwa kuanzia tarehe 1 Julai, 2008. (*Makofî*)

Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Usalama wa Anga imeanzisha Mfuko wa Mafunzo ya Marubani ili kuwawezesha vijana wa Tanzania kujifunza fani hizo muhimu hususan mwaka 2008/2009. Serikali imetenga shilingi bilioni 8.9 kwa matumizi ya Uwakala wa ndege za Serikali. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni tatu zitatumika kwa matengenezo ya ndege za Serikali. Katika usafiri wa njia za anga, Kamati iliitaka Serikali isawazishwe mizani ya *ATCL* ili iwavutie wawekezaji na kutoa fedha za kutosha kwa *ATC L* ili itimize majukumu yake. Pia Serikali itilie mkazo mafunzo ya taaluma za Rubani na Wahandisi wa ndege na wahudumu wa ndege. Serikali inakubaliana na hoja ya Kamati kuhusu kusawazisha mizani ya *ATCL* na itaendelea kutoa fedha kwa *ATCL* kulingana na uwezo wa Serikali katika bajeti yake. Kwa sasa Serikali inaendelea na mazungumzo na Sekta binafsi ili ziweze kununua hisa za Serikali ndani ya Kampuni ya *ATCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa niaba ya Kambi ya Upinzani alizungumza masuala ya reli ya kati hususan ulanguzi wa tiketi. Aidha, Kambi ya Upinzani pia ilihoji kuhusu uuzzwaji kiholela wa *Club* ya Reli ya Gerezani na wizi wa mataruma ya reli yaliyokutwa kwenye kiwanda cha kuyeyushia vyuma na mengine kadhaa ambayo Kambi ya Upinzani imehojoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuyarudia katika mtiririko wake, naomba nitoe ufanuzi katika haya yafuatayo:- Kuhusu ulanguzi wa tiketi, naomba nikiri kwamba ni kweli lipo tatizo hili ndani ya *TRL* na Serikali imekwishaigiza *TRL* kuweka utaratibu mzuri wa kukata tiketi za daraja la tatu. Kwa stesheni ya Kigoma, Serikali imeagiza *TRL* kurudisha utaratibu wa zamani ambapo nafasi huhifadhiwa kwa ajili ya wasafiri wanaotoka katika maeneo mbalimbali kama vile Kasulu na Kibondo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Club* ya Gerezani haijauzwa, bali majengo ya *Club* hiyo yamekodishwa kwa mwekezaji mwenye Hoteli ya *Paradise* ya Mjini Bagamoyo. (*Makofî*)

Kuhusu mataruma na kuhusu mataruma yaliyokutwa kwenye kiwanda cha kuyeyushia vyuma, mataruma hayo yalikamatwa ndani ya kiwanda hicho na mpaka sasa yapo chini ya ulinzi wa Polisi kwenye Kituo cha Kurasini na yatatumika kama kielelezo cha watuhumiwa wanne ambao wamekamatwa. (*Makofi*)

Msemaji wa Kambi ya Upinzani pia aliongelea masuala ya makuu mawili katika eneo la Bandari zetu. Masuala hayo ni kuitumia Bandari ya Mtwara kuhifadhi mazao kwa ajili ya kuuza nje ya nchi na matumizi ya bandari kavu ya Kigoma-Isaka na Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ni kiungo cha kuwezesha kupitisha mizigo kwenda ndani na nje ya nchi. Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imenunua eneo karibu na Bandari ya Mtwara kwa ajili ya kuendeleza shughuli za biashara ya nje ama *Export Processing Zone* ambapo maghala yanaweza kujengwa. Serikali inawahamasisha wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje kuwekeza katika Bandari ya Mtwara na *EPZ*. Tayari baadhi ya wawekezaji wameonyesha nia ya kufanya hivyo na sasa Serikali inafanya mchakato wa kupitia na kuchambua miradi yenyе tija kwa Taifa ili iweze kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia ilitaka kupata maelezo ya kina kuhusu ununuzi wa ndege za *ATCL* hususan *Boeing 757200* na *Boeing 737300* ambazo zilinunuliwa bila kuzingatia maslahi ya Kampuni na pia ufanyike uhakiki wa mali za *ATCL* ambazo ziliuzwa na *Air Tanzania Holding Company*. Mali hizo ni nyumba za Harare, Lusaka, Comoro na kadhalika. *ATCL* ilikodi ndege mbili na siyo ndege nne za *Boeing 737200* na wala haikununa ndege hizo kama Kambi ya Upinzani ilivyolezea. Ndege hizo zilikodishwa kwa utaratibu wa *dry release* kwa gharama za *dollar* za Kimerakani 50,000 kwa mwezi kwa kila ndege kwa muda wa miaka miwili kuanzia mwaka 2006. (*Makofi*)

Utaratibu uliotumika ni wa kupata *quotations* kutoka kwa Makampuni mbalimbali na baada ya ulinganisho ndege kutoka *SIETICO Corporation* zilioneckana kwamba ni ndege zilizokuwa na unafuu na ndiyo maana *ATCL* ikakodi ndege hizo. Nadhani utakubaliana nami kwamba ndege hizo zimeendelea kutumika tangu mwaka 2006 bila ya matatizo makubwa mpaka mwaka huu 2008 ambapo tunatarajia Mkataba wake wa ukodishaji kufikia ukomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mali za *ATCL*, ni kweli kwamba lililokuwa Shirika la Ndege la Tanzania (*ATC*) lilikuwa na nyumba kwa ajili ya wafanyakazi wake katika Miji ya Kampala, Nairobi, Lusaka, Harare Jonesburg, wakati Shirika lilipobinafishwa mwaka 2002 nyumba hizo zilikabidhiwa kwa Kampuni ya *Air Tanzania Holding Corporation* ili iuze na fedha zitakazopatikana zisaidie kulipa madeni ya iliyokuwa *ATC*. Suala la kuhakiki uuzwaji wa mali hizo tutalitazama upya. Tutalihakiki, tutalizama upya ili kuona kwamba nyumba hizi ziliuzwa kwa taratibu ambazo zilikuwa zimewekwa na kama kutakuwa na kasoro yoyote, basi Serikali itachukua hatua muafaka kwa wale wote ambao watakuwa wamehusika na ukiukwaji huo wa taratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia ilitaka tozo kwa abiria ama *passenger service charge* ipelekwe *TAA* kwa asilimia 100 ili kuboresha viwanja vya ndege na kiwanja cha Julius Kambarage Nyerere kiimarishe ili *Terminal One* iwe kwa ajili ya abiria wa ndani na *Terminal Two* iwe ni kwa ajili ya abiria wa Kimataifa. Serikali ifanye ukarabati wa Viwanja vya Ndege ili vitumike kwa Kombe la Dunia la mwaka 2010 wakati wa maandalizi ya Timu zitakazoshiriki katika mashindano hayo. Kambi ya Upinzani pia imeishauri Serikali iondoe ukiritimba wa *Swiss Port* ili pawepo na ushindani kwenye Viwanja vya Ndege.

Serikali italiangalia kwa makini suala hili na suala la *TAA* kupatiwa asilimia 100 ya tozo la *passenger service charge*, ni suala ambalo tayari lilikuwa kwenye mchakato na tutaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi kuhusiana na suala hili ili tufikie mahali ambapo tutaiwezesha *TAA* kuendesha shughuli zake kwa ubora zaidi kwa kuwa na rasilimali na fedha nyingi zaidi. (*Makofî*)

Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mpango wa Serikali ni kukiimarisha kiwanja hicho. Kama nilivyooleza hapo awali kwamba, *Terminal II* tutajenga pamoja na kujenga jengo jipya la *Terminal III*. Baada ya kukamilika *Terminal III* itakuwa kwa matumizi ya safari za kimataifa na jengo la *Terminal II* litakuwa kwa matumizi ya safari za ndani. *Terminal I* itakuwa kwa ajili ya *General Aviation* na *Low Cost Carriers* kama nilivyoongea awali.

Kuhusu matayarisho ya Kombe la Dunia, tunasema kwamba, viwanja vya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Kiwanja cha KIA na Zanzibar, vina uwezo wa kuhudumia timu ambazo zitataka kutumia viwanja vya Tanzania kwa mazoezi wakati wa Kombe la Dunia. Changamoto kubwa ni kuwepo kwa viwanja vya kufanyia mazoezi ambavyo ni vizuri na hoteli za kukaa wachezaji wakati wa mazoezi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia ilipendekeza matumizi ya Bandari Kavu za Kigoma, Isaka na Mbeya ili kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam ifanyike. Serikali tayari inalifanya kazi suala hili; haikuanza sasa, haikuanza leo wala jana, tayari Serikali tunalifanya kazi suala hili ili kutumia bandari kavu kusaidia kupunguza msongamano ya makasha uliopo ndani ya Bandari ya Dar es Salaam. Serikali kuititia wadau mbalimbali wa bandari kama vile Wizara yenewe ya Miundombinu, *TPA*, *TRA*, Wakala wa Mizigo na Wakala wa Meli na wengineo, wapo katika hatua za mwisho za kuanza kutumia Bandari Kavu ya Isaka kwa ajili ya kuhudumia mizigo ya Burundi na Rwanda na Bandari Kavu ya Mbeya kwa ajili ya kuhudumia Malawi na Zambia. Kwa upande wa Kigoma, Serikali itaendelea kuimarishe na kuboresha huduma za Bandari za Kigoma na Kasanga kwa ajili ya kuhudumia mizigo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo ama DRC.

Mheshimiwa Spika, nitoe ufanuzi kidogo katika hoja za Wabunge kwenye Sekta ya Barabara. Baada ya kutoa maelezo kuhusu hoja za Kamati ya Miundombinu na Kambi ya Upinzani, sasa naomba nitambue michango ya wale Wabunge waliochangia hoja yangu na hoja zilizolezwu kwenye Sekta ya Barabara. Nitaanza na mchango wa

Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi nyingi alizotupa Mheshimiwa Missanga, pia ametupa ushauri na changamoto nyingi ambazo tutazizingatia. Waheshimiwa Wabunge, waliochangia katika hoja hii kama nilivyosema awali ni wengi na itakuwa vigumu kuwapa ufanuzi au majibu mmoja mmoja kwa ukamilifu wao. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, amejaribu kwa kiasi kikubwa kuipitia michango hiyo. Naomba nirudie kwa baadhi ya michango hiyo. Katika eneo la ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, ambapo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelisemea kwa sauti kubwa, kwa hisia nzito na kwa manung'uniko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika hotuba yangu, barabara zote za vipaumbele zimejumuishwa kwenye Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Uchukuzi ama *TSIP*. Aidha, baadhi ya barabara hizo zinatekelezwa au maandalizi ya utekelezaji wake yameanza. Serikali itajitahidi kwa kadiri ya uwezo wake, kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo kwa njia mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezipendekeza. Niseme kwamba, kati ya barabara hizo zimo hizi ambazo zimesemewa kwa hisia nzito kama Barabara ya Musoma - Foti Ikoma. Bunda - Ikizu - Foti Ikoma. Iringa - Dodoma - Babati - Minjingu. Sumbawanga - Mpanda - Kanyani - Nyakanazi - Kyaka - Bukene - Mulongo - Manyoni - Itigi - Tabora - Kigoma. Masasi - Tunduru - Namtumbo - Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamehimiza barabara nyingi zilizoko katika ngazi ya Wilaya na Vijiji vipandishwe kuwa Barabara za Mkoa ambazo zitahudumiwa Kitaifa. Hadi sasa tumeshapokea maombi ya kupandisha hadhi Barabara za Wilaya zipatazo urefu wa kilomita 8,642 kupandishwa hadhi kuwa Barabara za Mikoa na jumla ya kilomita 2,798 Barabara za Mikoa kuwa Barabara Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wizara ipo katika mchakato wa kutengeneza Kanuni za Sheria ya Barabara ya 2007. Kanuni hizo zitaweka wazi zaidi vigezo vyta Sheria na kurahisisha utekelezaji wa zoezi la kupanga barabara zote nchini kwenye madaraja yanayostahili. Zoezi la kupandisha barabara litafanywa sambamba na kupitia upya mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara kutoka kima cha sasa cha asilimia 70 kwa 30 kwenda kwenye kima ambacho kitakuwa ni cha muafaka kufuatana na barabara hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge walipendekeza Serikali kujenga barabara na kuhakikisha ujenzi wa barabara nchini kwa njia ya kutafuta fedha toka mashirika ya fedha yanayotoa mikopo ya muda mrefu. Naomba niseme kuwa, ushauri huu umepokelewa na Serikali na itaufanya kazi kwa makini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mahitaji makubwa ya fedha za ujenzi wa barabara katika sehemu zote za nchi, fedha zinazotengwa katika bajeti nina uhakika hazitoshelezi. Hivyo, Serikali imeshaanza kuchambua fursa zinazojitokeza kama vile kutumia *cosessions*, mikopo ya muda mrefu, taratibu za ukodishaji na kushirikisha sekta

binafsi. Serikali inaendelea kuchambua fursa hizo zote na kuzainisha katika Sera Maalum. Tayari mafunzo ya *Public Private Partnership* yameanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kinyume cha Sheria ya Barabara kujenga ndani ya Hifadhi ya Barabara bila ya kuwa na kibali. Sheria hii inaruhusu kubomolewa kwa jengo au kitu chochote kilichopo katika Hifadhi ya Barabara. Hata hivyo, ambapo ujenzi utafanyika, wananchi watalipwa fedha endapo barabara itakuwa imewafuata katika maeneo yao. Pale ambapo barabara itakuwa imefuata wananchi, wananchi hao watakaobomolewa barabara zao watalipiwa fidia. Najua hii ni kero kubwa sana. Kuna wakati mwagine ambapo barabara imewafuata watu, wakati watu ndio waliotangulia pale barabara ikafuata nyuma. Palipofanyika makosa, Serikali imechukua taratibu za kurekebisha na tutakapoendelea katika zoezi hili, Serikali itahakikisha kwamba, zoezi hili linafanywa kwa umakini. Kila ambaye barabara itakuwa imemfuata, basi alipwe na wala asifanyiwe bugudha na pengine alipwe kwanza kabla barabara haijajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana ndugu yangu, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, kwa kutukumbusha wajibu wetu. Kwa mwaka 2008/2009, tuna fedha kwenye bajeti za kuwalipa Wananchi wa Kamwanga kwa upande wa Barabara ya Longido –Kitumbe - Longai na hii ipo kwenye mpango wetu. Hiyo ni Barabara ya Mkoa na *TANROAD* tutaendelea kuihudumia. Kuhusu Barabara ya Olmotonyi - Namanga hiyo ipo kwenye mpango wa kuhudumiwa na *TANROAD*, tutaendelea kushirikiana kuhakikisha kuwa Wizara inaendelea kutimiza ahadi zake bila upendeleo.

Mheshimiwa Nimrod Mkono, alitaka apatiwe ufanuzi kuhusu Barabara ya Musoma - Foti Ikoma; ina urefu gani na lini itajengwa kwa kiwango cha lami. Napenda kumfahamisha kuwa, barabara hii ina urefu wa kilomita 135 na usanifu wa kina kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami hivi sasa umekamilika. Hatua inayofuata ni kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Benito Malangalila, *Mnyalukolo* mwenzangu, alieleza kuwa barabara zake zipo katika hali mbaya na kwamba zinahitaji matengenezo. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara zote alizozitaja zimeanza kufanyiwa matengenezo baada ya mvua kwisha. Aidha, kwa Barabara ya Mbalamaziwa, Tanga, mkandarasi aliyepewa kazi hiyo anakaribia kuanza matengenezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Iringa - Dodoma – Arusha nayo itajengwa katika kiwango cha lami. Aidha, kipande cha Barabara ya Dodoma - Babati hadi Minjingu usanifu wa kina umekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka 2008/2009. Wakati mwagine inachukua muda mrefu wa kufanya upembusi yakinifu na usanifu wa kina. Kazi hii siyo nyepesi ni ya kitaalamu na ili ujenzi uwe kamili, upembusi lazima uwe yakinifu na usanifu ama *design* lazima uwe bora. Ni sawa sawa na ujenzi wa nyumba tu, bila *architecture* nzuri na bila *structure*, *engineer* mzuri ambaye atacheki *structure* ya jengo hilo atasema jengo linaweza likaporomoka. Kwa maana hiyo, kazi hizi lazima zifanywe kwa umakini na kwa utaratibu ili ujenzi wa barabara hizi uwe kamili. (*Makofi*)

Ndugu yangu Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, alieleza kutokuridhishwa kwake na kilomita chache za lami zilizopewa barabara ya Kyaka - Bugene mpaka Kasulu. Napenda kumfahamisha kwa unyekekevu kabisa kuwa, juhudzi za kujenga barabara hiyo zilianza katika mwaka 2004/2005, ambapo kilomita kumi zilijengwa kwa kiwango cha lami nyepesi ndani ya mwaka 2005/2006. Katika mwaka 2008/2009, shilingi milioni 550 zilitengwa kujenga kilomita tatu. Nimuahidi kwamba, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu ili kukamilisha barabara hiyo.

Mheshimiwa Damas Nakei, alitoa pongezi kwa Serikali kuboresha maslahi ya watumishi wa umma, lakini hakuvisikia Serikali ikizungumzia matatizo ya watumishi wa *TANROADS* ambayo imezungumziwa. Nadhani hii niliitolea ufanuzi huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya juhudzi mbalimbali kuimarishe Kanda muhimu za usafirishaji hususan zile ambazo zinahitaji kufunguliwa. Kanda hizo ni pamoja na Kanda ya Mtwara, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Mwambao wa Pwani na Kanda ya Kati. Mipango mbalimbali ipo katika hatua za utekelezaji kama ilivyoelezwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za maandalizi ili kujenga kwa kiwango cha lami barabara za Mtwara - Masasi - Tunduru - Namtumbo - Songea - Mbambabaya. Katika Ukanda wa Mtwara; Barabara ya Mtwara - Masasi kilomita 200 ilijengwa katika kiwango cha lami imeshaanza kuwa na mashimo. Samahani, juhudzi zinaendelea za kutafuta fedha ili iweze kukarabatiwa barabara hiyo na kuwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na *ADB*, ambao wamekubali kutoa mkopo kujenga barabara ya Tunduru - Mangaka - Daraja la Umoja, kilomita 195 kwa upande wa Tanzania na kilomita 170 kwa Daraja la Umoja hadi Pemba upande wa Msumbiji ili kufunga biashara kati ya Tanzania na Msumbiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya ufinyu wa muda, nadhani sitawezza kutoa ufanuzi kwa barabara za Tunduma – Sumbawanga - Mpanda kama ambavyo ningependa kufanya. Pia barabara ya Kanyani - Mpanda itafanyiwa usanifu. Barabara ya Mwandiga – Manyovu, Serikali imeanza ujenzi wake. Aidha, ujenzi wa sehemu ya Kigoma - Kidawe kwa kilomita 30 na kadhalika katika barabara hizi za Ukanda wa Magharibi.

Ningependa pia kutoa ufanuzi kwa taratibu zilizoko katika eneo la usafiri kwa njia ya reli na hasa kwa vile liliongelewa kwa uzito zaidi. Nilitaka kwenda hoja kwa hoja, lakini kwa sababu ya ufinyu wa muda niseme tu kwamba, Serikali imesikia na itafanya kazi kwa umakini na kwa ukamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili ambalo Mheshimiwa Damas Nakei na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi wamelizungumzia kwa uzito sana na kwa machungu la mgogoro wa utumishi *TANROADS*. Suala hili limezungumziwa pia na Mheshimiwa

Zitto Kabwe katika mchango wake wa maandishi. Naomba niseme kwamba, mimi nimechukua dhamana ya Wizara hii, sasa hivi ni wiki sita na masuala mengi hayajanifikia kwa kina chake.

Hili suala nimelipata hapa kwa kina kwa mara ya kwanza. Naomba niseme na kuahidi kwamba, suala hili nalipokea na nitalifanyia kazi kwa kina na kwa haraka. (*Makofi*)

Endapo taratibu zilikiukwa katika kutoa ajira kwa Meneja Mkuu wa *TANROADS* na kama taratibu zilikiukwa kuachishwa kazi kwa Wakurugenzi ndani ya Shirika lile, basi taratibu hizo tutazirekebisha kama nilivyosema kwa kina na kwa uharaka. Tayari mimi kama Waziri, nilipata fununu hizi. Nimepata dokezo moja au mawili ambayo hayakwenda kiasi hicho ambacho Mheshimiwa Mporeogomyi ameweza kulisema suala hilo hapa Bungeni. Pengine ningeshukuru kama Mheshimiwa angeweza kuniona kabla, lakini ni wajibu wake kulitoa hapa. Niahidi tu kwamba, Serikali hii italishughulikia kwa kina na tutalifanyia kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, pia ametoa mchango wake kwa unyonge sana. Naomba nimhakikishie kwamba, kupitia Mamlaka ya *TPA*, ukarabati wa Barabara ya Kajunjumele itafanywa ndani ya mwezi Septemba, 2008. Aidha, *TPA* imenunua mtambo wa kuondoa mchanga, ama *dredger*. Mtambo huu unategemewa kuwasili mwezi Agosti, 2008. Kutokana na mahitaji makubwa ya mtambo huo na kutokana na kujaa kwa mchanga kwenye Bandari za Maziwa, Bandari ya Itungi imepangiwa kuongezewa kina cha maji, pamoja na kuondoa mchanga kwenye lango la bandari Mungu akijalia ndani ya mwezi Februari, 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimtaja Mheshimiwa Kabwe Zitto kuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, naomba nitoe samahani, ye ye siyo Msemaji wa Kambi ya Upinzani, aliwasilisha mada kwa niaba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

#### Fungu 98 - Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu

Kif. 1001 – *Administration and General* .... .... Sh. 2,109,887,400.00

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa, Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Mporeogomyi, Mheshimiwa Arfi, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Selelii, Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Zambi,

Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Chilolo, Mheshimiwa Blandes, Mheshimiwa Mpendazoe, Mheshimiwa Masilingi, kuna watu wanansaidia hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mcemba, Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Dr. Mpanda nimekuona, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Mheshimiwa Shah, Mheshimiwa Lembeli, Mheshimiwa Luhahula, Mheshimiwa Ligalama, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Rwilomba, Mheshimiwa Shibuda, Mheshimiwa Lyamba. Wote nimewaandikisha, haya muda wetu ni mfupi, tutaanza na Mheshimiwa Dr. Slaa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza. Ninaomba kwa kutumia Kifungu cha 98, Programu ya 10, *Sub-Vote 1001* na Kifungu Kidogo 250100, nimwombe Mheshimiwa Waziri ufanuzi kuhusu barabara ambayo wakati wa mchango nilielezea kama barabara ya njia panda; Oldeani hadi Lalago Shinyanga. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza kwamba, kwa bahati mzuri barabara hii Serikali ilikwishakufanya usanifu, sijui inaitwa usanifu au ni nini. Lakini ilifika hatua ya kuweka *beacons* na miaka mitatu, minne iliyopita Serikali ilitumia milioni 200 kufanya kazi hiyo kwa fedha zetu za ndani. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa bahati mbaya barabara hii ambayo inatokea Oldeani, yaani inaungana na lami iliyoko Makuyuni - Karatu - Kandet - Mbuga Nyekundu - Jobaji - Matala - Lalago haikuonekana kabisa katika hotuba wala haikuonekana katika Kitabu cha Nne.

Daraja la Mto Sibiti ambalo pia liliwa limeshatajwa muda mrefu halipo na ilikwishaahidiwa katika kipindi kilichopita. Nina hakika kwamba, usanifu pia ulikuwa umeshafanyika na barabara hii inaunganisha Mikoa ya Arusha na Shinyanga. Barabara hii ndio inayotumika kusafirishia vitunguu ambavyo vinakwenda mpaka Kenya, lakini sasa vimeanza kwenda Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan. Barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa nchi, ukiacha masuala ya kijamii.

Je, Waziri anaweza kunipa ufanuzi; kupotea kwa barabara hii katika vitabu vyake ni dalili kwamba hii barabara sasa imeachwa na haina umuhimu na kama sivyo basi ni lini au kuna mpango gani wa kuhakikisha kwamba barabara hii itajengwa? Nashukuru Mwenyekiti.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Dr. Slaa, kama ifuatavyo:-

Nakiri kwamba, barabara hiyo hajatengewa pesa, lakini ni muhimu sana kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameielezea. Tatizo kubwa lililokuwepo ni pesa ambayo tulikuwa nayo, kwa ushauri wa Waheshimiwa Wabunge au ushauri wa Bunge lako Tukufu kwamba tuondokane na madeni ambayo tuko nayo. Kwa maana hiyo, tunatumia pesa nyingi sana, mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi bilioni 190 zitatumika kulipia

madeni. Ndiyo maana barabara nyingi muhimu, pamoja na ujenzi wa Daraja la Tusibiti, tumeshindwa kuingiza katika mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wote mliosimama hapa mko 30. Kwa mujibu wa Kanuni zidisha mara tano, ni dakika 150. Tulizonazo kihalali kwa Waziri ni saa moja, nikiongoza kwa mujibu wa Kanuni 30 itakuwa saa 1.30. Kwa bahati tulipoandika Kanuni kile kifungu cha *Guillotine* tuliiiondoa. Kwa hiyo leo nitatumia kifungu hicho hata kama kipo kwa mamlaka niliyonayo hapa na itaingia kwenye *desk* hapo. Ikifika wakati huo hamna kitu, na mjue kwamba mnachoomba hapa ni maelezo tu ya ufanuzi. Kwa hiyo, naomba tusibishane kwenye ufanuzi. Ndiyo ufanuzi. Hakuna atakayeongeza fedha wala kupunguziwa pesa kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni kipindi hiki hamuongezi wala hampunguzi. Kwa hiyo, tuelewane hapo. Msiseme Spika anawapelekesha hapana. Mheshimiwa Serukamba. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Program* ya 10, *Subvote 1001, item 250100 - Mshahara wa Waziri.*

**MWENYEKITI:** Naomba mtakaofuatia, tunajua mnataka mshahara wake, sasa sijui mtagawana kiasi gain, kwa hiyo msirudie, endeleeni tu kwenye hoja zenu. (*Kicheko*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi, niliomba ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri; ukiangalia kwenye nchi yetu kuna barabara nyingi sana tumemaliza *design* ambazo zinaenda karibia kilometa 700. Nilitaka kuuliza, kwa nini kuliko kuanza kuzijenga huku kilometa 20, huku kilometa 30, nadhani mwisho wa siku barabara hizi tutajenga kwa bei kubwa sana. Naomba nipate maelezo kwamba, sasa kwa kuamua kujenga kidogo kidogo, *are we getting economies of scale? Are we getting terms of time na price* kwa sababu mwisho wa siku bei zitapanda za kujenga barabara hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, amesema tunafikiria kutafuta mikopo kwa ajili ya kujenga barabara zetu. Nafahamu kwamba, Sheria ya Mikopo ya Nje ya mwaka 1974 inasema: "Mkopo wowote ambao nchi inatakiwa kuuwingia, lazima uwe na element ya grant kwa 50% au zaidi." Serikali inasemaje kwenye hili, kwa sababu sioni kama kuna watu wanaweza wakakopa kama bado sheria yetu hii haijabadilishwa? (*Makofi*)

La mwisho ...

**MWENYEKITI:** Hapana mawili tu. Wakatukopa au wakatukopesha? Haya wakatukopesha. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi wa hoja mbili ambazo Mheshimiwa Serukamba, amezitoa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuhusu ujenzi wa barabara zetu kwa vipande vipande. Naomba niseme kwamba, ujenzi wa miundombinu ya barabara ni wa gharama kubwa na kwa sababu nchi yetu ni kubwa, barabara hizi ambazo tunataka kuzijenga ni nyingi na kila mwananchi ana haki, ana hamu na dukuduku la kuweza kupata miundombinu ya barabara. Sasa kwa sababu hatuna fedha za kutosha za kuweza kufanya kazi yote hiyo kwa mara moja, pengine tungependa kufanya hivyo, kwa hiyo tunajaribu katika ujenzi huu, walau kufungua maeneo yale ambayo ni korofii zaidi katika barabara fulani au barabara mbalimbali ili ziweze kupidika.

Ujenzi kamili wa barabara nzima ufuate kadiri tunavyoweza kupata fedha. Badala ya kuiacha barabara nzima, usiligure hata eneo lile ambalo ukikiwekea lami kipande cha mlima kinaweza kupidisha magari hapo na ndio hicho hicho tu ambacho kinazuwia usafiri, ungoje mpaka upate hela zote ingekuwa vigumu. Kwa maana hiyo, Serikali imechukua hatua hiyo na kwa namna hiyo tumewezesha barabara nyingi kujengwa. Tutegemee kwamba, huko mbele tutaweza zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sheria yetu inahitaji *grant element* katika mikopo tunayoichukua. Bahati nzuri mpaka hivi sasa wahisani na wafadhili mbalimbali, wameweza kutupatia mikopo kwa kutumia kipengele hicho na kiasi hicho cha *grant element*. Sasa hivi tunahitaji *grant element* ya 50%, lakini tumeanza mchakato wa kuipitia hii na hasa baada ya kuona kwamba, tunahitaji kukopa zaidi na hasa kwa kujali hoja za Wabunge na Ushauri wa Wabunge kwamba, tukope kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, hili tunalifanyia kazi. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, maswali ya nyongeza nitawalangua tu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba usinitishe. Kwanza, nataka kusema kwamba ni *program* hiyo hiyo. Mheshimiwa Waziri, amejisalimisha yeye mwenyewe kwa majibu yake mazuri, kwa hiyo tusiwe na wasiwasi. Pamoja na hayo, mimi nina daraja langu la Simiwi linajengwa, kwa hiyo, sina matatizo makubwa. Nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri, azungumzie ile hoja ambayo nimeitaja kwamba, tunalia hatuna fedha, tunatengeneza mradi kama mlivyosema unaanza na shilingi bilioni 51 unamaliza na shilingi bilioni 140 kwa kilometra hizo hizo. Anijibu, anasema nini *is this the way forward?* Ndio namna ya kutumia bajeti finyu? Sikusikia akisema lolote juu ya hilo. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile lingine ambalo nilitaka kumuuliza, kwa kuwa nimemuona Mheshimiwa Kombani, yumo humu sitamuuliza. Nitamfuatilia yeye kwa nini tumepata nusu ya fedha za *road toll* za kutengeneza barabara? Sio lazima ujibu sasa, lakini hilo Serikali imesikia kwa sababu nimetumia hii nafasi kusema hilo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa John Cheyo na nitoe ufanuzi wa hoja yake kama ifuatavyo:-

Namshukuru kwa kunipa moyo na kwa kukiri kwamba, nimejitahidi kuwa mnyenyeketu kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ili mshahara huu ambao hautatosha kugawiwa kwa Wabunge wote, usichukuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, tatizo hili la kupanda bei kwa miradi ya ujenzi ni kubwa, sio tu katika ujenzi wa barabara lakini katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali. Kwa bahati, vigezo vingi ambavyo vinahusika katika ujenzi wa miundombinu vinakuwa *affected* na upandaji wa bei wa vitu mbalimbali, kwa mfano, upandaji wa bei ya mafuta hivi sasa; hakuna njia ambayo itaweza ku-control na inapotokea upandaji wa bei wa pembejeo, kwa kiasi kikubwa mikataba inaruhusu kupitia upya bei za mikataba hiyo. Tutajitahidi sana Serikalini kuhakikisha kwamba, hakuna upandaji holela wa gharama za ujenzi wa miundombinu ya barabara ndani ya miradi ambayo itasimamiwa na Serikali. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi kwa kweli ninayo mawili tu ya kisera, ambayo ningeomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie kupata ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba niishukuru sana Serikali na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Peramiho, naishukuru sana kwa kusikiliza kilio cha muda mrefu cha ujenzi wa daraja la kutuunganisha Tanzania na Msumbiji; *Unit Bridge Number Two*, ambalo linaendelea kukamilika kujengwa katika Jimbo la Peramiho. Namshukuru sana *Regional Engineer* wetu, anafanya kazi nzuri sana. Sasa ninachotaka tu kujua ni kwamba, katika hotuba zote na kila maelezo yanapotokea yanayohusiana na *Unit Bridge* hizi za kutuunganisha na Msumbiji. Linalozungumzwa zaidi ni lile Daraja la Mtambaswala. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, kuanzia mwakani sasa kila kitakachofanyika kuhusiana na *Unit Bridge* za kutuunganisha na Msumbiji, waanze ku-consider sasa na hii *Unit Bridge Number Two*, ambayo itafunguliwa nafikiri mwaka huu mwezi wa saba, kwa kiwango kile ambacho tumepewa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Waziri, anithibitishie hilo na hatimaye tupandishe pia hadhi ya barabara inayoenda kwenye hilo daraja. Hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninaishukuru sana Serikali, katika bajeti ya mwaka huu imezingatia pia ujenzi wa Barabara ya Namtumbo – Songea – Peramiho – Mbanga - Mbamba-bay. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imejikita katika kuonyesha kwamba barabara hiyo itajengwa kwa utaratibu huo. Katika vitabu vyake vya bajeti, barabara hiyo inasomeka Namtumbo – Songea – Mbamba-bay tu, sasa hilo linanitia shaka katika utekelezaji ile Peramiho inaweza kuachwa kwa sababu kwenye vitabu vya bajeti haitajwi lakini kwenye hotuba inatajwa. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri, aweke sawa kwamba, itakapoanza kujengwa ni Namtumbo – Songea – Peramiho – Mbanga – Mbamba-bay kulingana na maelezo yake ya hotuba na vitabu vyake viendelee kutambua na utekelezaji uwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani, naomba kufafanua hoja ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo: Kuhusu suala la kwanza, ushauri nimeupokea na tutauzingatia, pamoja na upandishwaji daraja kwa barabara husika.

Namba mbili, kuhusu barabara yake ya Peramiho – Mbinga – Mbamba-bay, hii ni barabara ya Ukanda wa Kusini, ikianzia Mtwara moja kwa moja kupitia Masasi – Tunduru – Namtumbo – Songea – Peramiho – Mbinga mpaka Mbamba-bay na ujenzi wake utaenda kwa awamu. Awamu ambayo inahusika hivi sasa ni ya *MCT*, ambayo itachukua kipande cha Namtumbo – Songea, lakini Mbinga na Peramiho, Songea – Peramiho na Peramiho – Mbinga, zimo katika utaratibu wa ujenzi. Kipande cha Songea – Peramiho, sikumbuki sawasawa, lakini nadhani hiki tayari kipo katika ujenzi na Peramiho – Mbinga – Mbamba-bay ipo pia katika mpango wa ujenzi. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika ujenzi wa Barabara hiyo Kuu ya Ukanda wa Kusini au Ukanda wa Mtwara, Peramiho haitosahauliwa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nimshukuru Waziri mwenzangu, kwa majibu mazuri. Nilitaka nimfafanulie tu kwamba, hata alipojibu suala la kwamba sio Kiongozi wa Upinzani pia hakuweza kukipatia vizuri cheo; mimi ni Waziri Kivuli wa Miundombinu, Msemaji Mkuu wa Upinzani, Wizara ya Miundombinu. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Kuonyesha jinsi msivyoshirikiana, haya.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Nakushukuru umejibu vizuri sana na pia napenda kwa mara nyingine kuishukuru Serikali kwa ujenzi wa Barabara ya Mwandiga – Manyovu na Kigoma – Kidahwe kwa kiwango cha lami.

Vilevile suala zima la kuchukulia umuhimu wa zile fedha za *passenger's service charges*, ili *TRA* watakaposikusanya zisiende kwanza Hazina ziende moja kwa moja *TAA* ili waweze kujenga viwanja vyetu kama vya Kigoma na vya Sumbawanga na ndege ziweze kufika kule vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swalii moja tu; suala hili la mali za lililokuwa Shirika la Ndege (*ATC*), ambazo zilikabidhiwa kwa *ATHATCO*, tuliliuliza mara ya kwanza mwaka 2006, Serikali ikasema hakuna kitu kama hicho. Mwaka 2007, Serikali ikakiri kwamba kuna tatizo hilo na watalifutilia na kutoa majibu. Mwaka huu pia, umesema kwamba mtafanya uhakiki, lakini ukiangalia katika hotuba yangu nilichokuwa nimeomba ni ushirikiano kati ya Wizara ya Miundombinu, Kamati ya Bunge ya Miundombinu na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, ili kwa pamoja, yaani kati ya Bunge kupitia Kamati hizo na Wizara ya Miundombinu, tuweze kufanya uhakiki na kulifanya suala hili liweze kufika mwisho. Hii ni kwa sababu mwaka jana mlisema kwamba mtafutilia, lakini hakuna majibu yoyote ambayo yametoka mwaka huu. Kwa taarifa yako tu Mheshimiwa Waziri ni kwamba, nyumba iliyopo kwa mfano ya Lusaka, hajiauzwa, bado anakaa Mzambia kwenye nyumba hiyo. Mzambia huyo halipi kodi yoyote na inamletea usumbu mkubwa sana Balozi wetu pale Zambia.

Kwa hiyo, naomba unihakikishie na utupe *commitment* labda ndani ya miezi sita hii Serikali na Bunge, kwa kuitia Kamati hizo mbili ambazo nimezitaja, tulifuatilie suala hili liishe na lisijirudie tena katika mwaka ujao wa fedha. Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe, Waziri mwenzangu, Waziri Kivuli, maana yake anapenda zaidi Waziri Mwenzake, lakini najua ni Waziri Kivuli, kama ifuatavyo:-

Suala hili kama tulivyolipokea katika hoja ya Kambi ya Upinzani leo, naomba niseme kwamba, Serikali imelitolea ahadi ya kulifanya kazi kina na tutafanya hivyo. Mimi ni Waziri ambaye nimepewa dhamana hivi karibuni na nadhani katika haya ambayo yana mgogoro, nimeyakuta yanafanyiwa kazi. Itakuwa vizuri sana niyafanyie kazi na pale nitakaposhindwa nitaomba usaidizi wa Kamati mbalimbali, lakini kwa sasa Serikali italishughulikia jambo hilo katika taratibu za kawaida. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nipate maelezo kutoka kwa Waziri wa Miundombinu, juu ya Barabara ya Pandaoldiyani kwenda Lago, kuitia Mto Sibiti. Mwaka jana, Serikali ilisema kwamba, hawana uwezo wa kujenga barabara hii yote ila watajenga daraja la Mto Sibiti na kutengeneza kipande cha kilometa 25.

Nimeona wametenga fedha kidogo kwa ajili ya daraja na fedha kidogo kwa ajili ya hizo kilometa 25. Nataka maelezo tu, hizo fedha kweli zitatosha kwa kazi hizi au Mheshimiwa Waziri ana njia nyingine ya kupata fedha ili tupate daraja na hizo kilometa 25, ili Wananchi wa Mikoa ya Ziwa, Mikoa ya Kati na Mikoa ya Kaskazini, waweze kupita wakati wote kwa mwaka?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Msindai kama ifuatavyo: Ni kweli kwamba, pesa hizi hazitatosha kufanya kazi hiyo kamili, lakini katika kuandaa bajeti hii, tuliona kwamba ni afadhali tutenge pesa kidogo ili Mradi huu usisimame kabisa na uweze kuwa ni kivutio cha uwekezaji wa pesa nyingi zaidi katika bajeti inayofuata. Tungeacha safari hii isifanywe kazi hata kidogo na wala tuisitengee hata fungu dogo, basi ingekuwa vigumu sana hata kuibeba katika bajeti inayofuata. Kwa hiyo, nikiri kwamba ni kidogo lakini tutaushugulikia katika mwaka unaofuata. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi yake nzuri na melezo yake mazuri sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, amekubali kuwepo kwa fununu ya matatizo ndani ya *TANROADS*; na kwa kuwa ninamheshimu sana; na kwa kuwa ninamwamini sana; je, yupo tayari kutoa Kauli ya Serikali hapa Bungeni kabla ya Bunge hili kwisha? Maana atambue kwamba fedha nyingi za Serikali zinapotea na watumishi ambao wangetoa mchango wao mkubwa kwa Taifa hili, hawalitumikii Taifa na fedha zinaendelea kupotea. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Na ninyi Waheshimiwa Wabunge mliosema, pia mumsaidie Waziri ili aweze kutoa tamko. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi ufuatao kwa hoja ya ndugu yangu, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi kama ifauatavyo:-

Nimezungumza katika jibu la awali kwamba, suala hili nimelipokea hapa kwa uzito wake na kwamba tutalifanyia kazi kwa kina bila ya utani, bila ya mzaha na bila ya kusitasita. Kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa Mporogomyi kwamba, ataona matokeo ya ahadi hii ambayo nimeitoa. (*Makofi*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimejikita sana katika maeneo mawili; reli na barabara. Lakini kwa sababu reli ipo katika Azimio la Bunge, sihitaji maelezo hivi sasa, nataka tu nipate maelezo ya ufanuzi kuhusu mpango ule ambao katika bajeti iliyopita, Waziri wa Miundombinu wa wakati huo alisema kwamba, kuna Mpango wa *PMMR* ambao utakuwa wa miaka mitano kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa, Mwanza na Tanga.

Angalau kwa kiasi fulani, mwaka huu wa fedha kazi katika barabara hizo zimefanyika. Katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 178, kwenye mpango huo huo naona hakuna fedha yoyote ambayo imetengwa kwa ajili ya Mpango huu wa Matengezo ya *PMMR* kwa Mikoa ya Rukwa, Tanga na Mwanza. Naomba maelezo.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kutoa ufanuzi kwa hoja aliyitoa Mheshimiwa Arfi, katika mpango huu wa *PMMR* au *Performance Management and Maintenance of Rural Roads* kwa mikoa hii ambayo tumeanza nayo Rukwa, Tanga na Mwanza. Mpango huu umekuwa na mafanikio mazuri sana katika kuboresha barabara zetu, lakini katika misingi ile ile tu ya ufinyu wa fedha hatukuweza kutenga pesa katika eneo hili. Tutajitahidi kwa kadiri pesa itakapopatikana kwa miaka inayofuata, tuweze kutenga pesa nyingi katika mpango huu. Ahsante sana.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipatia nafasi hii lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi ambavyo amejibu hoja za Wabunge. Nina hakika hoja nyingi amezijibu lakini nyingine hakuzijibu lakini atatupa kwa maandishi. Wakati nimetoa hoja yangu kwa maandishi nilikuwa na mambo makubwa mengi lakini hasa ni suala zima la ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba, ujenzi wa barabara ni gharama kubwa na sisi tunajua ni gharama kubwa na Waheshimiwa Wabunge wengi waliona kuna haja ya Serikali kukopa. Mimi naamini Serikali au Tanzania ni nchi ya amani na historia yake inajieleza vizuri na kwamba, tuna uwezekano kabisa wa kukopesheka. Sasa wakati Mheshimiwa Waziri anajibu amesema kwamba, wameeweza kupata watu binafsi, lakini bado naamini watu binafsi hawatakuwa na uwezo wa kuweza kujenga barabara zetu.

Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba kuna haja ya Serikali ya Tanzania kukopa? Ninakumbuka kabisa Mheshimiwa Mramba, ambaye alikuwa Waziri wa Miundombinu na Waziri wa Fedha, alisema hapa Bungeni wakati wa kuhitimisha Hotuba ya Waziri Mkuu kwamba, Serikali ya China ilikubali kwamba inaweza kutukopesha kwa ajili ya Miradi ya Ujenzi wa Barabara. Je, Serikali ina mpango gani katika hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la mpango wa barabara tatu Dar es Salaam. Barabara zile tatu zimekuwa ni kero kubwa mno kwa wasafiri Dar es Salaam na ninyi nyote ni mashahidi. Inakuwa ni jambo la ajabu kwamba, kunakuwa na barabara tatu lakin kwenye *junction* hakuna jinsi ya kuweza kuingia, kwa hiyo, inakuwa ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua hivi ni Sheria gani inayosema Tanzania tuwe na barabara tatu? Kibaya zaidi ni kwamba, hata mtu akipata ajali, bado linakuwa sio kosa la *ki-traffic* bali ni uzembe na watu hawapati *insurance*. Nilikuwa naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri; hivi ni Sheria gani inayosema Tanzania iwe na barabara tatu na je, hao walofikia hapo walifanya utafiti wa kina kuona kama itakuwa na matatizo au haina matatizo? Ahsante.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi wa hoja mbili za Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo: Moja, upande wa kutafuta mikopo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. Nina hakika kabisa Serikali inajiweka sawa kukopa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. Tumeangalia njia mbalimbali na tunaendelea kuangalia njia mbalimbali. Moja ya njia hizi ambazo Waheshimiwa Wabunge, wamezitaja ni kupitia *sovereign bonds*. Ili kuweza kupata *sovereign bonds*, kwa ajili ya kukopa kwa miundombinu, nchi inabidi itathminiwe ama *sovereign rating*.

Sasa hivi Serikali yetu kupitia Hazina, ipo katika mchakato wa kufanya hivyo na mara mchakato huo utakapokamilika, tukiweza kutathmini *positively* na kwa bahati nchi yetu ina kila kigezo cha kuweza kufanikiwa katika hili, hapo tutakuwa katika uwezo wa kukopa kimataifa na kukopa hela nyingi. Niwahakikishie tu kwamba, Serikali hii haitaogopa kukopa; kwani kukopa ndio njia ya kuweza kuboresha miundombinu yetu hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia tatu tumezijaribu baada ya msongamano mkubwa wa barabara na sio utaratibu mpya; ni utaratibu ambao unatumika katika nchi nyingi sana pamoja na nchi za Ulaya. Kati yetu ambao tumekwenda nchi za Ulaya, Marekani na nchi nyingine, nilisoma Uingereza, hizi njia zinatumika. Tatizo kubwa ambalo lipo ni elimu kwa watumiaji wa barabara. Ilipoanza ilikuwa ngumu zaidi, hivi sasa imekuwa nafuu, lakini nadhani tutaendelea kutathmini na kulifanya kazi.

*SUMATRA* itaendelea kulisimamia Jiji la Dar es Salaam na kusimamia utaratibu huu ili kero zake zizidi kupungua, wakati Serikali inafanya juhudhi kuboresha miundombinu ya barabara ndani ya Jiji la Dar es Salaam. Kama ambavyo nimeongea kwenye hotuba yangu, kupitia njia ya kuweka *ring roads* na kupanua barabara hizi badala

ya kuhitaji kupita katika njia tatu katika hali ile ya hatari. Naomba niseme pia kwamba, kisheria fidia ya bima ipo, maadam mtu ametumia barabara hii katika utaratibu huo kwa muda ule ambao umeelekezwa. (*Makofi*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Tabora, napenda kuishukuru sana Serikali kwa kutupatia shilingi 10,000,000,000 kwa barabara hii ya Manyoni – Itigi – Tabora, kwenda mpaka Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda nipaye ufanuzi kutoka kwa mwanangu, kijana wangu kabisa, juu ya hizi pesa ambazo Serikali imetupa. Je, hizi shilingi 10,000,000,000 zitapitia kwenye Mkoa gani? Maana yake hii barabara ni mtambuka; ina Mkoa wa Singida, Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Kigoma. Je, zinapitia kwenye Mkoa gani; kupitia kwa *RAS* au inapitia kwenye *trunk road*?

Katika hilo hilo, mwaka jana Serikali iliahidi kuipandisha hadhi hii barabara ili iwe *trunk road* na akasema inapewa nambari 18, lakini katika maelezo bado hajaonyesha kama kweli hii barabara imepandishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi shilingi 10,000,000,000 ni nyingi, kama zitajenga barabara kwa kiwango cha changarawe, lakini ni ndogo sana kama zitajenga barabara kwa kiwango cha lami. Je, maelekezo ya Serikali ni yepi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ...

**MWENYEKITI:** Aah, tayari mawili. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii, kutoa ufanuzi wa hoja mbili za mjukuu wangu, Mheshimiwa Selelii na wajukuu wenziwe wanafahamu kule Tabora, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwamba, pesa hizi zitapitia Mkoa gani? Naomba niseme kwamba, sasa hivi tunazitafakari pamoja na *TANROADS* tuone upande gani hasa tutaweka hizo pesa, lakini pia itategemea na barabara itaanza upande gani. Kuna zaidi ya kilometra 170 upande wa Tabora na kuna zaidi ya kilometra 100 na kitu pia upande wa Singida. Sasa tutatafakari na tutashirikisha mikoa hii miwili, kupitia *TANROADS* kuona barabara hii itaanza upande gani.

Najua kwamba Tabora wajukuu zangu wangependa ianze huko lakini Singida nao wangependa ianzie kwao. Tutaangalia taratibu wapi hasa tuanze na ikiwezekana, tuanze pengine kwa maeneo yote ili kila eneo lisije likawa na manung'uniko makubwa. Najua Tabora kuna manung'uniko makubwa kule. Hilo najibu tu kwamba, tutalichanganua na tutashirikisha mikoa hiyo kupitia *TANROADS* ili tuweze kuzitoa hizo pesa kufuatana na maeneo yale ambayo tunaanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu upandishwaji wa daraja kwa barabara hii. Upande wa Singida – Manyoni mpaka Itigi, tayari ni *trunk road*, lakini kipande kile kutoka Itigi mpaka Chaya, bado hakijapandishwa daraja. Kwa hiyo, tutaangalia tathmini ya barabara ile na upembuzi ambao umefanywa na maoni ya mikoa hii husika, kuona kama kutakuwa na haja ya kuipandisha daraja. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka ufanuzi kwa barabara inayotoka Nkolandoto - Lalago - Mwanuzi na ile inayotoka Lalago kwenda Maswa. Mwaka jana ilitengewa shilingi milioni 200 kwa ajili ya upembuzi yakinifu, pamoja na usanifu wa kina, lakini mwaka huu haijatengewa hata senti. Mheshimiwa Waziri amesema katika maelezo yake kwamba, miradi ambayo haijatengewa fedha kabisa itakuwa ngumu hata kwa kipindi kingine kutengewa fedha. Je, Serikali imesitisha mpango wake wa kuwapelekea wananchi hawa barabara ya lami kama ilivyowaahidi?

Pili, katika mchango wangu huo wa Maandishi, nilimtaka Waziri aniambie ni lini sasa barabara hii muhimu itapandishwa kutoka Halmashauri na kuwa ya Mkoo? Barabara inayotoka Bariadi inapita Gambasingu kwa Bwana Cheyo, inapita Kisesa, inakwenda Mwandoya na inakwenda Noboko Junction, ipandishwe daraja kuwa Barabara ya Mkoo?

Katika majibu yake, Mheshimiwa Waziri amekuwa akisema Sheria za Kanuni za Barabara bado hazijakamilika. Je, Mheshimiwa Waziri Kanuni hizi zinakamilika lini sasa kwa sababu zinachelewesha sana wananchi kupata huduma?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Mpina kama ifuatavyo:-

Ni kweli tumeshindwa kutenga pesa kwa barabara hii ya Nkolandoto – Lalago kwa mwaka huu wa fedha, lakini tunafahamu kabisa tatizo la usafiri kwa eneo hilo na niahidi tu kwamba, fedha zitakaporuhusu katika mwaka ujao tutaipangia fungu barabara hii. Barabara ya Bariadi – Kisesa mpaka Maboko Junction; samahani nyingine sijazikariri vizuri; lini ipatanda daraja? Hii inatarajia mapendekezo ambayo tayari Mkoo imeshayaleta. Kama nilivyosema, tunakamilisha Kanuni zile ili utaratibu uweze kueleweka vizuri zaidi. Sasa tunafanya zoezi hilo, lakini tunapofanya zoezi hilo bila Kanuni siyo sawa, kwa sababu inaelekea kwamba kuna upendeleo mahali fulani. Tutayashughulikia maombi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. OMAR S. KWANGW’:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi la kwangu ni la ufanuzi tu.

Nianze kwa kusema kwamba, Mheshimiwa Waziri anaonekana mtu makini na sisi tutamsaidia. Sasa ipo tabia ya Makandarasi kupewa kazi nyingi katika maeneo tofauti na katika miradi mbalimbali. Katika mchango wangu wa maandishi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba ni vyema atupe orodha au takwimu inayoonyesha majina ya Makandarasi na Miradi waliyonayo maana wengine wana Miradi ya Shule, Miradi ya Barabara, Maji na Hospitali. Sasa udhaifu wa utendaji katika maeneo haya unatokana na mtu kupewa kazi nyingi. Sasa tunataka kujua, tukipata hiyo orodha nadhani tutaanza kuona hawa makandarasi wana uwezo gani na sifa gani ya kutekeleza Miradi iliyo mingi.

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi, kama atakuwa tayari kutupa hiyo orodha kabla hatujaondoka hapa ili tuweze kujua udhaifu kwa sababu katika maeneo haya ndipo ufisadi na mambo mengine yanakotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kutokana na matatizo ambayo nimeyaeleza kwenye mchango wangu wa maandishi kuhusiana na barabara ya Babati – Orkesmeti pamoja na Kibaya kuunganisha Mkoa wa Manyara. Najua muda hautoshi lakini nilikuwa nimemwomba kama akipata nafasi basi afanye ziara Babati ili tumweleze kwa kina, matatizo ambayo yametokea pale. Kama barabara hiyo haiwezi kujengwa na kwa sababu ya udhaifu wa mkandarasi uliotokea, basi Mkoa wa Manyara hauna maana yoyote kwa sababu Wilaya zile mbili nadhani mpaka leo hazijaunganishwa na Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kwa kifupi naomba nitoe ufanuzi wa hoja mbili za Mheshimiwa Omar Kwaangw' kama ifuatavyo:-

Nianze na la pili, napokea mwaliko huo wa kuutembelea Mkoa wa Manyara ili kukagua barabara ya Orkesmeti. Hilo nitalifanya, inategemea nafasi yake tu, hata tukimaliza Bunge hili nipo tayari kuweza kutembelea eneo lake.

Kwa hili la pili la kupewa orodha, ni ruhusa nitaangalia namna ya kulifanya na ikiwezekana tutalifanya kabla hatujamaliza Bunge hili na hata kama tutamaliza Bunge hili ikawa haijakkamilika, ninachokiahidi ni kwamba, orodha hii tutaitoa. Ninasema kwamba, hivyo ni vigezo ambavyo vinatumika katika kumpa mkandarasi kazi. Wale ambao wana kazi nyingi, inakuwa ni kigezo cha kuwanyima kazi ambayo imetolewa zabuni hiyo. Kwa hiyo, mara nyingi TANRODS na Serikali kwa ujumla, inaangalia pia huyu Mkandarasi anayepewa barabara hii ana kazi nyingine zipi. Tutafanya hilo kama alivyoomba na tutajaribu kulitekeleza ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1) inasema, zikifika dakika kumi kabla ya saa ya kuahirisha Bunge, kwa Mamlaka mliyonipa hapa nitawapa dakika 30 na kama nilivyosema kwa Mamlaka hiyo zikiisha

dakika hizo 30 baada ya muda huo basi tunafunga kazi ya fungu hili. Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kusema mambo machache. Mimi pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa namna ambavyo wameweza kujibu hoja mbalimbali hapa, kwa unyenyekevu na upole sana. Hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nina mambo mawili madogo tu ya ufanuzi. Kwenye kitabu cha hotuba yake, ukurasa wa 127 na 128 kuna barabara mbili pale, yaani kuna Barabara ya Igamba, Msangano na Utambalila ambazo zimetengewa pesa kidogo kwa ajili ya matengenezo lakini pia kuna Barabara ya Zelezeta - Isansa - Itaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kwamba, maeneo haya kwa mfano Zelezeta, Isansa na Itaka, Kata ya Isansa na Itaka, kati ya Kijiji cha Magamba na Iporoto hakuna barabara kabisa. Kwenye *networks* ya barabara za mkoa zilizopo Mkoa wa Mbeya, maeneo haya nayo yanajulikana kisheria kuwa yana barabara. Hii sehemu nyine ya Msangazo na Itambalila pia hakuna barabara lakini pesa zinatengwa ili zifanyiwe *maintenance* na maeneo ambayo hayana barabara. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, *TANROADS* Mkoa wa Mbeya wanajua maeneo haya hayana barabara lakini yalishakubaliwa muda mrefu kwamba ni barabara za mkoa.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwanza, akubali kuja kutembelea barabara na aamini tunachokizungumza hapa ili ikiwezekana kwenye bajeti ya mwaka kesho, basi waone umuhimu wa kutenga fedha ili maeneo hayo sasa yaweze kuunganishwa kwa sababu tunatoka Point A, B, C lakini hakuna barabara. Namwomba Mheshimiwa Waziri atukubalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka niombe tu ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwa suala la Wafanyakazi wa *TAZARA*. Wafanyakazi wa *TAZARA* hasa wale wanaostaafu na kufariki, wanapata tabu sana kupata mafao yao, lakini pia kwa wanaofariki warithi wao wanapata tabu sana kulipwa mafao ya ndugu zao. Sasa hivi *TAZARA* inadaiwa zaidi ya shilingi bilioni tatu kama mafao ya wafanyakazi wanaostaafu, lakini pia na hawa wengine ambao wamefariki ndugu zao wanahitaji mirathi. Hebu naomba Mheshimiwa Waziri, atuambie *commitment* ya Serikali ni nini kuwasaidia hawa watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi, naomba nitoe ufanuzi wa hoja hizi mbili za Mheshimiwa Zambi, Mbunge wa Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la kutembelea eneo lake ni kwamba, nimekubali ukaribisho wake nadhani nitaweka kwenye ratiba, pamoja na ukaribisho wa Mheshimiwa

Omar Kwaangw' ili niweze kutembelea mapema iwezekanavyo. Kwa hiyo, hili nimelikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa wastaa fu wa *TAZARA*, Serikali inapenda sana kuhakikisha kwamba, wastaa fu hawapati matatizo yoyote na wale amba o watakuwa wamefariki baada ya kustaafu, basi warithi wao wataweza kupata mafao yao haya kwa wakati muafaka.

Yapo matatizo lakini nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itasimamia mafao haya ya wastaa fu wa *TAZARA* kwa juhudii kubwa iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI :** Waheshimiwa Wabunge, naomba hoja iwe moja moja halafu katika hizo mbili chagua moja tu angalau tufike hao wote. Mheshimiwa Dorah Herial Mushi.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kupata ufanuzi.

Nilipokuwa nachangia asubuhi, nilikuwa nazungumzia zaidi kilio cha akina mama wa Mererani wanaoathirika na barabara ya kutoka *KIA* kwenda Mererani. Kilio hiki kilishawafikia Marais wetu wawili, yaani wa Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne, ndipo wakawenza kutoa ahadi ya kujenga barabara hiyo tena kwa kiwango cha lami. Naomba ufanuzi kuhusu barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa kuwa *very brief* na Mheshimiwa Waziri pia nawe uwe *brief*.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Dorah Mushi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba, kweli kuna matatizo makubwa katika Barabara ya *KIA* – Mererani. Serikali inaifahamu, lakini ufinyu wa fedha ndiyo amba o umetufikisha katika hali hii. Tunalifahamu na huu ni mwaka wa pili na nusu tangu Serikali hii imeingia madarakani na uhai wa Serikali hii ni miaka mitano. Nimeeleza kwamba, tumefanya kazi kiasi kikubwa sana tangu Serikali imeingia madarakani.

Namhakikishia Mheshimiwa Mushi kwamba, tutajitahidi kuhakikisha kwamba, barabara hii inaingia katika Mpango wa Ujenzi kabla ya Awamu ya Serikali hii kumalizika.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni kaka yangu mpendwa kama alivyokiri yeye, wala sihitaji chochote kwake naomba tu ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia Barabara ya Misigiri kwenda Kiomboi Bomani, yenye urefu wa kilomita 21. Mheshimiwa John P. Magufuli alipokuwa Waziri wa Wizara hii, alishawahi kutuahidi kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami kilomita 11 na kubakisha kilomita 10. Vilevile Mheshimiwa Rais, alipotembelea Singida juzi aliwafahamisha wananchi kwamba, angetengeneza kiwango cha lami kilomita 11 na mimi mwenyewe hapa Bungeni niliuliza swali juzi Naibu Waziri alinijibu hivyo.

Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 122 ametenga kilomita tano tu; sasa sijui labda angenipa ufanuzi ili wananchi waelewe kwa sababu mpaka sasa wanaamini kwamba tunapata hela za kutengeneza kilomita 11.

**MWENYEKITI:** Hiyo ni hatua ya kwanza. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi wa hoja ya dada yangu mpendwa, Mheshimiwa Diana Chilolo kama ifuatavyo:-

Nakushukuru kwa kunipa au kunitangulizia jibu kama ulivyonisaidia. Ni kweli kwamba, kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, hatukupenda kutokutimiza ahadi kwani ahadi ni deni, ada ya mji ni maneno na muungwana vitendo. Tumesema walau hizo kilomita tano zianze na tutaendelea kutenga fedha kwa kadiri tutakavyoweza kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia kuhusiana na Barabaraya Kyaka hadi Kayanga, ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe na barabara hiyo ni Ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Waziri, wakati anajibu hapa ameelleza kwamba, barabara hiyo ilianza kujengwa tangu mwaka 2004 mpaka 2005. Nataka kumweleza na kuweka *record* vizuri kwamba, ahadi hiyo ilitolewa wakati wa kampeni mwaka 2005 wala siyo mwaka 2004. Barabara hiyo anayoizungumzia ya mwaka 2004 ni nyepesi sana ya kutoka Karagwe Mjini, yaani Kayanga kuelekea Hospitali ya Nyakahanga ambayo haihusiani kabisa na Ahadi ya Mheshimiwa Rais. Ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kuanzia Kyaka mpaka Karagwe Mjini, yaani Kayanga kwa kiwango cha lami nzito.

Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri, amenitengea shilingi milioni 550 za kuanzia kujenga kilomita tatu ingawa sijui kama zitatosha. Vilevile nimwombe ampelekee Mheshimiwa Rais, pongezi zangu kwa niaba ya Wananchi wa Karagwe kwamba ameanza kutekeleza ahadi yake.

Swali langu ni kwamba, hizi shilingi milioni 550 za kilomita tatu katika barabara ya kilomita 58; je, barabara hiyo itaweza kwisha katika kipindi cha utawala wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete mpaka 2010?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Gosbert Blandes kama ifuatavyo:-

Ahadi hizi za Rais kwa Serikali ya Awamu hii ya Nne ni amri. Kwa hiyo, tutazitekeleza kwa juhudzi zote ili tuweze kuzikamilisha. Tumetoa fungu hilo kwa sababu ya ufinyu wa pesa, lakini tutajitahidi kuhakikisha kwamba, tunaijenga barabara hiyo kwa ukamilifu.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Kwanza, naomba nimshukuru sana mheshimiwa Waziri kwa kutoa *commitment* leo kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Kolandotto - Lalago – Mwanhuzi. Kwa kwa kuwa amesema yeye mwenyewe kwamba, Ahadi za Rais ni amri na hii ni Amri ya Rais. Ashukuru ametoe *commitment* leo alipokuwa anafafanua kwa ajili ya Mheshimiwa Luhaga Mpina.

Mimi wakati nachangia kwa maandishi, niliizungumzia barabara ya kutoka Maganzo mpaka Maswa, kilomita 120. Mwaka jana ilipangiwa shilingi milioni 400, kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwa kina. Katika hotuba ameeleza kwamba, upembuzi umekamilika, kwa hiyo tunashukuru sana tuna matumaini kwamba barabara hii itajengwa.

Katika jedwali ukurasa wa 175 wa kitabu cha hotuba, barabara hii imetengewa shilingi milioni 80; nashindwa kuelewa ni za nini kwa sababu ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ni gharama kubwa, upembuzi umekamilika tunategemea ujenzi uanze kwa kiwango cha lami?

Pamoja na kutoelewa ile milioni 80 ni ya nini, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe *commitment* kwamba .....

**MWENYEKITI:** Inatosha ile milioni 80 ya nini.

**MHE. FRED MPENDAZOE TUNGU:** Atoe *commitment* kwamba, ujenzi uanze mwaka kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tupate maelezo ile milioni 80 ni ya nini?

**MHE. FRED M. TUNGU:** Basi naomba atoe *commitment* kwamba, ujenzi uanze mwaka kesho.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Fred Tungu kama ifuatavyo:-

Tutajitahidi kutenga pesa kwa kadiri tutakavyoweza kupata pesa kwa mwaka ujao wa fedha, kwa ajili ya barabara hiyo.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali; kwanza, kwa kutenga fedha nyingi, shilingi bilioni 15.8 kutengeneza barabara ya Kagoma - Muleba - Lusahunga na katika nyongeza ya taarifa tuliyopewa mchana huu, zimetengwa shilingi bilioni moja kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege cha Bukoba. Tunaishukuru Serikali kwa kusikiliza kilio chetu, tunajua kitajengwa kwa lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo langu ni moja; yalikuwa mawili lakini nakuheshimu sana la pili nimeliacha. Mheshimiwa Waziri ni rafiki yangu sana tangu tukiwa Chuo Kikuu, miaka 28 iliyopita. Niwie radhi maana mjumbe hauawi na wewe ni muda mfupi tangu umeingia kwenye Wizara hii, huna hatia na Naibu wako. Hili nimelianza miaka miwili iliyopita, fidia ya Wananchi wa Muleba, mbele ya Mheshimiwa Rais katika ziara yake mwanzoni mwa mwaka huu. Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga alisisitiza kwamba, Serikali imekamilisha taratibu za kuwafidia wananchi hao na wananchi wakashangilia mbele yengu. Sasa aliyefanya ukaguzi alijiua na Mawaziri wameondoka, nimeandika kwa maandishi sikujibowi, ina maana mmeamua kumezea kwa sababu mambo yamebadilika halafu mimi nimezwe huko! Hata kunijibu jamani mkasema inaendelea, lipa fidia yao wakusikie. Naomba mnisaidie hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, utapata barua.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu tena kwa unyenyekevu, masikitiko haya ya Mheshimiwa Wilson Masilingi, ndugu yangu na rafiki yangu ni mwenzangu tulikuwa pamoja Chuo Kikuu kwa muda mrefu.

Niseme kwamba, Serikali ni moja, kubadilika kwa Mawaziri au kuja kwa Mtumishi katika Wizara, haibadilishi jambo lolote katika yale ambayo yametekelawa na yameahidiwa na Serikali. Kwa hiyo, ninamuahidi kwamba, tutalifuatilia hili. Barua yake kwa bahati mbaya sijaipata, lakini nitalifuatilia na tutalitekeleza kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swalii moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 51 namba 70 amesema kwamba, safari za treni ambazo zilikuwa zinakwenda kwa wiki mara mbili sasa hivi angalau zitakwenda mara nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba sana hili tatizo ni huduma za wananchi, lisichukuliwe ni suala ambalo linatakiwa kutafutiwa mikopo, likaenda wapi na kadhalika. Tulipopata ajali ya treni, mabehewa yetu yalikuwa yanakwenda *routs* zake kama kawaida pamoja na umaskini wetu, lakini alipokuja mwekezaji akapunguza kabisa zile safari; kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali iseme na itamke kabisa kwamba, kuanzia lini utekelezaji huo utakamilika kwa sababu chakula nacho ni cha ovyo, watu wanakwenda vibaya na nimwombe Mheshimiwa Waziri ikiwezekana Jumamosi, twende naye akapande hiyo treni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waziri inabidi aendelee na kazi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Mwanne Mcchemba kama ifuatavyo:-

Kwanza, napokea ukaribisho wake wa kwenda naye Jumamosi kupanda treni, lakini pia niseme kwamba, kwa hili la kuongeza safari za treni kutoka mbili kwenda nne, tunalisimamia na kulifua tilia kwa umakini na kwa udharura wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijulishe tu Bunge lako Tukufu kwamba, katika ziara zangu kama Waziri mpya, ziara ya kwanza nimeifanya katika Shirika hili la Reli (*TRA*), sijafanya ziara sehemu nyingine. Viongozi wa *TRA* nimeshakaa nao si chini ya mara tatu mpaka hivi sasa tangu nimekuwa Waziri na sijakaa na Viongozi wa Shirika lingine hata mara moja. Kwa hiyo, hili tutalifuatilia kwa umakini na tutalihakikisha kama ambavyo wametuahidi kwamba, safari hizi zitaongezeka kuwa nne hivi karibuni. Kama nakumbuka sawasawa, ndani ya mwezi Agosti, 2008 safari hizi zitakuwa zimeongezeka na kuwa nne. Tutalifuatilia kwa karibu ili tuweze kupunguza sana kero hii ambayo tunaipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba maelezo katika eneo moja mionganini mwa maeneo ambayo nilichangia wakati nilipokuwa nikichangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Wizara ambayo kidogo imetusahau katika eneo hili ambalo ninataka kuliombea maelezo leo ni Wizara ya kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa.

Ninashindwa tu kukamata mshahara wake na kutoa shilingi kwa sababu ya maeneno ya faraja aliyonipa ya Mererani kwamba, sasa Mererani inafanyiwa *feasibility study* kwa ajili ya kuwekewa lami na *addendum* iliyotolewa leo ambayo ina shilingi bilioni moja kwa ajili ya maji ya Simanjiro.

Mtakumbuka mwaka 2002, Rais wa Awamu ya Batu, aliugawa Mkoa wa Arusha na kuunda Mkoa wa Manyara na Arusha na akaahidi kutengenezwa kwa barabara inayounganisha Barabara ya Simanjiro na Babati na Makao Makuu ya Wilaya ya Kiteto na Babati.

Mheshimiwa Waziri, bahati mbaya ni mgeni katika Wizara hii, ningependa sana aelewé tu kwamba, *feasibility study* iliyofanyika hapo awali ilikuwa inahitaji shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kukamilisha Mradi huo wakati huo. Kwa kiasi kilichokuwa kimetengwa mwaka jana cha shilingi milioni 900, ungehitaji miaka kama 20 kuunganisha Wilaya hizo na Makao Makuu ya Mkoa. Kwa kiasi alichotenga leo cha shilingi milioni 300, utahitaji miaka 60 kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro na Makao Makuu ya Wilaya ya Kibaya na Makao Makao Makuu ya Mkoa, yaani Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu, Serikali inawaeleza nini Wananchi wa Simanjiro kupunguza shilingi milioni 900 kuwa milioni 300 na kama Serikali ipo radhi tukae miaka 60 bila kwenda Makao Makuu ya Mkoa. Wana-Simanjiro watapenda kusikia kauli ya Serikali katika hili au pengine kutazama pia uamuzi wa awali wa kuunda mkoa huo kama jiografia inakuwa ngumu na kama Serikali inakuwa haina fedha. Nataka tu maelezo kutoka Serikalini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa; Simanjiro! Wenzako wanataka Mikoa wewe unataka wafunge? Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ufanuzi wa hoja ya ndugu yangu, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kama ifuatavyo:-

Tumeahidi ndani ya Ilani kwamba, tutajitahidi kuhakikisha kwamba, tunaunganisha Makao Makuu ya Wilaya zote kwa njia zinazopitika kwa mwaka mzima na kuziunganisha barabara za Makao Makuu ya Mkoa yote. Tupo katika harakati za kufanya hivyo, tutaendelea kufanya juhudhi kubwa kuhakikisha tunapata pesa nyingi zaidi kwa ajili ya kutekeleza miradi hii, ikiwemo na huu Mradi wa Kuunganisha Makao Makuu ya Simanjiro na Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara, Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kukumbuka kipande chetu cha Ndunu – Somanga na kwamba kitashughulikiwa kwa umakini. (*Makofi*)

Mimi ni mpenzi au ni mkereketwa wa *agencies*, ndugu yangu, Mheshimiwa Zitto Kabwe, alizungumzia kuhusu Wakala wa Barabara za Wilayani na mabasi yanayofukuzwa Dar es Salaam kwa jina la kipanya; je, yanaweza yakaletwa kwangu Kilwa Kaskazini? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Dr. Ferdinand Mpanda kama ifuatavyo:-

Mpango wa Serikali ni kupunguza msongamano wa magari katika Jiji Kuu hasa la Dar es Salaam. Kweli tuna mpango wa kuondosha vigari hivi vidogovidogo kutoka maeneo ya katikati ya jiji na kuyapanga katika maeneo mengine nje ya eneo la katikati ya Jiji la Dar es Salaam, lakini hii ni sekta binafsi.

Kwa maana hiyo ni kwamba, hawa wamiliki wa usafiri wa vipanya wana uhuru wa kuchagua kufanya kazi Kawe, Bagamoyo au kule Kilwa kwa Mheshimiwa Mpanda. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mpanda, awashawishi wenyе vipanya ili wavipeleke huko.

**MWENYEKITI:** Wamesikia wenyе vipanya kwamba, Mheshimiwa Mpanda anavitaka. Mheshimiwa Profesa Mwalyosi kwa kifupi, tumebakwa na dakika kumi na tano tu.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nataka kuzungumzia kuhusu Barabara za Wilaya ya Ludewa, Wilaya ambayo imesahauliwa na kutelekezwa na Awamu zote tatu zilizopita za Serikali, pamoja na hii kwa kutokuwapa miundombinu ya uhakika licha ya kuwa na rasilimali muhimu sana Kitaifa.

Kwenye Ilani sisi tunastahili kupata *trunk road* ambayo ni ya lami, Makao Makuu ya Wilaya ziwekwe lami nyepesi. Kule tuna madini tutaanza uchimbaji mwaka huu na Waziri wa Viwanda yupo, barabara iliyopo haifai kuitisha mizigo. Je, Serikali inasemaje kuhusu Mradi huo ambao unaanza mwaka huu?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wa Iringa tuna Barabara Kuu na za Mikoa. Wilaya ya Ludewa ni moja katika Wilaya ambazo tunajua kuna uwekezaji mkubwa wa makaa ya mawe na chuma. Kwa hiyo, Serikali mkakati wake ni kuhakikisha kwamba, inazijenga

barabara hasa zile Kuu na za Mikoa ambazo zinakwenda katika maeneo haya ya machimbo katika kiwango cha lami.

Sasa hivi tuna barabara kwa mfano, kutoka Itoni mpaka Ukumburu na ile inayokuja Mkwii ambayo inateremka mpaka katika machimbo, ambayo bado haijawekewa lami, lakini tunaelewa kwamba kuna uwekezaji mkubwa kule na tuna mradi ambao unataka kuanza. Fedha hazikutosha kuweza kufanya hivyo katika mwaka huu wa fedha, lakini tutajitahidi kufanya hivyo kwa miaka inayofuata.

**MWENYEKITI:** Hiyo pia inamhusu Naibu Spika.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nami nipate ufanuzi juu ya ujenzi wa gati, kwa sababu mwaka jana fedha zilitengwa Sh. 4bn na mwaka huu Serikali imetenga na tenda walisema imetangazwa na ilikuwa ifunguliwe tarehe 22 Desemba, 2007.

Sasa tulikuwa tunataka tufahamu ni lini ujenzi rasmi utaanza katika Gati la Mafia ili wananchi waweze kupata uhakika?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nitoe ufanuzi wa hoja ya ndugu yangu, Mheshimiwa Shah kama ifuatavyo:-

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi tu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio kwa kifupi. Sina taarifa kamili sasa hivi za taratibu za maandalizi kwa ajili ya gati. Kwa hiyo, mara tu nitakapopewa taarifa hizo, nipo tayari kumpatia Mheshimiwa Shah.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi katika Ahadi za Rais, pale Kahama aliahidi barabara ya lami. Mwaka jana wakati akiwa katika ziara aliwahakikisha wananchi barabara ya lami. Majibu yanayotolewa hapa sasa hivi ni bajeti finyu, uhaba wa fedha. Sasa nataka kujua katika bajeti hizi mbili zilizobaki, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba, ahadi zote za Rais zinatekelezwa vinginevyo wananchi waambiwe kwamba haiwezekani.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi wa hoja ya ndugu yangu Mheshimiwa Lembeli kama ifuatavyo: Ahadi zile zimetolewa na Mheshimiwa Rais, kwa maana ya kutekelezwa na Serikali yake ya Awamu ya Nne; imejipanga kuhakikisha kwamba ahadi hizi zinatekelezwa. Katika hotuba yangu nimeonyesha ni kwa kiasi gani tumeweza kutekeleza Ahadi za Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kiasi kikubwa na kwa namna hiyo hiyo tutakwenda kwa Ahadi za Mheshimiwa Rais mpaka tutakapofika ukomo wa uongozi huo. Ahsante sana.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi na nashukuru nilishawaandikia barua, wakanijibu kuwa, kuna barabara ya Ushirombo – Buseresere inayounganisha Wilaya ya Bukombe – Geita, ina daraja zuri sana lakini wakati wa ziara ya aliyejewa Waziri wa Miundombinu aliahidi kulitengeneza kwa moramu. Katika barua aliyonijibu, imeonyesha kwamba hii barabara wao hawaijui na wamesema ni ya Halmashauri, hatuhihudumii hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati tunapitia Sheria, kwenye Barabara za Halmashauri haimo na kwenye Barabara za Mkoa haimo, lakini inatakiwa kutengenezwa kwa kiwango cha moramu. Nilitaka tu ufanuzi ili waitambue kwamba, hii barabara iliahidiwa na Serikali lakini ikiwa ni pamoja na Barabara ya Bwaga – Lunzewe kuwekwa kwa kiwango cha lami. Nilitaka ziwe kwenye rekodi ili ifute hii barua ambayo imeandikwa ya kukanusha.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea maelezo yake hayo, tutayafanyia kazi na nitatuma majibu. Ahsante sana.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa napenda nipaye ufanuzi juu ya Ahadi ya Serikali ya kujenga Barabara ya Kidatu – Ifakara – Mahenge kwa kiwango cha lami, ambayo alitoa *timeframe* ya miaka mitano na inakaribia kwisha, pamoja na Daraja la Mto Kilombero.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya Kidatu na Ifakara ipo katika utaratibu wa ujenzi, pamoja na Daraja la Kilombero. Upembuzi yakinifu na usanifu wa daraja umeshafanyiwa kazi, kwa maana hiyo ni kwamba, tupo katika taratibu za ujenzi wa barabara hiyo. Ahsante sana.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombee baraka, Mwenyezi Mungu akubariki kwa kunipa nafasi hii.

**MWENYEKITI:** Ameshanibariki wewe endelea. (*Kicheko*)

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Sawa. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri yote yaliyotangulia. Nina jambo dogo tu lakini la muhimu nami ni mhusika, tunaomba Serikali itusaidie kutupatia kauli kuhusu upatikanaji wa meli mpya katika Ziwa Victoria. Ahsante sana. (*Makofifi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua sana tatizo hili la usafiri katika Ziwa Victoria na ni katika masuala au matatizo ambayo yanatupa uzito mkubwa katika Serikali. Niseme tu, nimelipokea na Serikali yetu inalifanyia kazi na tutajitahidi kwa uharaka unaowezekana, kuhakikisha tunapata usuluhishi wa tatizo la usafiri katika Ziwa Victoria.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 39, amezungumzia vivuko. Imenichanganya kidogo kwamba, atahamishia kivuko Nyakalilo na Kome, ukizingatia kwamba, maeneo yale kuna Kata ya Nyakasasa na Lugata. Sasa sijui anavyoniambia vivuko vitano na hiki cha Rufiji anapokitaja ndiyo atakihamishia Nyakalilo Kome. Naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Nyawazwa kwamba, nitalifuatilia kwa wataalam Wizarani kuona mpango uliopo wa taratibu ya mgawo wa hivyo vivuko halafu nimjibu, sasa hivi sina jibu la wazi.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, pamoja na Serikali....

**MWENYEKITI:** Endelea tu usiwashukuru muda umekwisha.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Kwa kutenga Sh. 50bn. Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipowashukuru kwa hizi Sh. 50bn nitakuwa siitendei haki Serikali.

**MWENYEKITI:** Muda umeisha nitatumia *guillotine* sasa hivi.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda nimwombe Mheshimiwa Waziri, wakati nachangia niliomba barabara hizi ambazo tuliomba zipandishwe madaraja, nilipenda kufahamu ni zifi sasa hivi ambazo wanazo, kwa sababu tangu mwaka 2002 tumeomba na sasa hivi tuna wasiwasi inawezekana wana rekodi nyingine sio ile ya mwaka 2002. Tungeomba waziweke wazi ili tuweze kufahamu ni zifi hizo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea maombi mengi sana, nakubaliana na maombi yake, tutazitangaza ili ziweze kufahamika ni zifi ambazo tumezipokea.

**MHE. JOHN P. M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwanza, nampongeza kwa...

**MWENYEKITI:** Aaaa.

**MHE. JOHN P. M. SHIBUDA:** Lakini jamani amefanya kazi nzuri.

**MWENYEKITI:** Muda haupo, basi ukae.

**MHE. JOHN P. M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Waziri, naomba ukubali kuratibu kikao ambacho tutajadiliana mimi na wewe, pamoja na Waziri wa TAMISEMI kuondoa matatizo ya maeneo korofii katika Jimbo la Maswa ambayo yapo kilomita 291. Naomba atusaidie.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubali ombi hilo na tutalitekeleza. (*Makofifi*)

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kutujulisha kama madaraja katika Kata ya Ulaya na Zombo kwenye *feeder roads* zinazokua kwenye barabara mpya ya Mikumi – Kilosa yameingizwa katika *detail design engineering*, ambayo ndiyo hatua inayoendelea hivi sasa, pamoja na daraja la pale Mjini Kilosa ambako sasa hivi treni, baiskeli, magari, ng'ombe, mbuzi na kuku wote wanapita kwenye daraja hilo kama watajenga daraja lingine.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana sina majibu kamili kuhusu madaraja ambayo ameyasema, lakini nitampelekea baadaye wakati tukiwa katika Bunge hili hili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa tuna dakika tano, kazi tutakayoifanya ni fupi kabisa, tutasoma *headings* za matumizi basi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i> ...	Sh. 920,618,800
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i> .....	Sh. 6,972,102,400
Kif. 1004– <i>Information, Education,</i> <i>Communication Unit</i> ...	Sh.96,390,200
Kif. 1005 – <i>Procurement Management Unit</i> ...	Sh. 162,910,900
Kif. 2001– <i>Electrical and Mechanical</i> ...	Sh. 00
Kif. 2003 – <i>Transport Division</i> ...	Sh. 35,508,648,400
Kif. 2004 – <i>Communication Division</i> ...	Sh. 00
Kif. 3001 – <i>Supplies and Services</i> ...	Sh. 1,404,038,500
Kif. 5001– <i>Buildings Unit</i> ...	Sh. 00
Kif. 5002 – <i>Safety and Environment Unit</i> ...	Sh. 275,951,400
Kif. 6001– <i>Trunk Roads</i> ...	Sh. 00
Kif. 6002 – <i>Road Division</i> ...	Sh. 161,334,010,000
Kif. 7001 – <i>Rural Roads</i> ...	Sh. 00

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 98 – Wizara ya Miundombinu**

Kif. 1001 – <i>Administration and General...</i> ... ... ... ...	Sh. 78,000,000
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning...</i> ... ... ... ...	Sh. 17,460,600,000
Kif. 2001 – <i>Electrical and Mechanical...</i> ... ... ... ...	Sh. 00
Kif. 2003 – <i>Transport Division...</i> ... ... ... ...	Sh. 40,220,902,000
Kif. 2004 – <i>Communication Division...</i> ... ... ... ...	Sh. 00
Kif. 5002 – <i>Safety and Environment Unit...</i> ... ... ...	Sh. 2,419,000,000
Kif. 6002 – <i>Road Division...</i> ... ... ... ...	Sh. 531,998,280,900

*(Bunge lilirudia)*

### **T A A R I F A**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Hakuna Mwongozo wa Spika. Mheshimiwa Waziri taarifa.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msafiri, taarifa hii kwanza.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu, limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu, makadirio ya matumizi ya fedha kwa Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Naomba kutoa hoja kwamba, makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Miundombinu  
kwa mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Msafiri, taarifa.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Kifungu gani?

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Kifungu cha 67(8).

**NAIBU SPIKA:** Soma kinasema nini.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Kinasema: “Vilevile Mbunge yeoyote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa.”

**NAIBU SPIKA:** Kifungu cha 67, hapana.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, *sorry* ni Kifungu cha 68(7) ndiyo ninachokisoma hapa: “Vilevile Mbunge yeoyote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa na kwa ruhusa ya Spika, atatoa taarifa au ufanuzi kwa Mbunge anayesema ambapo Spika atatamka Mbunge anayesema wakati akisikiliza taarifa hiyo.”

**NAIBU SPIKA:** Sawa, halafu inakwambia sema kifungu gani unachotolea taarifa.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na kifungu 103.

**NAIBU SPIKA:** Kinasema nini?

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Kwenye kifungu kidogo cha (1); jana nilipokuwa nachangia kwenye Hotuba ya Wizara ambayo tumeipitisha sasa hivi, nilipomaliza nilisema sitaiunga mkono Serikali mpaka itakaponipa ufanuzi kuhusu hoja zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepewa ufanuzi wa hoja na nimeridhika. Nilipenda kutamka kwamba, naiunga mkono hoja hii. (*Kicheko/Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ulipokuwa unasema hukutoa hoja, ulikuwa unapiga maneno yako tu kama ungekuwa unatoa hoja ungekuwa umetoa shilingi na hata ungetoa shilingi sisi tungekubali kwamba ukae na shilingi yako kifungu kipite, lakini hukufanya hivyo. Kwa hiyo, yale maneno yalikuwa ya kwako, tunashukuru sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimetumwa na Wabunge wengi sana kwamba, wanaopongeza wanapoteza muda kwa kweli *politically* nilitaka Mheshimiwa Waziri apongezwe.

Kwa sababu kazi ya wiki sita halafu na yeye mwenyewe kama tunavyojua ni mnyenyeketu kama alivyo, mnampa pongezi ili aweze kupata nguvu ya kufanya kazi vizuri zaidi. (*Makofi*)

Nimeombwa niseme, jana sikusikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa na wageni, sasa itabidi nisome wanasema, katika hotuba zote hii ni ya kwanza, kwa sababu imechambua ahadi za Ilani; ikasema ngapi zimetekelizwa, ngapi bado na baadaye watafanya nini katika muda uliobaki.

Kwa hiyo, wakasema na wengine wangesema hivyo, wangekuwa wanatupa upeo wa kutosha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 02.24 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 4 Julai, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*